

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Nane – Tarehe 20 Juni, 2008

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 67

**Ujenzi wa Barabara ya Bunambiyu Hadi
Mhunze Kupitia Idukilo**

MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali ilitoa shilingi milioni 270 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya kutoka Bunambiyu hadi Mhunze kupitia Idukilo; na kwa kuwa, ujenzi huo ulikadiriwa kugharimu shilingi milioni 840/=.

Je, Serikali haioni ni busara kutoa kiasi cha fedha kilichobaki (Shilingi milioni 570) mapema ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo ambayo ni muhimu sana?

NAIBU WAZIRI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu inahudumia sehemu ya barabara kutoka Bunambiyu kupitia Idukilo na kuishia kijiji cha Ngundangali, Sehemu ya kutoka Ngundangali hadi Mhunze yenye urefu wa Km.8 inahudumiwa na Wakala wa barabara yaani *TANROADS*.

Katika mwaka 2006/2007 Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iliwasilisha maombi ya shilingi milioni 840 kwa ajili ya kujenga Km.52 za barabara kwa kiwango cha changarawe kutoka Bunambiyu hadi Ngundangali kupitia Idukilo.

Kutokana na ufinyu wa Bajeti Serikali kupitia Program ya Usafiri katika Halmashauri (*Local Government Transport Program*) ilitoa kiasi cha shilingi milioni 270 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi katika Km.23 za barabara hiyo yenye urefu wa Km.52 kuanzia kijiji cha Bunambiyu hadi kijiji cha Ngundangali kufanya kazi hii. Katika mwaka huu wa fedha mwaka 2007/2008 kazi zinazofanyika ni:-

- (i) Kuchonga barabara hiyo;
- (ii) Kujenga makalvati;
- (iii) Kuweka changarawe na mifereji ya maji; na
- (iv) Kazi kwa ujumla inatarajiwa kukamilika mwezi Julai 2008. Serikali inatambua umuhimu wa barabara hiyo yenye urefu wa Km.52 na ndio maana ilitoa fedha ili barabara hiyo ianze kupatiwa matengenezo ya sehemu korofi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo maombi ya fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara kutoka katika Halmashauri ikiwamo Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ni mengi ikilinganishwa na uwezo wa kifedha wa Serikali. Serikali katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 ya Program ya Usafiri katika Halmashauri (*Local Government Transport Program*), fedha zilizopangwa kupelekwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iwapo Bajeti hiyo itapitishwa ni shilingi milioni 200, fedha hizi ni kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi (*Spot Improvement*).

Hivyo basi Halmashauri inashauriwa kuweka barabara hiyo katika vipaumbele vya Halmashauri ya Wilaya na kutumia fedha hizo kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi (*Spot Improvement*) kwenye kipande hicho cha barabara kilichobaki chenye urefu wa Km.29 ili barabara hiyo iweze kupitika.

MHE. FRED M. TUNGU: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa dhati kabisa nishukuru Serikali kwa kutoa hizo shilingi milioni 270 mwaka jana, ilitoa katika mazingira magumu sana na ninaomba nishukuru kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Kishapu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba vile vile nishukuru kwa ajili ya hizi shilingi milioni 200 ambazo zipo katika Bajeti na ninaamini kwamba Serikali na Bunge litapitisha Bajeti ili hizo fedha ziende na zikatengeneze hizo Km.29 ambazo zimebaki.

Mheshimiwa Spika, lakini nina swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa sehemu ya barabara ambayo imetengenezwa kutokana na fedha hizi milioni 270 ambazo zimetolewa inalalamikiwa na wananchi hasa kutokana na makalvati ambayo yamewekwa hayaridhishi na utengenezaji wa mifereji ya maji vile vile hauridhishi.

Je, Serikali itawahakikishia Wananchi wa Wilaya ya Kishapu hasa mahali barabara inapopita kwamba wakandarasi wanaojenga barabara hiyo hawatalipwa fedha zao za mwisho mpaka pale watakaporekebisha mapungufu yaliyojitokeza?

NAIBU WAZIRI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kupokea shukrani za Mbunge wa Kishapu na kusema ahsante kwa ku-*appreciate* mchango ambao umetolewa na Serikali na ninawashukuru pia kwa niaba ya Waziri Mkuu kwamba anafurahi kuona kwamba kiasi hicho cha pesa ambacho nimekitamka hapa kimetengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo ningeomba nijibu swali lake hili analolizungumzia kwamba ile shughuli ambayo inaendelea pale kwa sasa hivi inaonekana kwamba haifanyiki kwa kiwango ambacho kinatakiwa na anashauri hapa kwamba tuzuie inaitwa *retention money* ili malipo yasifanyike mpaka tuwe na uhakika kwamba kazi hiyo imefanyika kwa kiwango kinachotakiwa. Mimi ninadhani Mheshimiwa Mbunge Fred Mpendazoe anatusaidia sana hapa, pesa za Serikali zinazoenda katika Halmashauri zetu lazima zitumike kwa utaratibu unaotakiwa na kwa kiwango na kwa ubora ambao unatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninamwomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kuhakikisha kwamba yeye na Baraza la Madiwani wanaenda pale na kusimamia barabara ile na kwamba inatengenezwa kwa kiwango hicho kinachotakiwa na kwa vile ametutahadharisha hapa ninaomba nitamke kwa niaba ya Serikali kwamba tutamshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiwezekana tutume kikosi kutoka Wizarani hapa, kiende mpaka Kishapu kiende kikaangalie barabara hiyo kwa sababu haya ni baadhi ya matatizo ambayo tunayapata katika barabara zetu zote kwamba hazifanyiki kwa kiwango kinachotakiwa.

Kwa hiyo, ninawaomba na Wabunge wenzangu wote na Halmashauri zote zihakikishe kwamba tunapokuwa tumetenga hela kwa ajili ya ujenzi wa barabara, barabara hizo zinatengenezwa kwa kiwango kinachotakiwa. (*Makofi*)

Na. 68

Mpango wa Kuimarisha Njia za Usafiri kwa Nchi za Afrika Mashariki

MHE. MOHAMMED H. J. MNYAA (K.n.y. MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY) aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya malengo makubwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuimarisha njia za usafiri kwa Wanachama. Je, hatua hiyo imefikia wapi na ni maeneo yapi katika nchi zipi yatanufaika na mpango huo?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakary Khamis Bakary, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa moja kati ya malengo makubwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuimarisha njia za usafiri kwa Nchi Wanachama. Kwa sasa Nchi Wanachama zinatekeleza miradi mbalimbali iliyopewa kipaumbele na kuainishwa katika Mkakati wa Tatu wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Mwaka 2006-2010.

Katika Mkakati huo Mkataba wa kuimarisha njia za usafiri na uchukuzi umebainishwa. Lengo kuu la Mkataba huo ni kuunganisha Nchi Wanachama kwa kuimarisha njia za usafiri na uchukuzi ili kukuza biashara baina ya Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Spika, Hatua iliyofikiwa katika sekta ya usafiri ni kama ifuatavyo:-

(a) Kazi ya uhandisi na michoro kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga – *Athi river* imekamilika ambapo taratibu za awali za ujenzi wa mradi huo zinaendelea vizuri, na “*African Development Bank (ADB)*” na “*Japanese Bank for International Co-operation (JBIC)*” zinafadhili mradi huo.

(b) Mheshimiwa Spika, Kuhusu mradi wa barabara ya Malindi – Mombasa – Horohoro – Tanga – Sadani – Bagamoyo kazi ya upembuzi yakinifu inaendelea na lengo kuu la mradi huu ni kuwa na barabara inayounganisha bandari ya Dar es Salaam na Mombasa. Aidha, “*Millenium Challenge Co-operation (MCC)*” imetenga fedha kwa ajili ya barabara ya Tanga – Horohoro.

(c) Mheshimiwa Spika, mradi wa usalama wa usafiri wa anga ambao unahusu kanuni za usafiri wa anga katika Nchi Wanachama unaendelea vizuri na tayari Itifaki ya kuanzisha chombo kitakachosimamia usalama wa usafiri wa anga imekwishasainiwa mwezi Aprili mwaka 2007. Menejimenti ya chombo hicho imeshateuliwa na kuanza kazi ambapo Makao Makuu ya Taasisi hii yanategemewa kuwa Entebbe, Uganda. Aidha, mradi wa kuendeleza Karume *Airport* Pemba umekubaliwa kuwa mmoja wa miradi itakayofadhiliwa na *ADB*.

(d) Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Maendeleo ya Reli ya Afrika Mashariki (*The EAC Railway Development Master Plan*), umebainisha maeneo katika Nchi Wanachama kwa nia ya kuunganisha nchi hizo kwa maendeleo ya usafiri wa reli. Hivi sasa ripoti ya wataalam waelekezi imo katika hatua za mwisho na hivi karibuni inategemewa kuwasilishwa kwa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki kwa maoni ili utekelezaji uanze.

(e) Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa majini hatua mbalimbali zinachukuliwa ikiwemo kufanya utafiti kwa ajili ya kuelewa kina cha maji na njia za kuweza kupita meli katika Ziwa Victoria.

Aidha, hatua za kutafuta fedha kwa ajili ya vifaa vya kuongozea meli na ukarabati wa Bandari ya Kisumu – Kenya, Mwanza – Tanzania na *Port Bell* – Uganda zinaendelea vizuri, pamoja na jitihada hizo, jumuiya inaendelea na taratibu za kuunganisha Ziwa Tanganyika katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, miradi ya Zanzibar itakayoombewa ufadhili chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tayari imeshafikishwa kwenye Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na taarifa ya miradi hiyo imeshawasilishwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa hatua zaidi. Aidha, Nchi zote Wanachama wa Jumuiya ya Afrika

Mashariki yaani Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi zitanufaika na mpango huu wa miradi kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki.

MHE. MOHAMMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa swali la nyongeza.

Kwa kuwa, njia zote alizozitaja za kuimarisha usafiri ni za barabara na za maziwa pamoja na reli na hakuna njia hata moja aliyoitaja ya kuimarisha usafiri wa baharini ambayo ni *old traditional* iliyo zoeleka na kwa kuwa, njia ya baharini ndio ambayo inasaidia kwa kuimarisha biashara katika Visiwa vya Unguja, Pemba, Bandari za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara.

Je, ni kwa nini mpango huo haukuingiza njia ya baharini angalau ikapatikana meli moja kubwa ya mizigo na njia za usafiri wa meli za haraka za *speed boat*? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohammed Mnyaa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa usafiri kwa njia ya baharini na umo katika mpango na sasa mazungumzo yanaendelea, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa mara utaratibu utakapokamilika basi shughuli hizo pia zitafanikisha vizuri katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki, katika eneo la bahari.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hii barabara ya Arusha – Namanga – Nairobi kwa upande wa Kenya hiyo barabara imeshaanza kutengenezwa. Je, mkandarasi aliyeitengeneza hii barabara ni mmoja au ni wawili? Na kama ni wawili kwa upande wa Tanzania huyo mkandarasi ataanza kazi lini?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kaika Telele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakandarasi hawa watakuwa wawili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikukubaliana na mapendelezo ya awali ya mkandarasi yule aliyechukua sehemu ya Kenya na kwa nia ya kuhakikisha kwamba fedha za Jamhuri ya Muungano zinatumiwa ipasavyo tunahakikisha kwamba ufanywe utaratibu mpya wa kupata mkandarasi mwingine. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari mkataba umesainiwa na mwezi Agosti mwaka huu kazi itaanza rasmi kwa upande wa Tanzania na gharama yake ni bilioni 81.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALAAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, upembuzi yakinifu sasa hivi unafanyika katika barabara ya kutoka Bagamoyo, Pangani, Tanga na wakati huo huo sasa hivi barabara ya

kutoka Tanga – Horohoro itawekwa lami kutokana na pesa za MCC. Je, upembuzi huo yakinifu unaofanyika kati ya Bagamoyo, Pangani na Tanga je, utainisha na daraja katika Mto Pangani ili tuondokane na matatizo ya vivuko?

SPIKA: Sijui kama ni la Afrika Mashariki hili? Nadhani litasubiri, litajibiwa na miundombinu, baadaye.

Na. 69

Uvunaji wa Maji kwa Kutumia Mabwawa na Maporomoko

MHE. JUMA H. KILLIMBAH aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa matengenezo ya barabara ya Dodoma –Singida –Nzega kulichimbwa udongo mwingi ardhini na kuacha mashimo ambayo kwa kiwango fulani yanafanana na mabwawa na malambo:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuyatumia mabwawa hayo hasa yale ya kijiji cha Maluga, Msingiri, Kibigiri, Nswelembwe na Mseko kuvunia maji wakati wa mvua ili yatumike kwa shughuli za umwagiliaji nyakati za kiangazi?

(b) Je, ni mipango ipi iliyoandaliwa ya uvunaji maji kwenye maporomoko ya Wembere, Mto Keuka Ng’ombe, Kikonge na kwingineko ili maji hayo yasidie kwa kilimo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kimsingi Serikali haina tatizo na maji yaliyotuma wakati wa mvua kwenye mashimo yaliyochimbwa wakati wa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Singida – Nzega kutumika kwa shughuli za umwagiliaji wakati wa kiangazi. Hata hivyo suala muhimu ni iwapo tathmini ya wataalam itakayobainisha kama mashimo hayo yana ujazo unaotosheleza kwa kilimo cha umwagiliaji wa mazao wakati wa kiangazi na kama yanaweza kutoka katika mashimo hayo kwa kutiririka ni la kusukumwa na pampu ili kuweza kumwagilia mashamba. Wataalam wa umwagiliaji watawasaidia wakulima kupima ujazo wa madimbwi hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato wa kuibua na kupanga miradi ya Maendeleo, ikiwemo ya kilimo cha umwagiliaji kwa kuvua maji ya mvua, kwa wananchi wenyewe, tunashauri wataalam wa Wilaya ya Iramba wahamasishe wananchi wa Wilaya hiyo kuibua miradi ya umwagiliaji kama ilivyofanyika katika miradi ya Masimba, Mlandala na Tyeme Masagi, na waingize ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhi maji katika mipango yao ya Maendeleo ya kilimo ya Wilaya.

Hata hivyo Wizara yangu kwa kupitia Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Kati ilikwishabaini kuwa miradi hiyo ina tatizo la upungufu wa maji hata wakati wa msimu wa mvua kutokana na kukosekana kwa mabwawa ya kukinga na kuhifadhi maji. Kwa sababu hiyo Wizara

imeshauri Halmashauri ya Wilaya ya Iramba iombe fedha za ziada kutoka katika Mfuko wa Wilaya wa Maendeleo ya Kilimo cha Umwagiliaji (*District Irrigation Development Fund - DIDF*) kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa kama sehemu ya miradi ya umwagiliaji itakayoibuliwa. Miradi hiyo inaweza kuhusisha maporomoko ya Wembere, Mto Keuka Ng'ambe na Kikonge. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itatoa utaalam wa kusanifu na kufanya makadirio ya gharama na tayari Wizara imeshapokea maombi ya miradi kama hiyo kwa miradi ya Msingi, Masimba na maombi yanafanyiwa kazi kwa ajili ya kuombewa fedha za utekelezaji katika mwaka 2009/2008.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, madimbwi anayoyasema Mheshimiwa Naibu Waziri ni madimbwi ambayo wananchi wapo tayari kuyatumia na wana uhakika kwamba yale maji yanatiririka hapo, lakini kwa kuwa tayari ule ujenzi wa barabara yaani kutoka Shelui hadi Singida umekamilika na yule *contractor* ameanza kuyafukia yale mashimo. Sasa je, Wizara ipo tayari kuongea na yule *contractor* ambaye ni kampuni ya *CHICO* ili ayaache yale mashimo na waweze kuyatumia wananchi kwa shughuli ya kilimo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa pamoja akiwa anajibu ameelezea juu ya miradi ya Masimba na amezungumzia mradi wa Mlandala pamoja na ule wa Tyeme Masagi, lakini Mheshimiwa Waziri anayo taarifa kwamba miradi ile kwa mfano ule wa Tyeme Masagi ulijengwa mwaka 2005 na hii ya Masimba na Mlandala ilijengwa mwaka 2006 lakini miradi hiyo haijafanya kazi hata siku moja. Je, Wizara inayo taarifa ya pesa zinazopotea bila kufanyiwa kazi na hali miundombinu inaendelea kuibiwa?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Killimbah, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madimbwi ambayo yako pembeni mwa barabara, utaratibu ni kwamba kwa kawaida wakandarasi wanawekewa katika masharti ya ujenzi kwamba wayafukie madimbwi yale miradi inapokamilika. Lakini iko pia *provision* ya kwamba kama wananchi wa maeneo hayo wanaona kabisa kwamba wanaweza wakayatumia maji hayo bila kuathiri mazingira basi huwa wanaachiwa kama ilivyofanyika katika barabara kule Chalinze. Kwa hivyo, ombi la Mheshimiwa Mbunge ni sahihi kabisa tutaomba pia Wizara ya Ujenzi isaidie katika hilo kwa sababu kuna uwezekano huo wa kumwomba mkandarasi ayaache kama inaonekana yana faida kwa wananchi wale na haiathiri mazingira. Kuhusu miradi ya Masimba na Tyeme Masagi, labda nikiri kwamba ninaelewa leo kwamba haifanyi kazi, nimelichukua Mheshimiwa Mbunge na mimi nitafanya tena ziara kukagua kwa sababu tunatumia pesa nyingi kwenye mabwawa haya, nitakagua kama kuna mabwawa hayafanyi kazi au miradi haifanyi kazi basi tutafanya utaratibu wa marekebisho. (*Makofi*)

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ilitoa fedha nyingi kwa ajili ya kutengeneza Bwawa la Msingi na Mwangeza na kwa kuwa, Serikali iliahidi hapa hapa Bungeni wakati inajibu swali langu kwamba itatenga milioni 154 kwa ajili ya Msingi na 130 kwa ajili ya Bwawa

la Mwangeza. Je, hizo fedha mwaka huu wa fedha zitatengwa ili kusaidia kutengeneza mabwawa ambayo yalitengenezwa na yakaharibiwa na mvua?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *CRDB*, Mheshimiwa Mbunge Mgana Msindai, kama ifuatavyo. Kumradhi Mheshimiwa Mgana Msindai. Ni kweli kabisa tuliahidi kwamba Mabwawa ya Msingi na Mwangeza yatapatiwa fedha na ninafahamu kabisa kwamba wilaya tayari ilitenga milioni 25 zingine za ziada kupitia utaratibu wa *DADPs*, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mgana Msindai kwamba miradi yote siyo hii ya kwake tu ambayo kwa sababu imetokea dhoruba ambayo iko nje ya uwezo wao kama hiyo ya mvua kuharibu basi hiyo hata katika taratibu za ukandarasi tunaita ni *force module* hatuwezi tukasema tulikwishamaliza. Kwa hiyo, ninataka nimhakikishie kwamba tutaingalia miradi hii katika mwaka huu 2008/2009, lakini basi niwaombe mpitishe Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika swali la msingi limezungumzia Wembere na halikujibiwa kitu chochote kuhusu Wembere na kwa kuwa, Wembere iko mpakani mwa Mkoa wa Singida Wilaya ya Iramba na Mkoa wa Tabora Wilaya ya Igunga na ni sehemu nzuri sana kwa kilimo cha umwagiliaji na sasa tunahitaji chakula na kwa hali halisi ilivyo tuna upungufu wa chakula Duniani. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba lile bonde lote Wembere linafanya kilimo cha umwagiliaji ili kupata chakula kwa wananchi na vile vile kwa mazao ya biashara na kuondokana na umaskini kwa watu wa Igunga na watu wa Iramba? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la Wembere tunalifahamu na mimi mwenyewe ninalifahamu lakini tunavyolitizama kwa sasa ni kwamba katika Wilaya ya Igunga tunayo mradi mkubwa unaitwa Mwamapuri na uko katika *catchments area* hiyo hiyo na bwawa lile limejengwa zamani tu miaka ya 71 kwa gharama kubwa na Serikali imetumia mabilioni mengi kujenga mradi wa maji unatumia bwawa lile ambao uko pale Mwamapuri na unamwagilia hekta 540. Kwa hivyo tunachofanya sasa baada ya kupata maombi ya kuendeleza Wembere ni kufanya tathmini kwamba miradi iliyo juu ya bwawa hilo ambalo ni la tatu kwa ukubwa katika Tanzania haitaathiri bwawa la Mwamapuri, kutathmini kuonekana hivyo basi na Wembere *Plains* nazo zote hizo zitatekelezwa.

Na. 70

Mapinduzi ya Kilimo

MHE. JAMES D. LEMBELI aliuliza:-

Kwa kuwa, lengo la Serikali ya Awamu ya Nne kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ni kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo yatakayomwezesha mkulima wa Tanzania kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza kwamba, hadi sasa ni wakulima wangapi wa pamba nchini wamepata huduma na vyenzo za kilimo, za kuwawezesha kuzalisha zaidi bila matatizo na wameanza kupata maisha bora kama Ilani ya CCM inavyosema?

(b) Je, ni lini Serikali itawaondolewa wakulima wa pamba hususan wa Wilaya ya Kahama mfumo wa *passbook* ambao ukilalamikiwa kwa muda mrefu kwamba, unawanyanasa na kuwaibia fedha zao?

(c) Je, Serikali kwenye kipindi cha miaka miwili na nusu iliyopita ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM imefanya mambo gani mahsusi ya kuwasaidia wakulima wa pamba na hali halisi ya zao hilo ikoje nchini ikilinganishwa na hali ya mwaka 2005? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kati ya mwaka 2005 – 2007 Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo imetoa mikopo kwa wakulima 60, yenye thamani ya Sh.1,829,485,800/= iliyowezesha wakulima hao kununua matrekta 60 mapya.

Aidha, wakulima 43 walipatiwa jumla ya Sh.148,460,000/= kwa ajili ya kukarabati matrekta yaliyokuwa yameharibika. Mbali na mikopo toka Mfuko wa Pembejeo, *Program* ya kuendeleza kilimo *ASDP* inayotekelezwa kupitia *DADPs* za Wilaya zinazolima pamba imechangia jumla ya Sh.4,188,921,954/= (2007/2008), ili kuboresha kilimo cha mazao mbalimbali likiwemo zao la Pamba.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko ya wakulima kuhusu mfumo wa *passbook*, Serikali imeufuta na Bodi ya Pamba imeagizwa kutafuta mfumo mbadala utakaowawezesha wakulima wa pamba kupata pembejeo hususan madawa ya pamba na mbegu. Serikali imefika uamuzi huu kutokana na azimio la mkutano wa sita wa Wadau wa Sekta ndogo ya Pamba uliofanyika mjini Mwanza tarehe 6 Aprili, 2008 ambao ulionekana kutopendelea mfumo wa *passbook*.

(c) Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali kama zilivyoielezwa katika sehemu (a) hapo juu zimechangia kuongezeka uzalishaji wa zao la pamba.

Aidha, Serikali ilitoa ruzuku ya shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya vidudu vya zao la pamba. Hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali zimechangia kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kutoka marobota 258,900 mwaka 2003/2004 hadi marobota 700,000 msimu wa 2005/2006. Matarajio kwa msimu wa 2008/2009 ni kuzalisha marobota 800,000 kiasi ambacho hakijawahi kufikiwa katika historia ya zao hilo. (*Makofi*)

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa napenda niipongeze Serikali kwa hatua iliyochukua ya kufuta mfumo wa *pass book*, mfumo dhalimu ambao ulikuwa ukiwanyonya na kuwaibia wakulima wa zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, malipo halali kwa mazao anayouza mkulima kwa wanunuzi ni haki ya mkulima na ni kichocheo cha kuzalisha zaidi na kutokumlipa ni kosa.

Kwa kuwa, wakulima wa zao la pamba wa Wilaya ya Kahama na wenzao wa Wilaya Uyui na Bukombe tangu mwaka 2004 hadi leo hawajalipwa kwa mauzo yao ya pamba kwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama.

Kwa kuwa, ndani ya Bunge hili Serikali imeahidi mara mbili kwamba imelichukua deni hilo na itawalipa wakulima hao kwa mazao yao mwaka 2004.

Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi zake hizo?

Kama Waziri wa Kilimo mwaka jana alisimama kidete kutetea maslahi ya wakulima wa zao la korosho kwa Mikoa ya Kusini na akaahidi kwamba atajiuzulu kama hawatalipwa. Ni kwa nini mpaka leo ana kigugumizi cha kujiuzulu kwa sababu ya kushindwa kuwalipa wakulima wa zao la pamba wa Wilaya ya Kahama, Uyui na Bukombe kwa sababu na wao ni Watanzania kama wale wa Mikoa ya Kusini?

SPIKA: Sidhani kama ana kigugumizi alikuwa hajaombwa kujiuzulu. Sasa ndiyo umemwomba hivyo. Lakini ana majibu.

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa James D. Lembeli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme taratibu za kulipa madeni haya ya ushirika kwanza ni kuyahakiki na baada ya kuyahakiki ndiyo yanaingia kwenye mchakato mzima wa kuyalipa. Hatua tuliyoifanya mwanzoni ni kuhakikisha kwamba vyama vya Ushirika hivi vikuu vinalipiwa madeni yale ya mabenki ili viweze kukopesheka. Ndicho tulichofanya kwenye vyama vya Nyanza, *SHIRECU* na vyama vile ambavyo kuna wakulima wa korosho yaani maeneo ya Kusini.

Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa James Lembeli, kwamba kama madeni haya yalishahakikiwa mpaka 2004 Desemba basi madeni haya yatalipwa siku chache zijazo lakini siyo katika Bajeti hii.

Swali lake la pili, kama Mheshimiwa Waziri alisema atajiuzulu nadhani linamhusu Waziri mimi bado sijasema. Kwa hiyo, nadhani nitampelekea Waziri salaam hizi atamjibu mwenyewe.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ina mpango mzuri sana wa kuwafanya wakulima wa zao la pamba na kuboresha maisha yao na inapendeza.

Kwa kuwa, wakulima za kanda ya ziwa wamehamasishwa sana na wakalima pamba kwa wingi, hususan katika Jimbo la Bukombe lakini cha ajabu bei imeshuka sana kuliko mwaka jana. Mwaka jana bei ilifika shilingi 500 na mwaka huu ni shilingi 400.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hali ya wakulima hawa ili hawa waweze kulima zao hili la pamba kwa wingi na liweze kuleta pato la Taifa badala ya kuwadidimiza kwa kuwashushia bei?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Bei ya zao lolote hasa katika mazao haya ya biashara bei zake zinatokana na bei ya soko la dunia kama bei ya soko la duni ya pamba imeshuka basi italeta madhara pia katika pamba ya Tanzania. *(Makofi)*

Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kama pakitokea uzalishaji mwingi wa pamba duniani inasababisha kushuka kwa bei ya pamba.

Serikali inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa pamba zaidi kama nilivyosema kwamba Chama cha Wafanyabishara wa Pamba tayari walishatoa matrekta 100 ambayo wanayaaazimisha kwa wakulima ili waweze kulima mashamba yao na mfuko wa kuendeleza soko la pamba ulishatoa shilingi bilioni 14.5 kuanzia mwaka 2005 mpaka leo kwa ajili ya viuatilifu, vinyunyizi, utafiti pamoja na mambo mengine.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba Serikali itaendelea kuhakikisha uzalishaji wa Pamba unakuwa mzuri lakini tutaendelea kuhakikisha pia kwamba ni vipi tufanye ili bei ya pamba iwe nzuri.

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA aliuliza:-

Kwa kuwa jimbo la Kilwa Kaskazini huzalisha mazao mengi machanganyiko kama ufuta, mbata, machungwa, maembe, mihogo na kadhalika.

Je, ni lini Serikali itaunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili wananchi wautumie ipasavyo utajiri wa nchi walionao?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson Ferdinand Mpanda, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mapendekezo ya kuunda Bodi ya Nafaka na mazao mengine mchanganyiko yalikuwa yakisubiri kukamilika kwa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo inayoandaliwa na Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko.

Kwa sasa rasimu ya Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ipo tayari, hivyo Wizara imeandaa rasimu ya Waraka wa mapendekezo ya kuanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mengine machanganyiko ambayo inategemea kupitishwa na Serikali mwaka 2008/2009. Aidha, Wizara imetenga fedha shilingi milioni 300 katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 kwa ajili ya maandalizi ya kuanzisha Bodi hiyo.

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Bado nipo!

SPIKA: Samahani sana! Mheshimiwa Dr. Mpanda!

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Mheshimiwa Spika, mimi sikuoni lakini weweunaniona Mheshimiwa Spika! (*Kicheko*)

SPIKA: Kuna gizagiza kidogo hapo, mlingoti huo unazuia kidogo. Samahani sana!

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Ahsante sana. Ninaomba kuuliza je, ni lini tarehe kamili au Bunge gani maalum ambalo litakuja kusema badala ya kusema 2007/2008 au 2008/2009. Hivi Bunge gani maalum litakalokuja kuunda hii Bodi na endapo kama haitaundwa nitakuwa mtovu wa nidhamu kama sitatoa shilingi kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa niba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Mpanda kama ifuatavyo:-

Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mpanda kwa kufuatilia sana suala la uzalishaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, amekuwa anafuatilia kwa makini sana hata wakati ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi na Kilimo anapiga simu mara nyingi Wizarani kwa ajili ya kuulizia uanzishwaji wa Bodi hii. Kwa kweli nampongeza sana.

Niseme kwamba kama nilivyoeleza katika jibu la msingi tayari Serikali imeshatenga Shilingi milioni 300 kwa mwaka huu kitu ambacho kilikuwa hakujawahi kufanyika kwa maana ya kutenga fedha kwa ajili ya kuanzisha kwa bodi hii.

Kwa hiyo, mara baada ya kupitishwa kwa Bajeti yetu mchakato wa kuanzisha Bodi hii utaanza.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Bodi nyingi ambazo sasa hivi zipo na mazao mbalimbali Serikali imeahidi kuzihudumia kwa 100% lakini kwa bahati mbaya haifanyi hivyo na Bodi hizo huwa dhaifu katika utendaji wake. Je, Serikali inahakikisha vipi kwamba bodi hii inayaotarajiwa kuundwa sasa hivi itakuwa tofauti na hizi ambazo tunazo sasa hivi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:

Kwanza niseme kwamba ni kweli Serikali inazihudumia Bodi kwa asilimia mia moja, yanatokea tu matatizo yale madogomadogo ambayo ni rahisi na Serikali inaweza ikayarekebisha. Kwa hiyo, sidhani kama kutatokea tatizo lolote kwa Bodi hii kwa sababu hata hivyo kwenye Kamati ya Ardhi na Kilimo tumeshazungumza ni jinsi gani ya kuboresha mapato yaweze kufika vizuri kwenye zile Bodi ili waweze kuendeleza mazao yanayohusika.

MHE. HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi na ninataka niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Wilaya ya Kilwa inazalisha sana ufuta kuliko Wilaya zote hapa nchini. Kwa kuwa, wakulima wangu wa Kilwa hawakutendwa haki kwa zao la ufuta mwaka huu naiuliza Serikali kwa nini mwaka huu zao la ufuta Kilwa halikuleta ushidani ili wakulima wangu wangeweza kufaidika kama walikuma wa Dodoma wanaopata bei ya shilingi 1800 wakati tumelazimishwa kuuza ufuta wetu kwa shilingi 1300 ili Ushirika inunue. Je, Serikali haioni sasa kwamba Kilwa haikutendwa haki?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dewji, kama ifuatavyo:-

Niseme nimepokea lalamiko hilo tutakwenda kulichunguza na kulifanyia kazi ili tuweze kuwatendea haki wananchi wa Jimbo la Kilwa. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa ni zamu ya Wizarani ya Mambo Ndani ya Nchi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum.

Mauaji ya Kikatili Nchini

MHE. ANIA S. CHAUREMBO aliuliza:-

Kwa kuwa, imekuwa ni kitendo cha kawaida kwa jamii kufanya vitendo vinavyokiuka haki za binadamu kama mauaji ya albino; na kwa kuwa baadhi ya watu hufanya vitendo hivyo kwa imani za kishirikina ili wapate utajiri:-

- (a) Je, mpaka sasa serikali imefanya juhudi gani za kuihami jamii?
- (b) Je, ni wahusika wangapi waliokamatwa kuhusiana na viendo hivyo?
- (c) Je, serikali ina mpango gani kabambe wa kupambana na washirikina hao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja na kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumejitokeza matukio ya mauaji ya Albino yanayotokana na imani za Kishirikana. Miongoni mwa Mikoa iliyokumbwa na tatizo hili ni pamoja na Mwanza, Mara, Mbeya, Arusha na Kagera. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2008 jumla ya Albini 16 waliuawa katika sehemu mbalimbali hapa nchini na Albino mmoja amejeruhiwa kwa kukatwa mkono. Watuhumiwa 36 wamekamatwa kuhusiana na mauaji ya kishirikina dhidi ya Albino.

Mheshimiwa Spika, Matukio haya ya mauaji ya Albino yanahusishwa sana na imani za kishirikina. Hivyo Serikali kwa kushirikisha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, TAMISEMI, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Tume ha Haki za Binadamu na Utawala Bora na kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali kikiwemo chama cha Albino na Chama cha Waganga wa Jadi, pamoja na hatua zingine inaendelea kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuwaorodhesha waganga wa jadi na vituo vyao vya Tiba Asili na Tiba Mbadala katika maeneo mbalimbali kuanzia vijijini hadi Mikoani pamoja na vyama vyao ya Uganga. Hii itasaidia kuwabaini waganga pandikizi ambao wanatumia fani hiyo kwa kujitajirisha na kupandikisha chuki ndani ya jamii.
- (ii) Kutoa elimu (uhamasishaji) kwa waganga wa tiba asili kwa kuvihusisha vyama vya waganga, waganga wenyewe na Viongozi wa Serikali za Mitaa, wafanyabiashara wanaojishughulisha na uchimbaji wa Madini, uvuvi na biashara ya usafirishaji kuachana na imani potofu kwamba viungo vya Albino vinaweza kuwatajirisha.

- (iii) Kufanya upelelezi kwa lengo la kuwabaini watu wanaotumika kujihusisha na viendo vya mauaji kwa kukodishwa.
- (iv) Kuendelea kuwasajili Albino wote waliopo hapa nchini na kujua maeneo wanayoishi.
- (v) Kutumia falsafa ya Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii kwa lengo la kuwashirikisha wananchi ili waweze kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu wakiwemo waganga wa jadi wanaojishirikisha na vitendo hivi.

MHE. ANIA S. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswala madogo mwili ya nyongeza.

Kwa kuwa, jamii hii ya maalbino hivi sasa imekuwa ikiishi kwa wasiwasi mkubwa hapa nchini, na hata mtu akitoka katika nyumba yake hategemei kwamba atarudi tena katika nyumba yake.

Kwa kuwa Waziri katika jibu la msingi ameeleza kwamba Serikali inaendelea kusajili jamii hii ya maalbino na kujua sehemu wanazoishi. Je, kusajili huku kwa maalbino na kujua sehemu wanazoishi kutasidia kutoendelea na mauaji ya maalbino hapa nchini?

Kwa kuwa, Naibu Waziri katika jibu lake vilevile amejibu kwamba katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mbeya, Mara na Mikoa mingine hapa nchini ndiyo inayoongoza katika suala zima la mauaji haya ya maalbino. Ningependa kujua ni Wilaya ipo ambayo imeongoza katika mauaji hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ania S. Chaurembo. kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kusajili maalbino pale walipo popote hapa nchini hii ni baadhi ya hatua ambazo tunazichukua ili tuweze kujua kwa uhakika wako maeneo gani.

Lakini ningependakusema hapohapo na kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi ni hatua ambazo Serikali inazichukua lakini suala hili ni pana zaidi lingependa ushirikiano wa watu wote hata Wabunge wakiwemo, jamii ikiwemo kwa sababu ni suala la kuelimisha, kuhamasisha na kuwaondoa watu katika imani potofu za kusema kwamba wanaposhughulikia na au wanapopata viungo vya maalbino basi inawasaidia katika shughuli zao kibiashara ama katika kuwaletea utajiri.

Kuhusu suala la pili, mpaka sasa hivi bado tunakusanya takwimu lakini katika eneo ambalo linaongoza kwa mauaji ya maalbino ni Mwanza ambapo mpaka sasa kwa takwimu tulizokuwa nazo mpaka mwezi Aprili mwaka huu 2008 ni maalbino 10 na watuhumiwa waliokamatwa kuhusiana na mauaji hayo ni 25.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. AL-SHYMAA JOHN KWEGYIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa maalbino bado wanaendelea kuuawa Serikali haioni kwamba sasa hivi ni wakati muafaka kwa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Mbeya wananchi wa Mikoa hiyo kuandika kwa siri hao washirikina na waganga waandike kwa siri kupeleka kwa Mkuu wa Mkoa kuwataja hao wanaofanya vitendo viovu maana tena naona inazidi?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante saba Mama, ahsante sana Mheshimiwa. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali au ushauri wa Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Mimi nauchukua kama ni ushauri na ni kweli hiyo tunafanya katika jitihada za kuhakikisha kwamba tunawahamasisha wananchi kwamba watuletee habari na au wapeleke habari katika vyombo vinavyohusika ili watu ambao wanafanya vitendo vya namna hii waweze kushughulikiwa. Kwa hiyo, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo tunalizingatia na ni miongoni mwa hatua ambazo tunazichukua.

Na. 73

Mafao ya Askari wa Jeshi la Polisi

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI aliuliza:-

Kwa kuwa, Askari wa vyeo vya chini wa Jeshi la Polisi nchini wanapofikisha miaka kumi na miwili (12) kazini hutakiwa kuingia mkataba wa kiinua mgongo au pensheni, na kwa kuwa utaratibu huo hauwahusu Askari wa cheo cha Mkuu Mkaguzi hadi Mkuu wa Jeshi ambao hutawaliwa moja kwa moja na masharti ya pensheni;

Je, Serikali itakuwa tayari kubadilisha sheria hiyo ili askari wote wakifikisha miaka 12 kazini waweze kutawaliwa na masharti ya pensheni ili kuondoa ubaguzi ndani ya Jeshi hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, kwa usahihi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu swali Na. 27 la Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mbunge wa Fuoni, katika Mkutano wa 11 wa Bunge siku ya Tarehe 9 Aprili, 2008 nililitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa mujibu wa *Police Force Service Regulations 1995*, Kifungu

cha 12(b) 1-4 Askari anapofikisha miaka 12 katika Utumishi wake Jeshini. Baada ya Utumishi wa Miaka kumi na mbili (12) katika Utumishi wake Jeshin.

Baada ya Utumishi wa miaka kumi na mbili (12) Askari anakuwa na haki ya kuchagua atawaliwe na sharti mojawapo kati ya Mfumo wa malipo ya Bakshishi (*Gratuity*) au Pensheni. Aidha, Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi (*Police Force and Auxiliary Service Act*) sura ya 322 R.E 2002 kifungu cha 68 pia kimeainisha stahili za Askari waliopo chini ya mfumo huu wa bakshishi. Utaratibu huu unawahusu Askari wa vyeo vya chini ambao hawajafikia cheo cha Mkaguzi Msaidizi.

Mheshimiwa Spika, Askari wote kuanzia cheo cha Mkaguzi Msaidizi mpaka Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa mujibu wa Sheria ya *The Public Service Retirement Benefits Act, 1999* kifungu namba 22 (1)(a) & (b) na (2) wao hutawaliwa moja kwa moja na Masharti ya Pensheni.

Mheshimiwa Spika, Utaatibu wa Askari Polisi anapoajiriwa katika Jeshi la Polisi kulazimika kufanya kazi kwa Mkataba wa miaka mitatu mitatu kwa muda wa miaka 12 kabla hajachagua aina ya malipo baada ya kustaafu unafaa kuendelea kutumika. Mfumo huu haubagui kwa sababu Askari hupewa fursa ya kuchagua yeye mwenyewe kwa hiari yake ama kufanya kazi kwa masharti ya kudumu/pensheni au kufanya kazi kwa masharti ya bakshishi (*Gratuity*) ambapo anakuwa na fursa ya kukatiza mkataba/kuacha kazi na kuweza kulipwa mafao yake.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi litaendelea kuwaelimisha askari wote wanaoajiriwa na ambao hawajafanya chaguo juu ya faida za kumilikiwa na masharti ya pensheni na bakshishi. (*Makofi*)

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri napenda kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa, askari ambao wanajaza hii bakshishi hutumikia Jeshi la Polisi kwa zaidi ya miaka 25 na kushindwa kukatisha halafu wakalalamika na kupata mafao madogo sana ambayo yanakidhi haja kwenye maisha yao.

Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki askari hao na sasa wabadilishe mfumo huo?

Kwa kuwa, Wizara nyingi hukubali kufanyia marekebisho yale masuala ambayo yanalamikiwa kwa maslahi ya wafanyakazi pamoja na Taifa. Kwa nini Jeshi la Polisi linafanya kigugumizi kuufanyia marekebisho mkataba huu ambao mpaka leo nauita mkataba ambao ni wa ubaguzi kwa sababu wanaopata cheo kikubwa wanakuwa na mkataba mwingine na Jeshi la Polisi cheo kidogo wanakuwa na mkataba mwingine?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kuhusu swali la kwanza hakika nasikitika kusema kwamba kwa kweli kuna ubaguzi katika Sheria hii ya Polisi. Utaratibu huu umekuwepo na Jeshi la Polisi walipewa fursa ya

kuulizwa wachague wanalolitaka kati ya mawili na kwa kweli wote katika majibu ambayo tuliyapata siku za nyuma walitaka mfumo uliokuwepo uweze kuendelea ili wale wanaotaka kuachana na Jeshi la Polisi kabla ya kufikia miaka yao ya ku-*retire* wanaweza wakafanya vile na wale ambao watapenda kuendelea pia wanaweza wakafanya vile. Hili lilikuwa ni jambo ambalo waliamua askari wenyewe.

Kuhusu suala la maslahi ambayo wanapata na kwamba kuna utofauti ni kweli kwa sababu hawa wanaochukua mfumo wa *Gratuity* iko njia yake na wale ambao wanakwenda kwa mfumo wa pensheni pia iko njia yake. Kitu tunachokifanya na ni utaratibu wa kidemokrasia ni ningependa kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba hili ni suala ambalo Jeshi la Polisi huwa wanaulizwa. Pia ninataka kusema tu kwamba katika majibu ambayo tuliyapata kutoka katika Jeshi la Polisi ni kwamba walitaka mfumo uliopo uendelee lakini mlango haujafungwa na hii siyo njia ya kidikteta. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo liko wazi na tutaendelea kuzungumza na Jeshi letu la Polisi na hili tutawawekea maana yake hatuwezi tukawalamisha askari. Wale ambao watataka kuacha kazi kabla ya muda wao wawe na uhuru wa kufanya vile na wale ambao wataamua kwamba wanataka kwenda kwa mfumo wa pensheni pia na wenyewe wapate uhuru wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, kwa swali la nyongeza!

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Sheria hizi ni toka ukoloni na tulitaka kuchukua nchi yetu ili kuondoa yale ambayo si mazuri wakati wa utawala wa ukoloni.

Mheshimiwa Spika, je, hatuoni kwamba hili ni moja kati ya hayo wakati siku zote linakuja suala hilo kwamba panatokea matitizo katika taratibu hizi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri alikwishajibu lakini labda usisitize tu jibu lako.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Ndugu Yahya Kassim Issa, kwa kweli kama ifuatavyo:-

Katika jibu ambalo nimelitoa hapo awali nimesema kwamba Jeshi la Polisi walipewa fursa ya kuulizwa wangependa kuchagua lipi?

Tubadilishe mfumo mzima ama tuendelee na mfumo tuliokuwa nao kwa maana ya kusema kwamba wale ambao wangependa waende na mfumo wa *gratuity* na wale ambao wangependa kuendelea na mfumo wa pensheni. Majibu tuliyoyapata ni kwamba walitaka Sheria ilivyo iendelee kuwa vilevile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nasema kwamba hilo tumelifanya na tutazidi kulifanya.

Lakini Serikali haiwezi ikalazimisha hiyo katika Jeshi la Polisi. Itabiti Polisi wenyewe tuwape uhuru kwa sababu wapo wale ambao wanataka njia moja na wapo wale ambao wanataka njia nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 74

Uboreshaji wa Sekta ya Kilimo

MHE. LUCAL L. SELELII aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa kuwa na mifugo mingi na kwa kuwa kuna Mpango wa *ASDP* ambao ni mahsusi kwa ajili ya kilimo na mifugo:-

Je, ni fedha kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya kuboresha sekta hiyo muhimu ya mifugo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali kupitia Wizara za Sekta ya Kilimo ambazo ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Viwanda, Biashara na Masoko na Ofisi ya Waziri Mkuu- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inatekeleza Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme-ASDP*) itakayochukua muda wa miaka saba kuanzia 2006/2007 hadi 2012/2013.

Kiasi cha shilingi trilioni 2.492, zitatumika katika kipindi hicho ikiwa ni mchango wa Serikali, Wahisani, wakulima na wafugaji kwa utaratibu wa Maendeleo ya kilimo ya Wilaya (*DADP's*) kwa kutegemea vipaumbele vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2007/2008 kati ya shilingi 51,426,885,000/= zilizowekwa kwenye Mfuko wa pamoja wa *ASDP* (*ASDP Basket Fund*) kati ya hizo shilingi 14,376,587,000/= sawa na asilimia 27.96 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali katika sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uendelezaji mifugo na masoko, uboreshaji wa mifugo na nyanda za malisho na kutoa kinga dhidi ya magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, Halmashauri ya Nzega peke yake ilitumia jumla ya shilingi 121,856,600/= katika kuboresha Sekta ya mifugo kwa kujenga lambo moja na mabirika mawili ya kunywa maji mifugo, kujenga majosho matatu, kukarabati majosho sita, kununua madume bora ya ng'ombe kumi na tano, kununua majogoo bora mia sita kwa ajili ya vijiji sita, kutenga maeneo ya malisho katika vijiji sita na kutoa chanjo ya ugonjwa wa homa ya mapafu kwa ng'ombe 199,109 na kimeta kwa ng'ombe 5,841.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga trilion mbili na nusu kwa ajili ya kuendeleza mifugo lakini katika mifugo ya Mheshimiwa Waziri sijaona mikakati ambayo inaelekeza kupata soko la uhakika kwa maana ya ujenzi wa minada ya kisasa ili wananchi wafugaji waondokane na tabia ya kuuza mifugo kwa kulangua kuwe na minada ya kisasa inayotumia uzito au kilo. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minada ya kisasa na kuondokana na suala hili la ulanguzi kwa kukisia bei ya mifugo?

Mheshimiwa Spika, la pili, katika hizo pesa zote trilion mbili na nusu hakuna hata maelezo ya kujenga viwanda vya ngozi au vya nyama. Je, kuna utaratibu gani wa kujenga viwanda vya ngozi au nyama hasa kwenye maeneo yenye mifugo mingi kwa mfano Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mwanza, Arusha, Dodoma na Singida? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, nimesema kwamba, katika hizo fedha za *Agriculture Sector Development Programme* kwa kupitia mpango wa *District Agriculture Development Programme*, tunayo mipango mahsusi ya kujenga minada katika sehemu mbalimbali ambayo itatumika katika kuuza mifugo kwa kutumia mizani na hasa hii mipango mingine inayopitia Wizara yangu na mingine inayopitia katika Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, hiyo mipango tunayo katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujenga viwanda vya nyama, kama tulivyosema katika jibu la siku chache zilizopita, tulisema kwamba, kuna kiwanda kimoja pale Shinyanga ambacho kilikuwa cha Tanganyika *Packers* ambacho katika mwaka 2007 kilikabidhiwa kwa Kampuni ya *Triple S Beef Limited* ambacho mwezi Desemba, 2007 kiwanda hiki sasa hivi tunatarajia kitafanyiwa matengenezo na kitakuwa kiwanda cha nyama na hivyo kitanunua mifugo Shinyanga na sehemu za Kanda ya Ziwa.

Pia ukija Ruvu tumeshapata mwekezaji na kiwanda kinatarajia kuwepo pale. Arusha pia tuko katika harakati za kupata mwekezaji, tutaweka kiwanda pale. Sehemu za Kagera vilevile tunatarajia mwekezaji kuwekeza. Vilevile tukija Morogoro sasa hivi kina kiwanda cha Tanzania *Meat Pride* ambacho kinafanya kazi vizuri, ukienda Sumbawanga kuna kiwanda cha *SUMI*. Kwa hiyo, tunayo mipango na vingine vitajengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunauza mifugo ya wakulima kupitia viwanda hivi. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita na maswali yote yamekwisha. Matangazo; kwanza wageni, wageni waliopo Bungeni ambao nina taarifa zao hapa ni wanafunzi hamsini na saba pamoja na walimu wao kutoka Kata ya Zanka, Wilaya ya Bahi, hili ni kundi lingine sio lile la jana wakiwa wanaendelea na ziara yao, tafadhali vijana na walimu msimame. Karibuni sana. Tunawatakia mema katika masomo yenu pamoja na walimu. Kazi njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Gosbert Blandes, Makamu Mwenyekiti wa Sheria Ndogo kwa niaba ya Mheshimiwa George Simbachawene anaomba wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo wakumbuke kwamba kutakuwa na semina Jumapili tarehe 22 Juni, 2008 itakayofanyika Jengo la Utawala, Ukumbi Na. 428, saa tano asubuhi.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI anaomba wanakamati wote wa Kamati hiyo wakutane saa nane mchana leo katika ukumbi Namba 231.

Katibu endelea na *Order Paper* kwa shughuli zinazofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2007 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2008/2009

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimesalia na wachangiaji wa kutoka *back bench* wanne na baadaye kama kawaida Manaibu Waziri pamoja na Waziri mwenyewe watasimama kuweza kuchangia kwa namna ya kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kipindi hiki cha wiki nzima.

Sasa nimepokea ombi kutoka Serikalini ambalo nimelikubali kwamba kutokana na mchango mzito wa Waheshimiwa Wabunge sitini na sita na pia marekebisha mbalimbali ambayo yanabidi yafanyike wameomba, michango ya kujibu zile hoja ifanyike jioni saa kumi na moja halafu ndiyo tupige kura.

Hii itawapa muda wa kutosha na ni haki yao kuweza kuyafafanua masuala yetu vizuri na kwa hiyo msishangae tukishamaliza wenzetu hao wanne nitatoa tu mwongozo na ufafanuzi kuhusu niliyouliza jana. Baada ya hapo tutasitisha shughuli za Bunge mapema ili tukutane tena saa kumi na moja.

Baada ya tangazo hilo naomba nimwite msemaji wa kwanza, wachangiaji wa leo ni Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Maulida Komu, Mheshimiwa Devota Likokola na Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, tunaanza na Mheshimiwa Anna Abdallah.

Samahani vile vitabu *Volume one* kwa kawaida vimekuwa vikiwekwa mezani, ni utamaduni wa siku nyingi halafu vinashughulikiwa pamoja na *Finance Bill* lakini kwa kuwa kuna ombi na vipo hapa, kumekuwa na ombi la Wabunge kwamba wavipate basi nataka sasa vigawiwe ili kila mmoja apate hii *Volume one* ambayo ni *Financial Statement and Revenue Estimates*.

Volume three ni za Mikoa, hizi ni za Serikali Kuu yaani *Revenue Estimates* halafu *Volume Two* kama mnavyofahamu ni Matumizi ya Kawaida na *Volume Four* ni matumizi ya Maendeleo. Vile viwili tuligawiwa Dar es Salaam yaani *Volume Two* na *Four* na *Volume Three* ilikwishagawiwa.

Sasa *Volume One* ndiyo hii inagawiwa na tutaweza kuipata hapa na *in Addendum*, tena zote. Ile *Volume One* ina *Addendum*. Kwa hiyo, igawiwe pamoja na masahihisho na nyongeza na *Volume Four*. Pia kitabu cha matumizi ya Maendeleo nayo ina *Addendum* ambayo ni hii hapa.

(Hapa Vitabu husika viligawanywa kwa
Waheshimiwa Wabunge)

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walimpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi na wataalam wake wote kwa Bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja katika kuchangia hoja hii muhimu iliyo mbele yetu. Jana kuna baadhi ya Wabunge wenzetu walikuwa wanashangaa kwa nini upande huu wa Wabunge wa CCM wakisimama wanakosoa halafu wanaunga mkono. Ningependa kusema kwamba sisi tunayo sera iko katika mwongozo wa Chama cha Mapinduzi ya kujikosoa, kukosoa, kukosolewa na kujisahihisha. Nafikiri ndivyo wanavyofanya Wabunge hapa na ukishakosoa na ukitaka jambo lisahihishwe hakuna tena haja ya kukataa kitu ambacho unataka kisahihishwe, ndiyo sababu. Kwa hiyo, naomba na hili walielewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, nataka kusema tu kwamba hili jambo la *EPA* lisije kutugawa. Tangu nimekaa humu ndani ya Bunge sijasikia hata Mbunge mmoja anayekataa kwamba fedha za *EPA* zisirejeshwe, yupo? Sijamsikia, wote wanataka zirejeshwe. Tunatofautiana namna ya kusema tu humu ndani. Sasa kuna wengine wanasema sana, wanaweka na madoido, wengine tunasema kwa upole lakini lengo ni moja tu, fedha zirejeshwe. Kwa hiyo, hatuogopi, hakuna anayetishwa, lengo letu ni moja tu. Kwa hiyo, ningependa haya tuyaweke vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Chama kingine cha Siasa ambacho hakijaandikishwa kinachoitwa magazeti ndiyo wanaosaidia kufikiria kwamba humu ndani ya Bunge kuna mtafaruku, sijui kuna nini, na kadhalika. Kwa masuala haya ya msingi wote letu ni moja, hakuna anayeshabikia ufisadi wala hayo mambo ya *EPA*, wote tunataka yachukuliwe hatua na ndio lengo letu. Kwa hiyo, nilitaka nalo nilitolee maelezo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamesema kuhusu kilimo kwamba ndiyo uti wa mgongo wa nchi hii, ni kweli. Ningependa kuendeleza pale ambapo Mheshimiwa Kumchaya alimalizia jana. Nazungumzia juu ya *Finance Act* ya mwaka 2006 ambayo ilitiwa saini na Mheshimiwa Rais tarehe 30 Septemba, 2006. *Finance Act* hii katika *part II, amendment of the Cashew nut Board of Tanzania Act, Cap. 203* inasema hivi na alinukuu, wala sitaki kuendeleza ile nukuu lakini katika ile kodi ya *Export Levy* ile ya *ten percent* ambayo itakusanywa na *TRA* kifungu cha 1(a) kinasema:-

“Asilimia sita nukta tano ya mapato yote ya asilimia kumi ya kodi hiyo ya *export levy* shall be divided among District Councils which are cashew nut producers ndiyo sheria inavyosema na *three point five percent shall be remitted to the Consolidated Fund*”.

Mheshimiwa Spika, tangu sheria hii imepita mwaka 2006 *District Councils* zinazolima korosho hazijapata hii *levy* na kila tulipofuatilia tulikuwa na majibu, mwaka 2007 tuliambiwa,

eti Serikali imetoa ruzuku ya madawa ya korosho na hela hizo, nani amewaambia? Kwa sheria ipi? Sheria inasema wazi kabisa fedha hizi ni mali ya *District Councils* zinazo-produce korosho. Mwaka huu pia tumeambiwa kwamba, eti Serikali ilisema haya ni mapato ya Serikali. Hapana, mapato ya Serikali hapa ni ile *three point five*, hiyo ndiyo inayokwenda kwenye *Consolidated Fund*, zingine ni za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006 tangu sheria hii ilipopitishwa, korosho zilizosafirishwa nje ni tani sabini na saba elfu, mwaka 2007. Sasa tunaomba hizi fedha, haiwezekani fedha msembe hiyo ndiyo ruzuku, hapana. Hizi ni fedha za Halmashauri na mpaka hivi tunavyosema kule tunaolima korosho madawa tuliyokwishayapokea leo ni yale tu ambayo fedha zake zinatokana na wakulima wenyewe. Kwa mfano, Mkoa wa Mtwara, tulikubali kukatwa Sh. 60/= kwa kila kilo ya korosho ndiyo madawa tumeyapata. Haya mngetupa mapema tangu mwaka 2006, nina hakika leo dawa zote zingekuwa zimefika. Kwa hiyo, naomba jambo hili sasa lieleweke kwamba hii siyo ruzuku wala haya si mapato ya Serikali, hii ni motisha iliyo ndani ya Sheria ya Serikali ambayo inataka kutoa motisha kwa Wilaya zote zinazolima korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuzungumzia juu ya utengenezaji wa mbolea hapa nchini. Tunayo gesi hapa nchini na gesi ni pembejeo kubwa sana ya uzalishaji wa mbolea lakini tukizungumzia kutengeneza mbolea hapa nchini tunaambiwa eti gesi ile ikitengenezwa mbolea bei itakuwa kubwa sana.

Sasa najiuliza kama tunanunua mbolea tunatoa ruzuku, kama kuna furaha ya kutoa ruzuku kwa mbolea inayotoka nje. Kwa nini tuone huzuni kutoa ruzuku kwa mbolea tutakayotengeneza humu ndani. Nadhani hili ni jambo la kawaida, ningeshauri Serikali iangalie uwezekano wa kutengeneza mbolea sasa.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza hotuba ya Bajeti ya Kenya wanasema wanataka kutengeneza mbolea kwa gesi ipi, sisi tuwauzie gesi wao wakatengeneze mbolea halafu tena irudi Tanzania, halafu tuitolee ruzuku jamani. Nafikiri haya mambo ni yale ya kuangalia kwa sasa. Haya tunayoyasema wengine wakisikia wanasema unaona wenyewe wanakosoa. Hiyo ni sera yetu lazima tuiambie Serikali yetu, Serikali yenye masikio mazuri sana, wanasikia hili jambo na nina hakika watalijibu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii tunayokwenda nayo, nilimsikia vizuri sana Waziri wa Fedha na Uchumi katika hotuba yake ya Hali ya Uchumi siku ile ya Bajeti. Katika mambo mazuri mengi aliyoyasema alisema, Serikali ipo kwenye mchakato wa kupata asilimia hamsini kwa hamsini hasa hamsini kwa wanawake katika vyombo vya maamuzi akaishia hapo.

Nilikuwa nasema hivi jambo hili lipo kwenye sera na kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Sasa tuambiwe *time frame* ni lini? Hili jambo limezungumzwa, Serikali isizungumzie tena mchakato, mchakato tayari upo kwenye sera. Sasa tunataka mtuambie katika kutekeleza jambo hili mpango ni huu na huu. Tunataka Uchaguzi wa mwaka 2010 jambo hili liwe limetimia kwa sababu ndiyo miaka mitano ya ile Ilani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesoma vitabu hivi vya Bajeti, sikuona jambo moja ambalo nafikiri ni jambo, sijui labda pengine sikusoma vizuri, naishukuru sana Serikali imetoa fedha zake tunajenga daraja la Umoja pale Mtambawaswala, *Unity Bridge*.

Lakini *Unity Bridge* sioni mpango wa barabara kutoka pale kwenye daraja kuunganisha na Mangaka itakapotokea upande wa Tanzania. Daraja lile nafikiri linakwisha mwaka huu, litafunguliwa tu. Sisi tuliotembelea lilibakiza kazi ndogo tu litakwisha. Sasa inakuwa ni sawasawa na mtu umenunua suti umevaa, umeweka koti, suruali na tai lakini chini huna viatu, unapekua, sasa tunafanya nini? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukishavuka na daraja lile zuri tunakwenda na barabara gani kufika mpaka Mangaka. Kwa hiyo, hili lingefaa wakati ule tuna-*plan* hili daraja, barabara ingekuwa tayari, sasa tunapenda kujua kuna mpango gani wa kuunganisha daraja lile na barabara ya lami? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili suala la daraja msije kufikiri sisi watu wa Kusini tunafurahia tu mambo yetu yakienda vizuri, tunasema suala la madaraja katika nchi hii pia liangaliwe. Nafurahi kwamba, Malagarasi tumesikia mipango yake lakini kuna daraja la Kilombero pia jamani na lenyewe liangaliwe kwa sababu haya ndiyo Maendeleo. Sisi watu wa Kusini kwa mara ya kwanza kwa kweli tunafurahi sana. Lakini wapo wenzetu mpaka leo bado wana matatizo ya usafiri na usafirishaji wa barabara katika mikoa yao. Tunaomba mpango ule uliofanyika upande wa Kusini na wenzetu sasa kutoka Tabora kwenda Kigoma, Sumbawanga kote wakati umefika sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la umeme tumepitisha hapa Sheria ya Umeme, imeshatiwa sahihi lakini jambo linalosikitisha ni kwamba sasa hivi hasa Masasi katika kile kinu kikuu cha kutengeneza umeme ambacho kinapeleka umeme Masasi, Newala, Tandahimba, Nachingwea, Ruangwa na kadhalika kwa kweli sasa hivi vinu vile ni vibovu, vimekufa na wala siamini kama *TANESCO* wana hamu tena baada ya sheria ile kupita, ya kutengeneza vinu vile. Matokeo yake sasa Wilaya hizi zote maji hakuna, hospitali hazifanyi kazi kwa kuwa umeme hakuna.

Kwa hiyo, tunaomba sana juu ya jambo hili lichukuliwe hatua haraka sana, hata kama kuna mipango ya kuunganisha huo umeme kutoka kwa *ARTUMAS* itachukua muda, watu kule wanateseka, sehemu kama Newala, Tandahimba yaani kule hakuna hata kisima cha kuchimba kwamba kitatoa maji kwenye mchanga, haiwezekani. Kwa hiyo, tunaomba jambo hili lichukuliwe hatua haraka kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nasema haraka haraka ili muda wangu niweze kusema yale niliyonayo. Naomba kueleza kwamba sasa hivi tungependa kufahamu hivi Askari Magereza na Polisi na Askari wote, tungependa kujua kiasi gani maslahi yao yataboreshwa katika Bajeti hii. Kwa kweli tumewekeza kwenye elimu, kilimo, kila kitu lakini tusipowekeza kwenye ulinzi na amani maendeleo yetu yote yatabomoka. Kwa sababu tunapowekeza katika kufufua uchumi ujue kwamba na wengine nao wanawekeza katika kufanya uhalifu na tunategemea majeshi yetu haya yote yatusaidie katika kuendeleza ulinzi na usalama katika nchi.

Kwa hiyo, tunaomba sana suala la maisha yao litazamwe nami naishukuru Serikali kwamba wameanza kujenga nyumba za askari, kwa kweli baadhi ya nyumba wanazoishi askari hawa ni mba ya sana lakini Serikali inachukua hatua, tumechelewa lakini hatua imeanza.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Magereza hata Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wana vikosi vya ujenzi lakini ninachoshangaa hata zile nyumba za Polisi zinajengwa na wakandarasi wakati Magereza wamejaa vibarua wa bure wamejaa, wanao mafundi. Magereza wana mafundi sana, mmeona jengo lao la Makao Makuu, wamejenga wenyewe na vikosi vyao na wasanifu wao na *Engineers* wao. Hivi hii sheria ya Manunuzi kweli ndiyo inayokataza hivi vikosi visifanye kazi ndani ya vikosi vyao?

Mheshimiwa Spika, kama sheria hii iko hivyo tuibadilishe, Magereza, Polisi na Jeshi la Kujenga Taifa wote hawa watumie vikosi vyao katika kujenga nyumba zao wenyewe. Naamini Magereza wana wafanyakazi wengi tu na hawa tunaowapa kandarasi nyingi za ujenzi tunaofikiria kwamba ni rahisi wanatuletea *Engineers* wao wengi kule ni wahalifu walifungwa, sasa wanaona badala ya kuwafunga magerezani kwao wanawaweka kwenye makampuni yao wanawaleta hapa. Sisi tunafikiri ni rahisi tunaacha kutumia vikosi vyetu tulivyonavyo. Naamini tutajenga nyumba nyingi na rahisi zaidi kwa kutumia vikosi vya ujenzi vilivyoko katika majeshi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana nimesikia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ametoa kauli kuhusu Zimbabwe. Kwanza nasema kauli ile imechelewa sana, mambo yanayotokea Zimbabwe kwa kweli hayafai kuyanyamazia.

Nashukuru kwamba angalau tumesema hivi lakini tusiendekeze kuachia mambo ya namna hii yanatokea katika Afrika na hasa katika mwaka huu ambapo Rais wetu ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika. Ninachoshauri ni kwamba, tuhakikishe kabisa tunamsaidia Mwenyekiti na tumwambie ndugu yetu Mugabe kwamba.....

*(Hapa kengele ya pili ya kuashiria muda wa
mzungumzaji kumaliazika ililia)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. ANNA M. KOMU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri bajeti huwa tunazianza toka majumbani mwetu kwa familia zetu. Baba na mama tunatafuta pamoja baadaye tunakaa na kuangalia ukubwa wa familia yetu, watoto ambao tunao na watakaokuja baadaye na huwa tunapochuma, unapofika mwisho wa mwezi, ambapo ndiyo siku ya familia kukaa kupanga kwa sababu hatukai mwaka hadi mwaka, wote wawili tunakubaliana na kama tuna watoto wakubwa tunawashirikisha tujue mwezi huu tumepata laki mbili tunazitumiaje. Kwa hiyo, tunazipangia fedha zile ili kuhakikisha kwamba watoto watakula watashiba, watapata elimu, wakiugua watapelekwa hospitali na watapata matibabu. Pia tukijua kwamba kuna fedha ya dharura, pindi akitokea mmojawapo kati ya sisi, watoto au wazee wetu akiondoka duniani au mambo mengine ya kimaisha tutakuwa na wezo wa kukabili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapokaa pamoja kuangalia uchumi wetu kwenye Serikali yetu kwenye ukumbi huu, tunaangalia kwa mwaka jana tumechuma nini, tumekusanya fedha kiasi gani na wale ambao tumewapa madaraka, wanatuletea, wanatwambia sisi

tumekasimu hivi na sisi hapa ukumbini kila mmoja atoe mchango wake, yeye anafikiria nini katika yale ambayo wenzetu wametuletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kila mmoja ana haki ya kuchangia maoni jinsi yeye anavyoona bajeti yetu ya Serikali ilivyoletwa kwetu. Ana haki ya kukosoa, ana haki ya kusikilizwa na mchango wake utiliwe maanani, usiishie kwenye makaratasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutokana na hilo, tupo hapa tumetumwa na wananchi wa Tanzania, tuje tuangalie ule uchumi wao mwaka jana ulikuwaje, tuangalie mwaka huu tunapanga nini kwenye fedha yao iliyopatikana, maana hii ni fedha yao, siyo yetu. Tuangalie tumepata nini, tunatumia nini, watapataje maslahi yao, wataishi namna gani, watoto wao watakwenda namna gani shule, watasoma namna gani, watapata namna gani matibabu, barabara zitajengwa namna gani, watafika wanakotaka na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hatukutumwa kuja kuvunja migongo ya Watanzania kwa kuendelea kuwarundikia mizigo kwa sababu tayari wana mizigo! Tupo hapa tuwasaidie Watanzania kuinua gunia moja moja migongoni mwao ili na wao kesho wasimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hatutafanya hivyo, tukizidi kila mwaka kuja hapa kuwatwisha mizigo, tunawawekea magunia ya kilo 100 na kilo 200, mwisho wake wataavunjika, watahindwa kusimama na kura hawatatupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nisome Katiba ambayo ndiyo inayotuongoza. Ibara ya 9(i) inasema:-

“kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada ya kuondosha umaskini, ujinga na maradhi;

Ibara ya 9(j) inasema:-

“kwamba shughuli za uchumi haziendeshwi kwa njia zinazoweza kusababisha ulimbikizaji wa mali au njia kuu za uchumi katika mamlaka ya watu wachache binafsi.”
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuna kitu kinaitwa MKUKUTA. MKUKUTA una mambo matatu muhimu. La kwanza, kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Pili, ubora wa maisha na ustawi wa jamii. Tatu, utawala bora na uwajibikaji. Yote haya yanaendana na haya ambayo tumeyaweka kwenye Katiba.

Mheshimiwa Spika, sasa kila mwaka tunakuja hapa tunaongeza bei ya chakula, tuongeza bei ya petroli, tunaongeza bei ya sigara na tunaongeza bei ya pombe. Kila mwaka tukija hapa, kinachoongezeka, ni bei ya pombe, sigara na soda. Mwaka huu, tunaambiwa, hakuna nyongeza ya bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati tunaondoka hapa, bei ya mafuta lita moja ilikuwa Sh.1,200/=, leo miezi nane, tisa, kumi iliyopita, bei ya mafuta lita moja ni Sh.2,000/=, nani kaongeza bei hiyo?

Mheshimiwa Spika, hii yote ni kutowajibika na kumwangalia Mtanzania! Tumeacha biashara ya mafuta katika nchi hii kuwa holela kila mmoja anajipangia bei yake.

Mheshimiwa Spika, leo nimeona kwenye taarifa ya habari asubuhi, wenzetu bei ya mafuta imeshuka *crude oil* ilikuwa Sh.144, leo kwa pipa ni *dollar* 139. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Sawa kabisa!

MHE. ANNA M. KOMU: Sasa kama wenzetu kule ambako mafuta yanakotoka, leo yameshuka kwa *dollar* 5, je, sisi tutapunguza bei ya mafuta huku? Sijawahi kuona Tanzania hii, bei ya mafuta ikapanda, ikashuka ikipanda inapanda tu mpaka sijui itafika wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hapo hapo, tukishaacha mafuta mikononi mwa Watanzania ambao wao wanamudu kuagiza hayo mafuta basi tumewapa mzigo Watanzania na mafuta yakipanda basi kila kitu katika nchi hii kinapanda bei.

Mheshimiwa Spika, leo tunanunua sementi na bati kwa bei kubwa. Mchele na maharagwe vinatoka Mbeya sasa kusafirisha mchele na maharagwe kutoka Mbeya na Morogoro kuuleta hapa, ni siku moja kwa usafiri, tunatumia nishati ndogo kuyafikisha mazao hayo hapa. Wenzetu wanapakia kwenye meli, wanasafiri kwa muda wa miezi sita baharini, wanatuletea mataa ya mapambano, wanatuletea friji, wanatuletea televisheni, lakini bei zinabaki pale pale, hawasemi kwamba mafuta yamepanda bei wapandishe bei ya televisheni, leo tunanunua televisheni kwa Sh.120,000/= lakini sisi hapo Mbeya tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapo ukiangalia mkulima anapata Sh.400/- au Sh.500/=, kwa kilo ya mchele mpaka Sh.600/= lakini mchele huo ukifika Dar es Salaam kilo ni Sh.1500/=, maharagwe yakifika Dar es Salaam ni Sh.1500/=, ukiuliza mafuta ya Korie, sasa hivi ndoo ndogo ni Sh.22,000/=. MKUKUTA tunaweka *SACCOS*, tunasema tuwasaidie akinamama wetu hawa wenye biashara ya mamalishe, wapika chakula ili wawauzie wenzetu wanaotoka mbali kuja mijini kufanya kazi lakini leo mamalishe hamudu kununua mchele, maharagwe, mafuta na unga wa ngano ili auze wali maharagwe kwa Sh.700/= kutokana na bei ya vyakula ilivyopanda. Leo utakuta sahani ya wali maharagwe ni Sh.700/=, kesho ni Sh.1,000/= wakati mtu ametoka kazini ametumia Sh.600 kwa ajili nauli, kipato cha Mtanzania ni Sh.1500/= kwa siku, wenyewe tumeandika hapa, leo anatumia Sh.1,000/= kula sahani ya chakula kwa mama lishe, anatumia Sh.600/= kwa ajili ya nauli, nyumbani hajaacha kitu, Sh.1500/= iko wapi?

Mheshimiwa Spika, tuliwaalika akinamama wetu wakati wa Mkutano wa Sullivan huko Arusha. Tukawataarifu akinamama na tukawapigia mbiu ya mgambo kwenye matangazo ya televisheni na nini, njooni, njooni na biashara zenu Arusha. Akinamama wale walitoka kila kona, walitoka Kagera, walitoka Mbeya mpaka Zanzibar na kwenda Arusha kufanya maonyesho ya biashara zao. Akinamama wale waliambiwa pikeniki chakula wageni wakija watataka kuonja chakula cha Watanzania na walifanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, leo akinamama wale wanalia, hakuna mtu aliyewajali pale Arusha. Nimemwona Mheshimiwa Waziri mwenyewe amekwenda pale, wanamwambia chonde chonde, akinamama wanalia. Ndugu zangu wa Zanzibar mpaka juzi bado wapo Arusha, walikodi lile banda kwa Sh.500,000/=, wana wasaidizi ambao inabidi wawalipe, Arusha wakati wa Mkutano

wa Sullivan, hoteli ni ghali, wao wenyewe wanataka kuishi, mradi imekuwa ni balaa kwa wale akinamama, tumewaongezea mzigo.

Mheshimiwa Spika, vitu vya ajabu ajabu tu vinatokea kwa huyu huyu Mtanzania ambaye anasema jamani nendeni huko mkaniteremshie mzigo, ndio huyo huyo kila siku tunaendelea kumwekea mzigo, anaendelea kulia.

Mheshimiwa Spika, sasa huu MKUKUTA na hizi SACCOS, kama hatuwapi nafasi hawa wanaochukua fedha za watu ili waweze kuzirudisha, akinamama lishe na akinamama wengine wanaojitahidi kuhangaika na maisha ya watoto wao sijui tunakaa hapa kuzungumzia nini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri, ndugu zangu wa TRA wana miaka minne sasa. Nina hakika miaka minne hii waliyonayo, wanakaa kule nyuma wakibuni na kupanga jinsi ya kuweza kukusanya uchumi wa nchi hii ili fedha hizo ziweze kusaidia kupanga hiyo bajeti. Leo nawaomba wakae tena kwa sababu bado kuna fedha ambazo zipo mikononi mwa watu hazijakusanywa. Wajitahidi kukaa tena kubuni mbinu mpya za kuweza kukusanya hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, bahari bado hatujaitumia vizuri. Kwenye bahari hakuna samaki tu kuna vitu chungu nzima, kuna mwani, majogoo, mawe malaini ambayo wenzetu wanayanunua, ma-shells, kuna vitu chungu nzima, bahari bado hatujaitumia ipasavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bado misitu hatujaitumia japokuwa tumekata yale magogo yote ya miaka 100 lakini Wazungu wakija hapa wanakwenda Mwenge kutafuta vinyago. Tuwapelekee masoko ya vinyago huko huko kwao, tukawabanie huko huko. Tuwaambie akinamama watengeneze vitenge vyao vya tie & die, tuwabanie huko huko Wazungu. Serikali itapata na hao akinamama watapata na vijana wetu wanaochonga vinyago watapata.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, hapo ndiyo kwenye balaa. Ukizungumzia madini, kodi ya nchi hii inatoka kwenye pombe na sigara, kodi ya nchi hii inalipwa na *guest* ndogo ndogo, mahoteli makubwa makubwa wana msamaha wa kodi wa miaka mitano, wanapasiana. Sidhani kama mtu atatoka huko anakuja kuendesha hoteli katika Jiji la Dar es Salaam akae mwaka mmoja apate hasara, mwaka wa pili apate hasara, mwaka wa tatu apate hasara, mwaka wa nne apate hasara, bado tu yupo, hata ingekuwa nchi ya mama yake, asingekubali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini anajua ikifika miaka mitano, mimi Maulidah nitampisha Komu, si jina tu limebadilika na sura ya Maulidah haipo, tunaendelea kuila nchi lakini wenye *guest* ndogo ndogo kwa sababu namjua ni Maulidah, nitamfuata tu, atalipa ushuru na kodi.

Mheshimiwa Spika, pombe itapanda bei na sigara zitapanda bei, siku Watanzania wakisema leo Mungu kashuka, tunaokoka, tumekufa. Ikitokea leo Watanzania wote tunaokoka, hatunywi pombe, hatuvuti sigara, hatwendi *guest* basi nchi hii imemalizika. (Makofi Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa nguvu kazi. Kuna mahesabu yanasema, tumeunda ajira laki nne na kitu sijui lakini tulikuwa tunasema tutaunda ajira milioni moja. Hapo hapo, ninawaambia ndugu hao, hiyo nguvu kazi inashuka, kwa sababu kama tuna ajira 400,000, kuna walioachishwa kazi humu kutokana na wenye viwanda kushindwa kuendesha viwanda. Umeme umepanda bei, maji nayo wanataka kupandisha bei, kila kitu kimepanda, *oil* imepanda,

wanashindwa kulipa mishahara wanawaachisha kazi, hao wapo wangapi na tunajua idadi yao? Kwa hiyo, hata hiyo nguvu kazi na hizo ajira tunazozizungumzia bado hatujakaa kuzibuni.

Mheshimiwa Spika, nilizungumza hapa siku nachangia kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, tuna ardhi ya kutosha, je, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, imetusaikia kupembua ardhi yetu na kujua wapi panastawi nini na wapi panastawi kitu gani? Hivi kuna nini? Mwaka huu tungekuja na bajeti ya kusema tumetenga milioni fulani, tunachukua vijana hao waliorundikana mijini na akinamama na akinababa watakaokubali tuwapeleke kwenye ile ardhi ambayo wenzetu wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika wamepembua, waende wakakae pale, tuwakopeshe mitaji, tuwaweke Mabwana Kilimo pale ili tutumie ardhi yetu, kuna matatizo gani? Wakati tungewakopesha wananchi wetu na kuwaweka huko kwenye mashamba, tukawakabidhi hiyo ardhi na Mabwana Kilimo, wanguweza kufanya kilimo cha maana na kufuga kwa maana na wangepata kazi na Serikali ingepata mapato na kilimo kingeinuka.

Mheshimiwa Spika, tunateremsha bei ya majembe, hivi kweli tunawatakia mema wananchi hao? Mbona hatusemi tunawapelekea matrekta kama Ilani yetu inavyozungumza? Hayo hatusemi lakini tunazungumzia majembe.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo linaniumiza ni mikataba, madini yanapotezwa na mikataba. Madini ya nchi hii kuna siku tukija kuamka, kuna mwenzangu mmoja alisema hapa tutakuja kufufuliwa makaburini tuangaliwe hivi vichwa vyetu vilikaa *triangle* au duara? Tuliachaje watu kutoka nje wakaja wakachukua madini, wakabakisha mapango tu pale? Tukikaa sisi huku tunazungumzia pombe tu na sigara, lakini madini hatuyazungumzii. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tutalia na mikataba mibovu kila siku kama tunavyolia na fedha zetu. Tutalia kila siku mpaka mikataba iletwe Bungeni, tunaumia na mikataba hii. Mikataba ni mibovu, *ten percent* zinatumaliza katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi, Mungu wangu, ndiyo ninataka kuizungumzia. Hivi unamsamehe mtu kodi kwa misingi ipi? Baba yako huyo? Anakuja hapa, anaondoka na nchi hii, wewe unasema unamsamehe mtu kodi? Baada ya kumsamehe alete magari chungu nzima bure anakuja kuanzisha mradi hapa, tunamsamehe kila kitu, turudi tena tumsamehe na kodi? Hakuna kusamehe kodi mtu hapa. Anayesamehewa kodi hapa ni yule anayeleta gari linalohusiana na dini na pia tumchunguze kama ni kweli ni la dini. Ni kweli hilo gari linakuja masuala ya dini au basi ni taratibu za uongo? Tukusanye hizo fedha shemeji yangu Mustafa Mkulo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hapa tunaumia, Watanzania wanaumia Waziri wa Fedha, Watanzania wanaumia na Watanzania wamechoka. Mwaka 2010, wote tutawakuta wana vifaduro, wanakula vitu vya ajabu, wanaisha maisha ya ajabu. Tusione sisi tunaishi kwa raha hapa, hawakutuleta hapa kuwaongezea mizigo na kurudi kuwaambia.

Nyie tumewachagueni mkae hapo ili muangalie, mtuletee hapa ili sisi tuchangie, tutoe maoni yetu na myakubali. Sasa mmekwishaniletea hiki kitabu na mmekwishakukiandika hivi, mnaniambia ndiyo hivi, halafu mnaniambia nichangie, utakwenda kuyaweka wapi na nyie tayari

mmekwishaleta vitabu hivi chungu nzima, mmepoteza fedha za Watanzania? Mmekwishaandika kile mlichojaliwa kuandika humu, mnakuja kuniambia Anna Komu changia halafu nikishachangia mtarudi mkavitengeneze tena hivi vitabu mniletee vikiwa na vile nilivyochangia, si ndiyo imekwishatoka hiyo, watoto wanasema ikirudi pacha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tukae, tushirikiane kupanga matumizi ya Watanzania. Tukisema mwaka huu tunalia basi yale tuliyoyasema mwaka huu, mwaka kesho tuyakute kwenye vitabu. Mwaka kesho naomba nikute wametenga fedha kwa ajili ya wakulima, vijana wapelekwe mashambani wakakabidhiwe ardhi.

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakushukuru lakini ungeweka nusu saa, robo saa haitoshi. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, uamuzi mnao nyie. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Kwa hakika watu wanaongea kwa hamasa kubwa. Sasa ni Mheshimiwa Devota Likokola na wa mwisho ajiandae Dr. Charles Mlingwa.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti yetu.

Kwanza kabisa, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, Waheshimiwa Watendaji na wale wote walioshiriki katika kuandaa bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza kwa sababu kwanza kabisa katika uwepo wangu katika Bunge hili, bajeti hii ndiyo ambayo imeshirikisha wadau wote. Utaratibu wa bajeti, bajeti zinaletwa kwenye Kamati, Kamati tunajadili, safari hii sisi tutakuwa mashahidi, mpaka NGOs zimechangia bajeti hii. Kwa hiyo, bajeti hii ni bajeti shirikishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono bajeti hii kwa sababu baada ya kutoka hapa waliounga mkono, wasiounga mkono, wote tunakwenda kuitekeleza bajeti hii. Ninaomba niunge mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe shukrani za pekee sana kwa Serikali yetu kwa kuwa wasikivu wakubwa. Mwaka jana, kipindi cha bajeti, niliomba Idara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Jinsia, wapate ruzuku katika Halmashauri zetu ili waweze kuhamasisha maendeleo. Serikali imesikia na imetekeleza ombi hilo, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru pia kwa Serikali kutupatia fedha katika Mkoa wa Ruvuma ili tuweze kuwa na ukanda wa uwekezaji wa viwanda kwa mauzo ya nje yaani EPZ. Tunashukuru sana kwa ukanda huo kwa sababu utatusaidia sana sisi wa Mkoa wa Ruvuma na kwa kweli utakuwa ni changamoto ya maendeleo. Naomba niarifu Serikali, fedha mlizotuma kwa ajili ya kuanza shughuli za kuangalia maeneo ya ukanda wa wawekezaji wa viwanda katika eneo la Uwiko, zimefika na shughuli zimeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitachangia bajeti katika maeneo makubwa matatu. Eneo la kwanza, ni eneo lile linalohusu mfumo wa bajeti kijinsia. Eneo la pili, litahusu huduma za fedha na vyombo vya fedha nchini Tanzania. Suala la tatu nitachangia bajeti kuhusiana na masuala ya Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, ninaanza na eneo la kwanza ambapo napenda kuzungumzia mfumo wa bajeti kijinsia. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mkulo, katika kitabu chake cha Hali ya Uchumi wa Tanzania, ukurasa wa 30, ameeleza wazi kwamba kuna masuala ya mtambuka, likiwemo suala la jinsia. Pia amesema kwamba Serikali sasa hivi inahangaika na inafanya kila inaloweza katika kuweka mfumo wa kijinsia katika kila Idara.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali itoe maelekezo kwamba asilimia 33 ya bajeti ya kila Wizara ishughulikie masuala ya jinsia ili tuweze kuwa na bajeti ambayo watu wengi wanaifurahia. Kwa sababu bado tuna makundi ya walemavu, tuna makundi ya wazee, tuna makundi ya wanawake na tuna makundi ya vijana. Hao wote wakiwa na asilimia maalum, itaweza kusaidia katika kuona ni namna gani Serikali yao inawajali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia pawepo na ukaguzi wa kijinsia yaani *audit* ambayo inafanyika kijinsia kwa maana ya kwamba tutajua bajeti hii imenufaisha makundi mangapi, ni wanawake wangapi wamenufaika, ni vijana wangapi wamenufaika, ni wazee wangapi wamenufaika, bila kuwa na *gender auditing*, hatuweze kujua ni makundi gani yamenufaika na bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala zima la mifumo ya fedha. Hivi sasa ni asilimia tisa tu ya Watanzania ambao wanapata huduma rasmi za kifedha. Asilimia mbili wanapata huduma ambazo ni rasmi kidogo (*semi formal*), asilimia 35 wanapata huduma ambazo siyo rasmi na asilimia 54 wapo katika kundi ambalo hawapati huduma za fedha. Ninaomba Serikali iangalie hali hiyo. Huu ni utafiti uliofanywa na wenzetu wa *Financial Sector Deepening Trust* na kama watu wawapati huduma za fedha maana yake ni nini? Watu watakuwa hawana mitaji na kwa vyovyote vile hapatakuwa na uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanapenda kuanzisha *Community Bank*, lakini mtaalam mwelekezi ni wa ghali sana. Tunaomba Serikali ilipe watalaam waelekezi ili wananchi katika Wilaya zote waweze kumiliki *Community Bank*.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa wazo zima la kuanzisha Benki ya Wanawake. Hii itawasaidia sana wanawake katika kuinua uchumi na ni kweli, huo ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema kwamba wanawake watawezesha kiuchumi, kama patakuwa na Benki ya Wanawake, maana yake wanawake watakuwa na uwezo wa kupata mitaji na watafanya shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuwa imezingatia vipaumbele vya bajeti katika suala zima la elimu. Lakini ninaomba pia tujizatiti sana katika suala zima la uzalishaji mali kwa sababu huduma za jamii bila kuwa na uchumi endelevu bado na zenyewe zitayumba. Kwa hiyo, ninaomba wakati jitihada za kuboresha huduma za jamii kama vile ilivyofanywa kwenye sekta ya elimu na afya lakini pia tuongeze jitihada kwenye uzalishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala zima la kitengo cha *microfinance* katika *BoT*. Ninaomba kitengo kile kiimarishwe kwa sababu kitatusaidia katika kuendeleza mitandao ya huduma za fedha nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie Mkoa wa Ruvuma. Mkoa wa Ruvuma ni katika Mikoa sita ambayo Mheshimiwa Rais, alitangaza kwamba iko nyuma kimaendeleo. Mkoa wa Ruvuma, una kiwanja kizuri sana cha Ndege na hakuna ndege yoyote inayokwenda Ruvuma na kusababisha wawekezaji na watalii kutokwenda Ruvuma. Mkoa wa Ruvuma umejiandaa vizuri sana lakini kukosekana kwa usafiri wa ndege kunaathiri mambo mengi katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi niwahi kwenda katika ofisi za *TIC*, nimewahi kupata wawekezaji zaidi ya watatu, lakini waliponiuliza tunataka kwenda Ruvuma tuchukue *airline* gani? Nikawaambia, jamani Songea hakuna ndege, wakakata tamaa wakarudi. Kwa hiyo, ninaomba kwa kweli tuwe na ndege, sababu ambayo Serikali inaitoa kwamba hakuna mtu wa kuwekeza katika mafuta ya ndege, ninaomba kikwazo hicho kiondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala zima la elimu katika Wilaya yetu ya Tunduru. Katika bajeti hii, ninaomba sana Serikali iongeze bajeti ya elimu katika Wilaya ya Tunduru. Watu wengi wamekwenda Tunduru wameona kiwango cha elimu bado ni cha chini sana. Kwa hiyo, ninaomba kwa kweli tusaideiwe katika Wilaya ile ya Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie Manispaa ya Songea. Manispaa ya Songea, ni tofauti kabisa na Manispaa nyingine hapa nchini. *Stand* ya Manispaa ya Songea, haiko sawa na Manispaa nyingine hapa nchini. Tunafahamu ya kwamba palikuwa na mradi wa *sustainable cities* lakini katika Mkoa wetu wa Ruvuma na Manispaa ya Songea haupo. *Stand* ya Songea ukienda kuiangalia, ni tofauti kabisa na ile ya Morogoro ambako Mheshimiwa Mkulo anatoka. Kwa kweli nitaomba wenzetu na hasa ofisi ya Waziri Mkuu, atakapotoa bajeti yake, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, tuongozane ili akaone ni namna gani Manispaa ya Songea iko na ina tofauti na Manispaa zingine nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Songea hakuna taa za barabarani...

SPIKA: Mheshimiwa Devota Likokola, umesema unamtaka Naibu Waziri siyo Waziri mwenyewe?

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, ninamuomba Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mtandao wa lami katika Manispaa ya Songea kwa kweli ni mdogo sana na kwa kweli unasikitisha. Tunaomba tuongezewa fedha ili tuweze kutengeneza barabara za lami.

Vile vile mtandao wa umeme katika Manispaa ya Songea ni mdogo mno. Kata za Mletele, Kata za Subira, Kata za Matogoro, Kata za Luwiko, Ndilimalitembo, Mwenge Mshindo, kote huko hakuna umeme. Tunaomba umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Songea haina kiwanda, tuna kiwanda kikubwa cha Tumbaku kiko pale lakini hakifanyi kazi. Ajira kwa akina mama hakuna. Ni matatizo makubwa. Ninaomba sana kiwanda kile, Bodi ya Tumbaku inahangaika, Mkoa unahangaika, tatizo ni mwekezaji ambaye Serikali haiwezi kutoa ufumbuji wake, ni mwekezaji gani? Tunaomba kiwanda kile kifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la wakulima katika Wilaya ya Songea. Kwa muda wa miaka miwili sasa na nusu wanahangaika. Mara wanaambiwa walime kilimo cha umwagiliaji bondeni, mara wasilime, wamekaa wanahangaika hawaelewi. Kwa kweli tunapita katika Mikoa mingi, tunaona jinsi ambavyo watu wanalima kilimo cha umwagiliaji na kinavyowapatia fedha. Katika Wilaya yetu ya Songea, watu wanashindwa sasa kulima nyanya, wanashindwa kulima vitunguu, wanashindwa kulima vitu vyote hivyo, watavitoa wapi na huo ndio ukuzaji wa uchumi. Ninaomba Serikali itoe jibu kamili ili wananchi wa Wilaya ya Songea wasihangaika na kulima mabondeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la Ukimwi, ninaomba nizungumzie. Katika Mikoa saba iliyoko katika masuala ya Ukimwi, Mkoa wa Ruvuma upo. Juzi tu yamekuja magari 11, imepewa Mikoa mingine lakini Mkoa wa Ruvuma haukupewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie suala la mbolea. Mbolea waliopolekewa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, ilikuwa haifanyi kazi. Kwa hiyo, mwaka huu kwa vile mnafahamu Mkoa wetu ni katika ile Mikoa minne ya uzalishaji, msione ajabu suala zima la chakula kupungua kwa sababu ile mbolea kwa kweli imetesa wakulima. Ninaomba sana wenzetu wa Viwango husika wadhibiti viwango.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwazungumzie Madiwani. Ninaomba hiyo sheria inayoleta kigugumizi kwa kuwapatia Madiwani wetu manufaa na mapato na maslahi, iletwe haraka Bungeni, tuikebishe haraka ili Madiwani katika nchi hii wapate heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Devota Likokola na ombi lako, naona Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanri hayupo.

WABUNGE FULANI: Yupo.

SPIKA: Yupo, ahaa, basi looh, kumbe imefika moja kwa moja. Basi Mheshimiwa Mwanri, ujiandae kwa ziara maalum ya Ruvuma. Sasa Msemaji wa mwisho kwa asubuhi ni Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ambayo naitumia kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga Mjini. Kwangu mimi, naichukulia hii kama ni changamoto kwa sababu leo asubuhi ni kitinda mimba katika kuchangia bajeti yetu hii muhimu sana ambayo hatuna wasiwasi baadaye leo jioni tutaipitisha.

Mheshimiwa Spika, changamoto niliyonayo, ni kuhakikisha kuwa sirudii sana kuzungumzia yale ambayo wazungumzaji wengine waliotangulia wameyazungumza, yote ni mazuri sana. Mimi nina mambo makuu mawili, kwanza pongezi la pili ni ushauri kuhusu

kupanua wigo wa kuongeza mapato na hususan katika kuweka mipango na bajeti zijazo kwa sababu tunapopitisha bajeti hii inakuwa ni mwisho wa safari ya kwanza lakini ni mwanzo wa safari ya pili. Ndiyo hasa sehemu ya pili ile ya ushauri ambayo nitajielekeza na hasa tukizingatia yale ambayo nitakuwa nayazungumza, yako kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo hatimaye mwishoni mwa mwaka 2010, CCM ingependa kuona yametekelezwa ili kusudi ijijengee uhalali wa kuweza kuendelea kuongoza Taifa hili. Najua CCM itaendelea kuwa Chama Tawala kwa muda wa miaka mingi ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali, nikianzia na Mawaziri, Mheshimiwa Waziri mwenyewe na Naibu Mawaziri na watumishi wote wa Wizara na Taasisi za Fedha za Serikali zilizopo kwenye Wizara hii, kwa kazi kubwa waliyofanya kutayarisha bajeti hii ambayo inakubalika, ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni ya kujitegemea, imejieleza. Bajeti hii ni ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Bajeti hii vile vile katika mazungumzo yangu, imebeba agenda ya Jimbo langu la Shinyanga Mjini. Kwa hivyo, kwa nyakati mbalimbali, nitakuwa nafanya rejeo kwa Jimbo la Shinyanga Mjini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametamka bayana hapa kuwa mradi mkubwa wa maji wa Shinyanga na Kahama umekamilika, tunaishukuru sana Serikali katika hilo na nafahamu kuwa tayari majaribio ya kusukuma maji kuja katika miji ya Shinyanga na Kahama imekwishaanza angalau kutoa maji kutoka kwenye Ziwa kupeleka kwenye vituo vikubwa vya maji na inatarajiwa hatimaye mwezi Agosti sisi wananchi wa Shinyanga na Kahama, tutaanza kupata maji mengi safi ya kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kuipongeza Serikali kwa kuona haja ya kupunguza utegemezi wa bajeti yetu hii ya Serikali kwa fedha za kutoka nje. Sasa tuko kwenye kiwango cha asilimia 34, naipongeza sana Serikali katika hili. Nafahamu Mheshimiwa Waziri amezungumzia azma ya Serikali ifikapo mwaka 2010, utegemezi wetu huu uwe umefikia asilimia 20. Ushauri wangu katika eneo hili, ni kwamba inawezekana kabisa kwa kazi nzuri sana waliyoanza kuifanya, mwaka 2010 na 2011, utegemezi huu ukawa umebakia asilimia 15 tu. Kwa sababu bajeti nyingine ijayo ya 2009/2010 wakipunguza utegemezi kwa asilimia nane, tutakuwa tumebakiza asilimia 26. Bajeti ya 2010/2011 ambayo kwa majaliwa ya Mwenyezi Mungu, sisi wenyewe humu tutaipitisha, utegemezi ukipunguzwa kwa asilimia tisa, tutakuwa tumebakiza utegemezi wa asilimia 15 peke yake. Ndiyo maana naishauri Serikali ione haja ya kupunguza utegemezi kwa kiwango kikubwa sana na inawezekana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza Serikali katika haya ambayo naweza nikayasema na mengine nilishaandika kwa maandishi, ni kuona haja ya kuendeleza vile vipaumbele vilivyokuwa kwenye bajeti iliyopita, tunayoimaliza sasa, kwamba elimu na miundombinu vinakuwa ni kati ya vipaumbele vikubwa. Elimu ndiyo inayomwezesha binadamu ambaye ndiye *agent* wa kubadilisha dunia ikawa bora, aweze kuwa na huo uwezo. Kwa hiyo, hatua ya kwanza katika suala la maendeleo, lazima liwe ni elimu na tunafahamu tulikuwa nyuma kwenye suala la elimu kiasi kwamba mpaka mwaka 2005, Tanzania kwa miaka 44 iliyopita ilikuwa imeweza kujenga shule za sekondari 1,200 tu lakini miaka miwili iliyopita tumeweza kuongeza shule za sekondari 1,600 na kwa sasa tuna shule 2,806 za Serikali. Hii ni katika kumwaandaa Mtanzania ili aweze kumudu namna ya kuiendesha dunia ili kusudi maisha yake yaweze kuwa bora.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukishamaliza elimu kwangu mimi miundombinu inakuja namba mbili na ndivyo ilivyoweka Serikali. Kwa sababu miundombinu ndiyo inayokujengea mazingira ya kuendesha shughuli zako za kimaendeleo na za kiuchumi bila matatizo yoyote. Kwa mfano ukilima kama hakuna barabara, wewe utaishia kuwa maskini wakati una mazao yako mengi tu ambayo umeyalima lakini hakuna lolote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuona haja ya kuendeleza vile vipaumbele. Naamini kwa miaka michache ijayo angalau vipaumbele hivi vitabaki kuwa ni muhimu kuviendeleza kwa sababu bado tunahitaji kuongeza shule za msingi, tunahitaji kuongeza shule za sekondari, kuziboresha shule nyingi za sekondari, vyuo vyetu vya aina mbalimbali na vyuo vyetu vikuu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni ushauri kuhusu mipango na bajeti zijazo. Maeneo nitakayoyaongelea, ni suala la barabara, viwanja vya ndege, viwanda, mifugo, wanyamapori na utalii.

Mheshimiwa Spika, hebu tujiulize wakati tunaipitisha bajeti hii, tunajiandaa sasa kwa ajili ya bajeti nyingine ya mwaka 2009/2010 kwamba tumekaribia miaka 50 ya uhuru mwaka 2011, je, tuendele kuwa na Makao Makuu ya Mkoa ambayo hayaunganishwi na barabara za lami? Kwa hiyo, naona suala la barabara za lami, ni suala muhimu ambalo linapaswa liendele kuzingatiwa katika bajeti.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nafahamu katika miji yetu, barabara za lami ni muhimu. Kwa mfano ukienda kwenye Mkoa wa Shinyanga, Mjini ndiko Makao Makuu ya Mkoa, Shinyanga Mjini ni kati ya miji michache ya Tanzania ambayo bado ina barabara za vumbi lakini mimi nachukulia miji yote kama ni vituo vya kiuchumi, lakini haviwezi kuwa vituo vya kiuchumi kikamilifu kama haviwezi kuwa na miundombinu bora hususani barabara za lami.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba suala la ujenzi wa barabara za lami kwa mji wa Shinyanga, lizingatiwe kwenye bajeti zijazo. Nimeangalia kwenye bajeti hii, sijaona sana linajitokeza.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Wizara ya Miundombinu na bahati nzuri nimeshamweleza Waziri, kuna barabara inayotoka Shinyanga Mjini kwenda Old Shinyanga mpaka Bubiki, hii iko chini ya Wizara, naomba ishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia viwanja vya ndege hasa nikitolea mfano uwanja wa ndege wa Shinyanga ambao na Ilani ya Chama cha Mapinduzi imezungumzia. Uwanja wa Ndege wa Shinyanga ukiuchukua pamoja na Uwanja wa Ndege wa Mwanza, naviona ni viwanja vya ndege ambavyo kwa Kiingereza ungeweza kusema ni *satellite airports*. Kwa sababu eneo la Serengeti ambalo linajumuisha pori la Akiba la Maswa na Ngorongoro jirani, bado linaingilika kutokea Arusha ambapo Mbuga ya Serengeti haiko Mkoa wa Arusha iko Mkoa wa Shinyanga na Mara lakini leo hii tunaingia Serengeti kupitia Arusha na watalii wanatoka Arusha. Ukifungua viwanja vya ndege vya Mwanza na Shinyanga unakuwa umeufungua Ukanda wa Magharibi wa kuweza kulitumia eneo la Magharibi la Serengeti kwa ajili ya utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, barabara ya Mwigumbi, Maswa, Lalago mpaka Lamadi, tuhakikishe kuwa inajengwa inapofika mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, uwanja wa ndege wa Shinyanga, najua uko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tusichelee kuhakikisha kuwa unajengwa ifikapo mwaka 2010, sijauona kwenye fedha za maendeleo ya safari hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la viwanda, hata kama tutazungumzia suala la mapinduzi ya kilimo, hayawezi yakasahau suala muhimu la ujenzi wa viwanda. Kwa hiyo, ni vizuri tuhakikishe kuwa viwanda hasa vya kusindika mazao vinajengwa kwa sababu hivi ndivyo vitakavyowawezesha wananchi wetu ambao sehemu kubwa wanategemea kilimo kuweza kupata soko. Kuna mazao mengi sana ambayo yanaharibika kwa sababu hatuna viwanda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mifugo pamoja na wanyamapori, huwa nasema ni dhahabu iliyo juu ya ardhi lakini bado hatujaamua kuitumia ipasavyo. Wewe fikiria ng'ombe karibu milioni 19, mbuzi milioni 14, kondoo milioni nne, kuku wa kienyeji milioni 40, kuku wa kizungu milioni 30, huu ni utajiri mkubwa lakini ni lazima tutengeneze utaratibu ambao una mfugaji, una mnenepeshaji au mnunuzi kwa mfano *NARCO*, una kiwanda halafu una soko. Hii najua tulishaianza kule Wizara ya Maendeleo ya Mifugo wakati ule, naomba Serikali iendelee suala hilo ili kusudi tuwe na uhakika wa soko kwa mifugo yetu hii. Lakini suala moja ambalo inabidi tuliangalie ni kwamba tunapozungumzia ruzuku ya kilimo hatuzungumzii ruzuku kubwa ya mifugo. Kwa hiyo, kama tukiendelea hivyo hatuwezi kutegemea kuleta mabadiliko makubwa katika sekta ya mifugo ili iweze kuwa ni dhahabu inayofumuka kutoka juu ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, mimi vile vile, ni mtaalamu wa wanyamapori licha ya mifugo. Nchi hii utalii unaozungumziwa ambao sasa unaliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni, kwa sehemu kubwa unategemea wanyamapori. Mimi bado naona kuna nafasi ya kutumia wanyamapori vizuri zaidi ili kusudi tuweze kufaidika zaidi na tukavuna dhahabu iliyo juu ya ardhi kupitia utalii wa kiwindaji na ule wa picha.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi tunaweza tukayazungumza lakini ni vizuri Serikali ikaona na ikachukua hatua za makusudi za kuhakikisha kuwa wanyamapori tulionao, wakijumuishwa ndege, ambapo mimi ni mtaalam, hawa wanatumika vizuri zaidi kuinua utalii na kwamba kuna watalii wanakuja kwa ajili ya utalii wa ndege peke yake na Tanzania ni ya kwanza Afrika kwa kuwa na aina nyingi za ndege na mtashangaa majina ya Kiswahili ya ndege wote wa Tanzania, yameandikwa na Msukuma mimi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nakushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga Mjini kwa kunipa fursa hii ya kuwa kitindamimba. Natumaini ujumbe huu nimeufikisha sahihi na narudia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kabla hujatoa ule mwongozo wako kwa maswali tuliyokuuliza, nilikuwa nahitaji utoe mwongozo wako kwa sababu hii *Addendum* ambayo umetupa au tumegawiwa, bado ina tofauti kubwa kati ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwa mfano, Mheshimiwa Waziri, baada ya *Addendum*, anasema mapato ya ndani yameongezeka kwa bilioni mbili ambapo alikuwa

amesema ni trilioni 4.728 lakini *Addendum* ambayo ametupa sasa hivi, inasema trilioni 4.788. kwa hiyo, kuna tofauti ya zaidi ya bilioni 60.

Mheshimiwa Spika, sio hivyo tu, ukiangalia kwenye *vote 50*, *Addendum* ambayo pia ametupa au labda niendeleo kwa hili tu, ukiangalia kwenye mapato ambayo yametokana na Benki Kuu, kwa *Addendum* hii ameyapunguza kutoka bilioni 11 mpaka bilioni sita. Pia matumizi ya *National Bank of Commerce (NMB)*, ameyapunguza kutoka bilioni nne mpaka bilioni mbili lakini cha ajabu amekuwa na *total* ile ile baada ya kupunguza yote ile. Sasa hii sijui ni *calculator* za namna gani ambazo unaweza ukapunguza na bado ukaendelea kuwa na *total* hiyo hiyo?

Mheshimiwa Spika, sio hii tu kwenye *Addendum* ya fedha zinazotoka nje, pia Mheshimiwa Waziri ameongeza bilioni 66 ambazo zinatokana na *IMF/MDRI* lakini *total* aliyo *endup* nayo ni ndogo kuliko ile ambayo iko kwenye kitabu, sasa hii inanipa taabu.

Mheshimiwa Spika, halafu tulitegemea katika mizania kwamba zile bilioni za wafadhili angeziweka kama fedha zote za nje lakini ameendelea kuweka trilioni 1.551 na zile za ndani ameongeza tu kwa trilioni mbili ambayo inatokana na *NMB*, badala ya kuwa 58 ni 60.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nashauri na naomba Mwongozo wako, naona wengi tunataka kupitisha bajeti hii lakini maana ya bajeti ni takwimu, isingekuwa vizuri kwa muda tulionao, angalau kitabu hiki kiende katika Kamati ya Fedha na Uchumi ili waangalie *figures* zote ili tutakapokuja jioni, tupitische kweli takwimu ambazo zitaweza kufanya kazi na baadaye zinaweza pia zikakaguliwa kwa sababu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, atafuata vitabu hivi wakati anaikagua Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka mwongozo wako kwa jambo hilo.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Cheyo. Umeongezea tu kwa hoja yako ya jana kwa sababu jana pia, hii ni *Hansard*, ulisema na nanukuu:-

“Nilipokuwa nachangia, nilimweleza Mheshimiwa Waziri kwamba hata kwenye mizania yake, takwimu zake haziendi sawa sawa kwamba huwezi kusema umepokea trilioni 2.489 kutoka kwa wafadhili halafu kwenye mizania, ukurasa wa 48 ukaweka trilioni 1.551 ...” Leo umeongezea iliyopo kwenye *Addendum*.

Sasa uamuzi wangu kuhusu suala hili ni kwamba ni vyema kwa faida ya Bunge zima, kwa kuwa kitabu namba moja na hata *Addendum*, havikupitiwa na Kamati ya Fedha na Uchumi, basi kuwe na kikao kifupi cha dharura ili kiweze kuturekebisha. Maana huo ndio utaratibu, mambo hayafiki hapa bila kuwa yamepita kwenye Kamati, yale ya matumizi yalipita. Kwa hiyo, ni vizuri kuwe na kikao kifupi sana cha kuelewana kuhusu masuala hayo. Mimi nina hakika na Mheshimiwa Waziri amenihakikishia kwamba yapo maelezo. Kwa hiyo, ni kikao kifupi sana.

Kwa hiyo kuhusu hilo la utata wa takwimu, hatuwezi kuliongea hapa kwenye *plenary* wote nadhani likamalizike hapo kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa hiyo, naelekeza kwamba watumie baadhi ya muda huu tulionao asubuhi kuwa na kikao cha dharura ili wapitie mahesabu hayo.

Hoja nyingine ambayo niliomba mwongozo ni ya Waheshimiwa Wabunge wawili. Kwanza Kiongozi wa Shughuli za Kambi ya Upinzani Bungeni na pia Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa *POC* na zote zilihusu utaratibu wa kupitisha mapato ukilinganisha na matumizi kwa mujibu wa Kanuni ya 96 ambayo ina utata na utata huu unatokana na kwanza namna ilivyoandikwa halafu na historia ya Mabunge yote yaliyopita.

Utata wa kwanza, ukiangalia kwenye zile *marginal notes* pembeni, inasema ‘Kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali’ lakini Kanuni ya 96(1) inasomeka hivi nanukuu:-

“Waziri atapeleka kwa Katibu Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Serikali ya Mwaka wa Fedha...”.

Waheshimiwa Wabunge, hapo haisemi mapato. Kwa hiyo kwenye *marginal notes* inasema mapato lakini Kanuni yenyewe haisemi juu ya mapato mapato yanakuja kuonekana kwenye fasili ya 4, ninanukuu:-

“...Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaohusika”.

Sasa uamuzi wangu ni hivi, tukizingatia historia ambayo tumekuwa nayo ambapo Kitabu hiki cha Kwanza kilikuwa hakipitishwi kwenye Kamati ya Bunge Zima, ndiyo historia yenyewe ilivyo, hata wakati wa *Finance Bill*, hatupitii kifungu kwa kifungu na mimi nadhani mantiki yake ni wazi, utawezaje kuweka ukomo wa mapato? Kwa nini uweke ukomo wa mapato? Bunge linaweka ukomo wa matumizi na kupitisha zile hatua za mapato zinazopendekezwa na Serikali kwa mwaka ule yaani *revenue measures*.

Kwa hiyo, tafsiri ya Mabunge yote yaliyopita, hili ni Bunge letu la tisa, ni kwamba mapato yanayozungumziwa kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi kwenye bajeti, ni mapato yale yanayopendekezwa ndani ya hotuba yake ya bajeti ili tuyaidhinishhe, kama yale aliyoyasema Mheshimiwa Maulidah, yale ya bia, soda na kadhalika yote yale. Sasa hivyo ndivyo ilitafsiriwa kwa tafsiri finyu kwamba ndio mapato na ndio tunapitisha tunapopitisha hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Kwa hiyo, uamuzi wangu ni kwamba utaratibu huo uendelee kwa sababu ndio tulionao na naiagiza Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa siku za usoni, ikae, iangalie upya Kanuni ya 96 na Kanuni zake ndogo, zile fasili, ili ipendekeze utaratibu ambao utaondoa utata lakini kwa mwaka huu wa fedha, Waheshimiwa Wabunge, nimeamua kwamba ni vyema tuendelee na utaratibu uliofanyika katika Mabunge yote kwamba tutahojiwa kuhusu hotuba ya Waziri ambayo ndani itakuwa na mapendekezo ya mapato na pia itakuwa na mapendekezo ya matumizi, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kesho saa 3.00 asubuhi, kutakuwa na semina inayohusu masuala ya usalama. Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa, ataongoza mada hiyo pamoja na wataalamu wake. Tulipokwenda sisi Kamati ya Uongozi kule Zanzibar, tulikubaliana kwamba, ni vizuri sote tuelimishwe kuhusu masuala hayo pamoja na ya itifaki. Kwa bahati mbaya, wenzetu wa Mambo ya Nje, Idara ya Itifaki, hawakuwa tayari kwa wakati huu.

Kwa hiyo, semina itakuwa kesho saa 3.00 asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa. Tafadhalini naomba sote tuweze kuhudhuria ili tuweze kusikiliza mada hii muhimu na kuweza kuitolea maoni. Mambo yote yale ya usumbufu wa kuingia mlangoni na kadhalika, yatazungumzwa hapo. Utaratibu wa magari na mengine mengi kwa mfano safari zetu za kwenda Dar es Salaam, Majimboni na kadhalika. Kwa hiyo, nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge, tuwepo saa 3.00 asubuhi, kesho Jumamosi, tarehe 21 Juni, 2008, ukumbi wa Pius Msekwa.

Tangazo lingine ni kwamba wale Waheshimiwa Wabunge wote ambao walisahau vitabu vyao vya Makadirio Dar es Salaam, mathalani, Kitabu cha II, III au IV, tunazo nakala za kutosha katika chumba cha nyaraka pale jengo la Utawala. Kwa hiyo, wale ambao watahitaji kuja navyo, basi wavipitie kwa sababu Kitabu cha I, kimegawiwa hapa hapa. Kwa hiyo, ni Kitabu cha II, III na IV. Kitabu cha II, ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida, Kitabu cha III, ni Mapato kutoka Mikoa na Kitabu cha IV, ni Matumizi ya Maendeleo. Vipo katika chumba cha nyaraka, unaweza kumwona yeyote kati ya hawa Makarani Mezani, wataweza kukusaidia kuvipata ili wakati wa kupiga kura jioni, tuweze kuelewa vizuri.

Kwa maana hiyo pia kwa sababu nimeelekeza Kamati ya Fedha na Uchumi ikutane, nadhani pia itakuwa ni haki kutoa muda mfupi sana kwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dr. Kigoda na pia Kambi ya Upinzani, kwa dakika chache sana kuweza kutueleza sisi yale ambayo watakuwa wamekubaliana kule na Wizara. Chumba namba 231, jengo la Utawala, kiko wazi hata sasa na tumeandikiwa hapa na Katibu kiko wazi, kwa hiyo mkutane kwa muda mfupi tu ili kurekebisha masuala haya ili tusiwe na matatizo wakati wa kupiga kura.

Nikumbushe la mwisho, jioni hii kura ni zile za *rollcall*, kila mmoja wetu atatajwa jina na atasema kama anakubali ama hakubali, anaafiki ama vipi. Kwa hiyo, sio kura zile za sauti, jioni ni kura za *rollcall*. Nawasihi sana, wote tuwepo, ni tukio muhimu la kupitisha bajeti yetu. Kwa hiyo, nasihi sana muwepo.

Baada ya matangazo hayo na kwa kuwa nilikwishatoa maelezo kwamba kuna shughuli za kufanywa ili saa 11.00 jioni tuwe sawa sawa, basi nasitisha shughuli za Bunge kabla ya muda wake hadi hapo saa 11.00 jioni.

(Saa 05.28 asubuhi Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2007 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tunaendelea asubuhi na hadi nilipositisha shughuli za Bunge. nilitumia mamlaka yangu chini ya Kanuni ya Pili, kuweza kuweka utaratibu kwa lile jambo ambalo lilikuwa halijapitiwa kwenye Kamati ili liweze kupitia kwenye Kamati.

Sasa naambiwa Kikao hicho kilifanyika na kwa hiyo kwa utaratibu huo huo bila kuchukua muda mrefu sana, nitamwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ili atoe taarifa ya kazi waliyoifanya na baada ya hapo atafuatiwa na Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani.

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, kufuatia hoja za Waheshimiwa Wabunge, kuhusu tofauti zilizojitokeza katika tarakimu za baadhi ya vifungu vya mahesabu ya mapato katika Kitabu cha Mapato na katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi kwenye majadiliano ya bajeti yanayoendelea hivi sasa, uliagiza Kamati ya Fedha na Uchumi kukutana ili kupata usahihi wa hoja hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kukufahamisha kuwa Kamati ya Fedha na Uchumi imetekeleza kazi hiyo ikishirikiana na Waziri wa Fedha na Uchumi, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma pamoja na watendaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Kamati yangu imegundua kuwa, takwimu zote ni sahihi na hazina makosa yoyote, isipokuwa hazikutolewa ufafanuzi wa kina katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi wakati akiwasilisha hoja yake. (*Makofi*)

Katika kikao ambacho Kamati imekifanya mchana huu, maelezo ya kina yametolewa kuhusu takwimu hizo kama yatakavyoelezwa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge jioni hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa lililojitokeza, ni kutokulingana kwa takwimu zilizotolewa kwenye aya ya 58 na 59 ya Hotuba ya Bajeti, ikilinganishwa na jedwali la sura ya Bajeti 2008/2009, linaloonyesha mapato na matumizi. Katika aya ya 59 ya hotuba ya Waziri, inaonyesha kuwa matumizi ya maendeleo yatakuwa shilingi trilioni 2.489 ambapo kiasi cha shilingi trilioni 1.551 kitatokana na fedha za wahisani na shilingi bilioni 938.380, kitatokana na mchango wa wahisani kupitia msaada wa kibajeti, mapato yatokanayo na mauzo ya hisa za Serikali pamoja na ziada inayotokana na mapato ya ndani.

Hata hivyo, katika jedwali la sura ya bajeti 2008/2009, inaonyesha kuwa fedha za ndani ni shilingi 938,380 milioni, inawezekana ikaonekana hapa kuna tofauti ya mahesabu hasa tukiangalia jumla kuu ya fedha hizi kama zilivyoonyeshwa aya ya 59 na katika sura ya bajeti.

Kamati imepata maelezo kuwa ingawaje shilingi 938,380 milioni zimeonyeshwa kama fedha za ndani, ni kutokana na utaratibu wa kugeuza fedha za wahisani kuwa fedha za ndani (kwa utaratibu wa *General Budget Support*)

Kwa hiyo basi, kati ya shilingi 938,380 milioni, shilingi 812 bilioni zimetokana na *GBS*, lakini zimegeuzwa kuwa fedha za ndani, shilingi 66 bilioni zimetokana na kusamehewa madeni na Shirika la Fedha Duniani (*IMF*) na shilingi 60 bilioni zimetokana na mapato ya hisa za Serikali za *NMB* na shilingi 2.0 bilioni ni ziada toka katika makusanyo. Hivyo basi, ufafanuzi huu uliotolewa na Wizara ya Fedha na Uchumi, unaonyesha wazi kuwa matumizi ya maendeleo ya shilingi bilioni 2, 489, 480 ni sahihi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya nyingine ilikuwa takwimu zilizopo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hazishabihiani na zile zilizopo katika Kitabu cha Mapato (*Financial Statement and Revenue Estimates*). Kwa mfano, ukurasa wa (ix) wa Kitabu cha Mapato, unaonyesha jumla ya fedha ya mapato ya ndani ni shilingi 4,786,595,000 wakati kwenye *addendum* inaonyesha ni bilioni 4,788,995,000 na ile ya kwenye hotuba ni 4,728,595,000.

Ufafanuzi hapa ni kwamba tofauti kati ya trilioni 4.786 na trilioni 4.788 inatokana na kuongezeka kwa mapato ya shilingi bilioni mbili toka *NMB* ambayo mwanzo yalikadiriwa kuwa yatafikia bilioni 58. Aidha tofauti kati ya trilioni 4.728 iliyojionyesha kwenye hotuba ya Waziri, imetokana na kutozionyesha shilingi bilioni 60 za mauzo ya hisa hizo katika hotuba yake lakini kimsingi zimeshaonyeshwa kwenye *addendum*.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililoonyesha tofauti za mahesabu/takwimu zilizojitokeza ni ile *item* 080402, inayohusu Benki Kuu. Katika kitabu cha makadirio ya gawio ni shilingi 11.1 bilioni wakati katika nyongeza ya marekebisho (*addendum*) ni shilingi 6.1 bilioni. Aidha, kwa upande wa *NMB* takwimu inaoneka kuwa ni shilingi 4.0 bilioni katika kitabu wakati katika *addendum* ni shilingi mbili bilioni. Hii imetokana na makadirio ya awali kuwa makubwa kuliko hali halisi iliyojitokeza. Vilevile mapato kutokana na mauzo ya hisa za *NMB* yalikadiriwa kufikia shilingi 58.0 bilioni wakati jinsi muda ulivyoziidi kuendelea, yaliongezeka na kufikia shilingi 60.0 bilioni.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeelezwa kuwa baadhi ya tofauti zilizojitokeza katika machapisho haya ni kwamba vitabu hivi vilitolewa nyakati tofauti. Kitabu cha Mapato kilitayarishwa awali wakati mazungumzo yakiendelea kati ya Wizara na Mashirika mbalimbali ya Umma ili kupata makisio ya faida zao na hivyo kujua kiasi cha gawio toka mashirika husika

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine, hali hii inajitokeza kwa sababu kimsingi na kawaida wakati Serikali inapopanga mapato yake, huwa ni makadirio na zile takwimu zinazoonyeshwa, ni zile zinazowasilishwa (*as submitted to the National Assembly*) na sio zile zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu (*as passed by the National Assembly*). Zoezi hili la kuidhinisha, huwa linafanyika na kukamilika baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Muswada wa Sheria ya Fedha (*Finance Bill*) na Muswada wa Fedha (*Appropriation Bill*), unaoruhusu matumizi halisi ya Serikali na hivyo mapato.

Mheshimiwa Spika, tofauti za takwimu/mahesabu zilizotokea katika mjadala huu wa bajeti, zinadhihirisha umuhimu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, vilevile kuwa na jukumu la ziada la kuchambua bajeti ya Serikali kwa maana ya mapato na matumizi na hivyo kupitia vitabu vyote husika kabla havijaingia kujadiliwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kuwapongeza watendaji walio chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi pamoja na taasisi zake, kwa kufanya kazi kwa umakini na uadilifu na hivyo kumshauri vyema Waziri wao wa Fedha na Uchumi. Aidha, naipongeza sana Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kazi tuliyoifanya na kulisaidia Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Nadhani kazi yetu ya kuiwezesha Kamati kukutana, imeleta faida na kupunguza utata.

Kutoka upande wa Kambi ya Upinzani, nimearifiwa, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mwenyekiti wa POC, ndiye atakayewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

MHE. KABWE Z. ZITTO (K.n.y. KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, naomba kutoa taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuhusu utata wa mahesabu katika Kitabu cha Kwanza cha Mapato, *Volume I, Financial Statement and Revenue Estimates* kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi, ulitoa mwongozo ulioombwa na Kambi ya Upinzani, kuhusiana na kukiukwa kwa Kanuni ya 96(1) kuhusiana na matakwa ya Kanuni hiyo inayosema kwamba;-

“Waziri atapeleka kwa Katibu Makadirio ya Matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Serikali ya mwaka wa fedha unaohusika na nakala ya makadirio hayo itapelekwa na kumfikia kila Mbunge angalau siku ishirini na moja kabla ya Mkutano ambao utashughulikia makadirio hayo.”

Mheshimiwa Spika, ulitoa mwongozo kuwa kuna utata katika kipengele hicho na kuagiza Kamati ya Fedha kupitia Kanuni hiyo na kupendekeza marekebisho stahiki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja zilizotolewa na Kambi ya Upinzani wakati wa majadala kuwa kuna mapungufu katika takwimu za Kitabu cha Mapato, Serikali imewasilisha marekebisho ya takwimu hizo. Kitabu cha awali cha mapato, ni hiki na cha marekebisho ambayo Serikali imerekebisha, ni hiki. Kwa hiyo, kulikuwa kuna matatizo ya kitakwimu ndiyo maana Wizara ya Fedha imeleta marekebisho hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa takwimu za ziada zilizowasilishwa na Waziri leo asubuhi kwa njia ya ‘*Addendum to Volume I*’, kuonekana bado hazioani na takwimu zilizoko kwenye Kitabu cha Hotuba ya Waziri, uliagiza Kitabu hicho pamoja na *Addendum* kipitiwe na Kamati ya Fedha na Uchumi na baadaye Mwenyekiti wa Kamati husika na Kambi ya Upinzani, tuitolee taarifa ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii kutoa Taarifa kwa niaba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, moja, Kambi ya Upinzani imefarijika na unyoofu wa Serikali, wa kukubali kuwa kulikuwa na upungufu na makosa ya kitakwimu katika Kitabu cha Kwanza cha Makadirio ya Mapato (*Volume I, Financial Statement and Revenue Estimates*) na hivyo kuwasilisha Bungeni Nyongeza ya Marekebisho hayo (*Addendum to Volume I*). *(Makofi)*

Mbili, Mheshimiwa Waziri, amieleza Kamati ya Fedha na Uchumi, kuwa upungufu huo umetokana na Serikali kupata makisio ya awali ambayo miongoni mwake hayakuwa yamethibitishwa na vyombo vinavyochangia mapato ya Serikali (kwa mfano, katika Benki Kuu, Serikali ilikisia shilingi 11 bilioni lakini baadaye ikathibitika kuwa ni shilingi sita bilioni).

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, imeridhika na maelezo hayo isipokuwa inashauri kwamba, kwa miaka ijayo, kazi hiyo iwe imekamili kabla ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kuwasilishwa Bungeni, ili Bunge kwa niaba ya wananchi liweze kupitisha jambo lililo na uhakika nalo. *(Makofi)*

Tatu, baada ya maelezo ya Waziri wa Fedha na Uchumi, Kambi ya Upinzani imebaini kwamba, utegemezi wa bajeti ya Maendeleo kwa Wahisani, bado ni mkubwa mno kwa kiwango cha asilimia 97.5. Hii maana yake ni kwamba, tunafanya uchumi wa kuchumia tumbo (*stomach economy*). Kambi ya Upinzani, inasisitiza kwamba vyanzo vya mapato ilivyovibainisha katika bajeti mbadala, vifuatiliwe kikamilifu ili kupunguza utegemezi huu. *(Makofi)*

Nne, Kambi ya Upinzani, bado inasikitishwa na kitendo cha Serikali ya Muungano, kutogawa gawio sahihi kutokana na faida ya Benki Kuu kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa mujibu wa Kumbukumbu za *IMF*, ilikuwa inamiliki asilimia 11.5 ya hisa za Benki Kuu (*BOT*). Hivyo kugawa gawio kwa asilimia 4.5, ni kuipunja Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupata gawio sahihi kutokana na mtaji wake wakati Benki Kuu inaanza mwaka 1965 baada ya kuvunjwa kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika ya Mashariki (*East African Currency Board*). Kambi ya Upinzani, inaitaka Benki Kuu ya Tanzania igawe gawio kwa *SMZ* kwa mujibu wa hisa zake yaani asilimia 11.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, Kambi ya Upinzani, inasisitiza kuwa katika miaka ijayo, Bunge lizingatie Ibara ya 138 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inayosema kuwa, hakuna kodi au tozo yoyote inayoweza kutozwa bila idhini ya Bunge au kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.

Sita, Kambi ya Upinzani, inaona upo umuhimu pia wa kufanya marekebisho ya kifungu cha 96 cha Kanuni ya Bunge, Toleo la 2007 ili kulifanya Bunge kujadili na kupitisha mapendekezo ya Mapato na Matumizi kama yanavyowasilishwa na Vitabu vyote Vinne vya Bajeti badala ya kupitisha matumizi tu kama ilivyozoeleka.

Saba, kutokana na kasoro zilizoonekana hivi sasa ambapo Bunge limekuwa likijadili na kupitisha vitabu vya matumizi pekee na hata Kamati ya Fedha na Uchumi kutojadili vitabu vya mapato na kutokana na uzoefu wa Mabunge mengine, Kambi ya Upinzani, inapendekeza Bunge kuwa na Kamati ya Bajeti (*Budget Committee*) ambayo wajumbe wake watakuwa ni Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge. Kamati ya Bajeti, ndio itakuwa na jukumu la kupitia makadirio yote ya Mapato na Matumizi ya Serikali yaani vitabu vyote vinne. *(Makofi)*

Nane, kutokana na uzoefu tuliopata kutoka katika Mabunge mengine, Kambi ya Upinzani, inapendekeza kuwa kwa vile Mheshimiwa Spika anatoa maamuzi mengi ndani ya Bunge, wakati umefika sasa wa maamuzi hayo kuchapishwa rasmi katika umbo la kitabu ili kurahisisha rejea ya Wabunge kuhusu mambo yaliyokwisha kuamuliwa ndani ya Bunge na wewe Mheshimiwa Spika, Naibu wako na Wenyeviti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tisa, Kambi ya Upinzani Bungeni, imefuatilia kwa karibu michango mbalimbali ya Wabunge wiki hii ya mjadala wa Bajeti. Kambi imesikitishwa sana na mchango wa Mbunge mmoja jana aliposema kwamba Watendaji wa Serikali, hawana nia njema na CCM na hivyo kumkwamisha Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tabia ya sisi wanasiasa kupeleka lawama kwa watendaji kwa makosa ambayo sote twahusika, si tabia nzuri. Kambi ya Upinzani, ina imani kubwa na watendaji wa Serikali na tunawataka wafanye kazi zao bila upendeleo wa kiitikadi. Watendaji wote Serikalini, Watanzania wazalendo, endeleeni kuchapa kazi na mchukulie mchango wa Mheshimiwa Mbunge huyo kama Waheshimiwa binafsi sio mawazo ya Bunge. *(Makofi)*

Kumi, hatimaye, naomba kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, waliosimamia kidete ili kuhimiza kufanywa marekebisho kwa upungufu huu uliojitokeza na kuonyesha umuhimu wa Bunge kujadili Kitabu cha Kwanza ili kutimiza matakwa ya Katiba, Ibara ya 138.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, ina imani na watendaji wote wa Serikali hasa tukielewa mazingira wanayofanyia kazi hiyo. Natumaini kabisa kwamba upungufu uliotokea, haukufanywa kwa nia ya kumuanguasha Waziri, ila ni hali halisi ya matatizo ya kutokuwa na vianzio vya uhakika na vya kutosha matumizi yetu. Tunaomba waendeleo kujenga uadilifu wao kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kutokana na ushirikiano na unyoofu aliouonyesha Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, Kambi ya Upinzani, itazingatia maslahi ya Taifa wakati wa hoja ya kupitishwa kwa bajeti hii, itakapoletwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Niseme tu, baadhi ya yaliyomo katika taarifa ya Kambi ya Upinzani, ni maoni tu na kwa kuwa Spika amekwishakabidhi kazi ya kuiangalia Kanuni ya 96 kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, basi maoni haya yataingia huko ili yafanyiwe kazi na si lazima yatakaporejea yachukue sura iliyopendekezwa na Kambi ya Upinzani. Kwa sababu kama nilivyosema awali, namna ya kuidhinisha matumizi haiwezi kulingana na namna ya kuidhinisha mapato kwa sababu itakuwa ni nchi ya ajabu hapa kwetu sisi tuwe tunaweka ukomo kwenye mapato. Huwezi kuweka ukomo kwenye mapato, tunaweka ukomo kwenye matumizi, mapato yakiongezeka, ni vizuri zaidi kwa wananchi. Kwa hiyo, namna ya kupitia Kitabu cha I na III, itakuwa ni matokeo ya mjadala wa kidemokrasia ndani ya Kamati. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, pamoja na Viongozi wenzake, kwa kuandaa Bajeti ya Serikali inayojali wanyonge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo napenda kuchangia/kutoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mpango wa Maendeleo imara, wenye upeo, mwongozo unaozingatia vipengele unaohusiana na uandaaji na utekelezaji wa programu ni mhimili wa uchumi usioyumba. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kutuandalia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2008/2009, ambao umezingatia vipaumbele na mikakati ya utekelezaji wa vipaumbele. Hata hivyo, napenda kutoa ushauri kuhusu Mipango ya Kitaifa ya kuimarisha Sekta ya Afya

katika kuimarisha huduma za Afya popote duniani. Mpango thabiti wa kuleta mapinduzi, wenye ujuzi katika taaluma mbalimbali katika ngazi zote. Kwa miaka mingi, Mpango wa Maendeleo na Uchumi, haujazingatia katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa kuimarisha upatikanaji wa wataalam wa kutosha na kukidhi matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa, wakati umefika kwa Wizara kuweka mkazo katika kuandaa/kuingiza katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa, mahitaji ya Taifa kuhusu Madaktari, Wauguzi, Mabwana Afya na kada mbalimbali katika Sekta ya Afya. Jukumu hili ni la Wizara ya Fedha, Mpango na Uchumi. Wizara ya Afya ni mtumiaji. Hivyo, napenda kutoa ushauri kuwa, suala hili lifanyiwe kazi ili Taifa liweze kuwa na mpango endelevu lenye lengo la:-

- (i) Kuwa na “*data bank*” ya wataalam wa Sekta ya Afya;
- (ii) Kubaini mahitaji ya wataalam katika Sekta ya Afya; na
- (iii) Kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika kuandaa tathmini na idadi ya wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu vya IMTU, kwa lengo la kutambua wataalam wanaohitimu kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Uchumi na Naibu Waziri wake, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Nawapongeza pia kwa hotuba nzuri waliyoiwasilisha Bungeni, ambayo wananchi wengi inawapa matumaini, ikiwa na wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, nimepitia Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2008/2009, lakini kwa bahati mbaya sana, sijaona Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Naiomba Serikali iuone mradi huu kuwa ni muhimu na hasa kwa kuzingatia kwamba, ujenzi wa Daraja hili limo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 – 2010 na miaka iliyobaki ni michache. *NSSF* iungwe mkono juhudi zake za kutafuta mfadhili kujenga daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi haijapewa msukumo mkubwa kama Ilani ilivyotamka katika mambo yafuatayo: Kutoa mikopo kwa wavuvi ya zana za wavuvi na kujenga viwanda vya usindikaji samaki kwa nia ya kuweka soko la uhakika kwa wavuvi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ambayo ninaamini itatoa msukumo maalum kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, hasa katika maeneo hayo muhimu ambayo yanawagusa moja kwa moja wavuvi wetu/wananchi.

Mheshimiwa Spika, hatuna budi kwa hatua za awali za kilimo cha umwagiliaji maji, kupeleka nguvu zetu kwa kipaumbele katika Mikoa inayozalisha sana mazao ya chakula hasa mpunga, mahindi na kadhalika kama vile Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Iringa na Morogoro.

Kutoa kipaumbele hicho kwa mikoa hiyo ni kwa nia ya kuzalisha kwa wingi mazao hayo kwa mwaka mzima, badala ya kutegemea mvua. Hii itasaidia ongezeko la tija na kushuka kwa bei ya mazao hayo, ambayo ndio chakula kikuu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali haina budi kurudia utaratibu wake wa zamani wa kuitumia *TIPER*; *TIPER* imetupwa na ni rasilimali kubwa sana kwa Taifa letu (miundombinu yake) ni miundombinu kwa hifadhi ya mafuta Kitaifa.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, *Bureau de Change* nchini wanakataa kupokea noti za *USD* zenye vichwa vidogo wakati nchi nyingine zote duniani wanapokea noti hizo, pamoja na Marekani yenye.

Ningependa Serikali itoe tamko kuhusu hili, kwa sababu wageni wanakuja na noti hizo kutoka nchi wanazotoka na wakifika hapa zinakataliwa na hata *bureau* wanazozikubali, wanawabadilishia kwa *rate* ndogo sana. Kwa mfano, noti ya \$100 ya kichwa kidogo wanabadilisha kwa *rate* ya 900 – 1000, wakati yenye kichwa kikubwa wanabadilisha kwa *rate* ya 1200 – 1900. Kwa kuwatoza *rate* hiyo ndogo; huu ni wizi wa mchana. Je hili ni agizo kutoka Benki Kuu?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutoongeza kodi ya mafuta; haijatueleza ni kwa jinsi gani Serikali itaweza kubaki na bei iliyopo wakati bei ya mafuta inakuwa *controled* na Soko la Dunia (*OPEC*)? Kutoweka kodi katika mafuta kuna nia nzuri na ya dhati, kuwapunguzia makali ya maisha wananchi. Ili kumsaidia mwananchi katika hili, ningesauri Serikali ipunguze kodi katika mafuta ili mkulima wa kawaida kabisa kule kijijini, akishavuna mazao yake, aweze kuyasafirisha kuja mjini (sokoni) kwa bei nafuu. Pamoja na Serikali kudhamiria kuwasaidia wakulima wa kawaida, ambao ndio wazalishaji wakuu wa vyakula, kuna haja ya kuwasidia zaidi hawa wakulima katika kilimo cha umwagiliaji, ukizingatia wengi wao wanalima kwa kutegemea mvua na mvua haitabiriki na isiponyesha ndio balaa la njaa linakuwepo. Hivyo, kilimo cha umwagiliaji ni muhimu. Pongezi kwa kutoa kodi katika pembejeo kama matrekta na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kuipunguzia Serikali matumizi makubwa ya kodi za Watanzania, ningesauri Wizara zote ziwe na magari yasiyozidi matatu na yawe ya aina ya Suzuki, ambayo hutumia mafuta kidogo na *service* yake haifanywi kwa gharama kubwa. Pia magari haya ya Wizara yawe yanaegeshwa katika sehemu za kazi yalipopangwa. Wafanyakazi wote, ikiwa ni pamoja na Mawaziri na Makatibu Wakuu, watumie magari yao ya binafsi wanapokwenda kazini, kwa sababu Mawaziri wamepewa mikopo ya magari, hata maofisa wanapata mikopo kwa ajili ya magari. Kwa kutumia gari la Serikali wakati wa saa za kazi tu, kutapunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya fedha Serikalini.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali kuongeza kodi kwenye vileo na sigara ina maana bajeti yetu inaendeshwa na wanywa pombe? Hatuwezi kutegemea mapato yetu kutokana na vileo na sigara; kuna njia nyingi tu za kupata mapato. Kwa mfano mdogo tu, wachimba madini wakitozwa kodi ipasavyo, hii ni njia nzuri tu ya kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, katika biashara ya utalii, mfano, wakala wenye kupandisha watalii Mlima Kilimanjaro au kuwapeleka mbugani; Mamlaka ya Mapato (*TRA*) wanaweza kabisa kukusanya kodi nzuri tu kutokana na biashara hii. Wanaweza kuweka *target*, kila mpanda mlima watachukua kodi inayotozwa sio chini ya \$1300 kwa mtu, lakini *Tour Operators* wanaweza kutoza zaidi ya hizo. Kwa njia hii, Serikali itakuwa imepata mapato. Na hili lisiwe kwa ajili ya Kilimanjaro *National Park*, iwe katika *National Parks* zote.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa kwa Bajeti nzuri waliyoitoa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa asilimia tisini, bajeti hii inamlenga mwananchi wa kawaida, kwa sababu huduma nyingi za jamii, kama vile Miundombinu, Afya Elimu, Kilimo na kadhalika zitaboreshwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wananchi wa kawaida, wanaolima mazao ya kuzalisha mafuta ya kula (Alizeti, Karanga, Mawese na kadhalika), Serikali haikuwatendea haki kwa kuondoa ushuru wa forodha wa asilima kumi. Kwenye kitu unachokiita mafuta ghafi, yakiingia kwa wingi yatashusha bei ya mafuta ya ndani.

Mheshimiwa Spika, napenda nikueleze kwamba, hakuna mafuta ghafi; mafuta yanayoingizwa kutoka nje ni mafuta halisi. Kwa hapo, naiomba Serikali isiwe kigeugeu; wakati wa Bajeti ya 2005/06 Serikali ilitamka ndani ya Bunge hili kwamba, ushuru huo umewekwa kwa kuwasaidia wakulima wetu wa Mikoa ya Singida, Dodoma, Iringa, Kigoma, Manyara na Mikoa mingine yote, inayozalisha mbegu za kutengenezea mafuta ya Alizeti na Mawese.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali inataka tena kuanzisha malumbano kati yake na wakulima wa nchi hii; kodi hii inafutwa kwa faida ya nani?

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, inapongezwa sana kwa kazi nzuri inayowafanyia wananchi wake katika kuondokana na umaskini. Hivi kwa nini mnataka kuweka doa baya; mnajua kwa kutoa ushauri huu ni mbinu ya kutaka wananchi wasiondokane na umaskini?

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wote wa nchi hii nakuomba sitisha huo ushuru, huo uendeleo kuwepo kwenye mafuta gafi ili ujazie zile asilimia kumi zilizotolewa kwenye Bajeti hii.

Narudia kuipongeza sana Bajeti hii.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani kwako na Bunge lako Tukufu, kwa jinsi mnavyoshiriki katika uendeshaaji wa shughuli za Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mstapha Mkulo, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Omar Yusuph Mzee na Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha. Pia nitumie fursa hii, kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara, chini ya Katibu Mkuu, Ndugu Gray S. Mgonja, kwa kazi nzuri ya uandaaji wa bajeti hii ya mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka huu ni muhimu sana, hasa ikiwa inatimiza malengo makuu manne; Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005 – 2010; Mipango ya Milenia (*Millennium Development Goals*); Dira ya Taifa 2025; na Mkakati wa Kukuza Uchumi wa Kuondoa Umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo kwa pamoja, ndicho kigezo pekee ambacho kitalifanya Taifa letu liendelee na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Nne ni jambo la busara sana, hasa kwa bajeti ya mwaka huu katika kuhakikisha bajeti inalenga mambo muhimu kuanzia Elimu, Miundombinu, Afya, Kilimo, Maji na Nishati. Maeneo haya ni nyeti sana kwa ustawi wa maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza fedha katika Sekta ya Elimu kwa mwaka 2007/08 na na unyeti wa Sekta hii, bado inaonekana udhibiti wa fedha katika Sekta hii ni mbovu kutokana na kutofanya vizuri. Kwa uzoefu wa miaka miwili iliyopita, bado upo umuhimu wa kujifanyia tathmini, kuona namna fedha zinavyotumika kwa kuzingatia vigezo vya matumizi ya fedha za Serikali. Bado tunaona udhibiti wa fedha hizi umebaki mikononi mwa mtu mmoja mmoja kama vile Wakuu wa Shule za Sekondari na kadhalika na ubora wa vifaa vya elimu kuendelea kuwa duni na madai mengi ya walimu bila kukoma.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii ni dhahiri wizara ya fedha ni lazima itoe miongozo, ikiwemo ile ya ununuzi (*Procurement*) na kadhalika ili kuwa na ule utaratibu wa *value for money* ili hatua inayofanikiwa kwa kila mwaka isirejewe.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kuzungumizia Sekta ya Miundombinu, pamoja na ongezeko la takribani shilingi bilioni 196.1 zilizoongezeka kwa mwaka huu toka bajeti ya mwaka 2007/08, bado ongezeko hili ni dogo hasa ukilinganisha hali halisi katika Sekta hii. Kuimarishwa Sekta hii, kutaongeza Pato la Taifa hasa kwa kuwavutia wawekezaji wengi katika maeneo mbalimbali ya Viwanda, Utalii na kadhalika. Bado Sekta hii inapewa kipaumbele kisichostahili; maeneo kama usafiri wa anga (viwanja vya ndege), vinahitajika viwepo vya kisasa. Maeneo muhimu yale ya Arusha na Kilimanjaro. Kiwanja hicho kinahitaji fedha za kutosha za kuukarabati na kuufanya uwe wa kisasa.

Viwanja vya Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya, Mtwara na kwingineko katika kila Mkoa, kuwe na usafiri wa ndani (*Domestic Flight*), ambazo kwa pamoja zitainua pato. Barabara zote zinazotajwa, bado zinaendelea kwa kusuasua kwa mpango 2006/07 jambo ambalo linafanya kutoendelea kwa miradi mipya. *Central corridor* ikiimarishwa kwa pamoja kusaiana na Reli na Anga kwa kiwango kikubwa, kutaimarisha Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu katika kipindi hiki pia, imeahidi kuelekeza utekelezaji wa Sekta ya Afya ngazi zote za Kata kuwe na Vituo vya Afya, vijijini kuwe na Zahahati na kadhalika. Eneo hili lazima litazamwe kwa umakini sana ili fedha iliyotengwa ifanye kazi iliyokusudiwa zisiende mifukoni mwa watu huku utekelezaji ukifa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ni muhimu sana na kilimo ni uti wa mgogo wa Taifa letu kwa takribani 80% ya wananchi ni wakulima, lakini kilimo wanachotumia ni duni (kilimo cha jembe la mkono), mvua za kubahatisha na kadhalika. Eneo hili linahitaji fedha za kutosha kwani eneo ni la uzalishaji, ambalo kwa kiwango kikubwa linaweza kuongeza Pato la nchi. Mkulima wa nchi hii ametelekezwa na hali yake ya maisha kuzidi kuporomoka siku hadi siku. Mkulima anakabiliwa na changamoto nyingi za maisha; mwananchi anahusika kwa kila hali na hali ya maendeleo katika maeneo yao vijijini; anahitajika kuchangia maji, shule za sekondari/msingi, Afya na michango mingine mbalimbali, ambayo yote ni mzigo kwake. Hivyo basi, kuipatia fedha ndogo Wizara hii ni kumnyanyasa Mkulima.

Mheshimiwa Waziri, wakati akiwasilisha hotuba alilieleza Bunge hili, fedha za Kilimo zipo pia katika maeneo mengine hasa kwa *Private Sector* na kadhalika. Udhhibiti wa hili uko vipi na uhakika wa kumfikia mkulima uko vipi?

Mhe. Spika, mwisho, nisisitize juu ya kuhimiza matumizi bora kwa fedha za Wafadhili. Wizara iwe msimamizi makini wa fedha zinazotolewa na Wafadhili zitumike kwa miradi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Hata hivyo, ninayo Mapendekezo na Ushauri Serikalini kuhusiana na Bajeti ya 2008/09 kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuibua vyanzo vipya vya uhakika wa kodi ili kuongeza Mapato ya Serikali. Maeneo ya Sekta ya Mafuta (*Petroleum*) ni eneo ambalo Serikali inapoteza sana Mapato. Usimamizi mbovu wa *flow meters* pale *THA* na *KOJ* ni tatizo kubwa na *it is said we are losing between 20 – 30% of revenue in taxes* kwa imports ya Mafuta; *Petrol and Diesel*. *TRA, TPDC* na *TPH* waunde *task force* ya kufanya kazi hii kwa pamoja.

Pili, kodi katika visima vya gesi na Madini; ingawa taarifa ya Tume ya Jaji Bomani inasubiriwa ni wazi Serikali inapoteza sana Mapato yake katika sekta hii. Wizara ya fedha na Wizara ya Nishati na Madini, zikae pamoja wachambue na walete marekebisho ya sheria haraka Bungeni ili Serikali isiendele kupoteza Mapato yake. Bila shaka Ripoti ya Jaji Bomani itagusa pia Sheria za *TIC*; yote haya yatazamwe kwa pamoja ili Rasilimali za Taifa zitunufaishe sote.

Tatu, biashara na nchi jirani na utumiaji wa Bandari zetu. Eneo lingine ambalo hatuna budi kulisimamia vizuri ni *Transit Trade and Boarder Trade*. Eneo hili limegubikwa na udanganyifu/rushwa ambayo *TRA* lazima wasimamie vizuri na kwa umakini. Hili ni eneo ambalo *it is said TRA is losing 30 – 35% lost revenue through uncorrected taxes/corruption of TRA Officials*. Serikali haina budi kuiimarisha Bandari ya Kigoma na Reli ya Kati, kama kweli tunataka kunufaika na ufanyaji biashara na nchi jirani ambazo ni tajiri kwa madini kama *DRC*.

Nne, kupunguza Misamaha ya Kodi. Serikali lazima itazame upya mishamaha ya kodi; hivi misamaha yote ya kodi ni ya lazima? Nani ananufaika na misamaha hiyo?

Kodi kwenye magari maarufu “*Mashingiri*” na “*GX*” kwa nini ipunguzwe? Wenye magari hayo ni wafanyabiashara wakubwa, ambao wengi hawalipi kodi sawasawa, kwa nini wasibanwe kwenye kodi ya *Mashingiri* yao?

Tano, Menejimenti ya Uchumi/Biashara na Fedha (*Monetary Policy Management*); *BoT* lazima ifanye kazi yake kwa umakini sana. *BoT* lazima wasimamie uimara wa shilingi yetu ili iwe *competitive against other currencies*. Zaidi ya hayo, Kitengo cha Uchumi *BoT* kiimarishwe na Mapato ya Biashara ya Mabenki ambayo *BoT* hukusanya yaingizwe Hazina ili fedha zisaidie Sekta ya Elimu na Barabara. “Ufisadi na Rushwa *BoT* upigwe vita sana.”

Sita, matumizi makubwa ya Serikali; ni dhahiri upo ushahidi wa matumizi makubwa na yasiyokuwa ya lazima ya Serikali. Mikutano, Makongamano na safari nyingi ndani na nje ya nchi, hayana budi kusimamiwa vizuri. Aidha, Idara za Manunuzi za Wizara zinaweza kufanya kazi mbalimbali kwa pamoja. Kwa mfano, ununuzi wa magari na mitambo, unaweza kufanywa *centrally* badala ya kila Wizara kufanya manunuzi peke yake. Hii itaokoa fedha nyingi kupitia Bulk Purchases/Joint Procurement. Ununuzi wa *stationeries* za maofisi; Serikali inaweza kuokoa fedha nyingi kupitia *Bulk Purchases* na *Discounts*. Manunuzi haya yafanyike *centrally* au kupitia Wizara ya Miundombinu au Ofisi ya Waziri Mkuu.

Baadhi ya mambo haya yakizingatiwa yatasaidia.

MHE. DR.WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa vile nchi yetu bado ni tegemezi kwa asilimia zaidi ya 34 na kwa vile tusipodhibiti matumizi ya fedha zinazoidhinishwa na Bunge, tutaendelea kuwa na matatizo ya utegemezi katika nchi yetu; ninataka nipate ufafanuzi wa kina katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kwa vile ushahidi ulioko Brella unaonyesha kuwa, Kampuni ya *TANGOLD*, ambayo Serikali imetamka ndani ya Bunge kuwa ni mali ya Serikali 100%, imesajiliwa Mauritius na baadaye kupata Hati ya Makubaliano Tanzania (*Certificate of Compliance*):-

(a) Je, *TANGOLD* ni mali ya nani hasa, wanahisa wake ni akina nani?

(b) Je, *TANGOLD* ina akaunti ngapi Mauritius na zinakaguliwa na nani na mara ya mwisho zilikaguliwa lini na taarifa ya ukaguzi kwa vile ni *Public Document*; inapatikana wapi na au Serikali ipo tayari kuiweka hadharani?

(c) Je, Tangu imeanzishwa *TANGOLD* imeshatoa Serikalini kama gawio au kwa utaratibu mwingine wowote; kiasi gani cha fedha na kama ni Kampuni ya Serikali faida yake ni nini iwapo haijatoa faida yeyote Serikalini?

(d) Kwa vile tarehe 29 Desemba, 2005 Wizara ya Fedha iliamishia kwenye Akaunti Na. 011105011782, jumla ya Dola za Marekani 13,340,168,37, *NBC Corporate Branch* na ukiacha matumizi yaliyofanyika 22 Februari, 2006; hakuna *Transaction* yoyote iliyofanyika isipokuwa *Withholding Tax*; na kwa kuwa zimebaki kwenye Akaunti hiyo zaidi ya Dola 12 milioni na Taifa linakopa kwa wafadhili/wahisani; shule zetu hazina walimu, madarasa, vifaa na hata sehemu nyingine shule zimefungwa kwa kukosa chakula cha watoto wakati fedha zimekaa tu Benki; ninataka maelezo ya kina; Hazina inapohamishia *TANGOLD* hizo fedha zililenga nini hasa?

(ii) Mheshimiwa Spika, nataka maelezo ya kina kuhusu Kampuni ya *MEREMETA Ltd.* Taarifa nilizonazo ni kuwa, Kampuni hii nayo ilisemekana ni mali ya Serikali chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, iliandikishwa Uingereza na baadaye kupata *Certificate of Compliance* kama Kampuni ya kigeni (Tawi). Hivyo basi:-

(a) Nani hasa mmiliki wa Kampuni hii? Taarifa zilizoko ni kuwa 50% ni Serikali ya Tanzania (tofauti na maelezo Serikali Bungeni); 50% mali ya kampuni moja ya Afrika Kusini

na 1% mali ya *London Law Services Ltd.* Hivi Kampuni hii ina asilimia ngapi? Kwa utata huu mmiliki ni nani?

(b) Je, Benki - London MEREMETA ina Akaunti ngapi na Hesabu za mwisho zilizokaguliwa ziko wapi na kwa nini hazijawahi kufikishwa Bungeni hata siku moja?

(c) Kama umiliki ndiyo ulivyo; kwani nini Serikali kupitia *BoT* ililipa deni la MEREMETA la bilioni 155 kupitia Nedland Bank?

Mheshimiwa Spika, iwapo sitapata majibu ya kina, naomba nitamke kabisa kuwa, sipo tayari kuunga mkono Bajeti hii, kwani hakuna sababu ya kupitisha Bajeti iwapo hakuna uhakika wa uhibitaji wa fedha zinazopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia tena Bajeti hii katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, kufilisiwa kwa uzembe wa *TRA* Kampuni ya *Tango Transport Ltd.* Ninazo taarifa nyingi, zenye uthibitisho wa nyaraka kuhusu unyanyasaji mkubwa uliofanyiwa Kampuni ya Wazalendo ya *Tango Transport* bila maelezo ya kutosha. Vitendo vilivyofanyiwa kampuni hii kama ni vya kweli, vinatisha sana na kutia doa kubwa kwa *TRA*, ambayo siku zote tumeipa sifa nyingi kwa kukusanya vizuri mapato ya Serikali. Lakini Bunge halitegemei kabisa ukusanyaji wa mapato utakaoambatana na unyanyasaji wa aina yoyote ile, ambao hatimaye unaligharimu Taifa pale walionyanyaswa watakapodai haki zao. Hivyo basi, naomba maelezo yafutayo:-

(a) Madai ya *interest* ya zaidi ya 2.2 bilioni, yanayotokana na *Principle* ya 53,650,150,151. *Principle* hiyo ambayo maelezo ya jinsi ilivyochukuliwa inatia doa kubwa na hata wingu la rushwa, ililipwa kwa *PV No. 0021691* ya tarehe 26 Novemba, 2007 na *PV No. 0019750* ya tarehe 7 Agosti, 2007. Madai hayo ni ya miaka takriban 10, yaani tangu 1997. Barua Na. TRA/SB/L.1/Vol III ya Desemba 2007, iliyoandikwa Benki inakiri kuwa, *principle amount was collected wrongly*. Sasa basi:-

(i) Bunge hili lielezwe kwa kina ni vipi mwananchi alazimishwe kulipa kiasi kikubwa namna hiyo na kwa miaka kumi anyimwe haki ya kulipwa haki yake?

(ii) Kwa vile *principle amount* zimelipwa kati ya Agosti, 2007 na Novemba, 2007, kigugumizi cha kumlipa mwananchi/kampuni hiyo ya wananchi *interest* kwa *rate* ya Benki inatoka wapi? Hii ni Kampuni ya Biashara siyo *charity* na fedha zao zingefanya biashara zingepata faida.

(iii) Ni lini sasa *interest* hiyo italipwa ili haki ya mwananchi ilindwe? Kilichofanyika kama si unyanyasaji wenye siri kubwa nyuma yake ni uzembe na hivyo, mwananchi au kampuni ya wananchi haiwezi kamwe kuadhibiwa kwa uzembe wa Maofisa wa Serikali.

(iv) Kwa kuwa *TRA* imekiri kuwa, kiwango cha msingi (*principle amount*), kimekusanywa kwa makosa na bado mwananchi akazungushwa na kupigwa danadana kwa miaka zaidi ya kumi; afisa au maofisa husika watachukuliwa hatua gani kwa kulisababishia Taifa hasara kubwa kiasi hiki?

(b) Mheshimiwa Spika, unyanyasaji dhidi ya Kampuni ya *Tango Transport Ltd.* ulifikia kiwango cha kutisha pale Kampuni hiyo iliponyang'anywa *Registration Cards* za magari yote ya Kampuni yapatayo zaidi ya 61. Kati ya magari hayo, zaidi ya 30 ni magari makubwa ya biashara, yaani malori na trella zake. Ni kweli *TRA* inayo haki wakati wowote kukagua kadi za magari na magari yenyewe na hata kuzichukua kwa muda ili kuzifanyia ukaguzi huo. Lakini kuzichukua, tena kwa kutumia polisi na kisha kukaa na kadi hizo kwa zaidi ya miaka kumi (toka 1997 hadi leo) na kisha kukiri kuzipoteza kwa mantiki yoyote ile; ni kielelezo cha wazi cha uzembe wa hali ya juu, unaoambatana na unyanyasaji ambao ni vyema Serikali ikatafuta na kuona kiini cheke. Leo ni kampuni hii, hatujui ni makampuni mangapi yamefanyiwa unyanyasaji wa aina hii, hasa ikizingatiwa kuwa kuna minong'ono mingi ya rushwa ndani ya *TRA*. Hivyo basi:-

(i) Nataka maelezo ya kina ni nini hasa kiliichofanya *TRA* kuchukua kadi zote mara moja, kukaa nazo zaidi ya miaka kumi na kisha bila umakini kuzipoteza?

(ii) *TRA* ni wataalam; wanafahamu Kampuni ya Biashara ya Usafirishaji wakati wote inahitaji *Registration Card* kufanya biashara zake, hasa kupata tenda mbalimbali ikiwemo za *Transit Goods*; kupata *insurance* au hata kama ilivyotokea sasa kubadilisha namba za magari. Je, ni kweli kuwa *TRA* hawajui kuwa wameipotezea Kampuni hiyo kwa kuwakosesha *revenue loss* ya mabilioni ya fedha, zikiwemo za kigeni kwa unyanyasaji huo?

Nashukuru *TRA* wamekiri kuchukua kadi hizo kwa barua yao ya tarehe 7 Novemba, 1997 na pia ya tarehe 6 Julai, 2007, yenye Kumb. Na. TRA/SB/L.1/Vol. III.

(c) Je, baada ya kukiri kuchukua kadi hizo kwa miaka kumi, *TRA* haioni kuwa imeshiriki katika kuifilisi Kampuni hiyo ya wazawa kwa uzembe au kwa sababu yoyote ile; Serikali sasa inatoa kauli gani kuhusu uzembe huo?

Serikali itafidia lini kwa kiwango cha biashara kitakachokubaliwa kati yake na Uongozi wa Kampuni husika, ili kutekeleza sera ya kujenga mazingira ya biashara na kuimarisha uwezekanaji katika nchi yetu? Serikali iniarifu mpango au mkakati kamili wa kulipa fidia hiyo iliyosababishwa na uzembe wa wazi wa Watendaji wake?

Wakati suala la kulipwa fidia Kampuni ya *Tango Transport* ni la haki ya wananchi ambao Wabunge ni wajibu wetu kuwatetea na kuwalinda dhidi ya unyanyasaji wa aina yoyote; sisi kama Wabunge, tunataka Bunge lielezwe kinagaubaga nani kasababisha uzembe huu ambao siyo tu umeiathiri kampuni bali Taifa zima. Mhusika atachukuliwa hatua gain za kinidhamu na kisheria?

Mheshimiwa Spika, nisipopata maelezo ya kina kuhusu uzembe huu, hatua zitakazochukuliwa na ratiba ya kuilipa Kampuni hii kwa uzembe wa Serikali, nitaleta hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kupunguza makali ya maisha na kutoa afueni kwa

wananchi. Kwa hatua hiyo, sina budi kuipongeza Serikali, Waziri na Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini makubwa sana kwa Serikali kwamba, kwa mwelekeo huu wa Bajeti, basi itaweka Mkakati Madhubuti wa kwenda hadi vijijini ili kutoa mwongozo wa jinsi gani wananchi hao wataweza kujikwamua kiuchumi ili kuwawezesha kupunguza makali ya maisha yanayotokana na mfumko wa bei, ambao unatokana na upandaji wa bei za mafuta, vyakula na pembejeo.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe ushauri wangu kwamba, tusitegemee sana Sekta za Huduma. Utalii ambao kwa sasa unakuwa kwa kasi na Sekta ya Madini zote zinaleta fedha kwa Taifa lakini hazidumu, kwa maana ya kushuka kwa bei za madini au kutokuwa na watalii wengi nchini kutokana na sababu mbalimbali, hatimaye uchumi utalegalega.

Tutakapoimarisha uchumi kwa wakulima wadogo, tutakuwa tumewasaidia wao kuinua kipato chao na kuwapunguzia mzigo katika suala la kilimo. Wapatiwe mbinu za kisasa za kilimo ili kuweza kulima na kupata mavuno ya uhakika. Vile vile kuangalia uwezekano wa kuwapatia mikopo midogo midogo na elimu ya kilimo cha biashara, kwa kuwa Serikali imeonyesha dhamira yake na nia; bila shaka litawezekana.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Mabenki yakaongezwa kwenye wilaya zetu na huduma zikaelekezwa hadi vijijini, kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta tija katika Halmashauri zetu, kuna haja ya kuongeza kasi kwenye suala la usimamizi wa fedha za Halmashauri. Utaratibu na usimamizi wa *D by D* unahitaji kuimarishwa zaidi ili uweze kufika hadi ngazi ya vijiji. Hali hii itasaidia kuleta usimamizi mzuri wa fedha, kwani wahusika watakuwa na maamuzi yao katika kupanga matumizi ya fedha hizo na pia kutakuwa na usimamizi mzuri wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niulize; ni lini Serikali itaweka mikakati mizuri ambayo itapunguza urasimu na kuboresha sheria zetu kwa wawekezaji ambapo tukifanikiwa tunaweza kuongeza Pato la Taifa na kuleta ajira nchini?

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuwapongeza *TRA* na napenda kusema naunga mkono hoja.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, udhibiti wa Fedha za Serikali ambazo hivi sasa zinapelekwa katika Halmashauri za Wilaya; kutokana na uwezo mdogo wa kutunza na kusimamia fedha zinazopelekwa ili zitoe mchango unaokusudiwa (*value for money*), ipo haja ya kuhusisha Wizara husika ambazo zinatoa fedha hizo kwenda Wilayani. Kwa mfano, hakuna mantiki ya Wizara yoyote kupeleka fedha nyingi Wilayani bila kuwa na utaratibu wa kufuatilia fedha hizo zimefanya kazi gani.

Utaratibu wa *Management Audit* nao uzingatiwe badala ya *Financial Audit* peke yake. Kwa mfano, haitoshi kutoa taarifa ya fedha zilizopokelewa katika Wilaya, lazima fedha hizo ziendane na huduma iliyotarajiwa.

Aidha, bado kuna tatizo kubwa katika Halmashauri za Wilaya nyingi, ambazo kwa mawazo yangu, zinatumia vibaya Sheria ya Manunuzi na kuhalalisha ucheleweshaji wa miradi kutekelezwa. Eneo hili la ununuzi ni nyeti sana, kwa hiyo, muhimu liangaliwe katika ngazi zote.

HON. KABWE Z. ZITTO: First, Distribute Role of the Government; We have a control on our taxes not prices at the World Market for example, prices of fuel. The government shall act as a distributive agent. Reduce duties on road toll by 50bn TShs. and delete (futa) excise duty on fuel raised in 2007/2008 budget so that we reduce inflation pressure on goods and services.

Second, the challenge of rising food prices; the government shall give incentives to produce food to take advantage on rising food prices. A special campaign to produce more food for internal use (get out with label of net importer) and sell surplus. We should not complain with rising prices of food, we shall take advantage.

Third, Revenue Book; numbers do not add up between the revenue book (W1 I) and the Budget Speech. I have given an example on shares revenue of *NMB*. What do you collect from Tanzania Harbour Authority? There is no such campaign in the country.

Fourth, reduce dependence on trade taxes; 50% of the new revenue bonus from import duty and VAT on imports. With EAC–CU + EPA with EU, import taxes will cost us in the near future. Create economic activities in rural areas to create more jobs and revenue.

A concept on the money distributed to the regions for jobs creation.

In the standard definition, unemployment covers all persons who are not engaged in any economic activity but are available for such activities (whether seeking for employment or not). The national (Tanzania) definition includes those with marginal attachment to employment. In Tanzania, according to the report on the state of the economy 2005, 23.8% of the people who are able to work are unemployed.

The issue of employment has been one of the mind boggling things to most policy makers all over the world. In many countries, Tanzania inclusive, employment has been an issue for electoral politics and national debate. It is one of the issues raising concerns of most of the people especially the youths.

In Tanzania the Government of President Jakaya Kikwete has taken the issue of employment and unemployment with seriousness and just recently the Prime Minister of Tanzania announced in Parliament that the Government will offer TShs. 500 millions to each region of the country in order to create employment generation activities.

This is a very bold move by the Government and it has to be supported by patriotic Tanzanians so that the funds are utilized properly and enough sustainable jobs are created. If more jobs are created, the economy will grow and hence standard of living of the people will improve. Moreover, number of tax payers will increase and the Government's capacity to provide social services like schooling, health services and roads will improve.

A concept: Regions in Tanzania are endowed with different resources. This make regions to adopt different strategies and interventions to address unemployment, economic growth and hence reduction of poverty.

Additionally, different sectors of the economy of any region have different employment multipliers. This is due to the fact that some sectors are Drivers of Growth and others are Obstacles to growth. From Regional Profiles (available at the Ministry of Planning, Economy and Empowerment), these sectors can be identified and analysed for purposes formulating specific directives to specific regions on jobs creation.

It is therefore proposed here that a small study be conducted to establish Drivers of Growth and Obstacles to Growth in each region of Tanzania.

The results of the study would be used by the Minister responsible for Employment to give policy directives to regions from time to time in order to guide the efforts for jobs creation.

These policy directives will advise Banks (or financial institutions dealing with the fund) to offer credits to entrepreneurs who engage themselves in the sectors considered to be Drivers and with larger employment multiplier.

The study is advised to be supervised by Consultants who have worked on MKUKUTA in one way or the other: since MKUKUTA has identified strategies that can create more employment in rural and urban areas. This jobs creation effort shall be linked to MKUKUTA. It should as well take experiences of other organizations which are working on the area of jobs creation.

The study has to be done immediately so that Tanzanians will start to benefit from the funds and hence, work, increase productivity and quality of products, pay taxes, consume and contribute to the growth of the economy. By the end of September, report of the study shall be presented to the Minister ready for actions.

Conclusion: TShs. 500 millions can be seen as a drop in the ocean. However, it is enough money to spur economic activities in regions. The working nation can be created out of the initiative. But, care must be taken in order not to repeat mistakes of the past on similar initiatives.

The legislator, however, exhorted the government to raise import duty on imported jute bags. She said the more would protect the local sisal industry. Reducing suspended duty on jute bags from 50% to 40%.

The Tanzania has the capacity to produce about 16 million sisal bags annually at two privately-owned factories in Morogoro and Moshi.

The confederation of Tanzania Industries (CTI) says that imported jute bags sell at about TSh. 400 (55 US cents) per bag, while locally produced sisal bags sell for between TSh. 1,000 and TSh. 1,560 (\$1.50 and \$2.50) per bag, depending on size, excluding value added tax.

Sisal bags are superior packaging materials because they are made of biodegradable hard fibre, are stronger, reusable and protect the packed contents by not absorbing moisture.

Excise duty on mobile phones; Hawa watu wahalipi kodi ya mapato. Ushuru huu utozwe kama ilivyopangwa na *TRCA* wapunguze tozo zao kwa makapuni ya simu ili watumiaji wa simu wasipate gharama. Pia ondoa kodi zote katika simu za mikononi (*handsets*) ili ku-*balance excise duty* iwepo.

Introduction of Cotton Development Levy; Hotuba yako inalenga bidhaa za Kilimo za ndani ziongezwe thamani hapa nchini. Mwaka jana tuliweka kodi katika ngozi ili ku-*discourage export* ya ngozi ghafi. Ni muhimu tufaye hivyo kwa pamba ili kufanya pamba yetu iwe na thamani zaidi kabla ya kupelekwa nje. Hii itajenga ajira zaidi nchini kupitia viwanda.

Nashauri kodi iwekwe katika *export* ya pamba ghafi kwa kiasi cha asilimia 25. *All the best.*

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, pamoja na Wataalam wao, kwa kuandaa Bajeti nzuri. Pamoja na pongezi hizo, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei umekuwa ni tatizo kubwa sana, kwani umeendelea kuathiri maisha ya Watanzania kwa ujumla. Kama hali hii ikiendelea, basi hata Bajeti hii haitakuwa na maana yoyote. Kwa sehemu kubwa, mfumko wa bei umesababishwa na ongezeko la bei za mafuta kwenye Soko la Duniani.

Pamoja na uwezo wa kudhibiti bei za mafuta kwenye Soko la Dunia, naishauri Serikali ihakikishe kwamba, bei za mafuta haziongezwi kinyemela na wafanyabiashara wenye tamaa ya kujinufaisha.

Mheshimiwa Spika, bei kwa baadhi ya bidhaa za viwandani ni kubwa sana. Bidhaa kama vile saruji na mabati, ambazo sasa Watanzania wengi wanazitegemea katika kujenga nyumba zao na hivyo kuboresha makazi yao, bei zake ni kubwa sana. Kwa mfano, bei ya saruji mfuko mmoja Wilayani Mbozi ni Sh. 15,000, bati linaanzia Sh. 13,000 – 25,000 kwa kipande kimoja kutegemeana na *gauge* na futi ya bati.

Naiomba Serikali ichukue hatua madhubuti za kuhakikisha kwamba, bei za bidhaa hizo haziendelei kupanda. Vinginevyo, uboreshaji wa makazi kwa wananchi wetu utabaki kwenye makaratasi tu.

Mheshimiwa Spika, Waziri amekiri kwamba, riba za mikopo ya benki bado ni kubwa na hivyo kuathiri uwezo hasa wa wajasiriamali kukopa na kufanya biashara yenye tija na kuwanufaisha walengwa. Mimi nimeshindwa kuelewa; hivi tatizo ni nini? Amana za wateja wa benki (wanaoweka pesa zao benki kati ya asilimia 2 – 3, wakati ambapo riba kwenye mikopo ni kati ya asilimia 15 – 20; ni wazi kwamba, Mabenki haya yanapata faida sana (*super profit*).

Naishauri Serikali ihakikishe kwamba, *lending rates* haziwi kubwa kiasi cha kutowanufaisha wananchi. Aidha, ihakikishe kwamba, masharti magumu ya ukopaji (*stringent collateral*), yanaondolewa.

Mabenki haya pamoja na kwamba yanafanya biashara, lakini yasiachiwe yawanyonye wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunashukuru kwa msaada huo kutoka MCC wa Dola milioni 698 za Kimarekani. Hata hivyo, kiasi kilichotengwa kwenye bajeti ya mwaka huu, dola milioni 68.5 naona ni kidogo sana ukizingatia kwamba, fedha hizo zitatakiwa zitumike ndani ya miaka mitano. Kama mwenendo wa kutoa pesa hizo utakuwa hivyo, basi itachukua takriban miaka kumi ndipo zitumike zote. Ushauri wangu ni kwamba, Serikali izungumze na Serikali ya Marekani ili kasi ya utoaji wa pesa hizo iongezeke kwa miaka iliyobaki; vinginevyo, lengo letu halitatumia tunavyotaka.

Mheshimiwa Spika, Waziri ametueleza kwamba, Pato la Taifa litakua kama ifuatavyo: 2008 asilimia 7.8, 2009 asilimia 8.1, 2010 asilimia 8.8 na mwaka 2011 asilimia 9.2; kama hiyo ni kodi vizuri, lakini naomba tueleze ni formula gani ambayo Waziri ameitumia kuonyesha kwamba, Pato la Taifa litakua hivyo alivyoonyesha? Tuna hakika gani kwamba, bei za mafuta, chakula na hali mbaya ya hewa, hazitaathiri mwenendo huo wa Pato la Taifa?

Ahsante sana. Naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI SEIF ALI IDDI: Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia Hotuba ya Bajeti iliyowasilishwa tarehe 12 Juni, 2008 kama ifuatavyo:-

Kazi ya kuleta mahusiano kati ya Tanzania na nchi za nje siyo tu iko katika ngazi ya Taifa, lakini hata Taasisi mbalimbali zinaweza kusaidia kuimarisha uhusiano wetu na nchi za nje, kwa Taasisi hizo kuimarisha uhusiano na Taasisi za nje.

Baadhi ya shule nchini zina uhusiano na baadhi lya shule za nchi za nje. Katika hatua hiyo, shule hizo za nje huwaletea wanafunzi wenzao nchini, zawadi za vifaa vya kuwasaidia katika masomo yao kama vile vitabu, sare, baiskeli na vifaa vingine kama hivyo, vinavyoweza kutumiwa na wanafunzi. Vifaa hivyo vikiletwa huwa *addressed* kwa shule husika moja kwa moja. Lakini kwa sababu anayesimamia mchakato huo ni Mbunge, hulazimika kuvishughulikia vifaa hivyo ili vifike kunakohusika. Matokeo yake, vifaa hivyo hulipishwa kodi na Mbunge ndiye hulazimika kulipa kodi hiyo.

Ninashauri vifaa kama hivyo visamehewe kodi ili kuimarisha uhusiano kati ya shule zetu na shule hizo za nje. Uhusiano huo huanzishwa kwa *initiative* ya Mbunge ili wanafunzi wetu pamoja na walimu wao wawe na mwamko wa kuwa na urafiki na wenzao wa nchi za nje, ikiwa ni pia kutekeleza sera ya mambo ya nje ya kuimarisha uhusiano na nchi za nje katika kila ngazi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake yote, kwa Hotuba nzuri ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2008/09. Kwa ujumla Bajeti hii ni nzuri.

Suala la ukuzaji wa uchumi nchini mwetu ni kipaumbele cha kwanza. Wananchi wanapaswa kushirikishwa kwa kuwapa hamasa ya kutosha, kuweka mazingira mazuri kwa wananchi na wawekezaji wa nje.

Mheshimiwa Spika, malengo tunayojiwekea ya kujenga uchumi ni madogo mno. Tunaambiwa uchumi wa Angola unakua kwa asilimia 21 kutokana na mafuta na madini. Vivyo hivyo, Botswana. Sisi unalenga asilimia saba hadi nane; ni ndogo sana. Nashauri tulenge 10% hadi 12% ifikapo mwaka 2010, tunayo madini (dhahabu na gesi kwa wingi, matarajio ya mafuta na shughuli nyingine za uchumi. Tunayo kila sababu, kulenga zaidi ya asilimia zaidi ya kumi mpaka kumi na mbili.

Mheshimiwa Spika, kadiri madini yetu yanavyochimbwa na kuelekea kupungua na hatimaye kwisha, tuone yanaacha nyuma alama ya kudumu, hususan barabara za lami nchi nzima (barabara za kisasa). Pia tuone mtandao zaidi wa reli unajengwa ukiacha hata kukarabati na kuendeleza mtandao uliopo.

Tumebaki tu kusema barabara na reli tulizonazo hazitoshi kuleta maendeleo, lakini hatusemi wala kuonyesha nini tufanye ili kujenga barabara na reli haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, uwezo (*capacity*) wa watumishi katika Sekta za Kipaumbele kama Elimu (Walimu), Afya (Madaktari na Manesi), Miundombinu ya Barabara (wahandisi na wengineo) na kadhalika, ili kufanikisha majukumu na malengo ya Serikali uongezwe. Waongezewe pia motisha, ikiwa ni pamoja na mazingira mazuri ya kazi; kuwe na *compensation package* nzuri.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa changamoto zilizoko mbele yetu mojawapo ni miundombinu ya barabara. Wananchi wanajiuliza juu ya matokeo ya nyongeza ya Sh. 100 kwenye *fuel levy* mwaka jana kwamba, kungekuwa na *full maintenance budget* ya barabara lakini hali haifanani. Tatizo kubwa katika sekta hii ni uwezo mdogo wa *construction industry* katika eneo la upatikanaji wa vifaa/mitambo ya ujenzi. Kwa nini Serikali inashindwa kuwadhamini *contractors* au wakandarasi ili wakopeshwe mitambo yote ya msingi waweze kujenga uwezo wao wa kujenga barabara zetu?

Mimi naamini mazingira ya kuwakopesha *contractors* yakiwekwa vizuri, yakirahisishwa, hakika malengo yetu ya kuboresha/kujenga barabara zetu yatafanikiwa. Katika hatua hii, napenda kufahamu ni lini sasa Barabara Kuu ya Kaskazini (*The Great North Road*), sehemu ya Minjingu – Bababi – Dodoma – Iringa itaanza kujengwa? Naomba Serikali ifanye kila liwezekanalo ili kuanza kujenga barabara hii kabla ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha. Ahsante sana.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini ni nyeti sana na mpaka sasa bado nchi yetu haijaweza kutumia fursa ya kuwa na migodi ya madini ya aina tofauti hapa nchini kuliongezea pato Taifa letu.

Tuache kusamehe kodi kwa wawekezaji wenye migodi, kwa sababu wanapata faida kubwa na Serikali inapoteza mapato wakati nacho ni chanzo kimojawapo cha mapato ya nchi. Mbona Botswana uchumi wao kwa kiasi kikubwa unategemea madini waliyo nayo; je, Wizara inaweza kutueleza sababu zipi za msingi, zinazosababisha madini kutokuwa sehemu ya Pato la Taifa kwa kiwango kikubwa? Je, Serikali haioni haja ya kuangalia uwezekano wa kutowafutia kodi wawekezaji katika migodi?

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inabidi iwe makini hasa katika kutafuta vyanzo vingine vya mapato, ikiwemo misitu, uvuvi na shughuli za kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi hata ikiwemo Marekani, hawachimbi mafuta ya petroli na kadhalika, lakini kuna utaratibu wa kutoa ruzuku kwenye mafuta ili kuleta unafuu kutoka maisha yao ya kila siku na hadi kupunguza gharama za uzalishaji. Umeme pia ni anasa katika nchi yetu kwani gharama ni kubwa, hali inayosababisha uzalishaji viwandani kuwa juu na bidhaa kupanda sana. Sioni sababu ya Serikali ku-*maintain* kodi ya mafuta ya mwaka 2007/08. Serikali ilitakiwa itafute mbinu ya kupunguza kodi katika mafuta, kwa kuweka ruzuku katika mafuta ili kuleta unafuu wa maisha ya Mtanzania yanayopanda kila kukicha.

Inashangaza kuona Serikali inasamehe kodi kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, inapoteza mapato bila sababu wakati pesa hiyo ingekuwa na uwezo wa kutoa ruzuku kwa mafuta na umeme. Vilevile ingekuwa imepata mapato makuu, tungepunguza utegemezi kwa kiwango kikubwa katika Bajeti ya Maendeleo, ambayo kwa asilimia 100 inatokana na msaada kutoka nje na mkopo. Katika hotuba yake Waziri, nanukuu katika ukurasa wa 21 amekiri kuwa: “Upo wasiwasi kwamba, misaada ya mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo haitapatikana kama ilivyoahidiwa kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali.” Changamoto hii itaondolewa ikiwa tu Serikali itapunguza misamaha ya kodi na kuleta mabadiliko ya sheria yaliyowekwa, yanayotoa hitaji la kusamehe kodi kwa 50% ili mapato hayo yajenge nchi.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kuona 2005/06 makusanyo yalikuwa Sh. 883.6 bilioni wakati misamaha ya kodi ilikuwa Sh. 385.4 billioni (44%) ya mapato yote; hii ni aibu. Hata ukiangalia 2006/07 makusanyo Sh. 1132.4 billioni, misamaha bilioni 359 sawa na (32%). Kinachoshangaza zaidi ni upande wa Zanzibar, makusanyo bilioni 20.4 na misamaha 19.6 bilioni, sawa na 96% ya mapato yote. Serikali iache michezo ya kuigiza, izingatie hayo na sheria iletwe haraka Bungeni kubadilisha hilo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali haiku-*include* pesa za *EPA* zinazorudishwa. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atupe sababu ya msingi ya kutojumuisha pesa za *EPA* katika Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ni kawaida kwa Serikali kufanya semina nyingi mwisho wa mwaka wa bajeti, ambazo nyingine hazina msingi ili mradi tu kupata njia ya kutumia pesa zilizobaki. Kwa nini fedha hizo zisirudishwe Hazina ili ziingie katika bajeti ya mwaka unaofuata? Mfano, Mkoani Kagera katika Halmashauri kama sikosei, Halmashauri ya Bukoba Vijijini, Mwenyekiti wa Halmashauri na familia yake, wametumia bajeti iliyobaki kusafiri kuelekea Marekani, kusindikiza kikundi cha ngoma.

Katika Mikoa, Halmashauri zetu nyingi ni jambo la kawaida kwa viongozi kusafiri kwa ndege kwenda mikutanoni, wakati huo huo magari yao hutangulia pamoja na madereva; hivi haya sio matumizi mabaya ya Serikali? Kwa nini Serikali isikodi usafiri mwingine wa basi kutoka *airport* kwenda kwenye mikutano hiyo ya siku moja au mbili na kuacha matumizi mabaya; kwani mfano, *RC*, *DC*, *DAS*, Mkurugenzi wa Halmashauri, Meya au Wenyekiti wa Halmashauri kila mmoja anatanguliza gari na dereva wake; hizo pesa zinatoka wapi kwa ajili ya mafuta, spea na posho ya dereva; je, hayo si matumizi mabaya ya Serikali?

Hili si ngazi ya mikoa peke yake, hata ngazi ya Serikali Kuu, oanisha hilo na viongozi hao kusafiri kwa mtindo huo kutoka Kigoma – Dar es Salaam, kiasi gani kinapotea?

Mheshimiwa Spika, namtaka Mheshimiwa Waziri au Serikali itueleze shilingi bilioni tano za kufanikisha Mkutano wa Sullivan zilitoka wapi wakati Bunge halikupitisha?

MHE. SABELNA S. MWAIJAGE: Napenda kuchangia Wizara hii kwa sababu nyingi tu; mimi nikiwa Mbunge wa Kagera, bajeti hii sioni kama inamnufaisha mwananchi wa chini, bali inawanufaisha walioko mijini kwa sababu zifuatazo:-

Kitu cha kwanza, kuhusu mkulima; bajeti zinazotolewa zina unafuu gani kwa mkulima? Bajeti hii ni kilio kitupu kwa wakulima. Wabunge tunapigia kelele mambo yafuatayo: Wakulima, Wafugaji, Ajira, Elimu, Matibabu; kwa nini Serikali isijitahidi kuangalia vitu hivi? Huku ni kujidanganya sisi wenyewe, pamoja na wakulima wetu. Rasilimali tunazo nyingi za kuweza kupandisha uchumi wetu, lakini Serikali haijawa makini na vyanzo hivyo.

Tutaipitisha bajeti hii; sijui kama Bunge linajua mapato yake, mimi sikulielewa vizuri jedwali linalohusu mapato. Pamoja na hayo, naona uwezekano wa kupunguza kodi upo sana, tukiendelea hivi tunawaumiza wananchi wetu. Kitu kinachosikitisha ni kuona uchumi au bajeti yetu kila mwaka inagetemea kwenye vinywaji tu. Tuseme ndiyo vinaangusha uchumi au vinapandisha; je, Watanzania wakiamua kutotumia vinywaji tutaegemea wapi?

Kuhusu mafuta inasikitisha, unakuta kila mkoa una bei moja Tanzania nzima; kwa nini kila wilaya na mkoa wasiwe na bei zao? Huu nao ni upungufu, Serikali haipo makini na wafanyabiashara ndio maana kila mmoja anajiwekea bei anavyotaka. Hii si kwa mafuta tu, pamoja na bidhaa nyingine. Kwenye mitandao niliona masuala ya kilimo yapo tofauti kabisa na bajeti hii, pamoja na hayo Sekta ya Kilimo haiendi vizuri, kwa sababu utaalam pamoja na mitaji au kukosa sehemu ya kukopa hasa Mkoa wa Kagera uliosahaulika, mara kwa mara kwenye bajeti za miaka mingi sana, suala la mafuta ninalilalamikia sana, kwa ajili ya mwananchi wa Kagera. Vifaa vya ujenzi Kagera ni tatizo kwa kuwa mafuta yanaleta tatizo.

Wawekezaji wanaokuwa kwenye nchi yetu, wawe wanatozwa kipato kikubwa, wakishaingia wanapata mapato makubwa ambayo hufaidi nchini kwao wakati sisi hunabaki na umaskini.

Ninapenda kuiuliza Wizara ya Maji kuwa hivi zinazotengwa zinafanya kazi kama ilivyopangwa; pesa zinazokwenda kwenye Mradi wa Bwawa la Manchira Serengeti, zinafanya kazi gani miaka yote 31?

Mtoto aliyezaliwa wakati mradi huu unaanza sasa ni Mbunge; hizo pesa zingeenda Mkoa wa Kagera kutengeneza Uwanja wa Ndege au kumalizia Barabara ya Kigoma Rushahunga. Naomba kuuliza pesa zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya Wizara ya Maji hasa za Bwawa la Manchira ziko wapi?

Mwisho, naiomba Serikali; bajeti zote zinazotengwa kwa ajili ya miradi yoyote, uwepo ufuatiliaji mkubwa sana sio kuiachia Wizara tu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, tayari nimeshatoa maelezo yangu kwa kuzungumza na hata kwa kuandika pia. Nalazimika kuandika tena ili nipate ufafanunuzi juu ya jambo lifuatalo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nimefanya mkutano katika kata za Nambinzo, Itaka, Halungu, Msiya, Igamba na Isansa. Bahati mbaya sana, maeneo yote hayo wafanyabiashara hasa wa maduka, huzikataa sarafu za shilingi tano, kumi na ishirini kwa madai kwamba hazitumiki tena!

Naiomba Wizara itoe tamko kuhusu matumizi ya sarafu hizo na hatua za kuchukua kwa wanaozikataa na kama zimeonekana ni kero; kwa nini basi Wizara isiziondoe kwenye mizunguko?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, katika hoja hii naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake ambayo ndiyo dira ya maisha ya Mtanzania.

Pamoja na juhudi kubwa za Mheshimiwa Waziri za kuhakikisha kwamba, hotuba yake ya Bajeti inampa matumaini kila Mtanzania anayeishi Tanzania, lakini Watanzania walio wengi, hasa wale walio vijijini, wamekata tamaa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu bado bajeti haikumpunguzia ukali wa maisha Mtanzania maskini, mwenye kipato cha chini, hasa ukizingatia kwamba, kilimo ambacho ndio uti wa mgogo wa maisha na taifa kwa ujumla, hakikutendewa haki.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuangalia umuhimu wa pembejeo, kwanza, tungewatafutia wananchi nyenzo kama vile matrekta ili kuondokana na ukulima wa zamani wa majembe ya mkono. Hivyo, asilimia kubwa ya bajeti tungeipeleka kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, elimu ndio msingi wa maisha ya binadamu. Hivyo, pamoja na kutengewa asilimia kubwa kidogo ya bajeti, lakini elimu inayotolewa bado haitoshelezi kutokana na Serikali kutojikita hasa katika kusimamia elimu bora na sio bora elimu. Tunajenga mabanda mengi ambayo hayana nyenzo madhubuti kama vile walimu stahiki, ambao wanawezeshwa vizuri ili wamudu kuifanya kazi yao kwa upendo na uadilifu, maabara zetu hazijitoshelezi na hivyo kukosa wataalam wa sayansi waliobobea, jambo ambalo linaathiri taifa.

Pamoja na Serikali kufanya bidii ya kuhakikisha maji safi na salama yanapatikana, lakini wananchi walio wengi na hasa wale waishio vijijini, bado wanatumia maji yasiyo salama; maji ya mito, ambayo wanakunywa mifugo na machafu kupindukia na hivyo kupata magonjwa mbalimbali na pengine hata kupoteza maisha. Hilo nalo huchangia zaidi mzigo kwa Sekta ya Afya, ambayo nayo huduma zake ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania sio maskini ila utendaji wetu ndio maskini, kwa vile hatuna dhamira njema ya kuwapatia maisha bora Watanzania. Mipango ipo madhubuti na uwezo upo, lakini utendaji haupo. Hivyo, bajeti bado haijamkomboa Mtanzania wa kipato cha chini na badala yake imemkandamiza zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwananchi wa kijijini hajui hata kutumia hiyo gesi ambayo inatajwa, bei ya mafuta iko juu, umeme uko juu, kipato chake ni kidogo mno; je, tutamsaidiaji?

MHE. DORA H. MUSHI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa bajeti nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Bajeti hii imelenga kuwakomboa wanyonge, yaani wenye kipato cha chini, kutokana na sera sahihi za Chama cha Mapinduzi. Bajeti hii imegusa maeneo mengi, ambayo kwa kiwango kikubwa, yamejibu baadhi ya kero za Watanzania.

Uamuzi uliochukuliwa na Serikali wa kutokutoza kodi za mafuta, utatoa afueni katika maeneo yote ambayo kwa kiwango kikubwa, athari zake zinalenga sekta nyingine. Kwa mfano, bei ya mafuta ikipanda; gharama za chakula, usafiri na kadhalika nazo zitapanda. Matokeo yake, Watanzania wenye kipato cha chini, ndio wanaoathirika sana.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei umeathiri watu wengi wenye kipato kidogo. Kundi hili ni lile ambalo kipato chake hakiongezeki au huongezeka kidogo sana, kukilinganisha na kasi ya ongezeko la mfumko wa bei za vitu. Kwa hiyo, uwezo wa Watanzania hao hudidimbia mwaka hadi mwaka, kwa kiasi kikubwa maisha yao yameathirika; kwa mfano, wale wastaafu wanaoishi kwa pensheni, wafanyakazi au waajiriwa katika Sekta Binafsi na Serikalini.

Mheshimiwa Spika, mipango ya uwekezaji rasilimali huathirika na mfumko wa bei kwa kuwa ni vigumu kupanga mipango ya muda mrefu. Pia mabenki ya ndani ya nchi kutokuwa na amana za kutosha na hivyo kushindwa kutoa mikopo kwa wawekezaji. Vilevile Mabenki yanalazimika kutoa amana kwa riba ya juu, hali hii husababisha kupungua kwa ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei ulipanda na kufikia wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2007. Aidha, katika kipindi cha mwezi Januari hadi Aprili, 2008, ulipanda kutoka asilimia 8.6 hadi 9.5. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa bei za chakula, kulikosababishwa na mavuno kidogo kutokana na kukosekana kwa mvua za vuli katika robo ya mwisho ya mwaka 2007. Ongezeko la bei ya nafaka katika Soko la Dunia, ambapo baadhi ya nafaka zinatumiwa kuzalisha mafuta ya kuendeshea mitambo na gharama za uzalishaji kutokana na kupanda kwa bei za petroli na dizeli katika Soko la Dunia; kwa mfano, bei za petroli na dizeli zilipanda kutoka wastani wa Sh. 1,329 na Sh. 1,287 mwezi Mei, 2007 hadi wastani wa Sh. 1,282 na Sh. 1,720.2 mwezi Aprili, 2008.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inatakiwa kuchukuwa hatua za makusudi ili kupunguza mfumko huu wa bei. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kupitia upya kodi za ushuru wa mafuta (*review of road fuel tax*), kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha na kuangalia njia mbadala ya kupunguza kodi za kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Dira ya Taifa (*National Vision 2005*), kulenga kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini, ambapo malengo ni kufikia asilimia 6.9 ya Pato la Taifa ifikapo 2010; hata hivyo, ukuaji wa Pato la Taifa ulionyesha kuimarika na kukua kwa asilimia 6.8 mwaka 2005 na kuanza kushuka na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2007. Ukuaji huo sio mzuri hata kidogo, kwa kuwa hautaweza kuchangia kupungua kwa umaskini. Matumaini ya ukuaji wa uchumi yatatatikana ikiwa mkazo utatiliwa katika kukuza na kuongeza Tija katika Sekta zote, hususan Kilimo Viwanda, Madini Na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kuipongeza *TRA* kwa kazi nzuri wanayofanya katika kukusanya kodi, hususan *VAT* kwa bidhaa za ndani na zinazolingizwa kutoka nje, ongezeko la kodi ya mapato, pamoja na ushirikiano wa walipa kodi wakubwa. Aidha, mabadiliko katika usimamizi wa kodi, yamechangia kuongezeka kwa makusanyo ya kodi. Jambo la kusisitiza hapa ni juu ya matumizi mazuri ya fedha hizo za makusanyo, hasa ikizingatiwa kuwa, Serikali inatarajia kupunguza kiwango cha utegemezi kutoka asilimia 42 hadi asilimia 34. Vilevile Serikali pia inadhamiria kugharamia matumizi yake ya kawaida kwa asilimia 100. Matumizi yasipodhibitiwa, ufikiaji wa malengo yetu utakuwa ni mgumu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. FELIX N. KIJIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja iliyotolewa na Waziri wa Fedha na Uchumi kama ifuatavyo:-

Kuhusu kuhamisha Kitengo cha Ununuzi kutoka Wizara ya Miundombinu ni hatua ambayo naiunga mkono moja kwa moja kwamba, Watumishi wa Idara hii wamekuwa ni wezi wakubwa kwa kukubaliana na watoa huduma. Hata hivyo, wakati hatua hiyo inachukuliwa ni vyema pia kuwa na watumishi ambao ni waaminifu huko Wizara ya Fedha na Uchumi. Aidha, hali hiyo ya wasimamizi wa manunuzi Serikalini kuwa wakijihusisha na wizi, wanajifunza kutoka kwa wanunuzi ambao wapo kwenye mashirika binafsi, ambao ndio wamekuwa mstari wa mbele katika kufanya manunuzi hewa na kuwawezesha kuwa wadanganyifu kwa kushirikiana na watoa huduma. Hivyo, ninashauri kuwa, mbali na hatua nzuri za Serikali za kukabiliana na hali hiyo, pia watu wenye mashirika binafsi waelezwe ulaghai ambao umekithiri kwa kufanywa na maofisa manunuzi wao.

Vipengele vinavyohusu maendeleo ya maji, barabara na umeme, ninashauri vipengele viwe vinapewa kipaumbele kwa sababu ni vitu vinavyogusa maisha ya kila Mtanzania. Hapa nina maana kuwa, bajeti yake iwe ikipangwa mapema na kwa kiwango cha juu. Hata hivyo, katika kupitia Kitabu cha Bajeti, imeonekana fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hizo hazitatosheleza mahitaji ya maeneo ambayo hayana huduma hizo. Aidha, wakati zikingojewa fedha za wafadhili katika kutatua ama kuongeza uboreshaji wa huduma hiyo kwa wananchi, ningeshauri ziwe zikitengwa fedha zetu wenyewe na kuanzisha miradi hii.

Kupanda kwa gharama za simu za mikononi, ninashauri *TRA* wapewe maelekezo ya kusimamia zoezi zima ikiwa ni pamoja na kuwatoza kodi itokanayo na kile wanachokipata.

Bajeti ya Serikali, mbali na kuwa nzuri, lakini haikuzingatia uboreshaji wa usafiri kwa vyombo vya dola. Hivyo, ni dhahiri kwamba, sasa hivi suala la ujambazi limekuwa sugu na hasa kwa mikoa ile ya pembezoni. Ninashauri vyombo hivyo vinunuliwe magari ya kutosha ili kupambana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. HEMEDI MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Spika, ni vyema nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na Manaibu wake, kwa umahiri wao wa kufanikisha azma yao ya kutaka kuwakomboa Watanzania katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, naomba nitoe mchango wangu katika hotuba hii, pale panaposema Hali ya Usawa wa Jinsia Tanzania (*TGNP*). Inaonekana lengo la *TGNP* lilianza 1993, likiwa na nia ya kufanya uchambuzi wa nafasi ya wanawake na hali ya usawa na haki yao katika jamii ya Kitanzania ikilinganishwa na ya wanaume. Suala la usawa ni zuri ila linahitaji mtazamo ukilinganisha na imani za kidini.

Mheshimiwa Spika, asili ya Watanzania ni wakulima. Historia ya kilimo chetu ilianza kwa jembe la mkono. Watanzania wamejitawala takriban huu ni mwaka wa arobaini na tano. Serikali imemfikiria nini mkulima huyo ambaye hadi leo ni mkulima na anatumia jembe la mkono?

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ifahamu kukua kwa kilimo katika nchi yetu, kunahitaji mambo kadha kama vile kuwepo kwa soko la uhakika, mbolea, kilimo cha kisasa na ikiwezekana mkopo wa muda mfupi.

Tanzania ni nchi iliyozungukuwa na Bahari, pamoja na Maziwa. Samaki katika Bahari zetu na Maziwa ni wengi. Je, Serikali imemsaidia nini mvuvi huyo ili atokane na uvuvi usio wa uhakika? Kukosekana kwa mapato makubwa hutokana na uvuvi wetu kuwa mdogo, kulingana na samaki tulionao. Serikali yapaswa kuwawezesha wavuvi wetu ili waweze kujipatia pato.

Serikali inaweza kujipatia kipato kikubwa kutokana na umeme, lakini mpaka leo umeme wetu sio wa uhakika na wa gharama kubwa jambo ambalo hupelekea mtumiaji kushindwa kulipa na kudunduliza madeni yasiyolipwa.

Mheshimiwa Spika, kiujumla hali ya uchumi kwa wananchi wetu ni mbaya. Tafiti mbalimbali za Kitaifa zinaonyesha hali ya uchumi imeendelea kukua nchini. Tatizo ni kwamba, kukua huko bado hakujaweza kuboresha maisha na ustawi wa mwananchi wa kawaida vijijini na mijini. Kutokana na hali hii, kuna baadhi ya Watanzania hawana uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Spika, bajeti inaonyesha bado haijamsaidia mwananchi wa kawaida. Kikubwa kilichotendeka ni mfanyabiashara mkubwa kusaidiwa na mdogo kushindwa. Wachache ndio wanaoingiza na kutoa biashara. Mfanyabiashara wa kilimo, ambaye ndiye muinua hali ya nchi, atabaki kumuuzia mfanyabiashara mkubwa ndizi, embe, chungwa na kadhalika kwa bei duni. Lakini panga, kisu, jembe na kadhalika, vitabaki kuwa bei juu, kwa sababu vitu hivi vimeletwa na mfanyabiashara mkubwa.

Naiomba Serikali imfikirie mkulima na kumwezesha kuwa na bei nzuri. Ahsante.

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kuwapongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote, walioshiriki kutayarisha hotuba hii ya makisio kwa mwaka wa fedha 2008/09; ingawa ni mara ya kwanza Mheshimiwa Waziri kutoa Hotuba ya Bajeti Bungeni, amejitahidi sana na anahitaji pongezi nyingi.

Natoa pongezi nyingi kwa Bajeti hii, ambayo imeonyesha kuanza kupunguza nchi kuendelea kutegemea misaada kutoka nje, hasa kwa fedha za matumizi ya kawaida. Kwa upande wangu, nataka kuchangia juu ya suala moja ambalo linahusu Serikali kutoweka kodi ya mafuta ghafi ya kula (*Crude Oil*), ambayo ipo katika kifungu cha 53(vii) ukurasa wa 45. Hili ni jambo lisiloweza kukubalika kuletwa tena Bungeni, kwa sababu Wizara inajua fika kuwa, hakuna mafuta ghafi ya kula Duniani, isipokuwa mafuta yaliyosafishwa nusu (*semi processed*). Jambo hili sisi Wabunge tunashindwa kulielewa kwa nini Serikali inaleta jambo ambalo sote tulikwisha kukubaliana kuwa, lazima kodi ilipwe.

Serikali iliwahi kutuma ujumbe wa Makatibu Wakuu, Ofisi ya Rais; Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda; na Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, kwenda Malaysia na Singapore, ambako wenye viwanda huagiza mafuta. Ilithibitika wazi kuwa, nchi hizo haziuzi nje ya nchi mafuta ghafi (*Crude Oil*) ya kula.

Suala la kodi hii ya mafuta ya kupikia liliwahi kugharimu wadhifa ya Mheshimiwa Mbilinyi wakati alipokuwa Waziri wa Fedha, ambapo alitoa msamaha. Kwa upande mwingine, kitendo cha kufuta kodi hizo kitaua kilimo cha mbegu za mafuta ya kula nchini na kuua viwanda vidogo vidogo vya mafuta ya kula.

Kwa upande wangu, ninapendekeza siyo tu kutosamehe kodi hiyo kama Wizara inavyotaka, bali mafuga ghafi (*Crude Oil*) yafutwe kabisa katika orodha ya mafuta, kwa sababu hakuna aina ya mafuta hayo kutoka Malaysia, Singapore wala Indonesia.

Ni wajibu wetu kulinda wakulima wetu na viwanda vidogo. Tunahitaji kuwa na mpango wa kujitegemea kwa mafuta ya kula, badala ya kuendelea kuagiza bidhaa hiyo kutoka nje. Umeanza vizuri, achana na suala la mafuta ghafi; lisikuchafue bure.

Natoa tena pongezi zangu kwa hotuba nzuri.

MHE. GAUDENTIA M. KABAKA: Mheshimiwa Spika, naipongeza Bajeti hii na hivyo, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nampongeza Waziri, Mheshimiwa Mustafa Mkulo; Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Jeremiha Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi.

Nitatoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

(a) Naona kama vile Sekta binafsi tumeiachia majukumu mengi sana ya Sekta ya Kilimo, ikiwemo suala la pembejeo (mbolea, matrekta na kadhalika), viwanda vya usindikaji na wakati huo huo, hatuna uhakika kuwa utekelezaji wake utakuwa mzuri ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Nashauri Serikali inunue matrekta ya bei nafuu ili wakulima wayanunue au wakope na kuyatumia katika kuinua kilimo. Bila kufanya hivyo, itakuwa si rahisi wakulima hasa wenye uwezo mdogo kule vijijini, kuweza kukopa/kununua matrekta na vifaa vingine kutoka kwa wafanyabiashara wanaotaka faida kubwa hata kama ushuru umeondolewa kwa vifaa hivi. Kilimo cha trekta ndiyo pekee kitakachotuondoa kwenye hali mbaya ya uchumi na chakula nchini.

(b) Shule za Sekondari hasa za Bweni na Vyuo vya Ualimu, zinazidi kuongezeka na pesa inayotolewa kwa ajili ya chakula na vifaa vya kufundishia kila mwaka hazitoshelezi

kufanya hiyo. Hali hii inalazimisha wakuu wa shule/vyuo, kukiuka taratibu za fedha kwa kuagiza chakula kabla ya kupata fedha kutoka Serikalini, hali inayozalisha madeni makubwa sana. Aidha, hali hii inasababisha kuleta vurugu mashuleni, kwani wakati mwingi wazabuni hugoma kupeleka huduma hasa chakula mashuleni. Ili kuondoa/kupunguza tatizo hili, nashauri Hazina iwe inatoa fedha kulingana na idadi ya wanafunzi waliopo mabweni, kwa *unit cost* itakayotolewa na wataalam wa Wizara ya Elimu. Bila kufuata *unit cost* ya kila mwanafunzi, hakuna muujiza unaoweza kufanywa na Wizara ya Elimu, Mkuu au Wakuu wa Shule ila matatizo ya uvunjaji wa *financial regulations* na vurugu mashuleni vitaendelea kuwepo, jambo ambalo halipendezi kabisa.

Ili kuendelea kupata imani ya wananchi wetu kuhusu ahadi ya maisha bora kwa kila Mtanzania, nashauri kuwa, ahadi ya miradi ambayo haikutekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/08, itekelezwe katika bajeti ya 2008/09. Kwa mfano, malambo na visima vilivyoahidiwa na Wizara husika, mengine haijaguswa, kwa mfano, Lambo la Wegero Musoma Vijijini; wananchi walifurahi sana walipoona wataalam wameonekana kule wakipima lakini wakapotea hadi leo. Wananchi wale ambao wanaishi kwa kunywa maji ya madimbwi na wanyama wao, ambayo hupatikana wakati wa masika tu, hawaelewi kabisa kuona ahadi ile ya kupata lambo imeyeyuka.

Nashauri sana, mradi huu utekelezwe katika bajeti hii ya 2008/09, pamoja na miradi mingine ya aina hiyo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naunga tena mkono hoja hii, ni bajeti inayotekelezeka iwapo sote (Wizara), tutashirikiana pale ambapo tunalazimika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nawasilisha.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii, ili nichangie mada iliyopo mbele yetu.

Naomba kwa kuanzia, nitoe mchango wangu kuhusu suala zima la mafuta; ingawa Serikali haikupandisha bei ya mafuta, lakini bei ipo juu. Bado hapa hatujamsaidia mwananchi hususan aliyepo kijijini.

Mheshimiwa Spika, mwananchi kijijini au mlalahoi, bado ametwisha mzigo mzito. Kama tunavyotambua kuwa, kilimo ndio uti wa mgongo wa Watanzania, kusamehewa ushuru wa forodha kwenye majembe ya mkoni ni vizuri. Karne hii ya 21 ya Sayansi na Teknolojia na miaka 47 ya uhuru bado Watanzania tunatumia majembe ya mkono, hili linasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuihoji Serikali; je, kutokana na hali duni ya wananchi wetu, hususan wakulima wanaotumia majembe ya mikono; je, Serikali haiwezi kuwasaidia wakulima hao dhaifu, kuwalimia mashamba yao kwa kutumia matrekta? Matrekta haya yangeweza kutumiwa na wakulima wetu wadogo wadogo, kwa kuwalimua mashamba yao na kunyunyizia dawa ili waweze kupanda mazao mbalimbali na baada ya mavuno, watauza mazao yao na baadaye kuweza kulipa gharama zilizotumika kwa matrekta yaliyolima.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alitueleza kuwa, mafuta mazito yanayotumika kama nishati ya kupikia (kwa mfano, moto poa), ili wananchi wahamasishwe

kutumia mafuta hayo badala ya kuni na mkaa kwa matumizi ya nyumbani. Je, ni Watanzania wangapi watakaokuwa na uwezo wa kununua mafuta hayo hali ya kuwa hali zao ni duni?

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda; Wilaya ya Tanga ilikuwa na Kiwanda cha Mbolea kilichojulikana kama *Tanzania Fertilizer Company*. Kiwandha hiki kilifungwa ghafla na eneo la kiwanda kupewa mwekezaji mwingine. Je, Waziri anaweza kutueleza sababu zipi zilizopelekea kufungwa kwa kiwanda hicho ambacho kilitoa ajira kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu unaweza kukua kwa njia mbalimbali, ikiwemo miundombinu yetu. Miundombinu ya reli toka Tanga – Dar es Salaam, Tanga – Moshi – Arusha ilisaidia sana katika kuinua uchumi kutokana na usafirishaji wa mizigo.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Tanga ingekuza sana Pato la Taifa kwa vile ingechukua mizigo ya kutoka bandarini kwenda Mikoa ya Kagera, Mwanza, nchi jirani za Kenya na Uganda na mikoa mingine, ambapo pato la nchi lingeongezeka kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, suala zima la UKIMWI; kwa kweli ni tishio na ni janga kubwa sana kwa mwananchi. Nchi wafadhili wanatoa fedha zao kupitia NGOs mbalimbali ili kuwasaidia walioathirika na tatizo hili. Cha kushangaza, fedha zinazopangwa kupelekwa kwa walengwa haziwafikii. Mfano kwa taarifa zisizo rasmi, kuna Wilaya zilizopelekwa fedha hizo lakini kiasi kilichokusudiwa sio kilichofika. Mfano Wilaya ya Ngara, matarajio shilingi milioni 30, lakini zilizopelekwa shilingi milioni 18; Biharamulo shilingi milioni 99 zilizopelekwa shilingi milioni 62; Rungwe shilingi milioni 124 zilizopelekwa shilingi milioni 48; na Kyela shilingi milioni 86 zilizopelekwa shilingi milioni 33. Hii ni kupoteza imani kwa wahisani wetu ambao wanatusaidia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vyanzo vingi vya maji tulivyonavyo, bado wananchi wameendelea kunywa maji ya kwenye mabwawa, wakishirikiana na wanyama. Kwa hali hii, bado tutaendelea kupata maradhi kutokana na kunywa maji ambayo sio safi na salama.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ya Fedha isaidie wananchi walau kila kijiji na kitongoji kiwe na bomba moja (kisima cha maji safi). Hili litawawezesha kupata maji safi ya kunywa na kutumia maji ya mabwawa kwa shughuli nyingine.

Tunao wataalam wa kutosha, ambao wanaweza kufanya utafiti na kugundua sehemu ipi bora ya kuweza kuchimba visima na kupata maji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Spika, ni vyema nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na Manaibu wake, kwa imani yao ya kutaka kumwondolea Mtanzania maisha duni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia hiyo, napenda kutoa mchango wangu katika hotuba hii. Naanza katika maeneo ya kilimo. Tukumbuke kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu na Watanzania walio wengi ni wakulima. Ukiangalia makadirio ya 6.4 juu ya kilimo, utaona bado mkulima hajaangaliwa. Mkulima wa leo, anayetumia jembe la mkono, tumfikirie atawezaje kuitumia ardhi kwa kilimo cha jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali iitupie jicho la rehema Wizara ili iweze kumsaidia mkulima ili atelezewe mambo yafuatayo: Apatiwe trekta, wataalam, mbolea, mada na soko la uhakika. Azma ya Serikali ni kumwondolea matatizo mkulima. Leo imefikia kuna mtu anayeitwa mlanguzi; huyu ni nani? Jibu lake utaona ni mfanyabiashara anayenunua bidhaa za wakulima kwa njia za panya. Huyu anakuja pale ambapo Serikali haikumwandalia mkulima bei.

Watanzania bado wanatumia uvuvi usio na tija, inafaa Serikali iwapatie zana za kisasa ili waukuze uchumi wetu. Kukosekana kwa utaalamu wa kileo juu ya uvuvi, husababisha kuwepo kwa uvuvi haramu; jambo ambalo hupelekea uharibifu wa mazao ya samaki.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya nchi yetu si ya uhakika. Uchumi wetu ili ukue, unahitaji kuwepo kwa miundombinu ya barabara na reli. Barabara nyingi ni mbovu, jambo ambalo hupelekea mkulima wa vijijini kushindwa kupeleka bidhaa zao sokoni. Kukosekana kwa barabara, kunasababisha walio wengi kukosa huduma muhimu pia mara nyingi, ajali za barabarani husababishwa na kuwepo na barabara mbovu. Pamoja na hilo ni vyema sasa Serikali iwachunguze madereva wasio na sifa.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanahitaji nishati ya umeme. Nchi yetu katika hili bado tuko nyuma sana, kwani umeme tulionao si wa uhakika na baadhi ya vijiji hawaujui umeme. Jambo ambalo hupelekea nchi kukosa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini ni muhimu sana, kwani jamii zetu zimejenga shule na vituo vya afya na vyote hivi vinahitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa kuthamini ongezeko la kipato cha nchi yetu kinachotokana na madini. Madini yetu mara nyingi husimamiwa na wawekezaji na pato kubwa hupata wawekezaji kuliko nchi yetu. Kwa vile kuna wachimbaji wadogo wadogo, ambao ni Watanzania ni vyema sasa watengewe maeneo yao ili waweze kujiajiri wenyewe na kujipatia maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kiujumla pamoja na uchumi wetu kukua, lakini tujue kuna Watanzania vijijini ambao hawana uhakika wa chakula chao kwa siku. Hivyo basi, Serikali inapaswa kuwaandalia maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naishia hapa. Ahsante.

MHE. AME PANDU AME: Kwanza, nimpongeze Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu siyo maskini, bali hatujajua mbinu za kutumia ili kupunguza umaskini kwa Watanzania. Tanzania zipo bandari nyingi hazitumiwi kwa ajili ya kuiletea nchi hii maendeleo. Iwapo nchi yetu itazitengeneza bandari zetu, hapa nchini Watanzania wataondokewa na umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika hili la kupunguza umaskini nchini, napenda kuishauri Serikali iwaelimishe vijana kuwa, wajiunge katika vikundi vya ushirika (SACCOS) ili Serikali iweze kuwapa huduma za misaada kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo; iwapo kitapewa kipaumbele hapa nchini, Watanzania watakwamka na balaa hilo la umaskini. Serikali itafute mbinu za kueneza pesa zienee mpaka vijijini, kwani hapa Tanzania mzunguko wa pesa upo sana katika miji mikuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ijitahidi kwenye miundombinu hasa ya barabara na reli, kama hali hii itafanikiwa kuikamilisha au hata kama kupunguza tatizo hilo kwa kiasi kikubwa, nchi hii itaondokewa na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tunazo rasilimali za kila aina za kuiletea maendeleo nchi hii; tatizo ni nini au tatizo hatuwatumii wasomi wetu vizuri?

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei unarudisha nyuma maendeleo, pia hali hii inawavunja moyo wananchi katika hali ya kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali itadhibiti vizuri hali hii ya mfumko wa bei za bidhaa, Watanzania wanalijua la kufanya kwenye mambo ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, umeme ni miongoni mwa vichocheo vya maendeleo nchini mwetu. Nyaja hii ipo nyuma sana, iwapo Serikali itasogeza huduma hii kwa wananchi; kwa vyovyote wananchi hawa wataondokewa na hali mbaya ya maisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu, ambaye amenipa uzima leo hii na kuniwezesha kupata wasaa wa kuchangia walau kidogo kuhusiana na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2008/09 kama mtu ataiangalia juu juu tu, ataona inakidhi haja na ambayo imemlenga mwananchi wa kawaida. Ukweli ni kwamba, bajeti ina upungufu mwingi wa kuweza kumnusuru mwananchi na kumpa matumaini ya maisha bora.

Mheshimiwa Spika, kwanza, bajeti hii haionyeshi vyanzo vya kuaminika, ambavyo vinaweza kuchaniga mapato ya Serikali. Hatuwezei kutegemea kodi kutokana na sigara, vinywaji kama bia na soda, kwa maendeleo ya nchi. Kwa maana hiyo, shilingi 7.2 trilioni haziwezi kukidhi kiu ya kuleta maendeleo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sana ushauri juu ya vyanzo vipya vya mapato walivyovitoa wenzetu upande wa Upinzani viangaliwe na vitakavyoonekana vinaleta tija, basi vifanyiwe kazi, kwani sote nia ni moja tu ni kuweka mazingira mazuri ili mwananchi wa kawaida anufaike na afaidike.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeainisha vyanzo takriban 21, ambavyo vinaweza kukusanya mapato ya ndani zaidi ya shilingi trilioni 5.7, ambapo pamoja na misaada na mikopo kutoka nje, makadirio ya bajeti yangefikia karibu shilingi trilioni 8.166.

Mheshimiwa Spika, tupende tusipende, kwa Tanzania bado kilimo ndio sekta muhimu inayotegemewa na wengi katika nchi hii.

Kwa sekta hii, kutengewa asilimia 6.4 tu ya bajeti, Serikali haijatenda haki. Wakulima wanahitaji mbolea kwa ruzuku au kwa bei nafuu, sote tunajua hali za wakulima wetu huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itueleze kati ya hizo shilingi 460 bilioni, zilizotengwa kwa kilimo ni kiasi gani zimetengwa kwa mbolea ya ruzuku, kwa kipaumbele kipi na kwa kigezo gani? Umefika wakati sasa Serikali itambue kwamba, kilio kikubwa cha wakulima ni uhaba wa mbolea na kutopatikana kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kundoa ruzuku kwenye majembe ya mkono ni kurudi nyuma sana. Hii ni sawa na kuwahamasisha wafanyabiashara walete nchini majembe hayo ambayo wananchi wengi wataweza kumudu kununua kwa wingi na hivyo kuyatumia; kweli ukulima huo utaleta tija katika karne hii ya 21?

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii, Serikali imenyamaza kuhusu suala zima la ama kupandisha au kushusha kodi kwenye mafuta ya petroli na dizeli. Ni vyema Serikali ipunguze kodi katika mafuta hayo ili kupunguza ukali wa gharama za usafiri na usafirishaji, ambako kutapunguza bei za bidhaa muhimu na kwa maana hiyo, kupunguza ukali wa maisha.

Mheshimiwa Spika, katika karne hii na kila siku zikiendelea, inadhihirika zaidi kwamba, matumizi ya simu si suala la anasa, bali ni suala muhimu sana, sio tu kiuchumi bali hata kijamii na maisha kwa jumla. Kwa hiyo, Serikali kuchukua hatua ya kupandisha kodi ya matumizi (muda wa maongezi), kutoka asilimia saba hadi kufikia asilimia kumi, haikutenda haki. Maana ukiangalia ni akina nani wanaotumia simu, utaona wengi wao ni wananchi ambao vipato vyao ni vya chini mno. Kama hivyo ndivyo ilivyo, huruma na hekima ya Serikali kwa wananchi wake iko wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo; Serikali itilie mkazo juu ya matumizi ya matrekta kwa kuwawezesha wafanyabiashara kuleta hapa nchini mbolea kwa wingi na kuanzisha viwanda vipya vya mbolea nchini.

Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta vyanzo vipya vya kuongeza mapato kama vilivyoshauriwa na Kambi ya Upinzani.

Serikali ipunguze ukali wa maisha ya wananchi wa kawaida kwa kupunguzia kodi ya mafuta ya petroli na dizeli. Vilevile Serikali ione umuhimu wa kuuzwa kwa Ndege ya Rais, ambayo itatuingizia fedha nyingi kwa maendeleo ya nchi na kumpatia Rais wetu *Presidential Helicopter*.

Mheshimiwa Spika, yote haya na mengine, yanawezekana kama ipo ile inayoitwa *good will*.

Ahsante sana. Naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kutoa tafsiri ya “chanzo cha maji” kwa vile tafsiri zitakuwa tofauti kutoka mahala hadi mahala, taarifa zitatofautiana kutokana na tafsiri zitakazotumiwa.

Serikali haionyeshi “*baseline status*” ya hali ya Mazingira ya Ardhi na vyanzo vya maji, ambao ni msingi (*basis*) ya uperembaji. Kuperemba (*monitor*), bila *baseline data*. Kwa hiyo, uperembaji unaofanywa hauna msingi na hauwezi kuwa na tija.

Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mazingira na Mikakati yake na kukuza uelewa wa wananchi juu ya uhusiano kati ya mazingira, umaskini na maendeleo endelevu katika mwaka wa fedha 2008/09, bila tafsiri inayokubalika ya chanzo cha maji na bila *baseline data* ni kuendeleza kazi isiyo na tija na haiwezi kuzaa matunda yanayotegemewa.

Misingi ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii katika Kipindi cha muda wa kati; nataka kuoanisha msingi huu na changamoto ya ongezeko kubwa la idadi ya watu na kuhoji kama ifuatavyo:-

(a) Kwa vile tumejifunza vya kutosha kutokana na ujenzi wa daraja la Mkapu katika Mto Rufiji jinsi ulivyochangia uharibifu na upotevu wa rasilimali misitu katika maeneo ya kusini mwa Tanzania;

(b) Kwa vile Serikali iko kimya na haitoi mikakati ya kushgulikia ongezeko kubwa la watu lisiloendana na uboreshaji wa uchumi;

(c) Serikali imeweka mkakati gani kuhakikisha kuwa uboreshaji wa miundiombinu vijijini hausababishi uvunaji holela wa rasilimali zetu (ardhi, mifugo, misitu) ili iwe endelevu na kunufaisha wananchi kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupeleka madaraka kwa wananchi; Serikali inatambua changamoto ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu yaliyohamishiwa kwao, wakati huo huo inapanga kuzipa Halmashauri majukumu makubwa zaidi. Je, kwa nini Serikali inazingatia uimarishaji wa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala, Wenyeviti wa Halmashauri na Mameya bila kujali uwezeshaji wa Wataalam na Watendaji wa idara mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, changamoto zitokanazo na bajeti; Changamoto moja ya msingi inayohusu Miradi ya Miundombinu ni upungufu wa makandarasi wenye uwezo, ujuzi, vifaa na uzoefu. Tatizo hili ni sugu zaidi Wilaya za pembezoni kama vile Ludewa. Haitoshi kusema tatizo hili linahitaji kuwekewa mikakati ya kuliondoa bila ya kuitaja katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Matumizi; katika ukurasa wa 30, kifungu cha 44(a), fedha za kilimo zitaelekezwa kwenye ruzuku na Hifadhi ya Taifa ya Chakula. Wakati naunga mkono kipaumbele hiki, nashauri Serikali izingatie yafuatayo: Bei za kununua nafaka zitangazwe mapema; viwango (tani), vya nafaka za kununua katika kila Mkoa na Wizara vitangazwe mapema; na umakini zaidi uzingatiwe katika kusambaza mbolea za ruzuku.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani; naipongeza nia njema ya Serikali ya kuzingatia hifadhi ya mazingira kwa kuondoa kodi ya mafuta mazito (moto poa) na gesi asilia ili kupunguza matumizi ya mafuta, mkaa na kuni.

Napenda kuhoji kama ifuatavyo:-

(a) Je, nishati mbadala ni gesi asilia na moto poa tu; kwa uchambuzi upi?

(b) Kwa nini makaa ya mawe hayajazingatiwa?

(c) Je, Wizara inajua kuwa kutoa kodi hakuwezi kuleta tofauti kwani ingawa moto poa yanaweza kuwa rahisi kununua, lakini kupika hilo moja kunahitaji moto poa mengi sana?

(d) Majiko ya moto-poa na gesi asilia hayajafanyiwa *promotion* hasa vijijini, la sivyo sera hii inalenga mijini tu.

(e) Serikali inajua kwamba nishati mbadala hii ni kwa ajili ya kupikia tu? Je, mbadala wa nishati kwa kupasha moto majumba (*heating*), hasa maeneo ya baridi kama nyanda za juu (pamoja na Ludewa) iko wapi?

MHE. JOB Y. NDUGAI: Naomba kupitia *The Finance Act, 2008, Part IV, Amendment of the Income Tax Cap. 332, Fungu la 12 on personal income tax rates, the new rates are exorbitant.*

Kwa mfano, *income* ya 4,320,000 hadi 6,480,000 kodi ni shilingi 468,000 *plus 20% of amount in excess of shillings 4,320,000.*

Jamani, *say* mtu ana *income* ya 5,000,000 maana yake atakatwa $468,000 + 136,000 = 604,000$? Huu ni mzigo mkubwa. Nashauri *section 12* yote iangaliwe upya kwa kupunguza kodi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Spika, hoja yangu inahusu Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Mwaka 2007/08 katika Bajeti ya Fedha ya mwaka jana pia nilichangia kuwa, kwa nini Mradi huu takriban miaka 40 sasa tangu Uhuru hauendelei?

Ninaomba sana Waziri atoe majibu muafaka kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini, hususan Wilaya ya Ludewa; ni lini Mradu huu utanza?

Aidha, wananchi waishio pembezoni mwa eneo la Mradi wa Mchuchuma na Liganga pia wameambiwa wasiendelee maeneo wanayopaswa kuhama. Agizo hili tangu litolewe ni miaka mitano sasa, lakini bado hawajalipwa fidia zao ili wahame; hivyo, hawawezi kuendeleza lakini pia hawawezi kuhama kwa kuwa hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya kuridhisha juu ya suala hili, kabla ya kushika shilingi katika Wizara husika.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2007/08, ina dhana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania (safari yetu ya kufikia 2025 kiuchumi), kwani inazingatia msingi mkuu wa Ilani ya CCM na MKUKUTA. Bajeti hii imetambua kuwa maisha ya Mtanzania yamekuwa magumu na kwamba, utozwaji wa kodi/ushuru mbalimbali unapaswa kupunguzwa.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa bajeti hii imewezekana kuwa ilivyo kwa sababu Serikali makini ya CCM katika mwaka 2007, imekuza rasilimali kwa asilimia 29.6, ukilinganisha na asilimia 27.6 kwa mwaka 2006. Mpango wa kuongeza ujenzi wa majengo, uingizaji mitambo na vifaa vya uwekezaji kutoka nje, uendelezaji ardhi, barabara na madaraja na pia shughuli za uchumi na biashara uongezewe nguvu zaidi, kwa kuwa navyo vimesababisha kukua kwa uchumi.

Suala la Benki kutoa mikopo kwa sekta binafsi ni hatua moja ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Eneo hili lingelela mafanikio zaidi kama benki zingepanua zaidi huduma ya mikopo kwa watu binafsi mpaka vijijini.

Maamuzi ya Serikali kuacha kununua hati fungani ni jambo zuri sana, maana riba za benki kwa mikopo inayotoa kwa wateja wake nazo zimepungua na mikopo kupatikana kwa urahisi zaidi kwa wananchi. Mpango huo wa Serikali uendele.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuacha kuzungumzia changamoto ya ajira 1,000,000 zilizoahidiwa; hivyo, ajira 402,608 ambazo zimekwisha patikana hadi sasa ni hatua ya kuridhisha. Kama vile kutekeleza Pogramu ya Taifa ya kukuza ajira na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kukuza ajira kila mkoa nako pia kutatufikisha kwenye lengo la ajira 1,000,000.

Katika kuongeza ajira mkoani Rukwa, Serikali inashauriwa kuviwezesha vyombo vya fedha kufikisha mikopo kwa wananchi vijijini, kuboresha kilimo na kufikisha pembejeo kwa wakati, lakini pia kuboresha elimu ili watu waweze kukopesheka na kuajiriwa. Kilimo cha kudumu cha *Jatropha* kitasaidia sana kutoa ajira iwapo kitahamasishwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri sasa Serikali ijikite katika kutoa lishe kwa waathirika wa VVU, kwani wengi wa wananchi wanayo elimu sahihi ya UKIMWI. Kupima kwa hiari ndiyo njia rahisi kujua kuwa, Watanzania wameelewa kodi hili. Dawa za kupunguza makali, haziwezi kuleta mafanikio iwapo waathirika hawapati lishe.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inaenda vizuri katika Bajeti ya mtazamo wa jinsia. Sasa naiomba Serikali iongeze nguvu katika *Gender Mainstreaming* ili kutekeleza Ilani ya CCM kuhusu 50/50 ifikapo 2010, katika ngazi zote za maamuzi. Hili linawezekana. Finland inaenda vizuri sana katika mfumo huu. Wanawake ambao ni 51% ya idadi ya taifa ni hazina kubwa kwa nchi yetu, wawezeshwe.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mazingira ni eneo lingine la Serikali yetu kuongeza nguvu. Ingesaidia sana iwapo wananchi wangemilikishwa ardhi haraka (MKURABITA) ili kila mwananchi ahusike kikamilifu kutunza ardhi na misitu. Hapa tena Finland ni mfano wa kuigwa. Umiliki wa misitu/ardhi utaondoa uchomaji misitu na upandaji na utunzaji misitu yetu utakuwa rahisi.

Mheshimiwa Spika, ingawa Serikali inaboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii katika sekta mbalimbali, sisi mkoani Rukwa, tunaomba kasi iongezwe katika elimu, miundombinu (Barabara ya Kaengesa – Mwimbia – Kawimbe) iwekwe lami inatuunganisha na nchi ya Zambia na afya na maji viboreshwe zaidi.

Nashauri Mfuko wa Hifadhi ya Jamii utoe huduma kwa Watanzania wote, hasa wakulima na wastaafu, ambao hufa sana kwa kukosa *Insurance*.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali zsa kukuza uchumi na kuondoa umaskini zinaonekana wazi. Nashauri kuwa, wazalishaji chakula kama Mkoa wa Rukwa, wahamasishwe kulima chakula na mbono kama zao la kudumu kwa biashara ili wasiendeleo kukumbatia umaskini kwa kutegemea mazao ya msimu. Ukame na mvua vikizidi ni tatizo pia.

Haipendezi kuona wana-Rukwa wakiugua na kushindwa kulima wakati wa msimu wa kilimo wa kupata mateso ya kujikimu mwaka mzima. Haipendezi pia kuona wana-Rukwa wakilanguliwa mazao yao na wafanyabiashara kwa kuwa wanaharaka ya kuuza mazao yao ili wapate mahitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wakati Watanzania wengi wanafurahi kuuza Korosho, Kahawa, Vanila ni wazi na Rukwa ingependa kuwa na mbono kama zao la kudumu la biashara, ambalo tayari kiwanda chake kinajengwa Mpanda. Tumbaku kwa Rukwa imechangia sana kuharibu misitu na malipo kwa wakulima hayana tija.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mungu kwa kutufikisha au kutupa uhai na kuhudhuria kikao hiki cha Bajeti.

Nawapongeza sana na kuwatakia kazi njema na nzuri Mawaziri wote wa Wizara hii ambao ni wapya.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2008/09, tayari imewasilishwa na kwa mchango wangu ni nzuri, lakini hata hivyo, bado fedha hizi zilizopatikana ni kidogo. Tunafahamu kuwa, kitu kidogo unaweza kukitumia vizuri kuliko kuwa na kitu kikubwa kikatumika viabaya. Kwa hiyo, nashauri Wizara zote zitumie mgawo wa fedha kama ulivyopangiwa na zisitumike vibaya au kinyume.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya petroli, dizeli, mafuta ya taa ni mengi kwetu Tanzania; hatuna sababu ya ya kupandisha bei. Nchi wanaotuuza wanaotuuza kwa kupandisha bei mara kwa mara, lakini na sisi naiomba Serikali tuwe na mbinu ili utone tunafaidika kwa bei nafuu, kwani bila mafuta maendeleo ni finyu au hakuna.

Mheshimiwa Spika, *TRA* tunaipongeza kwa kufikia kiwango kizuri kila mwaka, hasa Tanzania Bara kiwango kinaongezeka. Hata hivyo, naiomba Serikali kwa upande wa Zanzibar, ifanye kama wenzao. Pamoja na hayo, nashauri hii *TRA* ya Bara na Zanzibar, makusanyo yote Bara na Visiwani, yawe ya pamoja na baadaye wapate mgao wao kuliko kubaki hivyo, tukakosa makusanyo mazuri.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tulikuwa tuingie katika *OIC*; hadi leo vipi au kuna nini? Naomba Serikali kwa faida ya Watanzania, tuingie tusicheleweshwe na kama kuna ubaya tuelezwwe.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali fedha itakayopatikana miundombinu ipewe kipaumbele. Pamoja na wawekezaji wa miundombinu, Serikali iipe umuhimu ili itumike vizuri na wataalam wahimize ujuzi ili tuweze kutumia na kufaidika kama nchi ya kileo. Baada ya haya, kwa niaba ya Wananchi wa Magogoni, naunga mkono hoja.

MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Nampomgeza Waziri wa Fedha, kwa Bajeti yake yenye lengo la kuleta ustawi mzuri wa kisiasa na kiuchumi katika Taifa letu hili linaloendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusiana na suala la Tume ya Pamoja inayohusika na fedha za Muungano, ambalo Mheshimiwa Waziri ameligusia katika bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, suala la fedha za Muungano kwa kweli linahitaji umakini mkubwa sana ili kuepusha na kunusuru mwanya wa mgawanyiko uliopo katika Taifa letu usije kuleta athari kubwa.

Mheshimiwa Spika, hisia za wananchi kuhusiana na kodi hili ni kuwa kuna aina fulani ya mzaha au mchezo, kwani hii ni bajeti ya kwanza ambayo inazungumzia suala hili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali hii ya Awamu ya Nne ilipoingia madarakani imeahidi kuwa, wataalam wa kigeni wametafutwa kuweka sawa na kupendekeza mfumo mzuri wa mgawanyo wa fedha hizo. Leo hii tunaambiwa katika bajeti kuwa, Tume iliyofanya utafiti hivi sasa inafanya uchambuzi kuhusu vigezo vya kuchangia na kugawana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuitahadharisha Serikali kuwa, umakini na uadilifu unahitajika, tukizingatia kuwa suala hili ni miongoni mwa kero za Muungano. Kwa hiyo, kuchelewa kwake kupatiwa ufumbuzi wa haraka ni kuonyesha udhaifu wa Tume hiyo na Serikali kwa pamoja, kwani Ilani ya CCM imeagiza kushughulikia kero za Muungano kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha kwa niaba ya Wananchi wa Magogoni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia eneo lifuatalo:-

Katika vyombo vya habari, Waziri wa Fedha alinukuliwa kuwa kutokana na ukaguzi wa Akaunti ya *EPA* ndani ya BoT kuwa hadi wakati ule, mwezi Machi; shilingi bilioni 60 zilikuwa zimerejeshwa:-

(a) Je, hadi tarehe 30 Mei, 2007 zimekwisha kurejeshwa jumla ya shilingi ngapi na zimewekwa kwenye akaunti ipi?

(b) Kama katika Bajeti kasma inayopokea fedha hizo ni *Vote 50, Program 10, Subvote 100100*; imekuwaje kasma hii inaonyesha shilingi 500,000,000 tu? Waziri alieleze Bunge ni kasma ipi inayotumika kupokelea fedha hizo?

(c) Bunge hili linahitaji kufahamu hadi mwisho wa zoezi linaloendelea la Kamati ya Mwanyika, tunategemea kukusanya kiasi gani na tunategemea kukielekeza kwenye shughuli ipi kwenye mafungu ya Bajeti (kasma ipi)? Bunge lazima liwe na taarifa za kina ili liweze kusimamia vizuri matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunapata tabu kwa vile Serikali haipo wazi, taarifa zimefichwa; hivyo, Wabunge tunapata shida ya kuchokonoa sana, jambo linalofanya kazi ya Wabunge kuwa ngumu sana.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari; na Wataalam wote wa Wizara hii, kwa kuandaa hotuba nzuri.

Kwa kuwa wananchi wengi wamefaidika na *TASAF I*; na kwa kuwa wamefanya kazi nzuri ya maendeleo kwenye maeneo yao na kutoa mchango mkubwa na Nguvu kazi ili waweze kufanikisha miradi yao; kwa mtazamo wangu, ningeonelea asilimia wanayochangia wananchi kwa kazi ya maendeleo, Serikali ipunguze kutoka 20, 15 – 10 ili miradi ambayo imeanzishwa iweze kukamilika.

Serikali ipeleke wataalam wenye uwezo wa kuibua miradi vijijini kuliko ilivyo sasa, kwani huachiwa wananchi kuibua na badala yake hawaoni faida hivyo, kuchangia kutokamilika miradi kutokana na jiografia ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matumizi kwa wananchi wa kawaida hutumia magari kama taxi, hususan vijijini; ningeomba Serikali iangalie viwango vya kodi hiyo kutoka shilingi 150,000 – 120,000, angalau iwe shilingi 100,000 ili waweze kumudu hali ya maisha. Wananchi wengi wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya viwango vya riba ili *SACCOS* zetu ziweze kumudu kukopesha wananchi kwa riba nafuu kuliko ilivyo sasa.

Serikali iangalie jinsi ya kuiwezesha Benki ya Wanawake kuanza ili wananchi wengi vijijini na mijini waweze kukopa kwa ukaribu zaidi na Serikali iweze kupitishia mikopo ya riba nafuu. Benki hii ni mkombozi wa wanawake, badala ya ilivyo sasa, fedha zote zinapitia Halmashauri za Wilaya (milioni mbili), ambazo zinatolewa na Serikali kwa ajili ya mikopo kwa wanawake.

Pamoja na hayo; je, Serikali imenunua hisa ngapi za Benki hiyo ili kuonyesha umuhimu wa chombo hicho ukizingatia ushindani wa Mabenki yaliyopo hapa nchini?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, Napenda nichukue nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kutoa mchango wangu katika hotuba ya bajeti ya fedha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda kuipongeza Serikali kupitia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii, ambayo Watanzania walio wengi, wameipokea kwa mikono miwili hasa wakizingatia imewajali sana wanyonge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali, napenda kuchangia maeneo kadhaa kama ifuatavyo hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kutoa mikopo mbalimbali kupitia Benki zetu kama vile *NMB*, *CRDB*, *NBC* na kadhalika, ambayo wanaopata kipaumbele ni wafanyabiashara zaidi na sio wakulima. Utataribu huu unawavunja moyo sana wakulima wetu, kwani kilimo cha kisasa bila mtaji wa kutosha, huwezi kulima kwa kiwango cha kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, hata wale wakulima wachache wanaofanikiwa kupata mikopo, hupata wakati ambapo msimu wa kilimo umepita. Hivyo basi, naishauri Serikali kuwasaidia wakulima kuanzisha Benki yao ili waweze kupata mikopo na kwa wakati muafaka ili kuinua kilimo ambacho kitazalisha Pato la Taifa, hasa kwa mazao ya biashara na chakula pia.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, eneo kubwa la ardhi katika maeneo mengi hapa nchini, ardhi haijatumika vizuri katika kilimo. Hii inatokana na wakulima kutohamasishwa vya kutosha kulima ekari nyingi ama hawajawezeshwa vya kutosha kupata nyenzo za kilimo kwa mfano, pembejeo, mbegu, mbolea na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Serikali ifanye utafiti wa kutosha wa mazao ya biashara, ambayo yana soko zuri huko nchi za nje ili wakulima waelimishwe kulima kwa wingi zaidi ili kuinua pato lao na la Taifa kwa ujumla. Kila eneo ijulikane zao ambalo linafaa kulima, kwa mfano, Singida kuna ardhi tele ambayo haijalimwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile mkulima anavunjika moyo kulima kwa nguvu mazao ya biashara, kwa sababu ya kutokuwa na soko la uhakika mfano zao la alizeti. Serikali iliwaeleza wananchi kuwa, kuna nchi tatu zitakazonunua alizeti, lakini hadi sasa hatujaona nchi hizo kuja kununua. Naiomba sana Serikali itoe jibu, soko hili la alizeti liko wapi ili wakulima wapate moyo wa kuzidisha kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zao hili limeonyesha kuwa na faida kubwa, naomba tueleze linafaa kulimwa mikoa gani ili tuweze kuwahasisha wakulima wetu waweze kuinua vipato vyao?

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inawajali sana wafanyakazi ambao wana mchango mkubwa sana kwa Taifa mfano: walimu, madaktari na kadhalika. Ukweli naona wafanyakazi

bado hatujafanya tathmini ya kutosha ili tuweze kuona kiwango kinachotakiwa kwa kima cha chini ni kipi. Mfanyakazi ana matumizi mengi sana ya kupita mshahara wake, ambayo yote ni muhimu sana, kwa mfano, nauli ya basi kwenda kazini na kurudi. Dar es Salaam wapo wafanyakazi wanaopanda mabasi matatu asubuhi na jioni, sawa na Sh.1500 kwa siku; kwa mwezi Sh. 45,000; hiyo ni nauli tu bado familia haijapata chakula, nguo, ada kwa wanafunzi na kadhalika

Mheshimiwa Spika, hivi hii ni haki kweli, naiomba Serikali itazame upya kima cha chini, kama sio mwaka huu basi mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, bado pia kuna tatizo la kodi kwenye mishahara zaidi ya Sh, 100,000. Naishauri Serikali iondoe kodi ya mishahara kwa wafanyakazi wote wenye mishahara chini ya Sh. 1,000,000 ili mtumishi aweze kupata angalau unafuu wa maisha, pamoja na kusomesha wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, mtumishi anapokatwa kodi, *take home* hubaki ndogo sana na kusababisha watumishi kuiibia Serikali au kufanya biashara saa za kazi ili kuweza kumudu maisha kwa mwezi, ambapo mshahara hautoshi.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, madiwani, wanasimamia Halmashauri ambazo zinapata fedha nyingi sana. Hivyo, bila kuwapa posho zitakazokidhi haja, watapata vishawishi vya kupokea rushwa toka kwa wataalam na makandarasi ambao wanatekeleza tenda zao kwa kiwango cha chini sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Serikali ione umuhimu wa madiwani ndani ya Halmashauri zetu na muda mwingi wanaoutumia kusimamia fedha za Halmashauri zetu. Naomba Madiwani waongezewe angalau kiasi ambacho watamudu maisha, kwani hawajamfikia hata mtumishi anayepata kima cha chini. Vilevile posho zao, Serikali itoe ruzuku, kuliko ilivyo sasa kutokana na vyanzo vya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupunguza kodi ya mafuta viwandani. Ingependeza zaidi, endapo Serikali ingepunguza kodi ya mafuta kwa watumiaji wadogo, ambao ndio wanaotoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, endapo muuzaji wa mafuta asipopunguziwa kodi, atamuuzia mwananchi bei ya juu. Hivyo, bado mwananchi ataendelea kuumia kwani mafuta ni miundombinu muhimu sana kwa mwananchi, hasa wa kawaida, pia nauli zitaendelea kupanda.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itafute njia mbadala kufidia ziada ya bei ya mbolea kuliko kuongeza bei ya mbolea kwa vile wakulima wetu bado wanahitaji unafuu ili waweze kukuza kilimo, kwani wengi wao bado hawajapata mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, wakulima waendeleo kuelimishwa juu ya matumizi ya mboleo za asili kwa mazao madogo madogo ili kupunguza gharama kwa mfano, mbolea ya samadi, pumba za mpunga na mboji, ambazo zinapatika bila gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kuona bajeti karibu za Wizara zote zimepanda. Hivyo basi, naiomba Serikali iendeleo kutenga asilimia kumi kwa Mfuko wa Wanawake na asilimia tano kwenye Mfuko wa Vijana ili waendeleo kukopeshwa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia juu ya bandari zetu za Tanga, Dar es Salaam na Kigoma ambazo nyingine zinahitaji matengenezo ya haraka, kwa mfano, Bandari ya Tanga, Mtwara na Kigoma, ambazo utafiti na matengenezo yake ni ya kusuasua. Matumaini yangu ni kuwa, bandari hizi zikitengenezwa na kuanza kutoa huduma, zitasaidia sana kutoa msongamano wa makontena katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, si kuondoa msongamano tu, bali hata pato la ushuru wa kuingiza na kusafirisha mizigo, litaongezeka na kukuza pato kupitia ushuru wa bandari zetu zote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nimalizie kwa kuunga tena mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia 100.

Naipongeza Serikali, kwa Bajeti, pamoja na mengine, kama ifuatavyo:-

- (a) Kujitegemea katika Bajeti ya Matumizi ya Kawaida.
- (b) Kupunguza utegemezi wa bajeti nzima kwa 8% na kubakiwa na utegemezi wa 34% tu.
- (c) Azma ya Serikali kupunguza utegemezi hadi 20% ifikapo mwaka 2010.
- (d) Kukamilishwa kwa Mradi mkubwa wa maji wa Shinyanga/Kahama, ambao ulikuwa unachukua sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali.
- (e) Vipaumbele vinavyozingatiwa na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ninashauri yafuatayo:-

(a) Tutoze ushuru kwa mafuta yote ya kula kutoka nje ili kwanza kulinda soko la bidhaa hiyo inayozalishwa nchini; pia kuzuia mianya ya kutumiwa na wachache kukwepa kodi stahili. Isitoshe ushuru kwa mafuta yote kutoka nje utatupatia mapato.

(b) Kwa kuwa barabara bora (za lami) ni kichocheo muhimu cha kuleta maendeleo, lakini ni ghali sana kuzijenga, nashauri tuanzishe *Self-help Projects* katika Halmashauri zetu za Mijini, kwa wananchi kushirikishwa katika ujenzi huo ili kuongeza kazi ya uwepo wa barabara bora hususan katika miji yetu. Si lazima kusubiri/kutegemea lami tu kujenga barabara bora; barabaza za mawe yaliyokatwa au matofali magumu na kadhalika, zinafaa sana. Hali hii itafanya miji yetu ichemke kibiashara na hivyo kuongeza Pato la Taifa.

(c) Utegemezi wa Bajeti ushuke zaidi hadi 15% ifikapo 2010. Tukope kwa makusudi kwa miradi mikubwa ya maendeleo; tena tukupe haraka kabla hatujachelewa.

(d) Misamaha ya kodi ipunguzwe sana ili kuongeza mapato ya Serikali na kupata fedha za kujenga barabara za lami, kuboresha shule zetu za sekondari na vyuo vikuu; pamoja na kuboresha huduma za jamii na kadhalika.

(e) Serikali iainishe *main economic drivers* na kuweka mipango na mikakati ya kuviendeleza ili twende kwa kazi zaidi katika kujenga uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa kwa kazi nzuri anayoifanya na naunga mkono hoja.

Napenda nifahamu ni kwa nini bajeti ya maji imepunguzwa? Bado kuna matatizo makubwa ya maji; Wilaya ya Geita maji ya chini/visima yamejaa madini na ni hatari kwa maisha yao. Mabwawa yamejaa *mercury* ambayo pia ni hatari. Maji ya mvua ni machafu sana kwa sababu ya vumbi la machimbo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inalionaje hili? Tunaomba Bajeti ya Maji iangaliwe upya; Geita nayo ipewe maji. Mito yote imejaa *mercury* hivyo, wakazi wapo hatarini pamoja na mifugo yao.

Bandari ya Dar es Salaam iimarishwe na kazi iwe saa 24. *TRA* wawepo muda wote, wanachelewesha mizigo. Bandari iangaliwe sana. Sheria za madini zirekebishwe ili tupate mavuno. Punguza *road blocks* za polisi ili watu wafanye biashara haraka. Wanachelewesha biashara kwa kuomba rushwa barabarani, hata kama hawana kosa.

Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinazojengwa zisitumie pesa nyingi. Kwa mfano, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara, inatisha wakati hata huduma ya hospitali hawana; wanatumia zahanati ndogo mkoa mzima. Tuangalie *priority*.

Naomba nielezwe Mradi wa Maji wa Chankorongo Nyakagomba, utaisha lini wakati bajeti imepungua? Mradi huu ulianza mwaka 1976, mabomba yameozea chini. Wananchi hawaelewi Serikali. Naomba maelezo.

MHE. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nina heshima kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu wake, pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha, kwa kutuandalia bajeti nzuri, ambayo ina mwelekeo mzuri wa kujenga uchumi wa Taifa na kuwanyanyua wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nina maeneo yangu machache ambayo ninaomba kuyachangia kwa lengo la kuishauri Serikali ili kuuimarisha uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndio mkombozi pekee katika kuimarisha uchumi wa taifa. Aidha, ndio njia pekee ya kumkomboa mwananchi. Pamoja na Bajeti ya Kilimo kuwa ndogo kwa mwaka wa fedha 2008/09, lakini bado naishauri Serikali ikiangalie kilimo kwa kuongeza matrekta, pembejeo na kutoa elimu zaidi katika kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, ninadhani sasa umefika wakati, tuangalie kwa nguvu zetu zote, kuuinua uchumi wetu katika Bahari Kuu na Maziwa yetu Makuu. Lazima tutafute vyombo vya kisasa vikubwa, kwa ajili ya uvuvi wa Bahari Kuu. Nchi yetu ina utajiri mkubwa katika bahari

yetu ya Hindi, ufike wakati sasa tuvune vyema utajiri huo, vinginevyo, uchumi wetu wa bahari unaporwa na meli za nchi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeumbwa na bahati kubwa ya utajiri wa madini ya aina mbalimbali, lakini kuna haja kubwa ya Serikali kujipanga vizuri katika kusimamia uchimbaji bora wa madini yetu. Inaonekana bado kuna uvunjaji mkubwa wa rasilimali yetu ya madini, hasa kwa wale wachimbaji wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, mgodi wetu mwingine mkubwa ni utalii, ni vyema tukaimarisha vizuri, fukwe zetu nzuri za bahari. Vituo vyetu vya kihistoria vilivyomo nchini, kama vile Bagamoyo, Kigoma, Mafia, Zanzibar, Mtwara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina bahati kubwa ya maeneo mazuri, yenye bandari zenye uwezo mzuri wa uvunaji wa fedha za kigeni, lakini juhudi kubwa ichukuliwe katika miundombinu yetu; lazima tuimarisha ujenzi wa kisasa katika bandari zetu zote hususan zile za Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar, Mtwara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nimeizungumza Zanzibar kwa sababu inahitaji sana isaidiwe, kwani uchumi wake umedorora sana na inawajibika sana kuchangia shughuli za Muungano; hivyo, inastahili sana kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu mdogo, kwa heshima kubwa ninaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia hoja hii. Ahsante sana.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Kwanza kabisa, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri, aliyoiwasilisha Bungeni pamoja na mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2008/09.

Bajeti imekuwa ya kujitegemea zaidi kuliko nchi kuwa tegemezi zaidi, kwa hatua hii naipongeza Serikali kwa hilo.

Kwa upande wa kodi kwa wafanyakazi, kwa kweli kiwango chenyewe ni kidogo mno, hakimtoshi mfanyakazi, hali ni mbaya. Bora kodi ingeanzia kukatwa kwa mwenye mshahara kuanzia Sh. 1,000,000. Ombi langu ni kuwa, Serikali iangalie hilo, kwani mwananchi wa kawaida anaumia sana.

Hali ya chakula ni mbaya sana, kila bidhaa imepanda bei; mchele, unga, maharage na kadhalika. Hapo hapo, Bajeti ya Kilimo imekuwa finyu mno, kwa kweli Serikali iangalie hilo kwani mkulima ana kazi kubwa.

Kwa upande wa madini, sekta hii haikuwa nzuri, sheria ingefaa ibadilike, hasa ukiangalia mikataba yenyewe, ingefaa ibadilishwe kabisa. Serikali ifanye mabadiliko upande huu wa madini; Wananchi wamenung'unikia sana sekta hii, hivyo iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na uzima na kunijalia kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na timu nzima iliyoandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, niungane na wananchi wa Jimbo la Fuoni, kwa kuiunga mkono bajeti, pamoja na wananchi wengine walioonyesha kuiunga mkono bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imewajali wananchi wa ngazi zote, hasa ukizingatia vipaumbele vilivyowekwa na punguzo la kodi lilivyozingatiwa. Lililobaki sasa ni kusimamia utekelezaji ili lengo lililokusudiwa lifikiwe na Mungu atujalie yale yote tuliyoypanga yafanikiwe na wale wote watakaoturidisha nyuma kwa kuharibu kwa makusudi, wachukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tumejenga madarasa, nyumba za walimu, lakini tatizo kubwa ni upungufu wa walimu kwa kila sehemu ya nchi hii. Ninaiomba Serikali kwa kipindi hiki, iangalie sana ajira ya walimu na kuwawekea mazingira mazuri, pamoja na kuwalipa mafao yao na mishahara kwa wakati. Serikali pia iipe kipaumbele, mikoa yenye upungufu wa walimu kwa kusomesha walimu kwa wingi halafu wagawiwe kwenye mikoa husika ili kupunguza tatizo la kuhamahama na kutofika sehemu walizopangiwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi kwa ujumla imepanda kwa asilimia saba. Hali ya uchumi ya Zanzibar si nzuri, kutokana na vyanzo vyake vya mapato kupata misukosuko ya mara kwa mara, baada ya karafuu kukosa soko la uhakika. Biashara ambayo ilikuwa ni tegemeo kubwa kwa nchi na wananchi wake, imeshuka kulingana na mifumo ya kodi. Hali hii imesababisha wafanyabiashara wengi kutoitumia bandari hiyo kama ilivyokuwa hapo awali na kusabaisha wananchi wengi kukosa ajira na nchi kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo yanayoikumba Zanzibar, umefika wakati sasa Serikali ya Muungano kuipunguzia baadhi ya masharti ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango wangu mfupi, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MWANTUMU B. MAHIZA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naipongeze Wizara kwa hotuba nzuri na bajeti yenye matarajio mazuri kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, maombi yangu rasmi kwa Wizara ya Fedha ni yafuatayo:-

Kwanza, kuondoa ushuru kabisa kwenye matrekta ili wananchi waweze kuyanunua na kuyatumia. Hivyo, kusaidia wengine katika kulima mashamba makubwa na kupunguza muda wa kazi katika kilimo. Kwa kuondoa ushuru, kilimo kitapanuka, chakula kitaongezeka na njaa itaondoka.

Pili, kuelekeza Mabenki kupunguza riba kwa wanaokopa na kuwekeza katika Elimu, kwa mfano, ujenzi wa Vyuo Vikuu, Vyuo vya Ufundi, Vyuo vya Ualimu na Shule za Sekondari. Kwa kuondoa au kupunguza riba kutoka 22% - 10%, kutasaidia kushusha gharama za uendeshaji na kupunguza ada katika vyuo na shule za sekondari za binafsi, ambazo ni kubwa

mno na kwamba, bila kuondoa riba hiyo kubwa, hakuna njia ya mkato. Aidha, itambuliwe kuwa, nafasi ya sekta binafsi katika elimu ni kubwa sana; sijui hali ingelikuwaje endapo hadi leo wasingelipewa nafasi ya kutoa elimu?

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa rai kuliona suala hili kipekee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HAJI JUMA SEREWEJI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya Waziri wa Fedha. Kabla sijaendelea, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza hotuba hii na bajeti hii ambayo imewafikiria wananchi wa chini. Naipongeza bajeti hii kwa kutoongeza kodi kwenye mafuta ya petroli na dizeli. Hii ni kwa sababu petroli hupanda bei kila mara, sasa Serikali ikizidisha kodi bei ya petroli itazidi kuwa mbaya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar, mgao wa fedha za msaada za Muungano, ufikiriwe upya kwani Zanzibar wanapata mgao mdogo sana. Kwa hiyo, suala hili lifikiriwe na kutatuliwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magari yaliyosajiliwa kwa namba za Zanzibar kutotumika huku Bara, naona si jambo la busara kwa sababu huu ni Muungano, kwa hiyo ni vizuri magari hayo yatambulike.

Mheshimiwa Spika, mwisho nazidi kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa bajeti nzuri. Nawapongeza Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote, walioandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia *TRA*, kwa kufanya kazi nzuri ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwenye maeneo yafutayo:-

Misamaha ya ya kodi: kwenye bidhaa za mafuta ya Petroli; Makampuni ya mafuta yanalipa *Fuel Levy* kwa kiwango kisichozidi USD 200,000 kwa mwaka ama Sh. 250,000,000 kwa kukadiria. Matumizi ya mafuta kwa makampuni ya madini ni makubwa sana, kwa mfano, inakadiriwa kuwa, *Geita Gold Mine* inatumia lita 58.0 milioni kwa mwaka. Kwa kiwango cha Sh. 100 kwa lita cha *Fuel Levy*, maana yake tungetegemea kupata (Sh. 58,000,000 x 100) = 5,800,000,000 (5.8 bilioni).

Mheshimiwa Spika, msamaha huu ni kwa Kampuni moja tu. Utafiti unaonyesha ya kuwa, Serikali inapoteza Sh.41 bilioni kwa mwaka, kutokana na Serikali kuyasamehe Makampuni ya Madini kulipa *Fuel Levy*. Hakuna sababu ya kuwasamehe maana wanapata faida. Sheria zetu zibadilishwe ushuru huu ulipwe.

Excise Duty on Petroleum Products; msamaha huu hauna maana yoyote kwa kuwa ni *production expense*, ambayo itawekwa kwenye mahesabu ya mwisho wa mwaka. Hakuna kampuni yoyote ambayo haina gharama wala hakuna sababu ya kuwasamehe. Tunapoteza zaidi ya shilingi bilioni 10 kwa mwaka. Hakuna nchi yoyote duniani, inayotoa msamaha wa namna hii kwa makampuni ya madini isipokuwa Tanzania; kitu gani kinatufanya tudanganyike hivyo?

Mheshimiwa Spika, makampuni yanazalisha vizuri lakini hatutaki kuwatoza kodi, turekebishe sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ya Fedha na Uchumi, ifanye yafuatayo ili kuongeza wigo wa kodi:-

(i) Kufuta mara moja msamaha wa ushuru wa forodha kwa Wafanyakazi wa Serikali kwenye magari chakavu yenye umri zaidi ya miaka 10.

(ii) Kufuta mara moja msamaha wa ushuru wa forodha kwa Makampuni ya Madini, kwa bidhaa zisizohusiana moja kwa moja na shughuli za madini kulipia 5% badala ya viwango vya ushuru vya Umoja wa Afrika Mashariki.

(iii) Kufuta mara moja msamaha wa Ushuru wa Mafuta (*Fuel Levy*) kwa makampuni ya madini, kwa sababu kodi hii ni moja ya gharama ya uendeshaji wa kampuni.

(iv) Kufuta mara moja msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta (*Excise Duty*) kwa makampuni ya madini.

(v) Kufuta mara moja msamaha wa ushuru wa mafuta (*Fuel Levy*), ushuru wa bidhaa kwenye mafuta (*Excise Duty*) na msamaha wa *VAT* kwenye Makampuni ya Uvuvi na uzalishaji kwa kufuta *notice* za Serikali zilizotumika kutoa misamaha hiyo.

(vi) Kurekebisha utozaji wa kodi za zuio (*Withholding Taxes*) kwa makampuni ya madini ili uendane na Sheria ya Mapato ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naiomba Wizara ya Fedha na Uchumi, ikusanye kodi kutoka kwenye makampuni ya madini baada ya kurekebisha sheria zilizowawezesha kusamehewa kodi mbalimbali. Makampuni haya yanapata faida kubwa, hivyo, inabidi yalipe kodi.

Mheshimiwa Spika, Mwarabu anafaidi mafuta yake, kwa hiyo basi na sisi tuweke utaratibu wa kufaidi kutokana na madini yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja maana hii ni Bajeti ya Serikali yangu, lakini Serikali vilevile iyafanyie kazi mapendekezo yangu.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ulinzi wake tangu bajeti ya 2007/08 hadi leo hii amenilinda.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, Naibu Mawaziri na Watendaji wote kwa kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii, naomba nichangie mambo yafuatayo:

Wananchi wengi wanategemea kilimo, hotuba imeeleza vizuri, hata hivyo, jukumu la upatikanaji wa matrekta kuachia sekta binafsi, bado wakulima wataumia. Kumbuka hata Mabenki mengi ni sekta binafsi, lakini yameshindwa kutusaidia. Nashauri pawepo na agizo la lazima, kwa kila Halmashauri ya Wilaya, kununua au kukopa matrekta kwa ajili ya wananchi wao. Hamashauri za Wilaya ndio zichukue jukumu la kuwakopesha wakulima wake.

Kwa kuwa Benki ya Wakulima imechukua muda mrefu sana bila mafanikio, sekta binafsi hatujajua ufanisi wake. Serikali iniambie Wananchi kama wa Bukombe watawezaje kupata matrekta na vitendea kazi vingine?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali izipitie upya Sheria za Wakala ili Taasisi na Mashirika ya Umma yaweze kutoa gawio (*dividend*) katika Mfuko wa Serikali. Yapo baadhi ya Mashirika, Taasisi na Wakala wa Serikali, ambao wanapata faida kubwa sana bila kupeleka gawio Serikalini, kiasi kwamba wanatumia fedha ovyo na kukosekana umuhimu wa wao kuwepo katika kusaidia taifa.

Serikali iangalie upya mfumo unaotumiwa na wachimbaji wadogo wadogo wa madini, pamoja na wanunuzi wao. Kwa kuwa Serikali haijawawezesha wachimbaji wadogo, wamejikuta wanadhibitiwa na wanunuzi uficho. Hawa wanunuzi uficho (Makota), hawalipi ushuru Serikalini, ambapo wanachukua fedha nyingi sana kupitia madini hayo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iwawezeshe wachimbaji wadogo wadogo, kama ilivyoahidi Ilani ya CCM 2005, ndipo itaweza kuwatambua wanunuzi na kujua mchango wao kwa taifa. Misamaha mingi ya kodi itolewayo kwa Makapuni makubwa ya wachimbaji, iondolewe. Naamini Makapuni haya yakilipa kodi ya malighafi yao, Pato la Taifa letu litaongezeka kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Manunuzi ya Umma, fedha nyingi za umma zinapotea na kusababisha Pato la Taifa kutumika ovyo ovyo. Nayapongeza maelezo yaliyoko kwenye hotuba. Hata hivyo, napenda kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Utaratibu wa Manunuzi katika Halmashauri za Wilaya zetu uangaliwe upya. Sheria ya Zabuni nayo ifanyiwe marekebisho, kwani sasa hivi upo mgongano mkubwa mno kati ya wanasiasa na watendaji. Kwa sehemu kubwa, Watendaji ndio wanachukua au wanapeana kazi zote zenye maslahi. Afadhali Bodi ya Zabuni inapopokea, kabla ya kutoa kazi Kamati za Fedha zipitie kwanza, tofauti na ilivyo sasa kwenye sheria ya kutoa taarifa. Udhibiti wa wanasiasa unakuwa mdogo, kwani ukilalamika tayari wajanja wamekwisha kula na pesa imepotea.

Ukosefu wa Huduma za Kibenki; ni vigumu sana kujua mzunguko wa Pato la Taifa kihalisia, kwani maeneo ambayo hayana Benki ni vigumu, kwa sababu wananchi wake wanachimbia hela zao chini ya ardhi. Zaidi ya hayo, wananchi wanaogopa kufanya biashara kubwa katika maeneo ambayo hayana Benki mfano, Bukombe.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anifafanulie; Wananchi wa Bukombe uchumi wao utaboreka vipi wakati hawana Benki? Ni halali wananchi wapatao 525,000 kukosa Benki? Kwa nini hata taasisi za kifedha kwa mfano, *NMB* walimfanya Mheshimiwa Rais atoe ahadi ya uongo Bukombe kwamba, Oktoba, 2007 *NMB* wangefungua Tawi Bukombe kulikoni?

Mheshimiwa Spika, kumbuka Bukombe ni tajiri sana kwa madini ya wachimbaji wadogo wadogo, watafiti na kuna mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Spika, watu wanaongezeka na mifugo pia, lakini ukubwa wa eneo hauongezeki. Katika Ilani ya CCM 2005, tuliahidiwa kutengewa maeneo. Je, hawa wafugaji wataboresha vipi mazingira yao kwa kuhama hama?

Naiomba Serikali waniambie wametenga maeneo ya malisho kwa kiasi gani. Kwa nini Serikali haiandai mazingira mazuri ya wafugaji mfano, Bukombe angalau kukawa na Kiwanda cha Maziwa ili kichangie Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mfanyabiashara ni Wakala wa Serikali kukusanya kodi ambapo yeye akishalipia mapato amemaliza, kodi nyingine zinaliwapwa na watumiaji. Mfanyakazi analipa kodi za aina mbili; *Direct Tax na Indirect Tax*. *Indirect tax* ni pale anapoenda kununua chochote toka madukani. Naomba nisaidiwe unafuu wa kodi kwa mfanyakazi uko wapi? Mbona kodi zake ni nyingi na kubwa sana?

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwapongeza tena na kwa imani kubwa, Serikali ijitahidi kutekeleza ahadi zetu ndani ya Ilani ya CCM ya 2005.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na Mungu awabariki.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nina hoja zifuatazo:-

Kwanza, ninaiomba Serikali iangalie suala zima la ukuzaji wa kilimo kwa kitaalam. Mimi naona ni aibu, kwa nchi yetu yenye ardhi nzuri, watu wengi na uongozi bora, inakosa mipango safi ya kuendeleza kilimo. Ni aibu nchi yetu kuwa na njaa.

Naishauri Serikali itenge maeneo ya mashamba makubwa ya kilimo na itenge fungu la pesa la kuyaendeleza. Aidha, kila kaya ijitosheleze kwa chakula. Wakati huo huo, Serikali ingalie upya suala la mishahara, iwe ya kweli. Ninamaanisha, mishahara uangalie mahitaji muhimu na uyakidhi, ili wafanyakazi wasiwe na dhiki.

Pili, sifa nchi yetu ni kujinasua katika umaskini. Naishauri Serikali isitafute kusifiwa eti bajeti imepunguza utegemezi, bali isifiwe kwa kupiga hatua kubwa ya maendeleo. Serikali ikope bila woga, la msingi uwepo usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za umma.

Tatu, Serikali iangalie upya, suala zima la pendekezo lake katika kodi za magari. Nimezungumza na baadhi ya wananchi, hawajaridhika na pendekezo la kodi lililowasilishwa na Serikali. Punguzo la sasa linataka kuwa kama ifuatavyo (bila malori na mabasi):-

(a) Ujazo usiozidi CC500 yanapunguzwa toka Sh. 50,000 – 30,000, hii ni sawa na 40% ya punguzo.

(b) Ujazo usiozidi CC1500 yamepunguziwa kutoka Sh. 80,000 – 50,000, hii ni sawa na 37.5% ya punguzo.

(c) Ujazo usiozidi CC2500 yanapunguziwa kutoka Sh. 250,000 – 120,000, hii ni sawa na 20% ya punguzo.

(d) Ujazo usiozidi CC5000 yamepunguziwa kutoka Sh. 330,000 – 140,000, hii ni sawa na 57.57%

Punguzo hili limezua malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba, wale wenye punguzo la 20% hawakutendewa haki. Wakati punguzo la ujazo la CC 5000, ambao wengi ni waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine Wakuu au Wafanyabiashara; kwa hiyo, wamejipunguzia sana.

Pendekezo langu ni kwamba, punguzo walau lifike 35% kwa wale wenye magari yenye ujazo wenye CC1501 – CC2500, upungue kutoka Sh. 150,000 hadi Sh. 97,500. Punguzo hili litaleta picha ifuatayo: (a)40%, (b)37.5%, (c)35% na (d)57.57%.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, apokee mapendekezo haya na ayafanyie kazi, hasa pendekezo Na. 3 linalohusu kodi mpya za magari.

Mheshimiwa Spika, nasubiri kwa hamu majibu ya Mheshimiwa Waziri hapo kesho kutwa.

MHE. MANJU S. O. MSAMBYA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutamka kuwa, naiunga hoja mkono. Sambamba na hilo, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, pamoja na Watendaji wote Wizarani, wakiongonzwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo ya utangulizi, napenda kutoa angalizo katika maeneo yafuatayo:-

Kutokana na kutoweka mipango madhubuti, bajeti yetu inaendelea kuwa tegemezi. Tunaweza kuondokana na utegemezi endapo tutaimarisha barabara zetu, hususan za vijijini ili mazao yaweze kufika sokoni na kuiwezesha Serikali kukusanya mapato ambayo yatatunisha Mfuko Mkuu wa Taifa. Kwa hali hiyo, Pato la Taita litawezesha kusimamia maendeleo na kuachana na suala la bajeti yetu kutegemea nje vyanzo vyetu.

Tanzania inazo shughuli nyingi zinazotendwa na watu wa makundi mbalimbali, kwa lengo la uzalishaji. Watendaji hao wanaitwa wajasiriamali ambao wanashughulika na biashara kubwa na ndogo. Wapo wakulima wakubwa na wadogo. Ni bahati mbaya sana kwamba, wajasiriamali wadogo hawawezeshwi kupata mkopo kutoka mabenki yaliyomo nchini. Mikopo hii wanapewa wafanyabiashara, wakulima na wavuvi wakubwa, ambao wengi wao wanatoka nje ya nchi.

Ieleweke wazi kuwa, wajasiriamali wadogo wanao mchango mkubwa endapo wataenziwa vizuri. Kuwapatia mkopo wajasiriamali hawa, kutaweza kuongeza uzalishaji ambao utakuza pato la uchumi wa taifa.

Kilimo na Bajeti 2008/09; kumekuwa na usemi jadidi kuwa, kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa la Tanzania. Ni wazi kilimo ndio mlezi wa uchumi wa Taifa hili, lakini hakuna juhudi maalum za kukiendeleza. Itambuliwe kuwa kilimo kinakuza uchumi na Pato la Taifa, kwa hali hiyo inafaa Wizara ya Fedha itafute utaratibu wa kuwawezesha wakulima ili kilimo kiwe cha kisasa, ambacho kinahitajika kukuza Pato la Taifa na uchumi wake. Kwa hali hiyo ni vyema Serikali ikaanzisha vituo vya zana za kilimo kwa lengo la kukodisha wale wakulima wadogo ambao hawawezi kukuza Pato la Taifa. Ni vyema kukopesha zana hizo baadae kwa hawa wakulima wadogo ili kuongeza uzalishaji na hatimaye kukuza Pato la Taifa na kuondoa umaskini.

Bajeti ni vyema iangalie kuendeleza na kukuza elimu. Uwekezaji katika elimu utakuza uchumi. Elimu ipatiwe fungu la kutosha ili uelewa wa mazingara uwape wananchi uwezo wa kuzalisha kisasa na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia uvuvi katika Ziwa Tanganyika, ambapo kutokana na kupanda kwa bei za mafuta, wavuvi wa Ziwa Tanganyika wanaathirika. Athari hizo zinagusa uchumi wa nchi, ambao unatakiwa uboreshe maisha ya Watanzania wa sehemu ile.

Namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, waangalie namna ya kuondoa adha inayowapata wavuvi ili Pato la Taifa likue na kuondoa adha kwa wavuvi hawa.

Mheshimiwa Spika, naamini Serikali itazingatia niliyoyaeleza na kwa hali hiyo, kuboresha uchumi wa nchi. Ahsante.

MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuwapongeza kwa asilimia kubwa, jitihada zinaonyeshwa na Wizara kupitia Waziri na Naibu Mawaziri na Watendaji wote. Bajeti hii ni nzuri lakini kuanzia sasa, lazima jitihada ziongezwe katika kutafuta njia mpya za kuongeza kipato Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi yetu kutofungmana na itikadi ya imani za kidini kwa upande wowote, tunapaswa kama Tanzania, tusiwe na mashaka kama ni Taifa miongoni mwa Mataifa; sisi Tanzania kama nchi maskini, hatuna sababu ya kutojiunga na *OIC*, kwani tungepata fedha nyingi za misaada, ambazo zingesaidia kujenga miundombinu mbalimbali kwa maslahi ya Wananchi wa Tanzania na sio kama jina linavyosomeka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa baadhi ya wawekezaji na makampuni makubwa bado wana kasumba ya kuagiza bidhaa muhimu kwa matumizi binafsi, ambavyo ndani ya nchi vinapatikana, bado Serikali ingetoza kodi kama zinavyofanya nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la misahama ya kodi ambayo inafanyika ndani ya nchi, kiasi ambacho hivi sasa inatisha na kupelekea nchi kukosa mapato kwa manufaa ya kuiendeleza

nchi yetu. Ningeshauri kama ni lazima, basi iletwe sheria Bungeni, irekebishe suala la mapengo kama lipo ili tuondoe kadhia hii ambayo inaweza kutatulika kimazungumzo.

Mheshimiwa Spika, lazima suala la chakula tulizungumze kiuzalishaji na kiuchumi; hivyo, tunapaswa kabisa Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na wadau mbalimbali, hasa Kamati ya Fedha na Uchumi, wakae pamoja mapema ndani ya mwaka huu, kikongamano la mikakati, kuona tunaanzia wapi kuhusu kilimo chenye tija mapema kabla ya Bajeti ya mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha ingeangalia kwa kina, suala la ulipaji kodi katika Sekta ya Madini hasa wawekezaji kutoka nje. Binafsi, naipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mipango yake mizuri ya kuanzisha viwanda vya machinjio, kwani vitaboresha pia mapato ya ndani kwa ajili ya mauzo ya nje.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Fedha, kwa umahiri wake katika kuhamasisha ujenzi wa Bandari ya Zanzibar, kwani itasaidia kuboresha uchumi wa Tanzania kwa ujumla.

Mwisho, nashauri katika bajeti zijazo; Mawaziri, Magavana, Makatibu Wakuu wa Wizara za Fedha za Afrika Mashariki, wakae pamoja kuboresha bajeti zao mapema. Suala hili lijumuishe na wastaafu wa taasisi hizo. Naitakia kila la heri Bajeti ya mwaka 2008/09. Ahsante.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyouliza katika swali langu kuhusu ucheleweshaji wa fedha za bajeti ni kweli kabisa fedha huchelewa sana; hivyo, utekelezaji wa bajeti huchelewa kwa miezi minne au mitano hivyo Serikali kushindwa kuteleleza bajeti yake. Miradi inayoathitika ni kama ifuatayo:-

(a) Miradi ya Ujenzi wa Barabara zote za *TANROAD* Mikoa na a Wilaya, hutekelezwa kwa miezi saba tu ya mwaka tena kwa kipindi cha masika; hivyo, huharibika mara tu zinapotengenezwa. Tunapoteza fedha za Serikali kwa mtindo huu.

(b) Miradi ya Ujenzi wa Majengo ya Serikali mfano, Zahanati, Hospitali, Vituo vya Afya, Madarasa ya Shule, Madaraja na kadhalika, mengi husimama kwa ukosefu wa fedha.

Kipo kifungu katika Katiba kinachomruhusu Rais kusaini kuidhinisha fedha mara Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali yanapopitishwa na Bunge. Ili kuondoa kero katika Halmashauri zetu, naomba utoe tamko mwaka huu wa 2008/09 fedha zitapatikana lini?

Uchumi wa Kijiografia wa Tanzania; usipotumia fedha kuwekeza katika miundombinu huwezi kuvuna fedha toka nchi jirani. Uwekezaji wa nchi yetu katika barabara za kuelekea DRC (Manyoni - Tabora - Kigoma) ni wa muda mrefu; Mtwara – Songea - Mbambay nao unakwenda mwendo wa kinyonga. Bandari zetu za Dar es Salaam na Tanga zipo *ICU*. Hivi Serikali inafahamu kweli somo la uchumi wa kijiografia?

Je, Serikali inafahamu mzigo wa madini uliopo Lubumbashi Congo, unavyoweza kuinufaisha Tanzania ukichukuliwa kupitia Kalemie - Moba - Kasanga - Tunduma? Hivi Serikali ikigharamia reli toka Tunduma hadi Kasanga km 280; reli hii inaweza kujilipa kwa

chini ya miaka kumi na pia kuongeza matumizi ya reli ya Tazara upande wetu wa Tanzania (Tunduma – Dar es Salaam – Kasanga).

Hivi toka tupate uhuru tuemshindwa kuongeza reli ya Mpanda kwenda Karema km. 130 tu?

Mheshimiwa Waziri, kwa taarifa, eneo la magharibi ndio eneo pekee lenye rasilimali itakayoweza kuongeza uchumi na Pato la Tanzania. Sehemu nyingine tunakopeleka miundombinu ni huduma tu wala si kwa ajili ya Biashara ya Kimataifa. Wakati ni huu, tusipoziba ufa tutashindwa kujenga ukuta; kwa nini ujenzi usianze mwaka 2008/09?

Tuwaombe Wachina waijenge reli hii na waiendeshe kibiashara, kwa sababu wao ndio wanaochimba madini huko *DRC* na *Zambia*.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, wakati nikichangia hoja hii tarehe 17 Juni, 2008 niligusia juu ya Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato (*Ammendment of Income Tax Act, Cap. 332*) na kuonyesha kwa mfano, jinsi mjasiriamali atakavyoathirika na ongezeko la viwango vipya vya kodi katika mfumo wa biashara. Napenda kutoa ushauri wa viwango vifuatavyo ili kuendelea kujenga msingi bora wa kodi kukuza biashara.

Kabla ya kutoa ushauri huo, napenda kueleza kwamba, viwango vya kodi vilivyowekwa miaka ya 2004 hadi 2008, kabla ya Mapendekezo haya ya kuvibadilisha, vilisaidia sana kuwavuta wafanyabiashara wadogo kujiandikisha kama walipa kodi na kuwa na *TIN* Namba. Hii ilisaidia kulipa kodi ya mapato ya viwango vya chini kati ya Sh. 36,000 na 95,000 kwa mwaka.

Ninao ushahidi wa vijana niliowashawi kufanya hivyo huko Muheza na Dar es Salaam (Mbagala).

Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo yafuatayo:-

1. *Where total income does not exceed* kiwango cha kodi Shs. 1,200,000 *per year*
- *Nil.*

2. Wigo wa Mapato

(i) Zaidi ya 1,200,000 – 360,000

(a) Wastani wa chini TShs. 2,000,000

kwa hiyo, $2,000,000 - 1,200,000 = \frac{800,000 \times 10}{100} = 80,000/=$

(b) Wastani wa Juu Tshs. 3,600,000

Kwa hiyo, $3,600,000 - 1,200,000 = \frac{2,400,000 \times 10}{100} = 240,000/=$

3. Wigo wa Mapato

(i) Zaidi ta 3,600,00 - 6,000,000 240,000/=

(a) Wastani wa chini TShs. 4,000,00

$4,000,000 - 3,600,000 = \frac{400,000 \times 10}{100} = 40,000/=$
280,000/=

(b) Wastani wa Juu: TShs. 6,000,000	240,000/=
$6,000,000 - 3,600,000 = \frac{2,400,000 \times 10}{100}$	+
	<u>240,000/=</u>
	480,000/=

4. Wigo wa Mapato

(i) Zaidi ya 6,000,000 – 9,000,000
480,000/=

(a) Wastani wa chini 7,000,000	
$7,000,000 - 6,000,000 = \frac{1,000,000 \times 10}{100}$	= <u>100,000/=</u>
	580,000/=

(b) Wastani wa Juu Sh. 9,000,000	=
580,000/=	
$9,000,000 - 6,000,000 = \frac{3,000,000 \times 10}{100}$	+
<u>300,000/=</u>	
	880,000/=

5. Wigo wa Mapato Zaidi ya Sh. 9,000,000	/=
+ asilimia 20% ya kiasi zaidi ya	880,000/=
	9,000,000/=

(i) mfano = 1,000,000	8800,000/=
Jumlisha $10,000,000 - 9,000,000$	+
$= \frac{1,000,000 \times 20}{100}$	<u>200,000/=</u>
	1,080,000/=

Mfano (ii)

Pato - Tsh. 15,000,000	=
15,000,000 - 9,000,000	+
$= \frac{6,000,000 \times 20}{100}$	<u>1,200,000/=</u>
	2,080,000/=

Mfano (iii)

Mauzo ya TShs. 30,000,000 – Kodi	=
880,000/=	
Jumlisha 20% ya Pato zaidi 15,000,000	
Sawa na $\frac{15,000,000 \times 10}{100}$	= <u>1,500,000</u>
	2,380,000/=

Mfano (IV) Mauzo ya Sh. 50,000,000	kodi	880,000/=
------------------------------------	------	-----------

$$50,000,000 - 15,000,000 = \frac{35,000,000 \times 20}{100}$$

$$\begin{array}{rcl}
 6. \text{ Pato - TShs. } 15,000,000/= & & 880,000/= \\
 \text{Kwa hiyo } 15,000,000 - 9,000,000 & & \\
 = \frac{6,000,000 \times 20}{100} & + & \frac{1,200,000}{100} \\
 & & \text{Kodi} \quad \quad \quad \text{2,080,000/=}
 \end{array}$$

Hata hivyo, ipo haja ya kuangalia viwango vya kodi kwa mapato yanayozidi Tshs.15,000,000/= kwa vile viwango vya malipo vinaweza kuzidi asilimia 10 ya mauzo jambo ambalo litakuwa mzigo mzito kwa wafanyabiashara hao wakubwa.

$$\begin{array}{rcl}
 \text{Mfano: Mauzo ya } 30,000,000/= & & \\
 \text{Kodi} & & 880,000/= \\
 20\% \text{ ya } \frac{15,000,000 \times 20}{100} & + & \\
 & & = \frac{3,000,000}{100} \\
 & & \text{Kodi} \quad \quad \quad \text{3,880,000/=}
 \end{array}$$

Kiwango hiki kinapingana na pendekezo katika kitabu cha hotuba ya bajeti, ukurasa wa 36, kifungu cha 50 sehemu (ii) ambapo kiwango cha asilimia 0.3 ya mauzo ghafi kinatumika.

Mheshimiwa Spika, naomba mapendekezo haya yafanyiwe tathmini ili tusiwakatishe tamaa wafanyabiasara wadogo wadogo ambao watakuwa wakubwa kesho.

Nilisema nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naiomba Wizara kupitia Hazina, watusaidie kuzingatia maombi haya.

MHE. ANIA SAID CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi bajeti hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi.

Napenda kumpongeza Waziri na Manaibu Mawaziri na Wataalam wao, kwa kuleta bajeti ambayo ina wigo zaidi katika kuleta maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, natoa maoni yangu kuhusiana na kupandisha kodi ya vinywaji. Maji ya kunywa ya chupa, ambayo hivi sasa wananchi wengi wameanza kunywa maji safi na salama ni muhimu. Hata vijijini utakuta maji safi yapo. Sasa kupanda kwa kodi, kutarudisha nyuma hatua tuliyofikia na kuanza kunywa maji machafu na kusababisha ongezeko la maradhi nchini, kinywaji hiki kiangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, bandari ya Dar es Salaam, Mtwara, Tanga na bandari za maziwa, zipewe kipaumbele. Bandari hizi zikiboreshwa, Taifa litapata mapato zaidi na kuinua uchumi wa nchi na nchi jirani zitatumia bandari hizi zaidi kuliko zinavyotumika hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvuvi, kuna meli za kigeni ambazo zinavua katika bahari yetu, naomba malipo wanayolipa yaangaliwe upya ili kukidhi haja kutokana na mavuno ya samaki wanayovuna na pato la Taifa liongezeke.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wavuvi wadogo wadogo, kumekuwa na kilio kwa wananchi hawa ikiwa pamoja na kuchomewa nyavu zao ambazo haziruhusiwi Naomba wafanyabiashara wa nyavu haramu, nao wachukuliwe hatua ili wasiingize nchini mwetu nyavu hizo haramu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, hivi sasa duniani kote, tunaelekea katika tatizo la chakula na mfumuko wa bei. Sekta hii tuiongezee uwezo kwa kuwapelekea mahitaji muhimu kwa kuwapatia mikopo wakulima wadogo wadogo, kuongeza viwanda vya mbolea na kuongeza wataalamu wa kilimo na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, umaskini unaendelea kuumiza Watanzania. Hivi sasa, nishati kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, imepanda sana. Nashauri matumizi ya Motopoa, itolewe elimu juu ya matumizi yake. Gesi hivi sasa inasaidia katika matumizi, iendele kupunguzwa kodi kwa sababu mkaa hivi sasa Dar es Salaam gunia ni Sh.30,000/- bado Mtanzania wa kijijini hawezi kutumia nishati hizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, naipongeze Wizara kwa kuiongezea fedha Wizara ya Elimu lakini lazima Wizara izingatie sasa kuboresha shule zetu kwa kuzipatia vitendea kazi na kuhakikisha Walimu wanalipwa mafao yao yote.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi, utaratibu huu mpya wa kuangalia ni vigezo gani vinastahili kwa watu kupewa misamaha kwa mfano, taasisi za kidini na Serikali na kadhalika katika kupunguza misamaha hii, Serikali itaongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza TRA kwa kazi kubwa wanayoifanya ya ukusanyaji kodi na kuongeza pato la Taifa.

MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuisikia hotuba ya bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid, kwa hotuba yake ya bajeti mbadala ambayo imezumgumzia maisha ya mwananchi vijijini na mijini.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wangu juu ya bajeti hii, naona haikumsaidia mtu wa kawaida bali imempa nafasi tena wafanyabiashara wakubwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika vitu vilivyoondolewa kodi, ni kitu gani kitakachomsaidia maskini ambaye chakula chake si cha uhakika?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu, ingepaswa Serikali kukipa kipaumbele katika bajeti hii lakini Serikali haionyeshi nia njema kwa mkulima wetu. Ni muda mrefu, mkulima huyu analima kwa kutumia jembe la mkono, atawezaje kuipatia nchi yake kipato? Kwa nini Serikali ishindwe kumpatia mkulima huyu vifaa vya kisasa ili aweze kulima kilimo cha kisasa?

Mheshimiwa Spika, wakulima wetu hawana uhakika wa kilimo chao kwani mara zote hutegemea miongo ya mvua. Kukosekana kwa mvua, mkulima huyu anaweza kukosa mavuno na ni mara nyingi sana hali hii hutokea.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa soko la uhakika, mbolea, Mabwana Shamba na pia bei nzuri, mambo haya pia ni dosari kubwa kwa wakulima wetu. Ni vema Serikali, iandae mikakati maalum ili wakulima wetu wawe wakulima bora.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, napoipongeza Serikali kwa kutayarisha mpango wa bajeti nzima kwa mwaka 2008/09 lakini nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jiji la Dar es Salaam na idadi ya watu, naiomba Serikali katika mipango yake yote katika sekta zote mfano huduma za afya (hasa maeneo ya pembezoni) na usafi wa Jiji, itoe ruzuku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la usafi katika Jiji la Dar, ni tatizo kubwa sana. Halmashauri hazina uwezo wa kugharamia usafi wa jiji. Ni bora Serikali kuu itoe ruzuku ili yapatikane makampuni yenye uwezo mkubwa na utaalum wa kusafisha jiji hilo. Usafi ni kivutio kimojawapo cha kuleta watalii hapa nchini na pia hupunguza fedha za Serikali kununua madawa ya magonjwa yanayotokana na uchafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu, ulinzi na usalama, ajira kwa vijana na wanawake. Sekta zote hizo zinahitaji mtazamo wa pekee toka Serikalini kwa sababu sekta hizo chache zina umuhimu mkubwa. Naomba Serikali kwa kila bajeti zake za kila mwaka, iangalie Mkoa wa Dar es Salaam kwa mtazamo mpana zaidi kulingana na idadi ya watu na shughuli zake na pia ikizingatiwa 80% ya mapato ya Serikali yanatoka katika Mkoa huu wa Dar.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. USSI AMME PANDU: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kuchukua nafasi hii, kuipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi, kupitia Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na wataalamu wao kwa kuweza kuwasilisha bajeti hii ya mwaka 2008/09 ambayo inaonyesha kukidhi haja na kumsaidia Mtanzania wa chini na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusu mapato ya ndani, naomba pia kuipongeza TRA, kwa juhudi kubwa wanazofanya za kukusanya mapato ya shilingi bilioni 328.6 katika mwezi Desemba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na TRA, namwomba Waziri ajaribu kuondoa tatizo linalofanywa na TRA kwa upande wa Zanzibar kwa kumaliza malalamiko ya kuwalipisha mara mbili ushuru watu kutoka Zanzibar ili kuondoa ile dhana ya uonevu katika Jamhuri hii moja ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, Tume ya Pamoja ya Fedha, pamoja na nia njema ya Serikali kuunda Tume hii, bado inaonekana kuna urasimu mkubwa ambao unakwamisha kumalizika kwa utekelezaji wake. Hivyo Mheshimiwa Waziri, ni lazima achukue hatua za makusudi kuona Tume hii inamaliza makubaliano hayo na Zanzibar ili kupata gawio jipya ambalo litawezesha Zanzibar kujikwamua na umaskini pamoja na kuendesha nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, naongezea kwenye maelezo yangu niliyotoa kwa kuongea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tozo la kodi ya 0.3% *on turnover* kwa *perpetual loss makers*, napendekeza baadhi ya sekta zisihusishwe nazo ni:-

(1). Wawekezaji katika Kilimo (*only those who till the land*). Hii ni kwa kuwa ukiwekeza kwenye kilimo, *retun* haipatikani haraka hasa kilimo cha mazao ya kudumu kama kahawa, korosho, minazi na kadhalika. Kwa kuwa "*gestation period*" mara nyingi, ni zaidi ya miaka mitatu hivyo tuifikirie sekta hii na pia tuvutie wawekezaji.

(2). *Fish farming* kuna sababu kama zilivyotajwa hapo juu kwenye Na.1

3. Elimu, uwekezaji kwa mtu anayejenga shule kwa mfano, huwa unaendelea kwa muda mrefu kabla ya kuanza kupata faida. Kwa mfano, katika ujenzi wa sekondari, huwa ni mpaka unapofikia *Form IV*, ndipo unaweza kuanza kupata faida. Uongezaji wa mapato ni *gradual*. Huwezi kuwa na *Form I* na *Form II*, ukategemewa kuanza kupata faida.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Spika, naomba kutamka wazi kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kulingana na bajeti hii, napenda kuipongeza Serikali kwa kuamua kujisimamia yenyewe bila ya utegemezi.

Mheshimiwa Spika, naamini bajeti hii baadaye huzaa uchumi kukua na kukopesheka katika nchi nyingine au pia hata katika Mabenki mengi ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bilioni moja kwa kila Mkoa, pesa hizo mimi zimenipa shaka, je, zoezi hilo litakuwa endelevu au ndio mwisho?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ZNZ, nina usemi usemao 'ukibebwa jibebekeze'. Iweje wenzetu hawa asilimia 96 ya bajeti yao kuwa na msamaha kiasi kikubwa hivyo? Nina imani, hapo kuna tatizo. Ni lazima kuwe na mazungumzo ya pamoja Bara na Visiwani ili kuwe na mapato makubwa kwa upande wa ZNZ na kupunguza shida mbalimbali zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mawaziri na watendaji, kwa kupanga bajeti ambayo imewajali wananchi ila sjaridhika na kutojali kilimo. Katika bajeti hii, kilimo ni moja ya chanzo cha mapato hapa nchini na nina imani, kadri miaka inavyokwenda, suala la kilimo litaongeza ukuaji wa uchumi kwa asilimia kubwa sana. Nchi yetu, ni nchi yenye ardhi nzuri sana, kwa kweli sekta hii inahitaji msaada mkubwa sana. Kuwepo na changamoto za kilimo kama ilivyo kwenye UKIMWI. Laiti kilimo tungekisimamia kama tunavyosimamia UKIMWI, tungefika mbali.

Mheshimiwa Spika, nina maoni yafuatayo:-

1. Kuunda Kamati za Kilimo Kimkoa, Kiwilaya, Tarafa na Kata;

2. Kuwepo na taarifa za kila kipindi cha miezi sita kuhusu suala la ongezeko la chakula kwa baadhi ya Mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka;
3. Kila Mkoa, wawe na ongezeko la mazao kwa kila mwaka na takwimu ziwe ni za kweli na wafanye mikutano ili watoe hoja zao na kufanya makubaliano kwa kushirikisha wananchi; na
4. Kuwepo na usimamizi wa upandaji wa bei ya vyakula kila Mkoa ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa bei hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ATHUMANI SAID JANGUO: Mheshimiwa Spika, Waziri na Wasaidizi wake, nawapongeza sana kwa bajeti nzuri iliyozingatia yafuatayo:-

1. Kuugawa uchumi wetu katika “clusters” nne badala ya sekta tisa zilizokuwepo miaka ya nyuma. Ugawaji huu utarahisisha upimaji wa utekelezaji wa maeneo haya machache;
2. Kwa mara ya kwanza, mmepanga bajeti yote ya matumizi ya kawaida kulipiwa kwa fedha zetu wenyewe; na
3. Mmepunguza utegemezi kutoka 42% hadi 34%.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rai ya kuelekeza rasilimali kwenye maeneo machache yatakayokuza uchumi kwa haraka lakini ugawaji katika bajeti hii hauendani na rai hii kwani sekta za kilimo na miundombinu, hasa barabara vijijini, hazikupewa kipaumbele kibajeti. Nashauri maeneo haya, yaongezewe rasilimali ili yaweze kuzalisha kwa manufaa ya sekta nyingine katika bajeti zijazo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bajeti ya kilimo imepunguzwa kutoka 6.2% na sasa ni 4%, ndiyo maana michango ya sekta hii imekuwa ikupungua kutoka asilimia 5.9 mwaka 2004 hadi 4% mwaka 2007. Matokeo yake ni ukuaji wa pato la Taifa kushuka kutoka asilimia 7.8 hadi asilimia 7.4 mwaka 2005 na asilimia 7.1 mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha “*The Maputo Declaration*” ya 2003 ambapo viongozi wa Afrika, kwa kutambua balaa la njaa Barani Afrika, waliamua kuwa bajeti za Serikali ziwe zinatenga si chini ya asilimia 10. Haitoshi kutegemea sekta binafsi, Serikali lazima ionyeshe njia katika bajeti zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgao wa bajeti, katika bajeti hii, miradi inayosimamiwa na Mikoa na Serikali za Mitaa, imegawiwa asilimia 16 tu wakati inayosimamiwa na Wizara za Serikali, imepangiwa asilimia 84. Nashauri katika bajeti zijazo, tupeleke fedha nyingi kule iliko miradi, hii ndio maana ya “Mpango wa *D by D*”.

Mheshimiwa Spika, naelewa kuwa upungufu wa uwezo wa usimamizi kwenye Serikali za Mitaa lakini tuanzie na “*empowerment*” kwa maana ya kutoa mafunzo kwa wahusika ili wawe na uwezo wa kusimamia miradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu riba ya mikopo, wakati riba ya kuwekeza Benki haizidi asilimia 2.6, riba ya mikopo ni kati ya asilimia 16 – 20. Hali hii haisisimui uzalishaji lakini riba katika benki za biashara, zinaongozwa na riba za Dhamana za Hazina (*TBS*).

Mheshimiwa Spika, mfano ulioonyeshwa kati ya mwaka 2007 na mwaka huu kwa Serikali kupunguza mikopo ya ndani na marekebisho ya sera ya fedha yaliyofanywa na Benki Kuu, hata riba za mikopo zikashuka kwa 1%, hapana budi uendelezwe ili riba zishuke, ikiwezekana hadi chini ya asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, Sheria mbalimbali za fedha zilizotajwa katika bajeti, ziletwe Bungeni nasi tutazipitisha.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya maji haina budi kuongezwa ili sehemu zenye matatizo, ikiwemo Kisarawe zipatiwe fedha ili zitatue tatizo la maji. Mji wa Kisarawe uliomba Sh.300m. Nashauri mumsaidie Waziri wa Maji asigombane na wananchi wa Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Kilimo, pamoja na kuongeza mtaji wa *TIB* na kumaliza mchakato wa *Morgage Financing*, nashauri Muswada huu uletwe hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja yako.

MHE. MOHAMED HABID JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Serikali ya mwaka huu 2008/2009, mafuta ya petrol, dizeli, *kerosene*, hayakuongezwa kodi yoyote lakini ile kodi ambayo iliongezwa katika bajeti iliyopita madhara yake tunayaona hadi hivi leo. Kutoongezwa bei ya mafuta ni kwa sababu ya bei zilivyopanda duniani. Jambo hili halijatoa nafuu hata kidogo kwa wananchi. Hatua zilizoweza kuleta manufaa kwa wananchi, ni mbili tu:-

- (a) Kufidia kiwango fulani cha fedha ili bei iwe “*stable*”.
- (b) Sheria tuliyoipitisha hivi karibuni ya “*Petroleum Act*” ambayo *TPDC* imepewa uwezo wa “*ku-reservice*” na kuagiza mafuta na kusambaza nchini.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu. Pamoja na kuwa mchango wake katika pato la Taifa umepungua lakini tutakapofanya juhudi katika kilimo basi hadhi ya nchi itapatikana lakini asilimia sita iliyotengwa, ni kidogo na inaonekana kama tunadharau kilimo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninataka kumwuliza Waziri wa Fedha na Uchumi, wakati akipanga bajeti hii kuhusu kilimo, je, alisahau “*Maputo Convention*” ya nchi za *SADEC* ya kutenga 10% ya bajeti kwa ajili ya kilimo? Naomba Mheshimiwa Waziri, atoe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, hivi leo hapa Tanzania, utafiti (*research*) imefanywa na ndugu zetu wa *Policy Forum* kuhusiana na vipaumbele vya wananchi na kuwauliza ni nini jambo la umuhimu kwao. Karibuni asilimia mia moja vijijini wanasema wao *priority* ya kwanza, ni maji, *second priority*, ni maji, *third priority*, ni maji, *fourth priority*, ni afya, *fifth priority*, ni miundombinu. Kwa faida ya bajeti mwakani, namwomba Mheshimiwa Waziri afikirie vipaumbele hivi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha, mtaalamu alichaguliwa na kuanza kazi tokea mwaka 2003, kushauri na kueleza vipimo husika vya kugawana mapato na matumizi ya Serikali zote mbili za Jamhuri ya Muungano. Pia kuna taarifa kwamba ameshakabidhi ripoti yake tokea mwezi Agosti 2006. Leo katika hotuba ya bajeti Mheshimiwa Waziri anatuambia Serikali ya Muungano na ya Zanzibar, zinaendelea na zoezi la kupitia na kuchambua ripoti ya Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Mkanyageni, wamenituma niulize swali hili ili liweze kupatiwa dawa. Sasa hivi, imetosha. Hatuwezi kila siku kuambiwa uliza kesho vinginevyo tunaamini Serikali haina nia njema kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Sheria za Forodha, katika ukurasa wa 44 wa hotuba ya bajeti, Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la kusamehe ushuru wa forodha kwenye malighafi na vifaa vinavyoagizwa na kampuni ya *TANALEC* kwa ajili ya kutengeneza mashine za kuongeza na kupunguza nguvu ya umeme (*transformers*) pamoja na *switch gears*.

Mheshimiwa Spika, hili sio jambo jipya, lilikuwepo tokea zamani, sioni kwa nini Mheshimiwa Waziri ametuingizia suala hilo ambalo tokea *TANALEC* ianzishwe, mfumo huu upo, sio mpya au ni ili tuone kwamba Serikali imepunguza ushuru wa forodha? Je, Serikali inamaanisha kwamba bei za *transformer*, sasa zitapungua?

MHE. MWAKA A. RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nimpongeze Waziri na Manaibu Mawaziri pamoja na Watendaji wote ambao wamesaidia kutengeneza hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Uchumi ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano ya Tanzania, ni Serikali ambazo zina nia nzuri juu ya wananchi wao kwa kuwaletea maendeleo, lakini bado suala la kero za Muungano halijapatiwa ufumbuzi hadi leo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba suala hili lishughulikiwe ili liweze kukamilika kwani sasa umekuwa ni muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kujiunga na *OIC* (*Organization Islamic Conference*). Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilijiunga na *OIC* lakini Waziri Mkuu wa kipindi hicho, alisema ijitoe ili Serikali ya Muungano wa Tanzania, ndio ijiunge. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilijitoa lakini mpaka leo hii, Serikali ya Muungano wa Tanzania bado haijajiunga na *OIC*. Tunataka kujua ni kwa nini mpaka leo hawajajiunga na *OIC*?

Mheshimiwa Spika, hii inatupelekea kukosa misaada mingi ambayo haisaidii taasisi maalum wala dini fulani ila ni kwa ajili ya Watanzania wote. Mfano wiki hii Uganda ilifanya mkutano mkubwa wa wajumbe wa *OIC* duniani na ilipangwa mikakati mizuri ya kuisaidia Uganda.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imedhihirika kwamba moja ya uvujaji wa mapato, ni misamaha ya kodi yaani *exceptions* na imeonekana kwamba labda kuna upungufu wa kisheria.

Hivyo nashauri yaletwe marekebisho ya sheria hiyo ili tuikebishe kwa kupitia upya na kuziba mianya hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sera ya ukusanyaji mapato inabagua *TRA* na *ZRB* hivyo kupelekea hofu ya kutoa mwaja kwa walipa kodi. Mimi napendekeza uwepo uhusiano wa karibu sana ili kuzima mwanya wowote unaoweza kutokea katika kuathiri zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba ufafanuzi wa maendeleo ya ujenzi wa Bandari ya Zanzibar ambayo mara kwa mara husita. Pamoja na kwamba Jamhuri ya Muungano imesimamia vizuri zoezi hilo, pia wananchi waeleweshwe kuhusu upanuzi zaidi wa bandari hiyo ambayo umependekezwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uvuvi, Serikali ifanye utafiti wa kutosha juu ya samaki waliomo katika bahari yetu, kwani tuna bahari ya kutosha na pia tuna samaki wengi wa aina tofauti. Hivyo Serikali itafute vifaa vya kisasa vya kuvulia na boti maalum za uvuvi ili kuweza kupata samaki kwa wingi na kuweza kusafirisha nje ya nchi ili kuweza kuipatia mapato nchi yetu. Zaidi ni kuunda benki ya wavuvi ambao ni wengi lakini ni maskini wa kipato, hivyo kupelekea sekta hii kutokuchangia mapato ya nchi yetu kwa manufa ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni jibu la mtu wa kijijini. Hivi maana ya jembe na nyundo ni nini? Ilani ya Uchaguzi ya CCM, hata kwenye nembo yake kuna jembe/nyundo. Jembe ni kilimo. Naiomba Serikali iwakomboe wananchi kwa kuwapatia majembe wakulima, kwa nini tunakuwa tegemezi wa chakula kila mwaka?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa bei za bidhaa za viwandani na chakula, ni wa dunia nzima. Hata hivyo, upo uwezekano wa kupunguza makali hasa kwa bidhaa za viwandani kwa kuweka sera ya *Pan-territorial Price Mechanism*. Maana yake ni kuwa wazalishaji wa bidhaa muhimu kama *cement* na kadhalika wanakuwa na wajibu wa kuhakikisha bidhaa wanayozalisha inawafikia watumiaji katika kila Mkoa kwa bei ile ile kwa Tanzania nzima. Maana yake ni kuwa walaji wa Mikoa ya karibu, kwa kulipa bei sawa na Mikoa ya mbali watakuwa wanafidia (*subsidise*) gharama za usafirishaji na kadhalika. Hivyo, itakuwa hatua ya kuleta usawa kwa sababu wananchi wanaokaa Mikoa ya mbali nao wanayo haki ya kupata huduma sawa kwa bei ile ile sawa na Watanzania wengine. Hiyo ndiyo jinsi ya kuleta usawa na pia kupunguza umaskini hasa kwa wakazi wa Mikoa ya pembezoni.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kufungua akaunti Benki Kuu kwa ajili ya miradi ya Serikali, ni jambo zuri. Haya mabenki ya biashara yamefaidika sana na pesa zetu. Kitendo cha kuondoa pesa zote za miradi kutoka katika mabenki haya, nchi itaaidika sana na huenda ikasaidia kupunguza kasi ya kupungua thamani ya pesa yetu.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu, je, Benki Kuu iko tayari na imejipanga vya kutosha kuchukua jukumu hili kubwa? Ieleweke kuwa zaidi ya akaunti 1000 zitafunguliwa na

pale Benki Kuu, kuna udhaifu kama uliyojitokeza kwenye Akaunti ya EPA. Je, mzigo huu mkubwa tunaowatwika, watauweza au ndio wigo wa ufasadi utakuwa umepanuka?

Mheshimiwa Spika, ili nchi ijitosheleze kwa chakula na kuwa na ziada, lazima tukubali tuwe na *commercial farmers* ambao watalima kwa wingi na sio kutegemea wakulima wadogo wadogo. Nchi jirani kama Kenya wana *commercial farmers*, ambao wanalima mazao ya chakula. Tuwe na wawekezaji wakubwa katika Kilimo. Tusiogope, hapa sio Zimbambwe! Ili Tanzania ikomboke katika kilimo, lazima tuwe na *commercial farmers, big ones*. Nchi kama America, wakulima wanaolima, ni wachache sana na wana jukumu la kulisha Taifa lote na kuwa na chakula cha ziada.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuna tatizo kubwa la bandari yetu ya Dar es Salaam lakini bandari ya Mombasa bado ina jina zuri kwamba bidhaa nyingi za Tanzania hupakuliwa Mombasa. Naiomba Serikali, ikishirikiana na Serikali ya Kenya, kufungua reli ya Mombasa – Moshi. Tungeweza kuwa na *Inland Port* pale Moshi na makontena yote ya Tanzania, yachukuliwe na Tvain mpaka Moshi *Inland Port*. Tutapata faida kubwa na mji wa Moshi ungefufuka na kuondokana na umaskini. Waingizaji wa bidhaa, wakijua mali zao, wataweza kuzifanyia *clearance* Moshi, nina hakika nchi itapata pesa nyingi sana.

MHE. MBARUKU K. MWANDORO: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa maandishi zaidi ya yale niliyochangia kwa kauli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, wananchi wa Wilaya ya Mkinga, wanashukuru sana kwa matayarisho ya barabara ya Tanga – Horohoro kwa kuwekwa lami chini ya MCC. Hata hivyo, wana masikitiko makubwa kwamba tokea uamuzi wa kuwekwa lami, barabara hiyo haifanyiwi matengenezo ya dharura. Matokeo mabaya ya mkwamo mkubwa wa magari yamejidhihirisha. Tunaomba matengenezo ya dharura yaendeleo kufanyika hadi hapo barabara hiyo itakapotengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, pili, Wilaya ya Mkinga bado ina kero kubwa sana ya maji. Mradi wa Benki ya Dunia unasuasua. Uamuzi wa kupunguza bajeti ya maji, si sahihi unastahili kutazamwa upya.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wilaya ya Mkinga nayo ina upungufu mkuwa sana wa Walimu na vifaa vya shule pamoja na maabara. Ni matumaini yetu kwamba mgao mkubwa wa sekta ya elimu, utafaidisha pia Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Spika, nne, Wilaya ya Mkinga ina nafasi nzuri ya kuchangia katika kupunguza makali ya janga la kupanda bei za mafuta kwani kuna uwezekano mkubwa wa kuipata gesi asilia na mafuta ya petroli katika Jimbo hilo linalopakana na Pemba kwa Mashariki. TPDC wawezeshwe kundeleva utafiti ili kuona uwezekano wa kugundua na kutumia gesi nyingi na petroli iliyoko huko.

Mheshimiwa Spika, tano, wananchi wa Wilaya ya Mkinga tunafarijika kwamba tunapatiwa umeme katika vijiji vitatu chini ya mradi wa MCC. Nashauri haya yafanyike mapema iwezekanavyo ili kuondoa kero kubwa iliyopo.

Mheshimiwa Spika, sita, uboreshaji wa bandari ya Tanga pamoja na ujenzi mpya wa reli ya Tanga – Arusha hatimaye hadi Musoma, sio tu utachangia kulisimua uchumi wa maeneo yanayozunguka miundombinu hiyo bali pia uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, saba, ufukwe mrefu wa bahari ya Hindi, unatoa nafasi nzuri kwa Wilaya ya Mkinga kutokana na uvuvi wa bahari hiyo, hivyo mipango ya uboreshaji wa shughuli za uvuvi zihusishe pia Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Spika, nane, upatikanaji wa matrekta na zana nyingine za kilimo, zipatikane chini ya Mifuko ya Pembejeo zaidi ya kuhamasisha sekta binafsi kuwa na vifaa hivyo chini ya Mpango wa Karadha.

Mheshimiwa Spika, tisa, mfumo wa Stakabadhi ya Maghala ambao umefanikiwa vyema huko Mkoa wa Mtwara, ufikishwe Wilaya ya Mkinga katika msimu ujao.

Mheshimiwa Spika, kumi, mgao wa fedha kwa ajili ya ujenzi na kuendesha Ofisi za Wabunge, uwe wazi zaidi na inapowezekana, mfumo bora zaidi wa kufikisha mgao huo kwa ofisi za Wabunge, ubuniwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Mawaziri wake wote wawili, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalamu wao wote, kwa kuweza kuwasilisha hotuba zao zote mbili, mbele ya Bunge lako hili Tukufu, kwa ufasaha na ufafanuzi wenye kueleweka na kwa kuwajali walio wengi ambao wanahitaji wapate jicho la huruma kwa Serikali yao. Hili limefanyika kwa kiasi kikubwa kutokana na hali halisi ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Spika, hali ya Tanzania hivi sasa, mafuta ni siasa. Hali ya mafuta pamoja na kuwa ni jambo lililosambaa ulimwengu mzima, ningeshauri Serikali kuwa makini zaidi kwani upandaji wake umekuwa si wa kawaida kwani leo unaweza kukuta bei nyingine na kesho ukakuta imepanda bila ya taarifa yoyote yaani ni kama mchezo wa kuigiza. Sasa hiyo ni hatari, haiwezekani biashara huria ikawa ndio huria bila Serikali kuingilia kati.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaa wawekezaji ambao kama tutaweza kuwatumia vizuri basi tunaweza kupata faida kwa kuwatumia wao hasa wale wanaowekeza kwenye ardhi. Ni vizuri waitumie ardhi hiyo kuzalisha chakula cha kuwafaa wao na kuwauzia wengine.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi, wana uwezo na akili ya kuweza kufanya mambo mengi ambayo yanaweza kuinua uchumi wa nchi hii lakini tatizo ni msingi wa kuleta maendeleo hayo kutokana na kukosa mikopo mikubwa ya kuweza kufanya kazi zenye kupata kipato kikubwa kwani mtaji mdogo hata mapato yake yatakuwa madogo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la magari yenye usajili wa Zanzibar. Pamoja na kutakiwa kulipa tofauti ya ushuru uliolipa Zanzibar, hivi sasa unatakiwa ulipie na uchakavu kwa gari inayotoka Zanzibar. Hivi najiuliza, Zanzibar nayo hivi sasa imekuwa sawasawa na Dubai au nchi yoyote ile ilioko nje ya Tanzania Bara?

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii, ahsante.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, vipaumbele vilivyowekwa kwenye elimu, miundombinu, afya na kilimo, ni sawa lakini nashauri bajeti ijayo ya mwaka 2009/2010, kipaumbele cha kwanza kiwe miundombinu. Uimarishaji wa miundombinu ya barabara na reli, ni muhimu zaidi katika kufikia maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla. Wananchi wengi watatumia fursa hii kujiajiri kwenye sekta ya kilimo na biashara ikiwa watakuwa na uhakika wa kusafirisha mazao yao na bidhaa za biashara kwenye masoko. Shule na vituo vya afya vitafikika pale ambapo kuna ukakika wa usafiri. Kilimo, elimu, biashara, afya, vyote vinategemea miundombinu ya barabara, reli na usafiri wa bahari na anga.

Mheshimiwa Spika, pili, ni lazima tuwekeze zaidi kwenye nishati. Mpaka sasa ni asilimia 10% tu ya watu wetu ndiyo wenye fursa ya kutumia umeme. Tunahitaji nishati hii zaidi kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo vijijini ili kuwakomboa wananchi kiuchumi.

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo yangetiliwa mkazo kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni miundombinu. Uuzwaji wa vyuma chakavu, biashara hii inaharibu sana miundombinu mingi katika barabara zetu hasa Mkoa wa Lindi kwani barabara nyingi zinahujumiwa na wananchi wasiopenda maendeleo katika nchi yetu. Wahujumu hao wanatumia gasi kwa kuchoma vyuma vilivyopo kwenye barabara hususani madaraja. Hivyo, naiomba Serikali, itoe tamko rasmi kuhusiana na ubadhirifu huu.

Mheshimiwa Spika, pili, Wakandarasi wasio waaminifu au wasio na uwezo, wasipewe mikataba ya kutengeneza barabara hapa nchini kwani wanarudisha maendeleo ya Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa mfano, Mkandarasi B.D. SHAPRIA, alipewa tenda ya kujenga barabara ya Tingi – Kipatimu, amedhoofisha sana maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kujua barabara ya Ndundu – Somanga (60km) ambayo ingekuwa chachu ya maendeleo ya wananchi wa Mikoa ya Kusini, mbona inacheleweshwa na wananchi wanazidi kuumia kiuchumi kutokana na barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuhusu bandari. Tunazungumzia bandari zilizopo hapa nchini kama vile Tanga, Dar es Salaam na Mtwara, mbona tunaisahau bandari ya Kilwa ambayo ina hadhi sawa na bandari zingine zisemwazo? Mbona Serikali mnaisahau Kilwa ili wananchi nao wafaidike kwa sababu kuwepo kwa bandari Kilwa, uchumi wa Kilwa utakua na ajira itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, nne, ni kuhusu nishati. Wananchi wa Kilwa Kaskazini wanasononeka sana kuona umeme unaozalishwa kwenye Wilaya yao na wenyewe wakiwa gizani. Tunaomba Serikali iwaangalie wananchi hawa kwa jicho la huruma. Kwa mfano, mradi wa SONGAS tueleweje?

Mheshimiwa Spika, tano, ni kuhusu benki. Benki ya *NMB*, ambayo ipo Kilwa Masoko, msaada wake ni mdogo mno kwa watu wa Kilwa Kaskazini ambao wanaishi mbali na Kilwa Masoko hasa wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza Serikali kwa kusimamia uuzaji wa korosho katika Mkoa wa Lindi msimu huu kwa kuuza katika Chama cha Ushirika cha Ilulu. Hivyo tunategemea na zao la ufuta lifanyike hivyo hivyo ili mapato ya Mkoa yapande na uweze kuendelea kama Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) isemavyo. Tunaomba hii tabia ya walanguzi kununua mazao yakiwa bado mashambani tena kwa bei ya chini, ikemewe. Naomba tabia hii ikomeshwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

MHE. BENSON M. MPYESYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niunge mkono hoja hii kwa sababu kubwa kuwa imezingatia mambo mengi mazuri yatakayoisaia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba msaada wa Serikali hususani Wizara hii, katika kuhakikisha kuwa soko la Mwanjelwa – Mbeya mjini, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, lipewe *go ahead* ya kukopa kiasi cha Tsh.15bil baada ya kuunga soko la awali miaka miwili iliyopita. Halmashauri yangu, inakopesheka. Tunachomba ni *facilitation* ya Wizara ili tuupate mkopo huo.

Mheshimiwa Spika, tatu, jiji la Mbeya, lilikuwemo katika mpango wa kuwepo kwa *EPZ* (*Export Processing Zone*), tatizo lilikuwa ni kupata eneo linalofaa kwa ajili ya mradi huu. Tayari tumepata eneo kubwa la kutosheleza ujenzi wa *EPZ*. Kimsingi, kukamilika kwa mradi huu, itakuwa ni kutimiza ahadi ya Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, juu ya kufufua viwanda Mbeya mjini.

Mheshimiwa Spika, naomba msukumo wa Serikali kuhakikisha jambo hili linaanza kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kuwa wazima na salama.

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia kwenye hali ya uchumi wa Taifa, ukurasa wa 20, Mheshimiwa Waziri anasema:-

“Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, Serikali itaweka mkazo katika kudhibiti uvuvi haramu na kuhifadhi katika maeneo tengefu...”

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na mazingira, mazingira ni muhimu lakini Serikali yetu inatilia maanani wavuvi haramu hawa wavuvi wadogo wadogo tu lakini wavuvi wakubwa wao hawaulizwi matokeo yake tunawaonea wananchi wetu kwa kuwazuia kutafuta riziki zao halali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo tengefu, nayo wanayafanya *marine park*, zile sehemu nzuri na kuwazuia wananchi wetu wasiweze kufanya kazi katika sehemu hizo na baya zaidi wanaposema uvuvi huu ni haramu au sehemu hii ni tengefu hawawapi sehemu nyingine mbadala, wanawaacha tu. Je, katika hali kama hii, kweli umaskini utamalizika Tanzania?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumza ni kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha kuhusu mgao wa mafao ya Muungano. Kila tunapofika wakati wa bajeti, tunaambiwa kuwa bado mazungumzo yanandelea, mazungumzo hayo yatakwisha lini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Serikali kupunguza utegemezi toka asilimia 42 mpaka asilimia 34, naona Serikali imetekeleza wajibu wake na wala sio jambo la kusifiwa san asana ilikuwa ni aibu kwa sababu tulikuwa tunapewa msaada hata fedha za matumizi yetu ya kawaida.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Spika, hii ni nyongeza ya mchango wangu siku ya leo. Muda wa dakika kumi na tano, haukutosha kumalizia ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuendelea kuimarisha uwezo wa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Mameya wote nchini ili waweze kusimamia utekelezaji wa bajeti, kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na usimamizi wa fedha za umma katika mamlaka zao, je, Serikali inafikiria nini juu ya nafasi ya Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji pamoja na Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Mameya ambao wako karibu na wananchi vijijini? Kwa kuwa, fedha nyingi ya Ruzuku ya Maendeleo (*Local Government Capital Development Grant*) na Matumizi Mengine “*Other Charges*” (OC), inayoelekezwa kwenye Halmashauri za Wilaya, hupotea kutokana na upotevu, ubadhirifu au kazi inayofanywa kutolingana na fedha zinazotolewa (*value for money*).

Mheshimiwa Spika, Serikali haioni kwamba ni vyema badala ya kujikita kwenye uongozi wa juu ngazi ya Wilaya pekee ikaongeza uwazi mwaka ujao wa fedha 2008/2009 ili Wabunge wajue fedha inayopelekwa kwenye Halmashauri na miradi inayogharamiwa? Pia Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wapewe posho na maslahi ya Madiwani mafao/posho zao ziboreshe zaidi ili usimamizi wa miradi uwe na tija. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atoe msimamo wa Serikali kwenye hili.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itumie Brigedi za ujenzi za Majeshi yetu kwa kuzipatia fedha za kutosha ili kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi wa nyumba, barabara, madaraja na mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji ili tukabiliane na changamoto ya upungufu wa makandarasi wenye uwezo, ujuzi, vifaa na uzoefu wa kutosha. Aidha, uamuzi huu utatuongezea uwezo wa kujitegemea na kuepusha fedha nyingi kupelekwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikope fedha kutekeleza mpango wetu wa umeme vijijini ili tuweze kuanzisha viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo. Aidha, Serikali inapaswa kuanzisha viwanda vya samaki kama ilivyoamua kuanzisha viwanda vya nyama.

Mheshimiwa Spika, Serikali isijiondoe kwenye biashara kabisa. Viwanda vya mboleo kwa mazingira ya uchumi wetu, vijengwe na Serikali na baadaye kuviuza kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kusimamia uchumi na mapato ya Serikali na hivyo kuweza kujitegemea kwa matumizi ya kawaida na kupata ziada ya kuchangia maendeleo, wakati umefika Wilaya ya Muleba kugawanywa katika Wilaya mbili. Jimbo la Muleba Kusini, ni kubwa, lina watu wapatao laki tatu sasa. Kwa mujibu wa makisio ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu Novemba 2007, Jimbo la Muleba Kusini linakadiriwa kuwa na idaidi ya watu 288,293. Naomba Waziri wa Fedha na Uchumi, aweke katika mipango yake ya mwaka 2009/2010, kutupatia hadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uchumi wetu na mapato ya Serikali yanatia moyo, Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa nini asiishauri Serikali watoto yatima na watoto kutoka familia maskini sana wasichangie chochote katika elimu ya sekondari hadi Chuo Kikuu? Watoto wetu hawa na walezi wao wahangaika sana na wengine wanaathirika.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Uchumi katika hotuba yake, ameeleza kuimarisha mtaji wa Benki ya Rasilimali (*TIB*) ambayo ni benki ya umma kama ilivyo Benki ya Posta, je, Waziri, anaweza kutueleza, Serikali imeweka juhudi gani kuimarisha mtaji wa Benki ya Posta ambayo ina mtandao mkubwa zaidi hadi Mikoani kuliko *TIB* na inahudumia watu wengi zaidi? Waziri atueleze mtaji wa Serikali katika Benki ya Posta ni shilingi ngapi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi ameeleza ukurasa wa 11, kuwa utaratibu wa kukusanya maduhuli (*retention*) umeimarishwa ili wale wanaokusanya maduhuli makubwa wasirudi nyuma. Je, Waziri anaweza kufafanua zaidi?

Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko kwamba Idara na Wizara zinazokusanya maduhuli hazifaidiki na ongezeko la makusanyo kwa sababu bajeti iliyoidhinishwa haiongezeki! Makusanyo ya maduhuli hupunguza gawio toka Hazina! Kwa mfano kama bajeti ni bilioni 70, Wizara ikikusanya maduhuli bilioni 10, Hazina igawie Wizara bilioni 60, motisha uko wapi? Mantiki ya "*retention*" iko wapi? Maelezo zaidi yanatakiwa kutoka kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wa kuchangia bajeti hii haukutosha, naomba mchango wangu uliosalia niuwasilishe kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya sheria zilizoanishwa ukurasa wa 34 wa Kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2008/2009, ndiyo yanayoifanya bajeti ya Serikali kuvuta hisia nzuri kwa wananchi kwani mapendekezo ya kupunguza na hata kufuta kodi kwa maeneo mengine, yatapunguza makali ya maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na msamaha wa kodi, ongezeko la thamani kwenye mafuta mazito yanayotumika kama nishati ya kupikia (mfano Moto poa), ninaimani bei ya mafuta hayo itakuwa haipandishwi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, kampuni kama hii ya Motopoa na nyinginezo zinabuni matumizi ya teknolojia ya matumizi ya nishati mbadala kwa kulinda mazingira. Serikali iziombe kampuni hizi kuisambaza elimu hii vijijini na mijini kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Serikali imetoa punguzo la kiwango cha kutoza ushuru wa bidhaa kwenye magari kutoka mfumo wa sasa wa asilimia 10 kwenye magari yenye ukubwa wa injini unaozidi CC2000 na kuwa na viwango viwili vya asilimia 5 na 10. Magari yenye ujazo wa injini unaozidi CC1000 lakini hauzidi CC2000 kiwango cha ushuru kitakuwa asilimia 5 ya thamani ya gari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tatizo liko kwenye thamani ya gari hasa yale magari yaliyotumika. Naiomba Serikali iweke utaratibu unaoeleweka ili mtozwa ushuru aridhike na fedha atakayotozwa kulingana na bei halisi ya gari aliyonunulia.

Mheshimiwa Spika, suala hili ndilo linaloleta utata kwa magari kutoka Zanzibar kutozwa ushuru mara mbili. Nashauri kuwa Serikali zote mbili zikae na zikubaliane taratibu za utozaji wa ushuru kwa magari hayo badala ya kuwaachia TRA kuendelea kupata lawama kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria zinazosimamia kodi za magari, Serikali imepunguza viwango vya ada ya mwaka leseni za magari kati ya asilimia 16.7 na 57.6. Punguzo hilo, itaiwezesha Serikali kukusanya mapato mengi kutoka kwenye magari hali mbaya kabla ya kiwango hiki kupunguzwa wengi walikuwa wakikwepa kulipa kodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, magari yenye ujazo wa injini unaozidi CC2500 lakini hauzidi CC5000, umepunguziwa kiwango kwa asilimia 57.6. Kundi hili linajumuisha magari madogo (*pickups*) yenye kati ya tani mbili hadi tatu ambayo huisaidia sana jamii ya Watanzania kwenye suala la usafirishaji wa mizigo. Ninaishauri Serikali punguzo la ada ya leseni kwa magari yaliyopo kwenye kundi hili yalipiwe ada zake za leseni sawa na yale magari yenye ujazo wa injini unaozidi CC5000. Hatua hii itawahamasisha sana wananchi kununua kwa wingi magari ya aina hiyo na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya usafirishaji wa bidhaa mbalimbali nchi hasa kwa wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu. Wakati akifanya kampeni ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2005, Mheshimiwa William Benjamin Mkapa, aliahidi kwa japokuwa hatakuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atahakikisha kuwa barabara hiyo isingependeza kuitwa jina lake kama haitakamilishwa kujengwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, naamini ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, haina tofauti na ahadi zote alizotoa Rais wa Awamu hii ya Nne. Je, ni lini ahadi ambayo ni moja tu kwa upande wa Tanzania Visiwani aliyohidi Mheshimiwa Rais, itakamilishwa?

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, naunga mkono mapendekezo ya Serikali, yanayohusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2008/09.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri na timu yake yote siyo tu kwa kazi nzuri kwa mwaka unaokwisha lakini pia kwa bajeti yake inayoashiria matumaini kwa Taifa letu. Pongezi maalumu ziifikie TRA kwa kazi nzuri katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili, hata hivyo, mafanikio yoyote hayakosi matatizo. Tatizo kubwa ninaloliona ni kukosekana mafaniko yanayoonekana katika maisha ya wananchi (*impact*).

Badala ya maisha kuwa bora, umaskini unazidi kudhihirika zaidi ijapo takwimu zinaonyesha kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu kadhaa zinazotuathiri. Kubwa ni upungufu katika utawala bora au “*good governance*”. Mabadiliko ya kila mara ya viongozi na uhamisho (*turn-over*) hasa upande wa Serikali, unaathiri mtiririko wa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, maamuzi yetu mara nyingi sio sahihi au yanachelewa na kukosa mtiririko. Mbaya zaidi, teuzi nyingine, hasa Mikoani na Wizarani, hazizingatii taaluma, uzoefu na sifa za uongozi. Katika hali hiyo, sitegemei ufanisi, kwani ubinafsi, tamaa na wasiwasi vinatawala na kupelekea ufisadi katika nyanja mbalimbali. Naishauri Serikali iangalie kwa makini maamuzi yake na pia teuzi zake zifanywe kwa uangalifu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tatu, baada ya kusema mambo hayo mawili ya msingi, napenda kuisitiza machache kwa muhtasari tu kwa vile wachangiaji wengi wamekwishayasemea, kama ifuatavyo:-

- (a) *D by D* – vijiji ambavyo ndiyo vitovu vya mipango havijawezeshwa vya kutosha kuweza kushiriki kikamilifu katika mchakato wa bajeti;
- (b) Wakaguzi wa Serikali za Mitaa, wawajibike kwa Baraza la Madiwani na siyo kwa *DED* au Mwenyekiti;
- (c) Vifaa vyote vya elimu, visamehewe kodi zote katika shule na vyuo vyote; na
- (d) Madiwani wapewe hadhi kwa kuwekewa maslahi yanayokidhi majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, nne, inaonekana kwamba hakuna fedha iliyotengwa kwa ujenzi wa barabara ya lami kutoka Dodoma – Iringa kama ilivyoahidiwa mara kadhaa na Rais na pia Ilani ya Chama. Kama ni kweli, ni jambo la kusikitisha kwa kuwa fedha iliyotumika hadi sasa (bilioni moja na zaidi), kwa upembuzi, itakuwa imepotea bure. Umuhimu wa kiuchumi wa barabara hii, hauhitaji kuisitizwa zaidi. Naomba sana fedha zaidi zitolewe ili angalau tuendeleze juhudi zilizokwisha gharamiwa.

Mheshimiwa Spika, tano, katika hayo yote, Mheshimiwa Waziri, katika majumuisho, anaweza kujibu kadri atakavyoona inafaa lakini hili la barabara ya Dodoma – Iringa, nitaomba sana aliwekee msimamo.

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya makadirio na mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru kinamama wa Mkoa wa Kusini, kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao pia ninawashukuru kwa ushirikiano mwema ambao wananipa.

Mheshimiwa Spika, sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, lengo la bajeti hii ni kupunguza kero na kupunguza ukali wa maisha, ndio maana ikaipa vipaumbele vya elimu, kilimo, afya na barabara na pia kupunguza na kusamehe baadhi ya kodi na kuongeza kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, huu ni ukombozi wa wananchi wa hali zote kuanzia mijini na vijijini pia inaenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala CCM.

Mheshimiwa Spika, kutokana na bajeti hii ilivyojieleza, nina mchango mfupi sana kuhusu suala ambalo sikuona likizungumzwa nalo ni Daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, daraja la Kigamboni limezungumzwa sana katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini hadi leo hakuna utekelezaji wowote. Hili suala nalo ni kero kubwa kwa wananchi waishio huko na wamechoka kutumia vivuko ambavyo havina uhakika, ni vibovu na ni kero kwa watumiaji vivuko hivyo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho, angetueleza hatua gani zimekwamisha chukuliwa kuhusiana na ujenzi huo ambao ukitekelezwa, utaongeza uchumi wetu na kuongeza kipato cha wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na kuweza kushiriki katika kuchangia bajeti hii. Nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mpasuko wa kisiasa Zanzibar baina ya CCM na CUF, bado ni kero kubwa ambayo ikiachiwa hivi hivi, inaweza kuleta maafa makubwa hapo baadaye. Ni matumaini yetu kuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, sasa atatekeleza ahadi yake aliyoitoa tena kwa mara nyingine alipokuwa Uingereza hivi karibuni ili kuvinusuru Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba (Zanzibar) visije vikaingia katika balaa litakalohitaji gharama kubwa kuvirudisha katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopita ilikuwa mzigo kwa wananchi wenye kipato cha chini. Bajeti hii ya sasa tunayojadili pia inaendelea kuwa mzigo kwa wananchi pamoja na kuongezeka kutoka trilioni 6.066 hadi trilioni 7.216. Hii inatokana na kupanda kwa bidhaa mbalimbali yakiwemo mafuta ya taa, dizeli, petroli, simenti, mabati, usafiri wa aina zote, chakula, mavazi, huduma za afya, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mgao wa asilimia 4.5 kwa Serikali ya Zanzibar, bado inaendelea kuwa kero kwani hii ni bajeti ya tatu tangu tuingie Bungeni lakini majibu yanayotolewa na Serikali humu Bungeni, si ya kuridhisha na yasiyokuwa na matumaini. Tunaiomba Serikali ishughulikie tatizo hili “*seriously*” kwa maslahi ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, kero za Muungano ni nyingi lakini ufumbuzi wa kero hizo unaonekana kusuasua kiasi kwamba wananchi wanaanza kupoteza matumaini ya kufikiwa kwa ufumbuzi wa kero hizo za Muungano. Serikali inapaswa sasa kuwa makini zaidi katika kutatua kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa dunia inakabiliwa na balaa la njaa. Tanzania Kilimo ni uti wa mgongo, ni sekta inayotoa ajira kwa wananchi wengi zaidi asilimia sabini (70%) na ni sekta inayochangia pato la Taifa. Watanzania walio wengi wanategemea kilimo kwa ajili ya chakula chao na kuuza ziada ya mazao kwa kupata mahitaji mengine kwa mavazi, elimu, matibabu na hata kujijengea nyumba za kuishi. Bajeti hii, haijatoa umuhimu unaostahili kwa sekta ya kilimo. Nchi yetu imo katika hatari ya kukabiliwa na balaa la njaa iwapo hatua za dharura hazitachukuliwa kurekebisha bajeti ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara vijijini, ni mbaya, maji safi na salama bado ni tatizo vijijini na mijini na wananchi vijijini wanasumbuka kwa usafiri pamoja na kuhangaika masafa marefu kutafuta maji kwa matumizi mbalimbali. Wakati umefika sasa kwa Serikali yetu kupunguza utegemezi kwa kiasi kikubwa zaidi ukizingatia kuwa nchi yetu ina rasilimali nyingi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu umuhimu wa mawasiliano kwa kutumia simu ikiwa ni moja ya miundombinu muhimu kama zilivyo barabara, reli, bandari na kadhalika katika kuleta maendeleo ya uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya 2008/2009, imelenga kuongeza kodi juu ya muda wa maongezi (*airtime*) kwa asilimia 3.0 (yaani kutoka 7.0% hadi 10.0%) kuanzia Julai, 2008. Ongezeko hili litaifanya Tanzania kuwa nchi yenye gharama kubwa zaidi kwa matumizi ya huduma za simu za mikononi Barani Afrika. Hili linadumaza kukua kwa sekta pamoja na kupunguza mapato ya Serikali kutokana na wateja kushindwa kumudu gharama hizi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba Serikali iangalie upya misingi ya utozaji kodi katika watumiaji wa huduma za simu nchini. Ni vema Serikali ikaweka malengo ya muda mrefu yatakayosaidia sekta ya mawasiliano kukua na hivyo kujiwekea msingi wa mapato endelevu. Hatua inayotakiwa ni kupunguza kodi ya *Excise Duty* kwenye muda wa maongezi na Kodi ya Ongezeko la Thamani. Hii kama ilivyoelezwa awali, itavutia wawekezaji wengi na kuchochea matumizi zaidi kwenye muda wa maongezi ambao hatimaye Serikali itapata kodi ya kutosha.

Aidha, inashauriwa kwamba badala ya Serikali kutoza watumiaji wa huduma hii kwa gharama kubwa, ni vema ikafuta msamaha wa kodi (*Corporation and Income Tax*), kwa makampuni ambayo yaliongezewa muda wa msamaha kwani Serikali inapoteza mapato makubwa sana kwani faida wanayopata makampuni hayo, haiwekezwi hapa nchini badala yake hupelekwa nje kwa wenye hisa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono bajeti hii ya 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali/Wizara ipokee changamoto zangu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ukusanyaji wa kodi (*revenue*), nina mashaka makubwa juu ya mapato yanayotokana na maeneo mawili.

(a) Sekta ya madini, Serikali iangalie upya juu ya chanzo hiki ambacho kina manung'uniko mengi toka kwa wananchi. Mikataba iendelee kuchunguzwa na kurekebisha na taarifa ya chanzo hiki ikiwa ni pamoja na pato halisi la sekta hii iwekwe wazi na Watanzania wote wafahamu kuliko malalamiko tu kuwa tunaibiwa, tunaibiwa wakati pengine hali si hivyo.

(b) Maliasili na utalii, pato la sekta hii bado halilingani na hali ya viwango na wingi wa maliasili zetu. Wananchi wanaona upungufu katika sekta hii maana maliasili zetu wao ndio wanaozitunza. Ni vema wakafahamu kwa uwazi mapato yanayotokana na sekta hii.

Aidha wigo wa kodi katika sekta hii uongezwe kulingana na hali ya sasa. Bado kodi kwa mfano katika uwindaji, ziko chini mno. Uvunaji wa utalii wa namna hiyo, ni vema ukaangaliwa kwa karibu, vibali vingi vya utalii wa uwindaji, vinavuna kuliko vibali vyao.

(c) Serikali ibuni vyanzo vingine vipya na kuachana na tabia ya kuongeza hivyo hivyo kila siku.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuzungumzia misamaha na punguzo la kodi kama ifuatavyo:-

(i) Motopoa, sina hakika kama ulifanyiwa utafiti wa kina. Binafsi, nilinunua jiko la Motopoa lita 5. Motopoa hauwezi hata kuchemsha maji, huwezi kusonga ugali ukaiva, moto ule hauwezi kupika chakula au mboga inayozidi dakika 10. Ninashauri kutafuta namna nyingine ya kumsaidia huyu mwananchi wa kawaida na njia pekee ni kupunguza kodi kwenye mafuta ya taa. Najua kwamba mafuta ya taa hutumika kwa kuchanganywa na dizeli na wafanyabiashara wasio waaminifu, njia pekee ya kufanya ni kuyatia rangi mafuta ya taa ili watakapoyachanganya yaonekane na wanaohusika wachukuliwa hatua.

(ii) Kodi ya mafuta ya dizeli na petroli, nakubaliana na hatua zilizochukuliwa na Serikali za kutoongeza kodi kwenye eneo hili. Sikubaliani na wala sifiki wazo la Kambi ya Upinzani kwamba tuondoe kodi ya dizeli na petroli kwa Sh.250/= kwa lita, *they just want to confuse our Government*, kiasi hicho ni kikubwa kitailazimu Serikali kupanga upya bajeti.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu bajeti ya kilimo, naiomba Serikali iwe *forecasted* kwenye *performance* zaidi katika *level* ya *Local Government* kuliko kupeleka tafiti katika *level* hiyo. Fedha zinazopelekwa chini ziende zikafanye kazi halisi.

Halmashauri ndizo zikopeshe *tractor*, *powertillers*, majembe ya kukokotwa na wanyama, mbolea na mbegu. Serikali iziagize Halmashauri zote kupitia *programme* mbalimbali za kilimo kwenda kwenye utekelezaji zaidi na kuachana na nadharia za kisera. Kazi hiyo, iachiwe Wizara.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya 6.4%, ni kubwa endapo itaelekezwa kwenye utekelezaji wa vitu halisi kama nilivyoeleza hapo juu. Taarifa ziwe zinatolewa kwa ushindani kwa Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, nirudi kuipongeza Serikali kwa bajeti nzuri iliyolenga utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Spika, kuhusu *Exchange Rate*, kwanza, tukazanie sana kuongeza *export* ya *traditional exports*. Nakisi ya urari iliyopo hivi sasa siyo nzuri sana kwa uchumi wetu na kwa ujumla haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, pili, madini yametupa mapato mengi sana nje mwaka 2007 mara tatu zaidi ya mazao yote ya kilimo kwa pamoja. Madini yaliingiza \$886 milioni wakati mazao mengine yaliingiza \$390 milioni na bidhaa za viwandani \$309 milioni. Madini yanaingiza mapato zaidi kuliko kilimo na viwanda *combined* lakini kwa nini mapato ya *forex* toka madini hayaisaidii thamani ya shilingi yetu, *something is wrong*!

Mheshimiwa Spika, tatu, napendekeza tuanzishe “*Nyerere Shilling*” ambayo itakuwa sarafu iliyotengenezwa kwa dhahabu na iruhusiwe wananchi kuwa nayo na thamani yake iwe ile ya soko, itasaidia sana ku-*stabilize* thamani ya shilingi yetu.

Mheshimiwa Spika, nne, thamani ya shilingi isiachwe ipande sana ama kwa ghafla kwa sababu itaathiri sana mapato ya wakulima wa mazao yanayouzwa nje kama pamba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *interest rate spread*, riba ya kuweka pesa benki ni 2.7%, riba ya kukopa ni 15.7%, *Interest rate spread* ni 13%.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba:-

- (a) Mabenki hayahitaji pesa za wananchi lakini pia zinakatisha tama watu/wafanyabiasha kukopa;
- (b) Mabenki yanatengeneza faida kupita kiasi; na
- (c) Mabenki yana pesa nyingi kwenye ma-*shelves* ndiyo maana yana *discourage deposits*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *tax (revenue)/yield*. *Tax yield* ya 18.5%, vyanzo vipya vya mapato ni vipi au wale wale wanatozwa zaidi? Mapato/faida toka Mashirika ya umma kuchangia bajeti ya Serikali, ni *innovation* nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba niongeze mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuhusiana na *coin chakavu*, kule vijijini Namtumbo nimelalamikiwa na wananchi kuwa *coins* za Sh.100/= zinawapa taabu kununua bidhaa dukani sababu zimechakaa, wenye maduka wanawakatalia. Tatizo hili nimelalamikiwa katika Kata ya Kitanda Tarafa ya Undendeule. Wanasema sisi tunawauzia karanga, miwa, nyanya, vitunguu lakini tunapokwenda dukani wanazikataa sasa tuzipeleke wapi? Sisi sio tuliozitetengeneza. Naomba kauli ya Serikali kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, pili, fedha za wajasiriamali maarufu kama Mabilioni ya JK, Namtumbo Awamu ya Kwanza hatukupata sababu ni kukosekana kwa Benki. Awamu ya pili, tumepitishiwa kupitia mtandao wa SACCOS ya DUNDULIZA, tunashukuru lakini tumepatiwa Sh.100,000,000/- tu ukitizama kwa mgao wa Wilaya tano, Mkoa wa Ruvuma tulipaswa angalau kupewa shilingi 200 milioni.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali hapa Bungeni kwa niaba ya Wizara ya Kazi (Mhe. Chibulunje), alisema, Wilaya zote zilizokosa awamu ya kwanza, sasa awamu ya pili wamepata milioni 200. Namtumbo hatujapata hizo milioni 200 bali tumepata milioni 100. Naomba kama mgao ulikuwa milioni 200, Serikali itufahamishe ili tuwaulize wenzetu wa DUNDULIZA, milioni mia ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ili wananchi wa Namtumbo waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara na Wafanyakazi wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na iliyoandaliwa kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja yangu ya awali kuhusiana na mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, napenda nisisitize kuunga mkono hoja kwa vile imeweza kuweka maeneo ya kipaumbele kwa bajeti ya mwaka 2008/09. Kimsingi, vipaumbele hivi vinalenga kutuwezesha kupiga hatua mbele kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite katika mapitio ya vipaumbele vya bajeti hii na hali halisi ya Jimbo la Mbozi Magharibi.

(i) Suala la elimu, elimu ni msingi wa maendeleo. Hakuna ubishi kuwa bila elimu hakuna maendeleo. Jimbo la Mbozi Magharibi, Wilaya ya Mbozi, Mkoani Mbeya, lina Tarafa tatu, Kata 11, Vijiji 75 na Vitongoji 25. Kila kijiji kina Shule ya Msingi na kila Kata ina Shule ya Sekondari hadi mwaka 2005, kulikuwa na Shule za Sekondari nne tu, hivi sasa kuna shule za sekondari 14.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni upungufu mkubwa wa Walimu katika shule za msingi na za sekondari. Shule za msingi zingine zenye watoto hadi 360 zina Mwalimu mmoja tu na shule za sekondari zingine kukosa Walimu kabisa. Sababu ni kuwa Walimu wamepangwa wamekataa kukaa Jimboni kwangu kutokana na kuwa pembezoni na hivyo kukosa miundombinu ya msingi kama barabara, umeme, mawasilino ya simu, huduma za afya na kadhalika. Naomba Wizara ya Elimu na Ufundi, itoe upendeleo maalumu kwa Jimbo hili katika mgao wa fedha wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu kwa Wizara ya Elimu, kwa kutoa upendeleo wa nafasi 38 za wanafunzi wa Mbozi Magharibi waliojiunga na vyuo vya Ualimu

Daraja la IIIA kwa muhula wa mwaka 2007/2008 ambao wakimaliza watajiunga kufundisha katika shule za msingi Jimboni pale.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa mwaka huu pia atupe fursa kama ile kwani vijana zaidi ya 200 kutoka Jimbo la Mbozi Magharibi wameomba kujiunga na Vyuo vya Ualimu.

(ii) Miundombinu ya barabara na mawasiliano ya simu. Hakuna mjalada kuhusu umuhimu wa miundombinu ya barabara na mawasilinao ya simu katika kusukuma mbele maendeleo ya uchumi.

Jimbo la Mbozi Magharibi ni changa (miaka 13), halina miundombinu ya barabara na simu. Jimbo hili limegawanyika kijografia katika ukanda wa bonde la ufa la Rukwa (ama Msangano *Trough*) na ukanda wa uwanda wa juu. Pamoja na eneo lake la zaidi ya 6,000 kilomita za mraba, ili kufikia sehemu moja ya Jimbo hili, inatulazimu kupitia Jimbo la Mbozi Mashariki kwa zaidi ya kilomita 150 au kupita Jimbo la Kalambo na Kwela Mkoani Rukwa kwa umbali ule ule usiopungua kilomita 150.

Mheshimiwa Spika, Jimboni Mbozi Magharibi kuna barabara ambazo zilitumiwa na Wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza lakini baada ya Uhuru, zimekufa. Barabara hizi zikitengenezwa na kupandishwa hadhi, zitainua uchumi uliolala wa Jimbo hili kwa kurahisisha usafiri na usafirishaji. Barabara hizi ni kama zifuatavyo:-

(a) Barabara ya Kakozi – Kapele – Kasinde –Ilonga. Barabara hii inaambaaambaa na mpaka wetu wa Zambia na kwenda hadi Kasanga, Ziwa Tanganyika. Ikitengenezwa, itarahisisha usafiri na usafirishaji kutoka Tunduma hadi Ziwa Tanganyika. Barabara hii inapita eneo lenye mbuga za kipekee kabisa na ardhi yenye rutuba kwa mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na kahawa na mpunga wa uwanda wa juu. Ni muhimu sana kwa ulinzi wa mpaka wetu wa Zambia.

(b) Barabara ya Chapwa – Chiwezi – Msamba II – Chindi – Msangano – Chitete – Chilulumo –Kamsamba. Barabara hii inaunganisha barabara ya Zambia na Ziwa Rukwa na hupitia Kata saba zilizoko Bonde la Ufa la Rukwa (*Msangano Trough*). Bonde hili lina misitu ya Miyombo, Mininga na miti ya Ukanda wa Savana kwenye kingo zake na ardhi yenye rutuba kwa kilimo cha mpunga, mahindi, ufuta, karanga, alizeti na matunda ya aina mbalimbali ya ukanda wa joto. Barabara hii, ndiyo pekee inayounganisha Kata za Jimbo hili. Barabara hiyo ikitengenezwa, itakuwa mkombozi kwa Jimbo hili. Pia sehemu iliyopendekezwa kujengwa ofisi ya Mbunge, iko kwenye barabara hii (Msangano).

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe upendeleo wa kipekee kwa wananchi zaidi ya 200,000 wa Mbozi Magharibi ambao kati ya mwezi Novemba na Juni kila mwaka hutengwa na dunia kutokana na kukosekana kwa mawasiliano ya barabara.

(iii) Kilimo, Ukanda wa Uwanda wa Juu, unahitaji mbolea kwa kila inchi ya ardhi inayolimwa. Bei mbaya ya mbolea, inawakatisha tamaa wakulima wa ukanda huu ambao ni wakulima hodari. Kwa bahati nzuri, ukanda wa Bonde la Ufa hadi sasa hauhitaji sana mbolea kwani mazao hustawi vizuri sana hata bila mbolea.

(iv) Kilimo cha umwagiliaji, Jimboni Mbozi Magharibi, kuna miradi mitatu ya umwagiliaji lakini ambayo mpaka sasa haijakamilishwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Mradi wa umwagiliaji wa Naming'ong'o uliogharimu Serikali karibu shilingi milioni 900 umebomolewa na maji kutokana na ujenzi mbovu.

(b) Mradi wa Iyendwe – umesimama kwa sababu zisizoeleweka.

(c) Mradi wa Chilangu, umesimama na ujenzi ni mbovu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie miradi hii na kuifufua ili ianze kuzalisha chakula.

(v) Huduma za afya, Jimbo la Mbozi Magharibi lina Zahanati chache sana na Vituo vya Afya vitatu tu. Kwa ujumla, huduma za afya ziko chini sana Jimboni kwangu. Sasa hivi wananchi wamejizatiti kujenga Zahanati ya kijiji. Ombi lao, ni kupatiwa vitendea kazi na watumishi mara watakapokuwa tayari wamekamilisha ujenzi.

(vi) Suala ya maji safi na salama, wananchi wa Mbozi Magharibi, wa vijijini, wanashukuru sana kwa mpango ulioanza wa kuchimba visima ambao unaendelea vizuri.

(vii) Wilaya ya Mbozi kugawanywa, eneo la Kilomita za mraba zaidi ya 9000 na idadi ya wakazi zaidi ya 600,000, inaleta ugumu katika utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, kwa ujumla pamoja na Watendaji, Wakurugenzi na Idara kwa kuandaa hotuba hii nzuri ambayo imewapa Watanzania matumaini angalau hasa katika eneo ambapo bei za vitu vingi hazikupanda, bei na bidhaa kuwekewa ruzuku ikiwemo pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie mambo yafutatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, bei ya mafuta ikiwemo dizeli, petroli na mafuta ya taa kupanda bila utaratibu ambao husababisha kupanda kwa biashara zote ikiwemo nauli, vifaa vya ujenzi na mahitaji muhimu. Naishauri Serikali isimamie mkakati uliowekwa wa kushirikisha makampuni kuanzisha ushirika wa kuagiza mafuta ambapo inaweza kushusha bei ya mafuta na kupunguza kupanda kwa bei. Naomba Serikali itueleze ni lini utaratibu na mkakati huu utakamilika?

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu mazingira, Serikali imepunguza bei ya mafuta ya Motopoa, gesi na kadhalika ili wananchi watumie gesi na majiko ya Motopoa ili kutunza mazingira. Ili utumie majiko haya lazima ununue majiko hayo ambapo jiko la Motopoa ni Sh.35,000 na kuendelea na mafuta yake ni Sh.2,000 kwa kila lita na mafuta hayo ya lita moja inatumika kwa masaa matano na haliwezi kupika ugali, maharage na kadhalika. Vilevile jiko la gesi la chini ni zaidi ya Sh.100,000 na mtungi wake ni zaidi ya Sh.30,000 na vyote hivi vinatumiwa na wale wenye uwezo wa fedha na kwa mijini zaidi lakini wananchi wa vijijini ambapo akinamama

wanahangaika kutafuta kuni na mkaa, wanaendelea kuchoma mkaa na mazingira kuendelea kuharibika.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba Serikali ieleze ni kigezo gani kilichotumika hasa kwa ajili ya akinamama vijijini ili na wenyewe watumie majiko hayo? Wakati Serikali inajua wananchi wa vijijini kipato chao hakitaweza kukidhi kununua majiko haya au ilikuwa ni kwa ajili ya wananchi wenye uwezo tu? Ninapenda kujua ni kwa nini utayarishaji wa matumizi ya makaa ya mawe ambao Serikali inaahidi kwa kila bajeti mpaka sasa haujakamilika?

Mheshimiwa Spika tatu, naomba sasa nizungumzie suala la Mheshimiwa Waziri kuleta masahihisho Bungeni ya takwimu za bajeti baada ya Kambi ya Upinzani kuonyesha makosa hayo. Hii inaonyesha ni jinsi gani watendaji wa Wizara wasivyo makini katika kazi zao. Mpaka leo hii Alhamisi, saa 5.00 hii, hatujapata marekebisho hayo kwa maandishi. Naomba hatua zichukuliwe angalau kuwaonya ili siku nyingine wakumbuke kufanya kazi zao kwa makini.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa ujasiri alioonyesha kwa kuleta marekebisho Bungeni, nasema hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu posho kwa Waheshimiwa Madiwani, naomba Serikali iangalie upya posho za Waheshimiwa Madiwani kwani posho ya Sh.60,000/= kwa mwezi haitoshi kwani viongozi hawa wanatumia muda wao mwingi kushughulikia wananchi. Vile vile wakopeshwe pikipiki au gari aina ya Suzuki ili ziwasaidie. Kutokuwasaidia, ni kuwafanya Waheshimiwa hawa watumie muda mwingi kutafuta mahitaji ya maisha yao muhimu.

Mheshimiwa Spika, la tano, ni kuhusu wastaafu, naomba tukumbuke kwamba kustaafu kila mtumishi ni hatua ya mwisho ya kupata kipato cha uhakika ukilinganisha na kipato kingine chochote hata kama ni biashara, watu hufilisika kwa namna nyingi. Naiomba Serikali ijue kwamba kuwaongezea wastaafu, itawasaidia waishi maisha angalau ya kawaida kidogo maana atakua na kitu cha uhakika cha kutegemea. Hivyo, naiomba Serikali iongeze kima cha wastaafu kuanzia kima cha chini mpaka cha kati.

Mheshimiwa Spika, sita, ni kuhusu elimu, suala la elimu limeonyesha mafanikio makubwa hasa katika ujenzi wa shule za sekondari, kazi kubwa iliyobaki ni ujenzi wa nyumba za Walimu, maabara, vyoo, maktaba na majengo ya utawala.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuwapelekea Walimu, umeme wa aina yoyote ile na kuzipandisha baadhi ya shule kuwa na Kidato cha Tano na Sita. Ingawa mpango wa Serikali zitapandishwa ifikapo mwaka 2010, nashauri mpango huu usingoje mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Mawaziri na Wizara hii kwa bajeti nzuri waliyoifikisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza, bajeti hii ni nzuri kwa sababu sasa Tanzania inagharamia Matumizi yake ya Kawaida (OC) kwa 100% badala ya kutegemea wahisani. Hili ni jambo zuri kwani hata wahisani sasa watatuheshimu.

Mheshimiwa Spika, pili, bajeti hii haikuongeza kodi kwa bidhaa na huduma zinazomgusa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, tatu, wafanyakazi wameongezwa mishahara ili kupunguza makali ya maisha kwa wananchi wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono bajeti hii kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nina machache ya kuyazungumzia.

Mheshimiwa Spika, kodi ndio mapato ya Serikali, misamaha ya kodi kwa kiasi kikubwa kama ilivyokuwa mwaka 2007/2008, ni jambo la hatari kwani jambo hili linakosesha mapato Serikali na hivyo kushindwa kutoa huduma kwa wananchi. Tunaomba hatua kali zichukuliwe kwa wale waliotoa misamaha hii na mtindo huu ukome mara moja.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya kilimo na sekta ya mifugo na uvuvi, ni mdogo mno. Hizi ndizo sekta zinazomgusa mwananchi wa kawaida. Hivyo kama tunataka kuondoa umaskini hapa nchini lazima tutenge fedha za kutosha katika sekta hizi.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi inaelekeza kuwa uwanja wa Kitaifa utajengwa Mugumu, hospitali ya kisasa itajengwa Mugumu Wilayani Serengeti. Vile vile barabara ya lami itajengwa toka Makutano kupitia Natta, Mugumu, Tabora B, Loliondo hadi Mto wa Umbu. Hadi sasa miradi haijaanza na uchaguzi wa mwaka 2010 unakaribia, hivi kweli wana CCM tutapata kura Wilayani Serengeti? Naomba majibu ya kina kuwa miradi hii itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Spika, hadi sasa ujenzi wa bwawa la Manchira limekamilika. Cha kushangaza hadi leo, hamna juhudi za kutandaza mabomba ya kupeleka maji mjini Mugumu na vijiji vinavyolizunguka hili Bwawa. Naomba majibu ya kina kwamba Serikali ina mpango gani wa kumalizia kazi hii ili wana Serengeti wapate maji?

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya Wilaya ya Serengeti, ni eneo la *Serengeti National Park*. Wawekezaji wengi wamejenga hoteli za kitalii. Kinachosikitisha, ni kuwa Halmashauri ya Serengeti haipati mapato yoyote kutoka hoteli hizi. Zamani tulikuwa tunatoza kodi ya kitanda, leo hii kodi hiyo haipo lakini mwananchi wa Serengeti ndio wanaolinda hifadhi hii ili isimalizwe na wawindaji haramu, wanawahakikishia watalii usalama wao, wanauwawa na wanyama, mazao yao yanaliwa na wanyama. Naomba majibu ya kina, ni lini Serikali itaturudishia kodi ya kitanda ili Halmashauri yetu ipate mapato?

MHE. HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu leseni ya magari kupunguzwa, mimi binafsi nimefurahishwa na punguzo hili na itafaya makusanyo ya *TRA* kuwa makubwa kuliko hivi sasa walipa kodi wengi wanabuni leseni hizo mitaani.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na punguzo la leseni hii ya barabara bado tuna tatizo moja na malalamiko makubwa ni kama gari limeharibika na liko *garage*, bado *TRA* wanalazimisha kulilipia *road licence*. Sioni kama ni haki kumtoa mwenye gari kulipa kodi kwa kuwa gari ni mbovu! Naomba Waziri alione hilo, siyo haki kwa kweli kama gari liko *garage* kulilipia kodi.

Mheshimiwa Spika, pembejeo za korosho zitolewe ruzuku ile wakulima wa korosho waweze kuzalisha zaidi kwenye kilimo hicho na pato la Taifa liongezeke hasa kwenye fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vifaa vya uvuvi, wapewe ruzuku kununulia nyavu, maboya, kamba boat na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, bado Wizara/Serikali inategemea sana (*TB*), *Treasury Bill* (Hati Fungashi). Serikali kuwa na *cash* bajeti na kufanya benki nyingi kutegemea hizo (*TB*), je, Serikali haioni bado riba za mabanki hazitapungua kutokana na suala hilo?

Mheshimiwa Spika, nashukuru na kwa haya machache, naunga mkono hoja.

MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri. Pili, nawapongeza Naibu Waziri wote wawili.

Tatu, nawapongeza wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TRA*. Bajeti ya mwaka huu ni nzuri kwa namna moja au nyingine. Ila ninaomba bajeti ijayo Wizara ya Kilimo, uwepo uwezekano wa kuongezewa fedha kutokana na majukumu mazito na kwa ajili ya maendeleo ya kilimo. Kilimo ndio uti wa mgongo wa kututoa kwenye umaskini.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kutoa hongera zangu za dhati, kwa Wizara hiyo ya Fedha, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuchambua bajeti ambayo imewagusa wananchi wa aina zote kwa namna moja au nyingine, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kusudi langu ni kuomba, tafadhali sana, katika bajeti hii, yule mjusi (*Dianasour Skeleton*), afanyiwe mpango wa kumrudisha Tanzania mwaka huu kwani ahadi ya kumrudisha ilishatolewa na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii mwaka 2006/2007 na Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje mwaka 2008. Kwa hiyo, wananchi wa Lindi, wana matumaini makubwa sana kuhusu kurudishwa kwa mjusi huyo.

Mheshimiwa Spika, mjusi huyo (*Dianasour*) ambaye sasa ni *skeleton*, alichukuliwa kijiji cha Mipingo, Wilaya ya Lindi, Mkoa wa Lindi. Mjusi huyo angetuletea mapato makubwa sana katika utalii nchini. Mjusi huyu ni maarufu sana kwa watalii na watu wengi huenda huko huko Ujerumani kwa sababu ya vile alivyoumbwa. Ana uzito tani 80, urefu kama mnazi uliopea na upana wa pekee. Mijusi kama hii duniani, huonekana sehemu tatu tu, nayo ni Tanzania, Afrika Kusini na Amerika ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, endapo Wizara itamrudisha mjusi huyo kutoka Ujerumani aliko kuja Tanzania, sisi wananchi tunaomba aje awekwe Lindi kwani Lindi sasa watalii wanakuja wengi kuona utalii uitwao “*cultural tourism*”, kwa hiyo, si vibaya wakamleta Lindi ili watalii wakitoka Zanzibar waunganishe kuja Lindi, pale ni karibu. Wananchi wa Lindi wametenga eneo kubwa huko Lindi karibu na Pwani ya bahari ya Hindi katika Kisiwa cha Lindi, kilomita mbili kutoka Lindi, eneo hilo zamani walikuwa wanalima katani lakini sasa hivi halitumiki, litafaa kuweka mjusi huyo, eneo ni zuri kwa kweli. Je, Wizara ya Fedha, ipo tayari kwanza, kumrejesha Tanzania na pili kumleta Lindi?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. FLORENCE E. KYENDESYA: Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu nyongeza ya mishahara. Naipongeza Serikali kwa kutenga bajeti kwa ajili ya kuongeza mishahara kwa watumishi wa Serikali kutokana na makali ya maisha. Nashauri kima chini kuwa Shs.150,000/= kwa mwezi.

Aidha, naiomba Serikali iwafikirie kwa huruma wastaafu ili waongezwe pensheni ili kima cha chini kiwe Sh.50,000/=. Wazee wetu hawa wameitumikia Serikali kwa uadilifu wa hali ya juu na kwa sasa wanaishi katika hali ngumu sana, baadhi yao hawana hata watu wa kuwasaidia, naomba Serikali ilingalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za mkopo wa wajasiriamali zinazojulikana fedha za JK. Kwa kuwa azma ya Serikali ilikuwa kuwawezesha wajasiriamali kukopa fedha hizo kupitia vyombo vya fedha, uzoefu umeonyesha wanaopata mikopo hiyo, kupitia mabenki hasa *NMB*, ni wale wa mijini tu, wanaoishi vijijini hawapati kabisa na hasa wanawake na hakuna uwiano sawa na wanaume.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Mbeya, hadi tarehe 8/5/2008, wanawake waliopata mkopo walikuwa 101 ikilinganisha na wanaume 859. Maafisa wa benki hawajawa wazi kutoa takwimu za idadi ya walioomba ili kulinganisha na waliopata.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inakusudia kutoa fedha za awamu ya pili, naishauri Serikali itoe utaratibu/mwongozo kwa mabenki husika ili taarifa zao kuhusu mikopo hiyo iwe wazi kwenye ofisi za Wakuu wa Mikoa, kwani kuna uwezekano mkubwa wa fedha hizo kukopeshana wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha, naunga mkono hoja.

MHE. ABBAS Z. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Waziri, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha, kwa matayarisho mazuri ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2007/2008, Wabunge tulitakiwa kutoa mawazo ili kuongeza pato la Taifa. Nilitoa mawazo mawili:-

1. Kodi za Majengo kukusanywa na *TRA*. Haya niliyasema wakati nachangia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu, nashukuru hili sasa limepita. Sasa ni wajibu wa Wizara kuhakikisha *TRA* wanasimamia vizuri makusanyo hayo.

2. Serikali kutangaza mishahara ya sekta binafsi, nashukuru Waziri wa kipindi hicho, Mheshimiwa Chiligati alitangaza mishahara kwa sekta binafsi kwa maana hiyo mchango wangu umefanyiwa kazi. Ushari wangu katika hili, naomba uhakikishe wafanyakazi wote wa sekta binafsi wanalipwa mishahara yao kupitia benki. Hili litasaidia sana pato la Serikali kwa kiasi kikubwa maana kwa sasa wafanyakazi wengi wa sekta binafsi hawalipi kodi. Tutakapohakikisha wafanyakazi wote wa sekta binafsi, wanalipiwa kupitia benki, wote watalipa kodi kupitia benki na pato la Taifa litaongezeka.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeze *TRA* kwa kazi nzuri ya ukusanyaji wa kodi kwa Taifa letu lakini wakijipanga vizuri wanaweza kuongeza mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, namktakia Mheshimiwa Waziri, kazi njema na afya njema.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. YONO S. KEVELA: Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana kwa bajeti nzuri kwa wahusika wote waliotayarisha chini ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi Mustafa Mkulo, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, ombi, Wizara ya Mambo ya Ndani, *Police Force* mwaka 2008/2009, wametengewa bajeti ya shilingi 522,503,000 kiasi hiki ni kidogo sana. Naomba waongezewe bajeti, walau ifike shilingi 800,000,000 ili kuboresha maisha ya Askari na vitendea kazi wapatiwe, sehemu nyingine nchini Polisi hawana vitendea kazi (*revenue estimates*).

Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kunijengea kituo cha Polisi, Ilembula, Njombe lakini hawana vitendea kazi kama vile usafiri. Naomba wapatiwe pikipiki au walau gari kwa ajili ya doria. Sasa hivi wanakodi baiskeli kukamata wahalifu. Naomba bajeti ya vitendea kwa kituo changu cha Polisi, Ilembula.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Wizara ya Utalii na Maliasili, wametengewa *revenue* shilingi milioni 54,866,257,000, je, kiasi hiki kimeweka fedha ya fidia ya waathirika waliohamishwa kwa ajili ya *Mpanga/Kipengere Game reserve*?

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalalamika sana juu ya fidia, baadhi hawakulipwa kabisa na wengine wamelipwa kidogo sana. Wananchi hao ni wa Kata ya Luduga, Njombe. Vijiji hivyo ni Mpanga Mpya, Luduga, Malangali na Mambegu hasa hasa waliokuwa wanalima katika bonde la Mpanga (Igalatilio).

Mheshimiwa Spika, pia naomba Serikali inapotaka kufanya maamuzi mazito yanayohusu maslahi kwa wananchi, Mbunge husika ni lazima ahusishwe kikamilifu. Kuna tatizo sasa la mipaka pale Kata ya Luduga, vijiji vya Malangali, Mpanga Mpya, Luduga na Mambegu. Kule kwa kweli hakuna wanyama wa kutosha, kuna paa kidogo wa kuhesabu, hivyo utalii bado ni tatizo, sijawahi kuona watalii pale, lakini wananchi wanasumbuliwa kwa kuhamishwa tena. Naomba Serikali isiwahamishe wafuate mipaka ya zamani na ili kuwa na

makusanyo makubwa basi tunaomba tunapate wanyama kama tembo, simba, twiga toka Ruaha na Mikumi.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ni kwenye miundombinu. Naomba bajeti ya miundombinu iongezwe ili barabara ya Njombe/Makete kupitia Igora na Kipengere (Moronga) ili barabara ya Wilaya mbili, iwe ya lami. Napongeza sana kwa Serikali kuamua kujenga barabara hiyo kwa kiasi cha km.2 kwa lami kwa awamu kutoka Njombe kupitia Igosi kwenda Makete. Barabara hii iko chini ya Wizara (*Tanroad*).

Mheshimiwa Spika, pia naomba bajeti iongezwe kwenye Halmashauri ya Njombe. Nina tatizo kubwa la madaraja ya Ilembula/Wangutwa katika Wilaya ya Njombe na kiasi cha Sh.60mil kinahitajika.

Mheshimiwa Spika, daraja lingine ni Dulamu/Kanawi Kata ya Usuka, Njombe kiasi cha Sh.30mil kinahitajika. Wananchi hao wa vijiji vya Kanawi na Dulamu, wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, daraja la Matowo/Ilembula, nashukuru sana Serikali kwa kulitengeneza lakini bado fedha zinahitajika, mafuriko yaliharibu daraja lile la Matowo.

Mheshimiwa Spika, naomba umeme kwenye shule zangu za Serikali za Ulembwe, Wanike, Mto Kipengere, Makoga, Saja, Kijombe, Ludunga na Ilembula.

Mheshimiwa Spika, mwisho upande wa maji, miradi ya maji ya Wanging'ombe na mradi wa maji wa Tove, Njombe bajeti iongezwe bado ni ndogo.

MHE. MERYCE M. EMMANUEL: Mheshimiwa Spika, naomba na mie nichangie na hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Fedha na mwelekeo mzima wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu kupandisha bei ya vileo. Hakuna hasara yoyote anayoipata Mtanzania wa hali ya chini au faida, kwani hilo si hitaji lake muhimu katika maisha yake. Kwa sababu wanaotumia vileo hivi ni watu wenye uwezo na usipokuwa nazo wala huwezi kufa au kushindwa kuishi.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni gharama kubwa ya mafuta ya taa ambalo ni hitaji muhimu la mwananchi yeyote yule. Hivyo, naomba angalau bidhaa hii izidi kupunguzwa bei ili Mtanzania aweze kupata huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni gharama kubwa ya mafuta ya petroli na dizeli. Wilayani gharama inakuwa kubwa zaidi ukilinganisha na gharama za usafiri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nichangie kuhusu uwanja wa ndege wa Shinyanga. Kwa kweli ni aibu kubwa mno ukilinganisha na thamani ya migodi iliyomo ndani ya Mkoa wa Shinyanga. Ukweli ni kwamba kiwanja hicho hakifai, ni aibu tupu. Naomba Serikali iangalie uwanja huo wa Shinyanga kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni kwa nini Wizara kupitia wakala wake *TCRA*, walitumia Sh.1.2 bilioni kwa ajili ya mahujaji waliokwama katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere. Je, kuna uhusiano gani kati ya Mahujaji na *TCRA* au ulikuwa ni mkopo na utalipwa lini? Waziri wa Fedha, anapoleta Muswada kwa ajili ya kuruhusiwa kuchukua fedha kwenye Wakala wa Serikali kama *TCRA*, *TFDA* na kadhalika wakati tayari alikuwa anachukua, je, alikuwa anachukuwa kwa idhini ya nani? Hatuwezi (Bunge) kuruhusu uvunjifu huu wa sheria. Hii ni sawa na kusaini *blank* cheque kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na bomoabomoa pale Tabata Dampo, Dar es Salaam. Ni kweli kwamba sikubaliani na ujenzi holela au sehemu ambazo si za makazi lakini tuna Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na watendaji kibao, hivi huwa wanakuwa wapi mpaka msingi uanze kujengwa mpaka ukamilike ndio wabomolewe?

Mheshimiwa Spika, kubwa linaloniumiza, ni Serikali ile ile kupitia Manispaa/Halmashauri kuvunja nyumba hizo na hapo hapo Serikali ile ile ndiyo inayowalipa fidia waliobomolewa. Kwanza, naomba kujua fedha walizolipwa watu wa Tabata zimetoka fungu gani au zimetoka wapi? Sh.1.8 bilioni, sio mchezo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina bahati kubwa sana ya kuwa na bandari na kuzungukwa na nchi sita zisizo na bandari (*landlocked*) countries. Hali hii ni fursa kubwa sana na hivyo tunapaswa kutengeneza miundombinu imara hususani reli ili iwe inasafirisha *containers* na mizigo mingine mikubwa kwenda nchi hizo na vile vile kuchukua mizigo kutoka huko ili iweze kusafirishwa. Kwa mfano, nchi kama Zaire yenye madini mbalimbali, Zambia yenye *cooper*, wangeweza kabisa kupitishia bidhaa zao hapa Dar es Salaam, hivyo kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, tumekuwa na malalamiko mengi kuhusu mlundikano wa *containers* pale Dar es Salaam na kwamba sasa wafanyabiashara wengi hupitisha mizigo yao huko Mombasa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ijenge reli ya Voi-Moshi, ili Moshi itumike kama *Inland Port*. Hii itasaidia sana kukua kwa miji ya Mikoa ya Kaskazini, lakini pia itaongeza pato la Taifa na kuhakikisha kuwa makontena mengi yanaingia ili tuweze walau kufikia nchi kama ya Singapore iliyondelea kiuchumi kwa kutumia tu bandari zake.

MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa 100% na nakupongeza sana wewe na Wizara yako nzima kwa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba msaada wako kwa kunisaidia matengenezo ya barabara ya Kaliua - Uyowa - Ulyankulumahazi – Kashishi – Kahama. Barabara hii itafungua uchumi wa eneo hili kwa kuunganisha Mkoa wa Tabora na Shinyanga kwa kupitia Wilaya za Urambo na Kahama. Najua inaweza ikawa ngumu kuzipata fedha zote kwa mpigo lakini angalau tufanye kwa awamu mbili.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema kwamba nakupongeza sana.

MHE. MAIDA H. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya afya, kwanza, mwaka huu niipongeze Serikali kwa kuitengea sekta hii asilimia 11 lakini naomba kuishauri Serikali kuwa na udhibiti mzuri katika matumizi ya fedha hizo ndani ya sekta hii kwa sababu mara nyingi huwa tunapata maswali kutoka kwa wananchi. Itakumbukwa kuwa Wizara ya Afya, ni miongoni mwa Wizara muhimu katika kusimamia afya ya binadamu. Mara nyingi wanawake ndio wanaoathirika katika kipindi cha uzazi kwa:-

- Kutoka masafa marefu kwenda vituo vya afya;
- Kupoteza damu nyingi wakiwa njia;
- Ucheleweshwaji wa matibabu wanapofika katika vituo vya afya;
- Uzembe wa wahudumu wa afya kwa visingizio vya rushwa; na
- Ukosefu wa madawa katika vituo vya afya. Matokeo yake akinamama hao hupoteza maisha bila kufanikiwa kupata matibabu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali kuwa na ufuatiliaji katika sekta mbalimbali ili fedha iliyotengwa iweze kutumika ipasavyo. Naomba ifikapo mwaka 2009/2010, kiwango cha asilimia 15% katika sekta hii kiweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya kilimo, nchini Tanzania bado hatujafikia hatua ya kilimo endelevu. Mara nyingi, kilimo chetu huwa ni cha msimu na hakiendelezwi kwa maana ya kujitosheleza kwa chakula nchini. Ninapenda kuishauri Serikali kuendeleza kilimo nchini Tanzania angalau kufikia asilimia 50% nchini. Hii itasaidia kufikia lengo la MKUKUTA lililokusudiwa na pia kuongeza fedha katika kipindi cha mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utegemezi, naipongeza Serikali kwa kufikia hatua ya kuondoa utegemezi nchini kwa asilimia 34. Bila shaka ifikapo mwaka 2009/2010 kiwango hicho kitazidi kupungua ili tuweze kuendelea kujitegemea kwa kutumia fedha zetu wenyewe katika matumizi ya ndani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Usalama wa Raia, naomba niipongeze Serikali kwa kuendelea kuweka majengo mapya katika Wizara hii. Vile vile ninajua Jeshi, ni watu walio na kazi kubwa katika ulinzi wa Taifa letu, ni vizuri tuwaboresheshe maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujenga majengo mapya sasa hivi yapo majengo yaliyochakaa na mabovu ambayo wanakaa Askari hao. Ni vyema tukaweka utaratibu wa kuyakarabati yale majengo makongwe ili yasiendeleo kupotea na tukiangalia kila mwaka huwa tunaongeza ajira mpya.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kisisitiza kuweka udhibiti katika ufuatiliaji mzuri wa matumizi ya Serikali katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. MAGALLE J. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, pamoja na kupata fursa ya kuchangia kwa mdomo, napenda kutumia fursa hii kuchangia kwa maandishi ili kukamilisha maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kuwapongeza kwa dhati kwa kazi nzito ya kufanikisha maandalizi yote kuhusu mipango ya maendeleo ya Serikali kwa mwaka 2008/2009 na mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Fedha na Manaibu wake wawili na Katibu Mkuu wa Wizara hii. Vilevile napongeza watumishi wote na watendaji wote waliohusika katika mchakato huu wa kuandaa maelezo ya mipango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa namna ya pekee, Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete, kwa juhudi zake za kimyakimya na za Diplomasia ya Uchumi ambazo zina sehemu kubwa katika ujenzi wa mipango na katika kusaidia Tanzania kupata misaada ya Kimataifa ya kuvuna michango mbalimbali na kuboresha misaada na matumizi ya bajeti ya Taifa na kwa kuvutia wawekezaji. Tusione chaelea kina wenyewe, hivyo tumtakie kila la kheri Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, napongeza mchango wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi inayoongozwa na Mheshimiwa Abdallah Kigoda, (Mb) wa Handeni na napongeza Wabunge wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri ya kuboresha mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hapa tupo katika majadiliano kuhusu mipango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2008/2009. Baada ya majadiliano, ndipo patazaliwa bajeti ya mwaka ya Serikali kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, hotuba za Waziri wa Fedha na Mipango, una changamoto nyingi sana. Moja ya changamoto, ni kauli ya Serikali ya kumalizia miradi inayoendelea ili pesa za matumizi zipate utimilifu wa thamani ya pesa za matumizi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari, naomba kuwasilisha yafuatayo ili kuikumbusha Serikali kuwa inahitajika gawio la pesa za matumizi ili mradi wa maji wa Maswa uweze kuwa wa tija. Jumla ya Sh.1.2bil zinahitajika kwa ajili ya ufundi ambapo nimewasilisha Serikalini, Wizara ya Maji. Aidha pesa hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa chujio na madawa, ununuzi wa dira, upanuzi wa mtandao na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili kuepusha malimbikizo yanayosababisha kuzaliwa uchakavu kwa pesa ambazo tayari zimetumika katika huu mradi wa maji wa Bwawa la Maswa, naomba matumizi ya nyongeza ya kukamilisha mradi huu yatolewe ambayo ni jumla ya Sh.1.2bil.

Mheshimiwa Spika, licha ya Bwawa la Maji, wananchi wanajuhudi za kuchangia ujenzi wa visima. Naomba tukamilishe miradi iliyopo ya visima ili tusiwakatishe tamaa wananchi. Naomba Sh.700mil kwa miradi ya visima ili tukamilishe zoezi la awamu ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri wa Mipango na Fedha, inahimiza Mikoa na Wilaya kubuni fursa za maendeleo ambapo Serikali itaboresha. Napenda kukumbusha kwamba Mheshimiwa Mramba alipokuwa Waziri wa Miundombinu, alikamilisha uchambuzi wa matumizi yanayohitajika kutengeneza maeneo korofi yanayotenganisha vijiji kupata huduma mbalimbali za afya na kuzuia mzunguko wa kijamii na kuzuia watoto wa shule kwenda shule. Tuliafikiana kilomita 291.7 zitengenezwe kwa kupachikwa viraka ili tufungue mawasiliano ya vijiji katika vipindi vyote.

Mheshimiwa Spika, kukamilisha mradi huu wa kuweka viraka, tunahitaji Sh.1.8bil kwa ajili ya mafuta, kalvati, *drift* na madaraja watenda kazi na gharama za *service* kwa mitambo tuliyonayo Maswa. Naomba gawio hili ili tukamilishe mradi huu. Msaada wa kuondoa adha hii, ndio utekelezaji wa maudhui ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kutoa rai kwa Waziri wa Fedha na angalizo la kuwa wakati umefika Tanzania iwe na utaratibu wa kuthaminisha viongozi wake hasa ambao muda wao wa kutumikia Majimbo yao unamegwa na uwajibikaji wa kutumikia Majimbo yote Kitaifa.

Naomba Wizara ya fedha ibuni jinsi ya kuenzi wakati wao usiotumika katika Majimbo yao ili upate fidia ya kushughulikiwa katika kutatuliwa matatizo yao ya Majimbo ambayo ni maji, barabara na mengineyo.

Rai hii sio tuwape pesa, bali Serikali iongozwe na hisia za umma dhidi ya kushangaa, vipi fedheha zinaposhamiri kwao? Je, wapi ni mfano wa utatuzi wa kero?

Rai hii inahitajika kutendwa kwa Wabunge wenzetu wenye majukumu ya kitaifa, nao ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, Spika na Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Mipango namwomba aboreshe huduma ya Afya Maswa.

Katika bajeti ya mwaka 2006/2007 niliwasilisha kuhusu vifo vya kutokana na kukosekana mawasiliano na vita ya kupambana na imani potofu.

Maswa ni eneo la *Square kilometre* 3400, wigo huu ni sawa na Majimbo matatu kwa viwango vya Taifa vya Majimbo. Maswa ina Waganga wa Jadi wanaokadiriwa kufika 2,000 na hawa ndio chanzo cha imani potofu.

Mheshimiwa Spika, naomba *ambulance* tatu ziwezeshe kuokoa maisha ya wagonjwa wa jinsia na marika yote. *Ambulance* zitahamasisha vita dhidi ya imani potofu na kuondoa utegemezi wa umma kwa Waganga wa Jadi na imani potofu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa muhtasari kuwasilisha ushauri ufuatao kwa hotuba za Waziri wa Fedha na Mipango katika kufikiria Maswa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ni malighafi kwa ustawi wa maendeleo ya jamii. Kwa hiyo:-

- Maswa tumechoka viimbo vya kuwa wananchi wanauana kwa imani pototu. Vifo vingi vinatokea kwa kutumia mikokoteni kwa sababu barabara ni mbovu kuvutia magari ya kufika vijijini;
- Naomba Serikali itusaidie kuondoa viamsha vifo vya watoto, wazazi na wagonjwa wengine ambao wangefikishwa hospitali wakapona; na
- Napenda kutambua kuwa Wizara ya Mipango na Fedha ndio Wizara mama ya kufaulisha uwezesaji wa Wizara zote za kutoa vipaumbele vya kutatua kero nzito za viwango vizito.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Fedha anasema maelezo gani kwa yanayotokana na mwongozo wa hotuba yake kwa utatuzi wa matatizo ili tufaulishe maendeleo na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Vile vile kwa kufaulisha Maswa kupata maisha bora.

Naomba kufafanua kwamba hali ya *maternal mortality rate* kitaifa ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kitaifa ni 529/100000.
- (b) Maswa 221/100000.

Hizi ni takwimu kwa wale ambao mikokoteni ya ng'ombe iliwafikisha hospitali. Takwimu za wale ambao hawakufikishwa hospitali na wale waliofia kwa Waganga wa Jadi hazipo na ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, *Ambulance* tatu ndio msingi wa kukabiliana na tatizo hilo. Mwendo ambao mikokoteni husafiri ni umbali wa kati ya kilometa 40 hadi 100

Mheshimiwa Spika, Maswa hakuna vituo vya uchunguzi na tabibu na hakuna hata hao wasaidizi wa tabibu ndio maana Waganga wa Jadi ni wengi.

Mheshimiwa Spika, pia Maswa mazingira ya maisha yake ni duni kwa kukosa maji, umeme na kuni shida hivyo vivutio hata vya kupata waalimu ni shida. Hivyo, hizi ndio fedheha za kuondolewa na CCM yetu, Chama cha ukombozi kwa watanzania wote.

Namwomba Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu wapokee maombi ya magawio haya kwa kuwa ndio msingi wa viamsha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kila mtanzania anawajibu wa kuchangia uchumi wa Taifa. Ni ukweli usioplingika kwamba pamba inachangia pato la Taifa. Azma ya Serikali kupitia bajeti ya Serikali ni kuzalisha mazao ya biashara. Hii ipo katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM.

Mheshimiwa Spika, zama ni kuzalisha marobota ya pamba kutoka 700 hadi milioni 1,500,000 ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, je, zao la pamba ni la mayatima? Kama sio zao la mayatima: Je, Waziri wa Fedha na Uchumi, anawaeleza nini wakulima wa pamba kuhusu kuiwezesha Bodi ya

Pamba isimamie wadau wa pamba ambao ni wanyonyaji wa haki za wakulima wa zao la pamba?

Mheshimiwa Spika, wakulima wa pamba wanadhulumwa na wafanyabiashara ya pamba kwa sababu Bodi ya Pamba haiwezeshe kupata fedha za Bajeti ya kutekeleza wajibu wake wa kusimamia.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Pamba inawatumishi 62. Mkoa wa Shinyanga pekee una Kata 157, vijiji 876, Bodi ina watumishi 7: Je, ufanisi uko wapi ili wakulima wasidhulumwe?

Mheshimiwa Spika, pamba inalimwa katika Wilaya 42 na Mkoa 13. Je, zao hili ni la mayatima, hivyo Serikali haioni umuhimu wa kuiongezea uwezo Bodi ya Pamba ifaulishe wajibu wake?

Mheshimiwa Spika, zao la pamba linachangia asilimia 40 katika pato la Taifa. Je, Serikali kwa nini haiboreshi Bajeti ya uendeshaji Bodi ya Pamba?

Je, kwani Waziri wa Fedha na Uchumi anataka tukuze uchumi na mapato ya Taifa kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya?

Je, Serikali inajua kuwa kutoiwezeshe Bodi ya Pamba kuwa na uendeshaji wa tija ni kudhibiti wakulima kuondoa umaskini wao, hivyo maisha bora ni ndoto kwa shinikizo la mfumuko wa bei ambao haukabiliki kwa vile wakulima wanadhulumika katika uzalishaji wa pamba?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha waelewe kwamba pamba ni agenda ya kisiasa ya kuvutia ushidani wa imani za wakulima.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba Serikali Ijali shida za Bodi ya Pamba ili tudhibiti upotoshaji wa siasa potofu na naiomba Serikali iongoze Bajeti ya Uendeshaji wa Bodi ya Pamba ili Bodi ifuzu kutekeleza wajibu wake vyema.

Je, lini mkulima atapumzika kudhulumwa baada ya makovu ya dhuma za ushirika?

Mheshimiwa Spika, naomba Bajeti ya mwaka 2008/2009 iwe mwanzo wa uamsho wa imani ya wakulima kuwa Serikali inawajali. Hii bajeti isaidie Bodi ya Pamba kudhibiti mifereji ya kudhulumu wakulima kupitia *Pass Book* ambayo haina usimamzi wa Bodi kwa vile hawamo watumishi na pesa za uendeshaji.

Sasa naomba Serikali idumishe imani za wakulima kwa Chama tawala dhidi ya viimbo vya siasa potofu.

Mheshimiwa Spika, Maswa tuna vijiji 104, Kata 18: Je, mtumishi mmoja wa Bodi atafanya kazi vipi ili dhuluma isitendeke?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumuko wa bei: Je, Serikali inaweza kuwa na maduka yasiyo na kodi ama yenye ruzuku ya Serikali kwa mauzo ya vifaa vya ujenzi kwa shule na vituo vya Afya? Hii itasaidia kuniua uwiano wa manunuzi kwa vijiji vyake na itachochea michango ya umma kuwa na kazi katika majengo ya shule na vituo vya afya.

Mheshimia Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba nipatiwe maelezo ya kujibu hoja nilizoziwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHESHIMIWA LUCAS LUMAMBO SELELII: Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kazi na kuwatakia heri ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa sana kwamba katika bajeti ijayo hakuna tena fedha kwa ajili ya barabara Itigi – Tabora –Kigoma na barabara ya Nzega – Tabora.

Mheshimiwa Spika, ukali wa maisha miongoni mwa wananchi wa kawaida (wenye kipato cha chini) umezidi kutokana na kupanda kwa mafuta na pesa yetu kukosa thamani.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa fedha yetu ya ndani na maskini katika sheria ya manunuzi.

Mheshimiwa Spika, Mifuko ya Pensheni *PPF/NSSF/NPF* inawekeza fedha nyingi katika kujenga majengo ya kukodisha jambo ambalo ni zuri.

Nashauri, kwa kuwa wafanyakazi ndio wanachama wanaounda mifuko hiyo, naomba mifuko hii ifanye utaratibu wa kuwa na sera ya kuwakopesha fedha ili wajijengee maisha yao, kujenga nyumba na kadhalika, fedha zao za mafao iwe ndio kinga ya kupewa mkopo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti zijazo zizingatie kuondoa tatizo sugu la maji na kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwamba Bajeti hii imepongezwa na walalahoi wengi. Inaleta unafuu kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, mambo ya kuzingatia:

- (1) Kudhibiti mfumuko wa bei;
- (2) Kudhibiti bei ya mafuta; na
- (3) Ruzuku ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma uko pembezoni, lakini wana fursa nyingi za maendeleo kutokana na Ziwa Nyasa. Utalii uongeze kunufaisha Taifa kwa wananchi wa kandokando ya ziwa lile ikiwa ni pamoja na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kuna Bandari ya Bambabay ambayo kama ingeimarishwa, basi *Mtwara corridor* kupitia bandari ile tungefanikiwa sana. Bandari ile inaweza kuwa kiungo muhimu sana kati ya Tanzania na nchi zote za Kusini mwa Afrika na *SADC*. Naomba Serikali iimarisha bandari hii.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege wa Songea ni kati ya viwanja vikubwa sana na vizuri vilivyojengwa kwa lami, lakini hadi sasa hakuna ndege inayotua Songea. Kisa! Eti hakuna kituo cha mafuta ya ndege. Kwa nini Serikali isitafute wawekezaji wawekeze kwenye mafuta?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. ZULEKHA YUNUS HAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu na Watendaji wake wote kwa hotuba yake nzuri yenye kueleweka. Pia naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa bajeti hii na kueleweka, bado kuna mapungufu mengi yakiwemo kwenye elimu, ingawa mashule mengi ya sekondari yamejengwa, lakini bado ifanywe bidii kwa kupatikana walimu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, pia iongezwe bidii zaidi kwa kupatikana Madaktari, madawa na vitendea kazi vyote vinavyohusika, kwani mtu ni afya.

Mheshimiwa Spika, kilimo pia hakikutiliwa mkazo sana kwenye bajeti hii, kwa hiyo, izingatiwe sana kwa kununuliwa matrekta pamoja na pembejeo zote za Kilimo.

Mheshimiwa Spika, pia nasikitika kuwa bajeti hii haikutoa mchanganuo kwa makundi maalum ambayo ni wazee, vijana, watoto na watu wenye ulemavu. Kama tunavyojua, watu wenye ulemavu wana mahitaji maalum ya kuweza kuwawezesha kama vile visaidizi vya elimu, vifaa ya kujimudu, mfano fimbo nyeupe, vibaskeli, magongo na kadhalika, pia majengo yanayojengwa waweze nayo kuyatumia na kufaidika na nchi yao.

Mheshimiwa Spika, naitakia Wizara utendaji mwema.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwa ujumla, hotuba hii ni nzuri na ina mwelekeo wa kuinua uchumi wa nchi yetu na inatekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hotuba kwa kuanzia na eneo/sekta ya kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili.

Sekta hii ndiyo inawahusisha wananchi wengi wa Taifa hili, lakini kwa kiasi kikubwa bado haijawa na uwezo wa kuchangia maendeleo sio ya wakulima pekee bali pia hata Taifa letu kwa ujumla. Serikali iweke mikakati mingi katika kuinua Kilimo, lakini mikakati hiyo utekelezaji wake bado haujawa mzuri.

Mheshimiwa Spika, unapotaka kuhimiza kilimo ni lazima uanzie na uwekaji wa miundombinu yake. Miundombinu hii ni pamoja na vitendea kazi (matrekta, plau na kadhalika), raslimali watu (wakulima).

Mheshimiwa Spika, hauwezi kuhimiza kilimo kama wakulima waliopo wataendelea kulima kwa kutumia jembe la mkono. Hadi sasa zaidi ya asilimia 70 ya wakulima wanatumia

jembe la mkono. Serikali kwa upande wake inajitahidi kupeleka fedha chini ya *Program* mbalimbali kama *DADPS*.

Mheshimiwa Spika, mpango huu wa *DADPS* kwa mwaka huu wa fedha zimepelekwa fedha nyingi kwenye Wilaya zetu, lakini miongozo iliyopo inaelekeza fedha hizo kupeleka kwenye vikundi vya wakulima ili kuboresha mazao.

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wangu na kutokana na hali iliyopo, hasa katika Jimbo langu la Kibiti na Wilaya ya Rufiji, fedha hizi zinapokwenda kwa wakulima haziwasaidii kuboresha kilimo chao. Ni vizuri sasa badala ya kutoa fedha hizi kwenda kwa wakulima moja kwa moja, ziweze kutumika kununulia matrekta ambayo yatasaidia kuongeza mapato yao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni maji, hasa kwa miji midogo iliyokuwa inafadhiliwa na Serikali ya Ufaransa. Kwa muda wa zaidi ya miaka mitatu sasa, utekelezaji wake haueleweki. Serikali iliahidi katika Bunge lililopita la Bajeti kuwa fedha zilizotolewa na Serikali ya Ufaransa zilikuwa hazitoshelezi kukamilisha miradi yote, hivyo Serikali itasaidia kwa kukamilisha ujenzi wake katika baadhi ya miji. Mheshimiwa Spika, miongoni mwa miji iliyo katika mpango huo ni Kibiti, Ikwiriri, Utete na Mpwapwa. Miji ya Kibiti na Ikwiriri imeondolewa kwenye mpango huo na sasa Serikali imeahidi kuikamilisha. Ahadi hii ni ya Serikali, utekelezaji wake haueleweki. Naiomba serikali iweze kutoa kauli kuhusu ni lini miradi hii ya maji itakamilika.

Mheshimiwa Spika, suala la kupatiwa umeme kwa Wilaya za Rufiji, Kilwa na Mkuranga kupitia mradi wa *SONGAs*, bado pia ni kitendawili. Ahadi nyingi zilizotolewa na Serikali kuhusu lini mradi huu utakamilika, nazo sio za kweli. Hadi sasa mjenzi wa *power station* pale Somanga Fungu bado haujakamilika. Pia kuna tatizo la namna ya kurusha umeme kwenye daraja la Mkapu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isimamie ipasavyo ujenzi wa *Power Station* hii na kukubaliana juu ya namna bora ya kurusha nyaya za umeme katika mto Rufiji ili ahadi ya kuwapatia umeme wananchi wa Wilaya hizo liweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uzima na afya njema kueleza yafuatayo juu ya Hoja ya Bajeti ya Serikali 2008/2008.

Mheshimiwa Spika, utafiti ni jambo muhimu katika kuhakisisha lolote litakalofanyika litakuwa na uhakika na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, lakini imegundulika kuwa watafiti wengi wanaondoka na kwenda nchi za jirani kupata maslahi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu tuboreshe maslahi ya watafiti wetu ili wasipate vishawishi vya kuondoka nchini. Mfano, kuboresha mishahara, usafiri na marupurupu yao kama motisha.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, imebainika kuwa pia watafiti wengi wanastaafu, jambo ambalo ni hatari kwa wataalamu kama hawa kupungua idadi siku hadi siku. Ushauri wangu ni kwamba, Serikali iwe na mikakati madhubuti ya kuhakikisha tunatayarisha watafiti wapya kila wakati kukabiliana na wimbi la wastaafu hao tunaowategemea.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kukabiliana na upungufu wa chakula duniani, sambamba na hilo kwa nchi kama Tanzania hatuna budi kukipa nafasi kubwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina mabonde mengi yanayofaa kwa Kilimo cha umwagiliaji, lakini hakuna mikakati madhubuti ya kuimarisha sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro una mito 176 iliyokauka, kiwemo 18 mikubwa zaidi. Lakini tunajiuliza hivi, raslimali hii Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuboresha kilimo hicho katika kuhakikisha uzalishaji wa chakula umeongezeka, hasa wakati huu dunia ikiwa na upungufu wa chakula? Ushauri wangu ni kwamba sasa ni wakati muafaka jitihada za makusudi kuhakikisha unatafuta fedha na kuufanya Mkoa wa Morogoro uzalishe zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, manunuzi ya umma ni tatizo kubwa na imeonekana hakuna uwiano wa manunuzi ya magari na samani katika Wizara na Idara za Serikali. Kila sekta inanunua magari na samani kulingana na matakwa ya maafisa wa sekta husika jambo ambalo ni hatari na baadhi ya magari na samani zinazonunuliwa haziko katika ubora unaostahili. Ushauri wangu ni kwamba Serikali iwe na utaratibu unaolingana katika manunuzi ya magari na samani.

MHE. RICHARD MGANGA NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Naomba nitoe ushauri ufuatao:

Mheshimiwa Spika, Hazina ndiyo moyo wa Serikali. Moyo wa binadamu ukisimama anakufa na bila Hazina Serikali itakufa. Hazina ikitetereka, Serikali itapata kiharusi (*strock*), siha ya Serikali inategemea utendaji mzuri wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, nidhamu ya matumizi endapo itadhibitiwa vizuri, manufaa yake yataonekana. Nashauri tusimamie vizuri nidhamu ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wasio waaminifu katika Serikali hasa fedha zinazokwenda katika Halmashauri ni kama hazina mwenyewe. Kwa mfano, *basket fund* ina pesa nyingi sana (*road fund*), mfuko huu una pesa nyingi sana. Lakini pesa hizi hazisimamiwi vizuri kwa sababu ya ukiritimba wa utoaji taarifa. Lazima Serikali iwe makini na mifuko hiyo, iwape semina waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayokusanywa kupitia *TRA* yangeweza kuongezeka zaidi kuliko hivi sasa endapo baadhi ya mianya itazibwa. Kwa mfano, leo hii ukienda Zanzibar, upo utaratibu wa magari ambayo yametoka Dubai na kupita Zanzibar na kuja Bara. Gari likifika Zanzibar linalipiwa ushuru mdogo wa Shilingi milioni 1.5, *Fusso* likiletwa bara linalipiwa ushuru Shilingi milioni moja au milioni 1.5, hivyo gari hulipiwa ushuru wa shilingi milioni 3.0

ambapo gari hilo hilo likipitia bandari ya Dar es Salaam ushuru wake huwa ni Shilingi milioni saba (7).

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, Serikali kwa gari moja hupoteza shilingi milioni nne na magari kupitia Zanzibar kila siku sio chini ya magari 10, hupitia Zanzibar kuja Dar. Kwa maana hiyo, Serikali (*TRA*) hukosa shilingi milioni 40 kila siku kwa kupitia Zanzibar. Hilo ni eneo moja, hata leo ukienda, haya utayakuta.

Mheshimiwa Spika, nashauri utaratibu huu uangaliwe ili mapato yetu yaongezeke. Mimi kama mjumbe wa kamati ya fedha na uchumi nimeshiriki katika kuandaa ripoti yetu iliyosomwa na Mwenyekiti Kigoda. Nimeona niongezee na hili la magari Zanzibar.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchukua nafasi hii kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inayohusu mpango wa Maendeleo wa mwaka na ile ya mapendekezo ya matumizi kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba uchumi wa nchi umekua kwa asilimia 7.1. Hili ni jambo la kupongezwa, lakini kasi hii ya ukuaji wa uchumi ni ndogo ikilinganishwa na raslimali tulizonazo hapa nchini. Aidha, ninaamini kwamba kama Serikali ingekuwa makini zaidi kuzuia uvujaji wa mapato, basi hali ya ukuaji wa uchumi ingekuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu fika kwamba madhumuni ya kutoa misamaha ya kodi ni:-

- (i) Kufikisha huduma za kijamii zilizo bora kwa wananchi;
- (ii) Kushuka bei za bidhaa ili kupunguza ukali wa maisha; na
- (iii) Kukuza uchumi mdogo na kuongeza pato la Taifa.

Kwa bahati mbaya, pamoja na Serikali kutoa misamaha ya kodi, huduma za kijamii zimekuwa hazipatikani za kuridhisha, bei za bidhaa zimekuwa juu mno na mpango wa kaya kuwa mbovu. Wananchi wameshindwa kumudu maisha yao. Wanaoneemeka na misamaha hii ya kodi ni wafanyabiashara na wawekezaji.

Naishauri Serikali kupunguza misamaha ya kodi kwa kuanzia angalau asilimia 50 ili kuongeza makusanyo na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

Eneo lingine ambalo Serikali imekuwa ikipoteza mapato ni kutokana na Mashirika na taasisi za umma, ambayo Serikali imewekeza hayatoi gawio kwa Serikali. Masharika ya umma kama *TANAPA*, *TPA*, Benki ya Posta na kadhalika kama ambavyo ripori ya *CAG* ilivyobainisha. Kwa bahati mbaya Serikali imekaa kimya wala haijali, hususani jambo hilo.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 45 Waziri anazungumzia kurekebisha sheria ya usimamizi wa fedha za umma ili asasi, wakala wa mamlaka za umma ziweze kuchangia mfuko wa Serikali. Hili ni jambo la kusikitisha kwani kwa muda mrefu Serikali imekuwa inapoteza mapato yake.

Naishauri Serikali kwamba utaratibu wa kukusanya *arrears* zake za miaka ya nyuma kutoka Taasisi na mashirika ya umma, ambayo yalikuwa hayalipi gawio kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kadhalika Serikali imekuwa inapoteza mapato kadhaa kutoka katika sekta ya madini, mirahaba imekuwa ni midogo 3% misamaha ya kodi imekithiri na kadhalika.

Mimi naishauri Serikali kwanza kuzingatia maoni ya Kamati ya Madini iliyoongozwa na Jaji Bomani na kuchukua hatua zinazofaa ili wananchi wafaidike na Serikali ya nchi yao.

Serikali pia imekuwa inapoteza mapato mengine mengi sana kwenye sekta ya Utalii. Jambo hili limekuwa linapigiwa kelele sana na Wabunge wengi na wananchi ambayo nia yao ni kuisaidia Serikali kudhibiti mapato yake kwa manufaa ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi nayo ni miongoni mwa maeneo ambayo kama Serikali ingekuwa makini na kuyatumia vyema, uvuvi wa bahari kuu umekuwa haujapewa uzito unaostahili. Meli kadhaa za kigeni zimevuna rasilimali ya Taifa hili bila sisi kufaidika na chochote. Ahsante.

MHE. KHERI K. AMEIR: Mheshimiwa Spika, wakati huu nchi yetu inasomwa bajeti ya mwaka 2008/2009 na kuombwa kupitishwa. Dunia inapiga kelele juu ya janga la njaa inayoikabili na tishio la ukame na upungufu wa chakula. Mimi sielewi na sijui kama nitaelewa. Kwa nini na kwa misingi/kigezo gani vimetumika bajeti hii isiweke kipaumbele sekta ya Kilimo kwa kutengea fedha nyingi zaidi na badala ya kuzipunguza?

Mheshimiwa Spika Kilimo kutengewa Shilingi bilioni 460, au asilimia 6.4 wakati huu ni upuuji. Inapaswa tuelewe jambo moja muhimu. Wakati wa nyuma au miaka iliyopita panapotokea ukame, mataifa makubwa yakiwemo Marekani, Uchina, Japan, India na hata Uingereza huwa yanatusaidia au wanatupa chakula cha msaada. Vipi leo? Itakuwaje na hasa kwa wakati huu nchi hizi zinapoamua waache kutoa msaada bali kununua chakula chao na kinachozalishwa katika nchi zao? Lakini kubwa zaidi ni onyo na tahadhari inayotolewa na vyombo vya kimataifa kuhusu janga la sahara na sisi tukiwemo.

Mheshimiwa Spika, kwa akili ya kawaida tu, inatutuma kwamba tahadhari yapaswa kuchukuliwa mapema, kuongeza au kupanua wigo wa sekta ya Kilimo badala ya kuiviza.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato *TRA*, mimi binafsi nawapongeza sana Wizara ya Fedha na hasa kwa jitihada zao za ukusanyaji wa mapato. Kima cha makusanyo ya zaidi ya Shilingi bilioni 300, kwa mwezi jitihada zinazofanywa na *TRA* ni upeo wa utukufu wa utendaji mzuri wa kazi za kusifiwa.

Mheshimiwa Spika jitihada kama hizi zilipaswa zielekezwe vile vile kwa upande wa pili wa nchi yaani Zanzibar .

Hiki ni chombo cha muungano, naelewa fika matatizo yaliyopo Zanzibar, lakini haitoshi hilo kwani mashaka ya ugumu na ukali wa maisha hasa huduma za jamii kama vile Hospitali, Sekta ya Elimu, Maji na kadhalika, zinawagusa watu wa kawaida moja kwa moja. *TRA* Zanzibar kukusanya asilimia 4.0%, sio jambo jema! Hiki sio kitendo cha kuachiwa kwa kusingizia ni kwa *TRA* Zanzibar wana mipango yao ya makusanyo.

Aidha, mimi sikubaliani na hili wala sitakubaliana nalo kuachia fedha kuibiwa kupitia mgongo wa msamaha, jamii ikiwa inapata taabu na fedha hizo kuachwa kufaidisha watu wachache wafanyabiashara na viongozi wa Serikali. Sio jambo la kulifumbia macho. Nashauri na nawaomba *TRA* waliingile kati, kuna hatari na madhara makubwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la mafuta na gesi, hili nalo limefikia wapi? Mshauri mwelekezaji amefikia wapi mpaka sasa? Niliwahi kutoa ushauri hapa kama suala hili linachukua muda mrefu, kwa nini hatuwatumii wataalamu wetu wa ndani kusaidia kuchanganua mgawanyo wa mapato kati ya Zanzibar na Bara? Wakati huu uchumi wa dunia unakuwa na uchache wa nishati ya petroli na uchumi wa mataifa makuwa kuyumba, nadhani ni wakati mwafaka, kulisimimia jambo hili ili taratibu za ufuatiliaji wa mafuta uendelee na nchi ipate kutononoka.

Mheshimiwa Spika, kuna kauli mbalimbali ambazo ni vigumu kuzithibitisha. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuleta majumuisho tunamwomba suala hili alieleze na aliweke bayana: Je, ni kweli suala hili limekwamishwa na Serikali ya Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, uvuvi wa bahari kuu, naomba Mheshimiwa Waziri aje kutueleza ni lini chombo hiki *Tanzania Deep Sea fishing Authority* kitateuliwa na kuanza kazi. Nchi hii inaibiwa sana na kuna meli kubwa kubwa zinavua na kuibia Taifa hili mabilioni ya fedha. Serikali hili inalijua hilo? Je, tumejitayarisha vipi kuvua raslimali ya bahari hasa samaki na kuzilinda?

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli nashindwa kuelewa, sisi Watanzania tuna matatizo gani! Njaa inakuja, bajeti ya kilimo tunaipunguza; ardhi nzuri tunayo kwa kilimo Tanzania ina maji wataalam wa kutosha na raslimali, hatuitumii; tuna *sources* za mafuta na gesi hatujipangi vyema kuvuna; tuna bahari, mito, maziwa, tunazembea; wageni wanaleta meli kubwa kubwa za uvuvi wanatuibia; Ziwa Victoria Waganda nao na Kenya wanavua kiholela bila mpango wa makubaliano; tunayo maafikiano? Sielewi! Nadhani pana tatizo hapa.

MHE. IDDI AZZAN: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikupongeze kwa umahiri wako wa uendeshaji wa Bunge. Pili, naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara ya Fedha kwa jinsi ilivyoweza kuandaa bajeti hii nzuri yenye kumlenga mwananchi kwa kumpunguzia ukali wa maisha.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikaangalia uwezekano wa kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza mapato na kuweza kuongeza miradi mingi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi hasa mafuta ghafi ya kula, *industry suger*, petroli na dizeli kwa makampuni ya madini ni miongozi mwa mambo yanayoinyima Serikali mapato makuwa sana. Hivyo nashauri bidhaa hizo zitozwe kodi kama kawaida ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia Serikali na taasisi zake wakaangalia uwezekano wa kupunguza matumizi hasa kwa magari kutokana na ongezeko kubwa sana la bei ya mafuta, posho mbalimbali, *furniture* nakadhalika.

Mheshimiwa Spika, upo unyonyaji na unyanyasaji mkubwa sana hasa kwa wenye mahoteli ya kitalii Kinondoni, Bagamoyo na kadhalika kwa kuwalipa mishahara midogo na kuwafanyisha kazi kwa muda mrefu bila kuwalipa *overtime* kinyume na maagizo ya Serikali.

Naiomba Serikali ifuatilie kwa makini maelekezo inayoyatoa hasa kwenye kima cha chini cha mishahara ili hawa wawekezaji wasiendeleo kuwanyonya wananchi wetu.

Kuhusu Miundombinu ya jiji la Dar es Salaam, naiomba sana Serikali itenge bajeti maalum kwa ajili ya kuboresha barabara, mitaro ya maji taka na maji ya mvua ili kuondoa kero hiyo kubwa katika jiji letu ambalo ndio kioo cha nchi yetu. Kutegemea Halmashauri pekee ni kujidanganya, kwani uwezo wa mapato wa Halmashauri zetu ni mdogo sana. Hivyo, uwezekano wa Halmashauri kuondoa kero hiyo ni ndoto, lakini kama Serikali itaruhusu Halmashauri zitoze kodi magari yote yanayoingia Dar es Salaam kutoka mikoani na nje ya nchi, angalau tungeweza kukusanya zaidi na kuondoa kero hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AZZAN ZUNGU: Mheshimiwa Spika, Miundombinu ya Ilala ni muhimu sana na uwezo wa Halmashauri ni mdogo, vyanzo vyetu mmevichukua na fidia mnayolipa haikukamilika. Kwa mfano, makisio yetu ya vyanzo ni Shilingi bilioni 2.7, lakini kila mwaka zinashuka. Mwaka 2007/2008, Shilingi bilioni 1.7; 2008/2009 Shilingi bilioni 1.5 badala ya Shilingi bilioni 2.7. Tunaomba tupewe idhini ya kukopa na mkopo utalipwa kwa kodi za majengo na turuhusiwe kurudisha ada ya leseni ya biashara. Serikali nina *share 40% Celtel*, ni lini gawio limepokelewa?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuweka sheria ya wataanzania kumiliki hisa kwenye mabanki ya nje.

Mheshimiwa Spika, kodi ya matairi ya *tractor* ni kubwa sana pamoja na *spares* zake, hivi kodi hizi zinapotangazwa kuna *interaction* yoyote na Wizara ya Kilimo?

Natoa pongezi kwa *TRA* kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato.

Kwenye mchango wangu wa awali nimeomba mwongozo wa kujua lini Serikali itaanzisha *National Strategic Planning Centre* na kiwe chombo cha pekee kitakachotoa dira, sio kila Wizara iogeele kivyake.

Mheshimiwa spika, naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA: Nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja. Hotuba ya hali ya uchumi ukurasa wa 26 *paragraph* ya 48; ili kuukabili upungufu mkubwa wa waalimu nchini Serikali ifikirie haja ya kufungua angalau chuo kimoja cha ualimu katika Wilaya zenye shule nyingi na idadi kubwa ya wanafunzi kama ilivyo Wilaya ya Lushoto. Ubunifu mwingine ni kuanzisha *satellite TTCS* kutumia mathalan sekondari ya Shambalai ikisimamiwa na Korogwe *TTCS*.

Katika ukurasa wa 44 (iii) Serikali ina mipango gani ya kukopa mikopo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi kuwekeza katika *transit infrastructure*, eneo ambalo lingesaidia uchumi wa nchi upae kwa kasi kubwa? *TPA* wawezeshwe kukopa, wajenge bandari zote za Pwani na maziwa ikiwemo Mwambani Tanga.

Katika ukurasa wa 46 (ix), ni lini Tanzania itakuwa na *National Institute of Strategic studies* kuchabua vipaumbele vya uwekezaji wenye maslahi makubwa kwa uchumi na usalama wa nchi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi, Naibu Mawaziri pamoja na timu nzima ya Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kilimo ndio tegemeo la Wanatanzania walio wengi, nashauri Serikali iondoe kodi katika mazao ya chakula kama wanavyofanya Serikali ya watu wa Swaziland. Kuondoa kodi katika mazao ya chakula, itawanufaisha sana wananchi walio masikini, kujipatia mapato ya kujikimu.

Mheshimiwa Spika, kupitia Serikali za Mitaa/Halmashauri wananchi wakopewashwe matrekta. Matrekta yatakayokopeshwa kwa watu binafsi yatawanufaisha wananchi wasio na kipato. Serikali ikidhamiria kuinua kilimo, ni lazima kuweka mikakati madhubuti ya kuwania wakulima wadogo, wa kati na wakubwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2007/2008 Serikali iliahidi kuajiri walimu 6,000 ili kuondokana au kupunguza upungufu wa waalimu mashuleni, hasa katika shule mpya za Kata. Naomba kujua, ni walimu wangapi walioajiriwa na upungufu wa walimu umepungua kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Dodoma mjini ni Manispaa isiyokuwa na ardhi kwa kuwa mmiliki wa ardhi ya Manispaa ni *CDA*. Manispaa ya Dodoma hukosa mapato makubwa ya kuendeleza Manispaa kwa kutokuwa na ardhi. Je, Serikali haioni umuhimu sasa kuunganisha vyombo hivi viwili, yaani Manispaa na *CDA* ili mapato yanayotokana na ardhi yaweze kuendeleza Manispaa ya Dodoma?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya faida ya kuwa na vyombo hivi viwili katika Manispaa moja au hasara itakayopatikana *CDA* ikiunganishwa na Manispaa ya Dodoma Mjini?

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwa, riba ya mikopo ipinguzwe hadi chini ya asilimia 15 ili wananchi wa kawaida waweze kunufaika na mikopo inayotolewa na mabenki yetu.

Mheshimiwa Spika, sioni mantiki ya Serikali kutoa kodi katika *pampers*, mafuta poa, na kadhalika, bidhaa ambazo watumiaji hawafikii hata asilimia mbili ya Watanzania. Nashauri Serikali itoe kodi kwenye vinywaji kama vile maji ya chupa; soda na *juice*. Hivi Serikali imeshindwa kupata vyanzo vingine vya mapato mpaka inatoza maji kodi?

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke utaratibu wa makampuni binafsi ya mawasiliano kama *Vodacom*, *Celtel*, na *TIGO* kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili makandarasi wetu wapate ujuzi, uwezo na uzoefu iwe ni sera ya Serikali kwamba mkandarasi kutoka nje lazima aingie ubia na mkandarasi mzalendo katika kutekeleza mradi wowote mkubwa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. OMARI ALI MZEE: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia uhai na afya njema.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mkakati wa kuhifadhi mazingira ya Ardhi na vyanzo vya maji, tatizo la maji bado ni kitendawili ambacho kinawakabili watanzania wengi wengi wao bado wanatumia maji yasiyo salama na ambayo hayafai kwa matumizi ya binadamu yanayotuletea matatizo ya magonjwa ya kuharisha kama vile *cholera* na mengi mengineyo ambayo humharibu mwananchi maskini na wengi wao kupoteza maisha, kwa vile hawamudu gharama za maisha hasa kwenye matibabu.

Mheshimiwa Spika, watanzania wengi bado hawatumii choo. Milioni tano hawana vyoo vya aina yoyote, milioni 20 hawana vyoo vya kutambulika ambavyo ni safi na salama. Kutokana na kutotumia vyoo, bado Serikali haijalichukulia jambo hili kuwa linaweza kuongeza kipato cha Serikali, kwani Taifa ambalo halisumbuliwi na magonjwa yanayotokana na kutotumia vyoo, linakuwa imara na watu wake wanaweza kufanya kazi vizuri, kwa ukuwaji wa watu wake, afya nzuri, elimu nzuri na utu wa kujitambua.

Mheshimiwa Spika, mgao wa asilimia 4.5 bado ni tatizo, kwani tume ya pamoja ya fedha ina nia thabiti, hivyo ni kupiga danadana jambo hilo, ni bajeti ya tatu lakini hakuna chochote kinachoendelea na hii inaonekana itamaliza uhai wa Bunge hili bila ya tatizo hilo kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, hakuna ongezeko la bidhaa za mafuta ya petroli, lakini bado tatizo lipo na litaendelea kuwepo kwani hata kiwango cha bidhaa hiyo katika bajeti 2006/2007 bado inaendelea mfumko wa bidhaa kwani sisi sio wazalishaji wa bidhaa hiyo, hivyo basi, Serikali ina wajibu wa kudhibiti mwenendo mzima wa mafuta ingawa kuna ongezeko la mara kwa mara kwa bidhaa hiyo katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru mara kwa mara katika vinywaji si haki na wala hatuwatendei haki watumiaji wa bidaa hizo, wao hunywa kwa starehe, kimila au hata njia nyingine wote hao ni binadamu hivyo kama kambi ya upinzani iliyopendekeza kuviangalia baadhi ya vyanzo vya mapato ili kutoa unafuu kwa wanywaji.

Mheshimiwa Spika, anayekukumbusha na akakuelekeza, huyo anakuonyesha njia. Hivyo basi, vile vyanzo ambayo vimeonyeshwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani unaweza ukachagua kipi kizuri na ukakifanyia kazi. Lengo ni kumsaidia mtanzania ili na yeye aweze kujikomboa na aishi kwa matumaini na mwenye furaha katika nchi yake.

MHE. MOHAMED ALI SAID: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchangia kwenye kilimo. Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu, ingefaa kupewa kipaumbele sana baada ya elimu. Kwa kuwa elimu ilipangiwa asilimia 19.8 ya mgao kwenye

bajeti, basi kilimo kingepewa angalau asilimia 18 ya mgao kwenye bajeti, lakini imetengewa asilimia 6.4 ya mgao kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kiwango kidogo sana ukilinganisha na umuhimu wa kilimo nchini.

Ili kuendeleza kilimo na watu wetu waondokane na njaa na umaskini, basi tunahitaji pesa nyingi kutoka kwenye Bajeti ya 2008/2009 na hapo ndipo tutakapoweza kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ambacho ni mkombozi wa Taifa letu. Pia tungeweza kununua mbolea kwa wingi na kuwapa wakulima ama bure au kwa bei nafuu sana. Vile vile tungeweza kuwafanya wakulima wetu waondokane na vijembe vya mkono.

Tungeweza kufanya hivyo, basi wananchi wetu wengi wangevutika na kilimo na wangeweza kwenda vijijini kutoka mjini. Kwa sababu hiyo, ajira zingengezekana na umasikini ungeondoka.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia kuhusu muafaka wa kisiasa kati ya CCM na CUF

Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri sana kama mpasukuo huu wa kisiasa uliopo kati ya Wazanzibar utaondolewa kwa kutumia hekima na utaalam walionao viongozi wetu kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010, kwani viongozi wetu uwezo wa kutatua migogoro wanao na hii imeonekana Kenya, Mziwani na kadhalika.

Kwa hiyo, sioni kwa nini viongozi wetu wasiutatuwe mgogoro wa Zanzibar ambao umeshachukua muda mrefu sasa. Ikiwa mpasuko huu wa kisiasa Zanzibar hautaondolewa kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010, basi ni aibu kubwa kwa Taifa letu ambalo ni Taifa la amani na linajitapa katika kuendeleza demokrasia.

Mheshimiwa Spika, nitafurahi sana ikiwa mgogoro huu utaondolewa kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia pia kwenye miundombinu. Miundombinu ni muhimu sana katika Taifa letu, lakini mbali na umuhimu wake huo, bado imepewa mgao mdogo. Kwani imepewa asilimia 13.5 tu kutoka kwenye mgao wa bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, ikiwa kweli tunataka kuondoa umasikini na kukuza uchumi wa nchi hii, basi tungeongeza bajeti hii ingalau ifikie asilimia 17.5 kwani barabara zote zingeweza kutengenezwa mpaka vijijini ili wakulima na wananchi waweze kusafirisha mazao yao hadi kwenye masoko na wananchi wangeweza kufanya biashara mbalimbali na kuweza kukuza uchumi na kuondoa umasikini kwa kazi, ari na nguvu mpya.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana ninakushukuru.

MHE. ESTERINA J. KILASI: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na timu yake kwa kazi nzuri wanaliyoifanya katika kuandaa bajeti hii na kuandaa hotuba nzuri ya bajeti. Bajeti hii ni nzuri sana na inaonyesha kuwa iwapo utekelezaji wake utakwenda kama ulivyopangwa, ni imani yangu kuwa uchumi wetu utaweza

kukua kwa kazi inayoridhisha na kupelekea kuondokana au kupunguza umaskini. Kwenye bajeti hii nina mambo ya kupongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele muhimu hasa Elimu na Kilimo, kimsingi, kwenye kilimo ni kuhakikisha kuwa sekta binafsi zitakazosaidia katika upatikanaji wa zana za kilimo kama matrekta makubwa na madogo na mbolea zifuatiliwe kwa karibu, ni ahadi ya Serikali iweze kutekelezwa kama Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2005.

Mikakati iliyowekwa katika kuongeza mapato ya ndani ni kupunguza utegemezi wa bajeti yetu kwa wafadhili kutoka asilimia 24 hadi 34 na mchango mkubwa unaotolewa na *TRA* unapaswa kupongezwa sana. Serikali kwa muda mrefu imekuwa haitilii mkazo mapato ya ndani yasiyotokana na kodi. Kuna Taasisi, Mashirika ya umma, wakala ambazo zingeweza kuchangia kwa asilimia kubwa sana, lakini sera zao na sheria zinazohusu matumizi ya mapato yao na uwasilishaji wake zinapitwa na muda. Wizara ya Fedha kupitia Msajili wa Hazina wazipitie upya.

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa vile Mheshimiwa Waziri Fedha na Uchumi ameliona hilo nashauri utekelezaji wake uende kwa kasi kabla hatujapoteza mapato mengi kwenye matumizi yasio muhimu.

Nampongeza na vile vile naunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na *TRA* katika kuongeza wigo wa walipa kodi ili kuongeza mapato. Ushauri ni kuweka mkazo mkubwa katika kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari ili kupunguza gharama za kukusanya kodi (*tax compliance*) ipande angalau tufike zaidi ya asilimia 50.

Kitengo cha ushuru wa fedha kiimarishwe kwa kuwekwa watu wenye uaminifu, kwani mapato mengi yanapotea eneo hili kwa kushirikiana kati ya walipa kodi na wafanyakazi.

Mapendekezo na ushauri kwa Serikali ni kama ifutavyo:-

- Kwa kuwa kiwango kikubwa cha fedha za maendeleo kinatokana na fedha za wafadhili na fedha hizi zinahitaji masharti ya kutimizwa na Serikali, ni vizuri sasa Serikali ikajipanga mapema ili kuhakikisha kuwa inatimiza wajibu wake mapema ili pesa ziwasilishwe mapema kwenye miradi iliyopangwa kufanyika katika mwaka huo wa fedha.
- Usimamizi wa matumizi uimarishwe hasa upande wa manunuzi kwa kuimarisha kitengo cha Maafisa Ugavi na kuhakikisha sheria za manunuzi ya mali na vifaa vya umma zinafuatwa. Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kiimarishwe, Wahasibu wapangiwe kazi kwa kuzingatia kiwango cha ukubwa wa mafungu wanayosimamia (*Level* ya taaluma iendane na mahali anapopelekwa kwa kuzingaria ukubwa au udogo wa fungu (*vote*)).
- Ushuru ulioondolewa wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi urudishwe ili kulinda soko la mafuta yanayotokana na mazao ya ndani.
- Misamaha ya kodi imekuwa ni kikwazo kikubwa katika kuongeza mapato yanayotokana na kodi. Ni vizuri utaratibu mpya ukaangaliwa ili kodi isipotee kupitia misamaha inayotolewa. Utaratibu wa *voucher system* bado ni mzuri.

Mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Pongezi kwa Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo (Mb) – Waziri na Mheshimiwa Omary Y. Mzee, Makatibu Wakuu na Manaibu wake na Wataalam wote wa Wizara. Pongezi Mwenyekiti wa *TRA*, Kamisha Mkuu na timu yake yote ya *TRA*.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuipongeza Serikali kwa kuongeza mapato ya ndani na hatimaye kuweza kugharimia matumizi yote ya kawaida kwa fedha za ndani.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa *TRA* kwa kuweka marekebisho katika mfumo wa kodi kwa kupunguza kodi kwenye bidhaa muhimu za nishati na Kilimo. Huu ni mkakati mzuri, kwani unajibu kilio cha wananchi kuhusu gharama za maisha na pia uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha bajeti hii na mkakati mzima wa kujiongezea mapato ya ndani, naomba kutoa mchango ufutao:-

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuongeza mapato yetu bila kupanua wigo wa kodi. Ili kuongeza wigo huu, nashauri yafuatayo:-

- (a) *Middle Class - income earners* wasaidiwe. Wafanyabiashara wa kati ni wachache sana. Biashara chache zinakua kutokana na urasimu, rushwa na kutofanya kazi kwa kutathmini wataalam.

Wataalam wetu wa fani za uhasibu, biashara na uchumi hawatumiki. Ni vizuri kuhimiza mabenki yanayotoa mikopo, kwa mfano yatambue kazi za *consultants* hawa. Kwa sasa, *business plans*, *audited financial statements* na kadhalika zinaandaliwa na benki zenyewe (*credit section*) kwa kupokea rushwa toka kwa waomba mikopo. Hivyo *auditors* na *registered Accountants in Public practice*, hawapati kazi. Jiulize ni *firms* ngapi za Wahasibu na *Auditors* zimeanza na kushamiri? Kama zipo ni chache sana!

Aidha, katika kuboresha mazingira ya biashara, lazima tuache urasimu unaopelekea rushwa uondolewe. Hivi sasa, hata *TIN* au *VAT Registration Certificate* lazima ziweke “*consultant*” anayejuana na Maofisa wa *TRA*! Hatuwezi kuendelea hivi!

- (b) Mfumo wa kodi uboreshwe ili usiwabane sana wafanyakazi (*PAYE*) pekee. Hivi sasa mfanyakazi analipa kodi zaidi kuliko mfanyabiashara hata pale mapato yao yanapolingana. *We need a friendly tax regime for all.*
- (c) Viwango vya kodi, hasa *VAT (20%)* vipunguzwe. Kwa sasa watu wengi wanakwepa, anaobaki kulipa ni walaji/watumiaji wa mwisho. This VAT rate, hasa kwenye *raw materials*, maji, umeme na mafuta ya mitambo viwandani inafanya bidhaa zinazozalishwa nchini ziuzwe bei ghali, hivyo kutoweza kuhimili ushindani toka bidhaa za Afrika Mashariki na nje ya hapo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo iachiwe soko huria

zaidi. Hivi sasa kuna malalamiko kuhusu Serikali kuzuia wakulima wenye ziada ya chakula kuuza nje. Kitendo hiki cha Wizara ya Kilimo, ku-*regulate* bei na ugavi wa chakula bila ku-*regulate* bei ya pembejeo hakitendi haki kwa wakulima. Hivi sasa, wakulima wanapata hasara, kwani bei ya pembejeo iko juu wakati bei ya kuuzia mazao yao iko chini na Wizara hairuhusu ipande (kudhibiti *inflation*)!

Mheshimiwa Spika, mfumo huu ni kuwalazimisha wakulima ku-*subsidize* wafanyakazi na wafanyabiashara (wa mjini). Ndio maana kilimo hakina faida na kila mtu anakimbilia kwenda mjini kutaka kuwa mfanyabiashara na hivyo kuishia kuwa Machinga.

Ninashauri, turuhusu wakulima wetu wauze *at whatever best price possible, to whichever market which will be able to give the best price*. Kama hili sio zuri, basi tuwasaidie kuwa ruzuku ili gharama za pembejeo ziwe ndogo na hili liwe kwa wakulima wote, sio baadhi yao tu.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi kwa lengo la kuvutia wawekezaji ipunguzwe. Mazingira ya uchumi wa dunia ya kibebari ni unyonyaji. Hakuna mwekezaji atakayewekeza bila kuangalia faida yake kwanza. Jinsi faida ya mwekezaji inavyokuwa kubwa, ndivyo mapunjo kwetu (*FDI recipient country*) yanavyokuwa makubwa pia.

Mheshimiwa Spika, hakuna *shortcut*, njia pekee muafaka ya kukuza uwekezaji ni kuboresha mazingira kwa wafanyabiashara wetu wa ndani ili wakue, wapate faida ndipo watakapokuwa wawekezaji wa uhakika. Uchumi wa Thailand unakua na unahodhiwa na Wathailand wenyewe.

Uwekezaji mkubwa katika miundombinu kama reli, bandari, viwanja vya ndege, ndege za abiria na hata barabara, lazima upewe kipaumbele na Serikali. Dhana ya ushiriki wa sekta binafsi katika maeneo haya sio sahihi kutegemewa sana. Tukope kwenye masoko ya fedha ili tuwekeze kwenye miundombinu hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele viwe vya kijiografia. kwa mfano, sio sahihi kutoa ruzuku ya mbolea pekee wakati kuna wananchi wengine wako kwenye maeneo ya madini, uvuvi na kadhalika. Ni vizuri kuyaangalia makundi haya, wafugaji, wavuvi, wachimbaji wa madini na kadhalika. Taratibu za kuyafanya makundi haya yashamiri – *licencing, taxation, coordination, technical support etc.*, lazima hizi huduma ziangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kutatua kero za wananchi kwa wakati, mfano, katika Wilaya ya Kahama wananchi wamekuwa wakilalamikia vumbi kutokana na barabara ya Kahama – Bulyankulu.

Naomba Wizara ya Miundombinu ilifanyie kazi jambo hili hasa kwa kuwa wawekezaji wa *Barrick* wameonyesha nia ya kushirikiana na Serikali kuweka lami barabara hiyo.

Aidha, barabara ya Nzega – Kahama kupitia Itobo – Kagongwa, nayo iliahidiwa kutiwa lami (wakati wa Kampeni za Mheshimiwa, Rais 2000). Naomba ahadi hii nayo ikumbukwe na itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, sasa naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE: Kwanza, napenda kukupongeza kwa hotuba yako ya Bajeti.

Pili, naipongeza *TRA* kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato; tatu, pamoja na pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Kamishna wa *TRA* na Wataalam wote wa Wizara yako naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa Bunge limepitisha Sheria ya Kodi ya Majengo ya Halmashauri za Wilaya, Miji na Majini kukusanywa na *TRA* na kuzipeleka fedha hizo kwenye Halmashauri husika, *TRA* wana uzoefu, uwezo na ujuzi wa kukusanya mapato na pia wana wataalam wa kutosha kufanya kazi hiyo. Hata hivyo, naomba maelezo:

Je, fedha hizo baada ya kukusanywa na *TRA* zitapelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri husika au zitapitia Hazina? Ushauri wangu ni kwamba, fedha hizo zipelekwe moja kwa moja kwenye Halmashauri husika.

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga Ofisi ya *TRA* Wilaya ya Mpwapwa na tayari kiwanja kilikwishapatikana/tengwa kwa ujenzi wa ofisi hiyo: Je, Serikali ina maelezo gani kwa wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa? Kwa nini ofisi hiyo haijajengwa hadi sasa? Pia napenda kuwapongeza watumishi wa *TRA* Wilaya ya Mpwapwa kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mpwapwa kuna madini ya aina ya *Sofaya/Ruby* na *Blue copper* na wapo wachimbaji wadogo wadogo wengi: Je, Serikali inanufaika vipi na madini hayo (pato la taifa)?

MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN: Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja hii, ningependa kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza kabisa ni eneo la mafuta. Katika bajeti hii ya Serikali, tofauti na bajeti ya mwaka 2007/2008, Serikali imelinyamazia kimya. Ukimya huu wa Serikali haumaanishi unafuu utakaopatikana kwa wananchi. Bajeti ya mwaka 2007/2008 bei ya mafuta ilitamkwa wazi, lakini lipo ongezeko kubwa toka bei halisi iliyotangazwa. Hii imeongezea ukali wa maisha kwa wananchi kwa kiwango kikubwa. Kutokutamkwa na kudhibitiwa kwa bei ya mafuta katika bajeti hii kunaweza kupelekea kupanda kwa bei ya mafuta kiholela na kuongeza ukali wa maisha kwa wananchi.

Ninaishauri Serikali, kwa vile mafuta ndio kitu kinachomgusa zaidi mwananchi wa kawaida, Serikali ifikirie kupunguza bei ya mafuta na punguzo hilo lifidiwe kwenye vyanzo vingine vya mapato. Aidha, ni vyema Serikali kutenga fedha za kutosha na kununua mafuta kama akiba kwa siku za baadaye pale yatakapopanda bei katika soko la dunia.

Pili, kuhusu suala la misamaha ya kodi kwa bidhaa ya chakula zinazolingizwa nchini, Serikali imekuwa ikipoteza kiwango kikubwa cha mapato kupitia misamaha ya kodi. Hii inapunguza nguvu ya Serikali kutekeleza majukumu yake kwa upungufu wa fedha inazozisamehe.

Baya zaidi, misamaha hii haiwasaidii wananchi wa kipato cha chini, bali ni njia ya kuwaongezea utajiri wafanyabiashara wachache wakubwa. Kumbuka zinaonyesha bidhaa za

chakula zilizopata misamaha ya ushuru hazikushuka bei kwa walaji bali ziliendelea kupanda hadi leo.

Eneo la tatu katika mchango wangu ni eneo la kilimo. Kama inavyoimbwa kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu na hili ni kweli na kwamba zaidi ya asilimia 80 ya wataanzania wanaishi kwa kutegemea kilimo. Kilimo kinacholimwa na wataanzania walio wengi ni kile cha kutumia jembe la mkono.

Ili kukifanya Kilimo kiweze kuzalisha na kusaidia kukuza pato la Taifa na kuwatosheleza wananchi kwa chakula na mauzo, Serikali itenge fedha za kununulia matrekta ya kutosha, isimamie upatikanaji wa mbolea ya ruzuku kwa wakulima, mbegu bora na wataalam wa kutosha wa kuelekeza wakulima. Katika shughuli hii ya kilimo, kilimo cha umwangiliaji kipewe umuhimu na usimamizi mkubwa.

Mifugo na uvuvi ni maeneo ambayo yakisimamiwa vizuri yatazalisha na kuongeza pato la Taifa. Yaandaliwe mazuri kwa wawekezaji kwenye maeneo hayo na uwepo usimamizi mzuri wa mapato, hasa kwa wavuvi wa kigeni ambao imebainika wanavua kwa kiwango kikubwa katika bahari zetu, lakini kodi wanazolipa ni ndogo sana.

MHE. JAMES DAUDI LEMBELI: Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kuchangia hoja hii, ninapenda kwa dhati kusema kwamba ninaunga mkono hoja. Hata hivyo sina budi kumpongeza Waziri wa Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu na Watumishi wote wa Wizara na taasisi husika kwa kazi nzuri waliyofanya hadi kuleta hapa Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unajikita katika eneo moja tu ambalo ni mapato. Kwa mwaka 2008/2009 mapato ya ndani yanakadiriwa kufikia trilion 4.728 ambazo ni sawa na asilimia 18.5 ya pato la Taifa. Hili ni ongezeko kubwa kama ambavyo hotuba ya Waziri inavyojieleza katika Ukurasa wa 25, 26 na 27.

Hata hivyo, pamoja na nia njema ya Serikali ya kutaka kuona taasisi na Mashirika ya umma yanayotengeneza faida, lakini hazichangii katika mfuko wa Serikali. Hili ni wazo zuri, lakini nina wasiwasi mabadiliko ya sheria ya fedha za umma, sura 348 yakifanywa bila kuzingatia umuhimu na wajibu wa taasisi hizo unaweza kusababisha madhara makubwa kwa uhai wa baadhi ya taasisi.

Mfano mkubwa, sheria hii ikibadilishwa kijumla jumla itaathiri mustakabali wa baadhi ya taasisi hususan za *TANAPA* na Ngorongoro.

Hifadhi za Taifa ni taasisi ya Serikali kwa asilimia 100, kwa maana nyingine faida inayopatikana ni ya Serikali, tofauti tu ni kwamba badala ya fedha hiyo kwenda Hazina wenyewe wanaiweka kwa ajili ya maendeleo ya uhifadhi nchini.

Ni muhimu na ni lazima ieleweke kwamba faida ya *TANAPA* ikipelekwa Hazina na dharura ikitokea urasimu wa mlolongo wa taratibu zilizopo Hazina utasababisha mapungufu makubwa, hivyo taasisi kushindwa ku-respond kwa dharura zinazohitaji fedha mara moja.

Uzoefu wa hapo nyuma wakati *TANAPA* na Ngorongoro walipokuwa hawazalishi na hivyo kutegemea Hazina kwa mahitaji yao ya pesa, hali ilikuwa ni mbaya sana kwa vile walipohitaji fedha toka Hazina, hazikuwepo na matokeo yake, nyingi zilikuwa taabani.

Nina wasiwasi mkubwa, sheria hii ikirekebishwa, basi hifadhi zetu za Taifa zitakufa. Mfano halisi ni *Selous Game Reserve*. Hifadhi hii ni mali ya Serikali, mapato yake huenda Hazina, lakini angalia hali ya *Selous* ni mbaya. Je, ingeruhusiwa kujiendesha kama *TANAPA* isingekuwa katika hali iliyonayo leo. Ninachelea kusema kwamba mabadiliko haya ya sheria yataua Uhifadhi na Serengeti itatokomea jambo ambalo litakuwa ni pigo kwa nchi yetu na dunia. Ahsante.

MHE. MARGARET AGNES MKANGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha kwa kuandaa bajeti ambayo imeonyesha mwelekeo na dhamira ya kujitegemea kwa kiasi kikubwa kwa kutumia fedha zetu wenyewe.

Pamoja na uzuri wa bajeti kwa ujumla wake kwamba katika maeneo kadhaa Serikali imetoa unafuu wa maisha kwa wananchi wake, lakini kwa upande wangu naona kuna mapungufu kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nashauri kodi iliyofutwa ya mafuta yasiyosafishwa ya kula irudishwe kwa vile kuna uwezekano wa kutendwa udanganyifu mkubwa ambao utaweza kudhoofisha jitihada za wakulima wa mbegu za mafuta, mfano alizeti, ufuta, na kadhalika ambao wanahitaji alizeti na ufuta huo usindikwe mafuta.

Kwa vile masuala ya watu wenye ulemavu ni mtambuka kwa maana ya kwamba wana mahitaji na haki mbalimbali kama wanajamii wengine, nashauri kila Wizara itenge fedha za kushughulikia walemavu katika sehemu za Wizara mbalimbali mfano elimu, afya, Kilimo, viwanda, biashara na kadhalika kuliko ambavyo masuala yote ya walemavu yanaachwa chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tu.

Pamoja na kwamba Sekta ya Elimu imepata mgao mkubwa wa Bajeti, lakini mahitaji ya watoto/wanafunzi wenye ulemavu katika ngazi zote za elimu bado watoto hawa wanahitaji vifaa vya kutosha vya kujifunzia na kufundishia kwa vile zile *USD 10* zinazotolewa kama *capitation* kwa kila mwanafunzi na kwa walemavu. Fedha hizi hazitoshi kwa vile sio vitabu pekee wanavyohitaji, bali vifaa vya usikivu kwa viziwi, *braille machine*, *tapes*, *tape recorders* kwa wasioona na kadhalika ambayo vinapatikana toka nchi za nje tena ni ghali kwa bei.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache, naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA MOSSES MLATA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hotuba ya Wizara ya Fedha kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mara nyingi bajeti imekuwa ikipangwa, lakini inakuwa haitumiki kwa wakati uliopangwa na huenda kwa sababu ya kutoendana na hali ya hewa au kwa wakati na kusababisha kuwa na muda mfupi wa kutumia fedha za bajeti na kujikuta fedha nyingi zinarudishwa Hazina, sasa swali ni kwamba, Wizara inasema nini au ina mkakati gani kwa kuhakikisha fedha zote zinazopangwa kwenye bajeti zinatumika zote bila kurudishwa Hazina?

Kwani kurudisha pesa Hazina na hali zinahitajika kunadumaza maendeleo ya nchi na kuacha watanzania wengi kuumia na kubaki katika hali ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la miradi ya maji yanayopangwa na Serikali kuchukua muda mrefu na hatimaye kusababisha gharama kubwa kutumika tofauti na Kiwango kilichopangwa. Je, Serikali au Wizara inasema nini juu ya jambo hili? Haioni kuwa huu ni ubadhirifu wa fedha za umma kwa kutekeleza miradi hii? Mfano bwawa la Mugumu – Serengeti. Mradi huu ulianza miaka ya 1970 una umri wa miaka 31. Hadi sasa bado unasuasua na umegharimu fedha nyingi sana. Je, Wizara inatoa maelezo gani juu ya hilo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikataba mbalimbali, kuna makampuni ambayo yanashindwa kutekeleza kwa muda uliopangwa. Maoni yangu ni kwamba, makandarasi wanaoshindwa kutekeleza mradi kwa wakati au kwa mujibu wa mkataba husika, washitakiwe na wasipewe kazi nyingine tena kwani kutokumaliza kazi kwa mujibu wa mkataba, huo ni ubadhirifu mkubwa na kuliibia Taifa.

Mheshimiwa Spika, fedha za Wizara ya Afya zilizotengwa kwa ajili ya kupunguza vifo vya mama na mtoto mwaka uliopita, zilitumika sio zaidi ya asilimia 38 kwa kisingizio cha kukosa wahudumu kwenye sehemu husika na hatimaye 6% zilirudi Hazina. Je, ni kwa nini fedha hizo zisitumike kutengeneza miundombinu katika maeneo hayo ambayo yamepelekea kutokubalika kwa wahudumu kwenda? Je, kwa nini fedha hizo zisinunuliwe hata *pick-up* ili kusaidia akina mama wanaohitaji usafiri wakati wa kujifungua? *Pick-up* hizo zingetumika kama *ambulance* ili kunusuru uhai wao! Naomba nipate majibu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nijue hezo pesa zikirudi Hazina zinakwenda kufanyiwa nini?

Mheshimiwa Spika, naomba kujua, kwa nini kilimo hakina kipaumbele katika bajeti hii? Kwa nini wakulima hawajawekwa kwenye utaratibu nafuu wa kukopeshwa zana za kisasa za Kilimo?

Mheshimiwa Spika, je, bajeti yetu hii ya Wizara ya Elimu, inalinganishwaje na bajeti za Wizara ya Elimu za Nchi kama Uganda, Kenya (*EAC*)? Na kwanini ni tofauti? Au ni sawa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nyingi ninazozitoa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu Waziri na Wasaidizi wao, pongezi nyingi kwa menejimenti nzima na wafanyakazi wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu wa ziada ufuatao, mbali na mchango niliutoa kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya maendeleo ya muda wa kati (2008-2010/2011) yanahitaji dhama *D by D* isogeze zaidi ushirikishwaji wa wananchi katika ngazi za Kata na Vijiji.

Kwa hiyo, baadhi ya Wilaya na Majimbo ya Uchaguzi yenye maeneo makubwa mno, itabidi yagawanywe ili kusogeza wawakilishi kuwa karibu zaidi na wanaowawakilisha. Kwa maana hii, Serikali ijiandae kutenga fedha zitakazogharamia kuanzishwa Halmashauri mbili katika Wilaya ya Kilosa au kuigawa Wilaya ya Kilosa katika Wilaya mbili kwa sababu Wilaya hii sasa ni kubwa mno, inazidi Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mikumi lenye ukubwa wa *square kilometre* 7,353 za mraba, linapaswa kugawanywa katika Majimbo mawili. Lilivyo sasa, ni kubwa mno likiwa na makadirio ya idadi ya watu 173,000 kwa takwimu za mwaka 2007. Jimbo la Kilosa lina ukubwa wa *square kilometre* 1,851.9. Kwa hiyo, Jimbo la Mikumi linayazidi ukubwa Majimbo ya Kilosa na Gairo, yakijumuishwa pamoja kwa *square kilometre*. 1,101.

Uwakilishi halisi wa Mbunge kwa maana ya kuwafikia wananchi wote katika Jimbo la Mikumi, ni finyu kutokana na ukubwa wa Jimbo na umbali wa jinsi Kata zilivyosambaa katika Wilaya. Kwa hiyo, maombi ya kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa yanaandaliwa ili kuomba idhini ya kuyagawa.

Mheshimiwa Spika, fedha za kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wananchi, hususan vijana wanaoishi vijijini katika Wilaya ya Kilosa haijawafikia, kwa sababu Halmashauri kutokuwa na usafiri wa gari la kudumu kwa kazi. Kutokana na ukubwa wa Wilaya ni budi gari maalum liwepo kwa kazi ya uhamasishaji vijijini. Semina na warsha Mkoani na Wilayani zimetosha. Fedha zitakazookolewa sasa zitumike kupeleka semina katika kata na vijiji, pia ili kuwavuta vijana kwenye semina hizi wapewe posho hata kama ni Sh. 500/= kwa kila mtu, kama inavyofanyika Wilayani na Mikoani. Vijana watafutwa na kuhudhuria kwa njia hii. “*Awareness*” ya elimu ya ujasiriamali itaenea na kuwashawishi kuandaa vikundi vya kuweka na kukopa. Utoaji wa elimu kwa wajasiriamali wadogo ni kazi ya kudumu kutoka eneo moja hadi lingine. Usafiri ni wa lazima.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kifupi kijacho, zitahitajika fedha za kugharamia upimaji upya wa mipaka baina ya *National Park* ya Mikumi na vijiji vinavyopakana katika mji mdogo wa Mikumi na vijiji vya Lumango, Ruhembe, Kihelezo, Kitete Msindazi na Kidogobasi. Hili litalazimika kwa sababu upimaji uliowahi kufanyika awali ulikiuka maelekezo yaliyomo katika *Government Notice (GN) No. 121* ya tarehe 13 Juni, 1975. Ukiukaji huo umeleteleza mpaka uliobainiwa kuingia na kumega maeneo makubwa ya mji mdogo wa Mikumi na vijiji vingine vilivyotajwa hapo juu. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi analifahamu suala hili, kwa kuwa nilishamuandikia barua kuhusu tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya ziada, narudia kusesitiza kuwa naiunga mkono hoja kwa asilimia zote.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa M. Mkullo pamoja na timu yake kwa bajeti hii. Nampongeza pia Mwenyekiti wa *TRA* - Dada M. Chijoriga.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibiwe haya pamoja na kwamba sikutoa katika mchango wangu wa kuongea, naomba ufafanuzi. Tumepunguza kodi kwenye ushuru wa matrekta: Je, hiyo ni pamoja na *spare* zake na *tyre* zake? Maana matrekta mengine yapo, lakini *spare* zake zipo juu na kutokupatikana kirahisi.

Mheshimiwa Spika, nilipata malalamiko kutoka kwa baadhi ya wafadhili kuhusu kupeleka umeme hasa miradi ya Makao Makuu ya Mikoa kama Ruvuma, kuhusu kuchaji *VAT* katika miradi ya misaada. Je, Serikali haiwezi kuondoa *VAT* katika hiyo *project cost* ambayo mhisani amekuwa yupo tayari kusaidia?

MHE. DR. GUIDO SIGONDA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha bajeti yenye mwelekeo wa kumkomboa mwananchi wa kawaida.

Pamoja na uzuri wa Bajeti, wasiwasi wangu uko katika utekelezaji wake. Ili kumkomboa mwananchi na kero ya umasikini Serikali ingeshughulikia yafuatayo:-

- (a) Kuwa na kilimo endelevu kwa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji maeneo yenye mabonde kama lile bonde la Ziwa Rukwa;
- (b) Miundombinu ya barabara vijijini iendelezwe kurahisisha usafirishaji wa mazao;
- (c) Kuwaendeleza wajasiriamali walioko vijijini kwa kuwapa mikopo yenye riba nafuu ili wasikimbilie vijijini;
- (d) Wilaya ya Chunya imejenga shule za sekondari na msingi nyingi. Tatizo ni upungufu wa walimu;
- (e) Serikali ifikirie kwa makusudi kuwaongezea pensheni yao wastaafu kulingana na hali ya uchumi inavyokua. Wastaafu wengi maisha yao ni duni sana;
- (f) Serikali iamue kwa makusudi kugawa zile Wilaya kubwa kama vile Wilaya ya Chunya ambayo ukubwa wake ni nusu ya Mkoa wote wa Mbeya;
- (g) Kuna watumishi wengi ambao bima zao zimeiva, lakini kila wanapodai malipo yao wanaambiwa wasubiri. Serikali ingechukua hatua za makusudi kulipa madai yao;
- (h) Wapo vile vile wadai wa mirathi ambao wamekuwa wakiomba wapatiwe malipo ya mirathi bila mafanikio; na
- (i) Zipo ahadi nyingi Serikalini ambazo bado hazijaanza kutelelezwa. Ni vyema Serikali ikaanza kushughulikia ahadi hizo.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kukipitia kitabu cha Bajeti yake, napenda kupata maelezo ya ziada katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika nukta ya 22 ukurasa wa 15/16 Waziri anasema juu ya kutafuta ushuru wa mahindi, ningepeda kujua ni kiasi gani Serikali imepoteza kutokana na hatua hiyo na ilileta unafuu kiasi gani kwa wananchi?

Pia ameendelea kueleza kutopatikana kwa mahindi katika soko la nje: Je, bajeti hii inaelekeza vipi ili kuweza kuzalisha chakula cha kutosha kuliko kutoa misamaha na kutokuwepo mkakati wa kuongeza usalishaji wa chakula?

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 20 nukta ya 30 Waziri anazungumzia kuongeza uwezo wa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala, Wenyeviti na Mameya waweze kusimamia utekelezaji wa Bajeti, nafasi za Madiwani upo wapi? Ni nani yupo karibu na usimamizi wa fedha za Halmashauri kati ya Diwani na Afisa Tawala? Kundi hili la Madiwani lisipuuzwe.

Mheshimiwa Spika, aidha, Waziri amesema katika ukurasa wa 22 nukta ya 33 (v) juu ya bei ya mafuta, vyakula, malighafi na pembejeo zikiendelea kupanda zitaathiri utekelezaji wa bajeti: Je, Serikali imejiandaa vipi katika kukabiliana na hali hii ambayo haiepukiki ili bajeti isiathirike.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo kadhalika, nukta 36(II) namna gani tutadhibiti misamaha wakati baadhi ya misamaha ni kwa mujibu wa sheria hasa wawekezaji ambao hadi sasa wanapata misamaha na tumepoteza kiasi kikubwa cha mapato?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutenga fedha nyingi kutokana na vipaumbele vyetu, vipaumbele hivyo ni vya Serikali au ni vya wananchi?

Mheshimiwa Spika, maji ni kipaumbele cha kwanza kwa wananchi na kwa watawala ni cha tano na hata kupunguziwa fedha za bajeti, eti kwa sababu mradi mkubwa wa Shinyanga/Kahama umekamilika nukta 44 (d). Ni kweli kukamilika mradi huo, ndio tatizo la maji limekwisha nchini?

Mheshimiwa Spika, nitapenda pia kupata maelezo juu ya ongezeko baada ya marekebisho ya ushuru wa bidhaa katika huduma za simu kutoka 7% hadi 10%, hatua hii haitakuwa mzigo kwa mtumiaji wa simu? Kasi ya kupeleka huduma hiyo vijijini wananchi wataweza kumudu gharama kutokana na ongezeko hilo au wananchi kijijini huduma hiyo siyo muhimu kwao?

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, nina hofu kwamba bajeti hii haijakidhi na kutoa mwelekeo mzuri kwa kupunguza ugumu wa maisha kwa wananchi masikini ambao wengi kati yao kipato chao ni chini ya dola moja ya Kimarekani.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkullo kwa hotuba nzuri na kamilifu ambayo ninaunga mkono kwa asilimia 100. Nachukua fursa hii kuwapongeza Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam husika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa fedha zilizotolewa na bajeti hazitoshi na hivyo ndivyo ilivyokuwa katika bajeti zilizopita, lakini pamoja na mapungufu hayo, maendeleo yamefanyika na nina imani kwamba hata katika bajeti ya mwaka 2008/2009 maendeleo yatafanyika katika nyanja mbalimbali. La msingi, kiasi hicho cha fedha zitakazotumika katika bajeti hii zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa na kwa uangalifu mkubwa na kuzuia ubadhirifu. Hivyo ndivyo inavyofanywa na nchi zilizoendelea kama Marekani, nchi za EU na

kadhalika, usimamizi wa matumizi yao ni nzuri sana. Ni wajibu wetu kuiga ili nasi tupate maendeleo ya kuonekana.

Mheshimiwa Spika, siamini kwamba tutaweza kupata bajeti ya kutosheleza mahitaji yetu yote kwa bajeti ya mwaka mmoja. Haiwezekani na haijawahi kutoka hata katika nchi zinazoendelea! Hivyo, tuwe na mipango inayotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ijaribu kuziba mianya ya Ubadhirifu, kwani fedha zinazotolewa kwa maendeleo zinaweza kabisa kuonyesha mwelekeo wa maendeleo kama zikitumika kwa uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka kabla ya bajeti mpya kutolewa, Wizara nyingi zinakuwa na fedha zinazobaki, kinachofanyika ni kuzitumia fedha hizo kwa mipango ya dharura kwenye semina na mikutano ili mradi fedha hizo zitumike tu kabla ya bajeti mpya. Kwa nini fedha hizi zinazobaki zisitumike kwa shughuli za maendeleo? Kama bajeti za kila mwaka hazitoshi, kwa nini kila mwaka Wizara hubakiwa na fedha ambazo zinalazimika kutumika kwa dharura kabla ya Bajeti inayofuata?

Mheshimiwa Spika, Makampuni ya simu sio yote yanalipa kodi husika, kwa mfano *Vodacom*. Hadi leo imesamehewa *cooperation Tax, income tax*, ambapo makampuni mengine yote ya simu za mkononi yanalipa kodi zote, *Voda* ina wateja wengi na kiasi tunachokosa ni kikubwa na kingeweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye bajeti hii. Sababu zipi zinaifanya Kampuni ya *Voda* isilipe kodi hizo?

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa kwa Serikali kutoa mishahara kwa Madiwani na kuwaongezea posho zao. Madiwani wapewe mikopo ya usafiri kwani ndio wanaofanya kazi za kila siku za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hali ya umeme katika Wilaya ya Masasi ni mbaya sana. Wakati tukisubiri umeme wa Zanzibar, tunaomba Serikali ichukue hatua ya dharura ili wananchi wa Masasi wapate umeme.

MHE. ABDULKARIM H. SHAH: Mheshimiwa Spika, naomba nimpungeze Mheshimiwa Waziri wa fedha, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara hiyo. Lakini Mheshimiwa Spika, ni jambo moja tu katika hoja hii ya Bajeti kuu ya Serikali, kwanza kwa niaba ya wananchi wa Mafia, tunashukuru sana kwa kutengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mafia, hakika tunashukuru sana, lakini naomba kufahamu kuwa Je, katika bajeti hii zimetengwa kiasi gani kuhusu ujenzi wa gati Mafia?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, hii ni nyongeza kwenye mchango wangu kwa maandishi niliyokwishawasilisha.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kuhusu hotuba ya Sheria ya *VAT* ukurasa wa 34 Na. 49 (vi).

Mheshimiwa Spika, napendekeza na kushauri na nimeona ni mapendekezo ya Wabunge wengi kwamba kilimo cha katani kipewe msukumo na kwa hiyo, sekta hii ijumuishe magunia yanayotengenezwa kwa katani, hata kama yanahifadhi mazao ya kilimo hata kama siyo nafaka, kwa mfano kahawa, magunia ya katani ndiyo mazuri kwa kahawa, kwa kuwa yanapumua.

Rekebisho jinsi lilivyoandikwa halijumuishi magunia ya katani ya kuhifadhi zao ambalo siyo nafaka kama kahawa. Isiwe nafaka tu, iwe mazao ya Kilimo badala ya neno nafaka.

Mheshimiwa Spika, naomba tusaide kilimo cha katani na wakati huo huo mkulima wa kahawa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo - Mbunge na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba nzuri ya mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2008/2009.

Kwa kuzingatia kuwa mapato yetu kwa ujumla sio makubwa na changamoto za maendeleo zinazotukabili siku hadi siku ni lukuki, kazi ya kupendekeza makadirio ya mapato na matumizi ili kila mtu aridhike kwa kiasi fulani, sio nyepesi, ni ngumu mno.

Hivyo, Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wanastahili pongezi za dhati kwa mapendekezo waliyotuletea ambayo kwa ujumla wake yanaridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika kurasa za 34, 35 na 36 za hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi kuhusu mapendekezo ya Bajeti, zinabeba mapendekezo kadhaa ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Nakubaliana na Serikali kwa kila kipengele cha marekebisho na kuipongeza Serikali kufikiria kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye magunia yanayotengenezwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ni uamuzi utakaokuwa na tija ikiwa utafuatiwa kwa hatua za makusudi za kuongeza uzalishaji wa mali ghafi (kwa sasa katani) na uzalishaji wa magunia ya katani ili kukidhi mahitaji ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naweka msisitizo huo kwa sababu nina uelewa mpana wa eneo hili unaotokana na kujihusisha kwangu na biashara ya magunia nchini muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya magunia ya nchini kwa sasa ni zaidi ya magunia milioni sitini kwa mwaka. Uzalishaji wa magunia ya katani nchini kwa sasa hauzidi magunia milioni tatu kwa mwaka. Hivyo basi, unafuu wa kodi ya ongezeko la thamani unaopendekezwa na Serikali kwa magunia yanayozalishwa nchini hauna budi kuchochea uzalishaji zaidi wa mali ghafi, yaani katani, ili uzalishaji wa magunia uongezeke na bei ya magunia iwe nafuu kwa wakulima au watumiaji.

Mheshimiwa Spika, leo hii zaidi ya asilimia 95 ya mahitaji ya magunia nchini yanakidhiwa na *PP Woven Bags* au viroba ambavyo sio salama kiasia kutunzia chakula kutokana na utengenezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mali ghafi ya viroba ni kemikali mbalimbali. Watanzania wengi wameshuhudia chakula kilichohifadhiwa kwenye viroba kwa muda mrefu kikibadilika rangi. Hii inatokana na *chemical compostion* ya viroba na ukweli kwamba viroba hivyo vikikutana na joto la jua, *chemical reaction* inatokea. Lakini Watanzania wanaendeleo kuvitumia kutokana na bei yake kuwa nafuu (Sh.250/= hadi Sh. 500/= kwa kiroba kimoja) kulinganisha na magunia ya katani (ambayo huuza kati ya wa Shilingi 2,300/= hadi 2,800/=).

Mheshimiwa Spika, dawa ya kuongeza matumizi ya magunia ya katani nchini ni kuongeza uzalishaji wa katani nchini, ubora wa magunia ya katani yenyewe na kupunguza bei yake ili iendane na vipato vya wakulima.

Lakini napenda kutoa tahadhari kuwa matumizi ya magunia ya katani ni kwa aina fulani fulani tu za mazao kama vile kahawa, korosho, mahindi, kokoa, maharage, njegere na mazao mengine yenye punje kubwa kubwa. Mazao yenye punje ndogo ndogo kama vile mchele, ulezi, uwele, ngano, mtama na kadhalika yanaweza kuhifadhiwa kwenye magunia ya katani, lakini kwa hasara kubwa ya kuvuja kwa sehemu ya nafaka kutokana na utengenezaji wa gunia lenyewe.

Aidha, baadhi ya mazao tuliyonayo huharibika au hupungua thamani yake yakihifadhiwa kwenye gunia la katani kama viazi mviringo na vitunguu huchubuka; pamba huungua, tumbaku na pareto hupoteza thamani yake kutokana na gunia lenyewe kuwa na nafasi pana za kupitisha hewa na urahisi wa gunia hilo kuhifadhi unyevunyevu.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na umuhimu wa kuwa na aina nyingine ya gunia linaloweza kuhifadhi hata nafaka zenye punje ndogo ndogo na lisilokusanya unyevunyevu kwa urahisi, Serikali ya awamu ya kwanza ilianzisha nchini zao la *kenaf* linaloota vizuri sana Mikoa ya Pwani na kujenga kiwanda Moshi, *East African Kenaf Industries*, kwa kutengeneza mafunia ya *Kenaf*. Gunia la *Kenaf* hufanana kabisa na gunia la *jute* yakapata soko kubwa Tanzania, soko ambalo hatuwezi kulifunga bila kupata gunia mbadala la *jute*.

Kwa sasa tunaingiza kutoka nje magunia ya *jute* kiasi cha milioni tatu kwa mwaka kwa hayo matumizi maalumu. Kumekuwa na rai ya kuongeza *suspended duty* kwa magunia ya *jute*. Rai hiyo haitasaidia kuongeza uzalishaji wa magunia ya katani wala haitaondoa matumizi ya viroba ila itamuumiza tu mkulima anayelazimika kutumia gunia la *jute*.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na hali hiyo ya utata baadhi ya wafanyabiashara nchini wameamua kufufua zao la *kenaf* kwa kutumia njia ya *contract farming* na kuanzisha viwanda vya kutengenezea magunia ya *kenaf*.

Ni vyema Serikali ikawatia moyo wafanyabiashara hao ambao wataleta ushindani bora na wenye tija kwenye soko la magunia nchini.

Aidha, walionunua viwanda vyetu vya katani wafuatiliwe ili viwanda hivyo vizalishe magunia ya katani ya kutosha, badala ya kugeuza baadhi wa viwanda hivyo kuwa bohari za magunia kutoka nchi za nje kwa visingizio vya kuingiza nchini mali ghafi, huo ni uhujumu wa uchumi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Sasa namwita sasa msemaji wa kwanza kutoka Wizarani, Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, kwa dakika kumi na tano. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE): Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nataka nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuchangia hoja iliyowekwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, juu ya bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, pili nataka nimshukuru sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha kwa makini zaidi hoja ya bajeti hii na hatimaye leo hii tunaihitimisha.

Mheshimiwa Spika, tatu, nataka niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali hii ni sikivu na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Waziri Mheshimiwa Sumari na mimi mwenyewe pamoja na watendaji wetu wote wa Wizara ya Fedha, ni wasikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa tulilopewa na Serikali yetu, ni kukusanya mapato ya nchi hii. Ninakushukuru sana wewe mwenyewe kwa kutotuwekea ukomo wa kukusanya mapato.

Nataka niliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutakusanya mapato ili yawawezeshe Watanzania kufanya maendeleo kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda vilevile niseme kwamba Wapinzani hatuwaoni maadui kama ilivyosemwa na Ndugu yangu, mwanafunzi wangu, Mheshimiwa Sanya. Wapinzani ni ndugu zetu na ni Watanzania wenzetu. Tutafanya kazi nao usiku na mchana kwa faida na manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya dibaji hiyo, sasa naomba na mimi nichangie kwa kujibu baadhi ya hoja ambazo Mheshimiwa Wabunge wameiuliza Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ambayo Wabunge wengi wameihoji au wameuliza au wametaka ufafanuzi, ni suala zima la ukuaji wa uchumi kwamba mafanikio yake hayajawafikia wananchi. Nataka niseme hivi, ukuaji wa uchumi unapimwa kwa kuangalia thamani ya bidhaa na huduma zinazozalishwa ndani ya nchi. Ukuaji wa uchumi, unaangaliwa kila baada ya mwaka na mchakato wake huchukua muda mrefu ili uweze kuonekana kwa mwananchi mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nilikumbushe Bunge lako Tukufu kuwa, wastani wa pato la kila Mtanzania mwaka 2002 ilikuwa shilingi 311,776/- lakini mwaka 2007 tunazungumzia wastani wa shilingi 548,388/-. Lakini tuisahau kwamba katika nchi kuna vijana ambao wapo katika *labour force*, asilimia 11 hawana ajira, tuna vijana ambao wako chini ya miaka 15, ni asilimia 44, kuna wazee ambao umri wao ni zaidi ya miaka 65, ni asilimia nne, hawa wote wanawategemea hawa ambao wanafanya kazi. Kwa hiyo, unapochukua hili pato la Taifa, ukaligawa kwa mtu mmoja mmoja, ni dhahiri *effect* yake huwezi ukaiona kwa mtu wa chini, haraka kama tunavyokusudia.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme, ni jukumu letu sisi Waheshimiwa Wabunge, kuhakikisha kwamba tunapunguza vijana wasiokuwa na ajira. Serikali tayari imeshatoa kwa kila Mkoa shilingi bilioni moja, ili kupunguza idadi ya vijana wasiokuwa na ajira.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameizungumzia, ni suala la ukuaji wa uchumi kwamba hauendani na ubora wa huduma tunazozitoa. Nataka nieleze kwamba Waheshimiwa Wabunge lazima tuwe tunatizama na nyuma, tusitizame tulipo tu, tutazame na nyuma. Huko tulikotoka, kwa upande wa elimu, azma yetu ilikuwa kila mtoto aende shule. Leo nataka nikwambie *enrolment rate* ya *Standard I*, ni asilimia 98. Huko tunakotoka tulikuwa tunataka vijana wetu waende sekondari leo vijana hawa wanojiunga *Standard I*, karibu asilimia 90 wanapasi mtihamu wa kuingia *Form One*. Ni dhahiri kwamba baada ya muda mfupi, hizi maabara tunazozingumzia kwamba haziko katika shule, zitakuwepo katika mashule yetu yote. Lazima twende kwa mujibu wa tunavyojipangia wenyewe. Huwezi ukataka kuwa na keki yako wakati huo huo ukataka kuila, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba lazima Wabunge tukumbuke kwamba ongezeko la watu ni asilimia 2.9. Sisi kama ni Wabunge, tumefanya nini katika kuwashajihisha wananchi wetu kuendana na mpango wa kupunguza uzazi?

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe takwimu, mwaka 1978, kwa kila mwanamke mmoja akimaliza umri wake wa kuzaa, kwa Kiingereza wanaita '*menopause*' alikuwa anakuwa na watoto wanane leo Serikali imehamasisha programu za *family planning*, akina mama wakimaliza umri wao wa kuzaa wana watoto watano. Lakini bado tunakubali ni wengi, lazima tuhakikishe kwamba familia zinazaa watoto watakaowaweza na kuwamudu na Serikali itatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vifo vya watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja, kwa mwaka huo 1978 walikuwa watoto 112 wanakufa kati ya watoto 1000, leo *through the Government programme of family planning*, watoto 68 na bado tunafanya juhudi tufikie chini ya watoto 68. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja inasema kwamba uchumi unaotegemea huduma si endelevu. Mimi nataka kukubaliana na hili na nataka niseme kwamba uchumi wowote ambao unategemea sekta moja si endelevu hata ukitegemea kilimo likitokea jua, balaa. Ukitegemea viwanda, kama unategemea umeme wa maji, kama maji hakuna, ni balaa kwenye viwanda. Lakini uchumi mzuri ni ule uchumi ambao unategemea sekta zote na ndiyo uchumi wa Tanzania. Ni kipindi hiki tu kwa sababu madini yamekuwa mengi sana, huduma imejionyesha kwamba imechukua nafasi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie, ni hoja ambayo ilitolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu nafasi ya kilimo katika kupunguza makali ya umaskini. Pamoja na kupunguza makali ya mfumko wa bei lazima tukubali kwamba tatizo kubwa la mfumuko mkubwa wa bei lililolikumba Taifa letu pamoja na dunia kwa ujumla, ni bei za vyakula. Bei za vyakula hazikupanda hapa Tanzania tu, bei za vyakula zimepanda *almost* dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, nataka ninukuu tu mfano, bei ya mahindi Mei mwaka jana, tani moja kutoka nchi ambazo zinazalisha mahindi kwa wingi sana kama vile Marekani ilikuwa inauzwa kwa dola 159 lakini ilipofika Mei mwaka huu, tani moja ilikuwa inauzwa kwa dola 244.

Ndugu zangu wa Zanzibar mnaokula wali, mchele ulikuwa unauzwa dola 325 Mei mwaka jana, lakini ilipofika Mei mwaka huu ilikuwa ni dola 963 kutoka *Thailand* wafanyabiashara wanaelewa tatio hili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ngano, ilikuwa ni dola 203, lakini ilipofika mwaka mwaka 2007 ilikuwa ni dola 349.

Mheshimiwa Spika, suala la bei ya vyakula ndilo lililosababisha mfumuko wa bei Tanzania, kwa sababu takwimu za bei Tanzania, asilimia 80 ni vyakula. Kwa hiyo, la msingi hapa, lazima tujitahidi katika suala zima la kuzalisha mazao ya chakula humu ndani ya nchi yetu. Nataka nitoe takwimu nyingine, mahitaji ya vyakula Tanzania ni tani milioni 10 lakini, mahitaji ya nafaka ni tani milioni 6.25. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba kuna haja kubwa ya kuzalisha chakula humu humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo lilikuwa linazungumziwa, ni suala la vipaumbele. Kupanga ni kuchagua, tumepanga kuwa elimu ndio kipaumbele. Nani ambaye hakubali kwamba msingi wa maendeleo ni elimu? Msingi wa maendeleo ya nchi yoyote, Waheshimiwa Wabunge ni elimu. Elimu ni mtambuka, hakuna sehemu hata moja utakapokwenda bila elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele kingine tumepanga pia miundombinu. Mheshimiwa Zitto alikuwa anasema kwamba mkulima anazalisha chakula chake, lakini bei anayoipata ni ndogo kuliko bei anayonunulia, ni kweli kwa sababu hana *access to the market*, ndiyo maana tukasema kwamba miundombinu ya barabara lazima tuipe kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo lilikuwa linazungumziwa, ni suala la Benki. Nataka niseme kwamba, *TIB* tumeiongezea mtaji na sasa hivi tayari, yuko mtaalamu anaiangalia, tunasubiri atupe ushauri. Kama itawezekana kuwa na *window* tukaitumia *TIB* iwe inatoa mikopo kwa ajili ya kilimo, tutafanya hivyo lakini kama hakuna uwezekano huo, tutaangalia uwezekano mwingine.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa kwamba, tuongeze mtaji wa *Twiga Bank*, sisi tunasema tukimaliza Benki ya *TIB*, tunakwenda *Postal Bank*. Tukimaliza *Postal Bank*, tutakwenda *Twiga Bank* lakini, lazima twende Benki moja moja baada ya nyingine hatuwezi tukazibeba Benki zote.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo lilikuwa linazungumzwa, ni suala zima la Tume ya Fedha ya Pamoja. Nataka niseme kwamba, ndugu zangu, Tume ya Fedha ya Pamoja, siyo suala la kutafuta 4.5%, kuna mambo mengi sana ambayo tumependekeza, mambo mengi, ni lazima yaangaliwe. Kuna vyanzo vya fedha vya Muungano, lazima viangaliwe, tutagawana vipi hayo mapato na kwa utaratibu gani, lazima iangaliwe. Tunasema kwamba lazima utaratibu wa kugawana uwe *sustainable*, isiwe leo mnagawana hivi, kesho hivi, kesho kutwa hivi. Kwa hiyo, tunasema kwamba, tupeni muda. Serikali zote mbili tunasema, mtupe muda. Tutakapokuwa tayari, tutakuja kuwaambieni kwamba sasa tuko tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie, ni suala la wawekezaji wazawa kupewa kipaumbele. Nasema mipango na mikakati ya Serikali inaelekeza huko. Nikitoa mfano, Serikali imeuza hisa za *TBL*, wazawa wamenunua hisa. Kama *TBL* haitoshi, *Twiga*

Cement, wazawa wamenunua hisa. *CRDB*, wazawa wamenunua hisa lakini, vile vile wazawa wanamiliki *hundred percent* viwanda, wazawa wanamiliki hoteli, wazawa wanamiliki Mashirika ya Ndege, wazawa wanamiliki viwanda vya kusindika samaki, wazawa wanamiliki mashamba ya maua. Nasema bado tuna nafasi ya wazawa kushiriki katika suala zima la uwekezaji. Linalogomba hapa ni kwamba wazawa tunaogopa kuingia kwenye *risk*, lazima tubadilike. Hatuwezi tukakaa tu tukasema wazawa hatuwapi nafasi, nafasi ziko, hatuchukui, ni lazima tubadilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka niseme kuhusu vyanzo vya mapato. Kambi ya Upinzani wamependekeza vyanzo vingi sana vya mapato. Mimi nakubaliana nao, wanaweza kupendekeza lakini, sisi kama Wizara ya Fedha, tunasema kwamba tuko tayari kukaa na mtu yeyote, kukiangalia chanzo chochote cha mapato lakini tunachoomba ni kwamba hicho chanzo kiwe *sustainable*.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia hapa kwamba kuuza Ndege ya Rais, ni chanzo, kesho utauza nini? Mimi nina wasi wasi sana, kesho utakuja kuniambia ukauze koti la Rais. Nasema hiki siyo *sustainable* chanzo cha mapato! Tunataka chanzo cha mapato ambacho kiko *sustainable*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tuko tayari, Mheshimiwa Hamad Rashid, kaka yangu, tuko tayari kukaa na wewe, mimi niko tayari kukaa na wewe, tuviangalie yanzo vyote ulivyopendekiza, *are they sustainable?* Kama viko *sustainable*, tuko tayari kuvi-*introduce* katika vyanzo vyetu vya mapato kwa faida ya nchi yetu na wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante sana! (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mambo hayo! Mheshimiwa huyu sijui alikuwa anafanya nini kule Ulinzi! Nadhani hapa alipo sasa ndio penyewe, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Nilifanya utafiti kidogo, kumbe Mheshimiwa Omar Mzee, ni Mchumi ndiyo maana *material* iliyotoka hapa, wengine tulikuwa katika darasa. Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi/Kicheko*)

Namwita sasa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Jerry Solomon.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, kwa kusimamia vizuri sana sera za kodi na matumizi ya Serikali (*Fiscal Policy*) ambalo ni jukumu la msingi la Wizara yetu ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Namshukuru Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, kwa ushirikiano wake, Katibu Mkuu Grey Mgonja na watendaji wengine wote wa Wizara na taasisi zake, ambao wanafanya kazi nzuri sana na ambao nawahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, wengine wengi hawakulala usiku huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napongeza Gavana, Prof. Beno Ndullu, Manaibu Gavana, Dr. Enos Bukuku na Bwana Juma Reli na watendaji wa Benki Kuu, kwa kusimamia kitaalamu Sera zetu za Fedha (*Monetary Policy*) na kuwezesha uchumi wetu kuendelea kutulia na kukua. (*Makofi*)

Ninampongeza Bwana Harry Kitilya na watendaji wote wa *TRA*, kwa kazi nzuri ya kizalendo wanayofanya wakati mwingine kwenye mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Kamati ya Fedha na Uchumi, ikiongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, kwa ushauri, mawazo na msimamo tulioshuhudia wakati wa majadiliano ya bajeti hii na leo mchana, tuliona kwamba walikaa vile vile.

Mheshimiwa Spika, ninatambua mchango na mawazo ya Upinzani kama yalivyowasilishwa na Kiongozi wao Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Tayari tumeshachukua hatua za awali za kuyachambua mawazo yaliyowasilishwa kwa lengo la kuona ikiwa hatukuona kuna lolote wakati wa kuandaa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa mawazo yao na ushauri waliotupa kwenye michango yao ya maandishi na kwa kusema hapa Bungeni ndani na hata nje ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nijibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Kwanza, nianze na vifungu kwenye matumizi ya Serikali vinavyoitwa '*employment allowance* na *Not Clasified Above*'. Tangu mwaka 1999 na 2000, Serikali ilianzisha kuainisha kasma za mapato na matumizi ya Serikali kwa utaratibu wa Kimataifa ambao unaitwa *Government Finance Statistics*. Chini ya utaratibu huu, Serikali nyingi Duniani huainisha kasma zao kwa mfumo mmoja na kuziweka kasma hizo katika mafungu ya kiuchumi (*economic clusters*). Utaratibu huu, unatuwezesha sisi Serikali kujipima ufanisi wa utekelezaji wa bajeti na Mataifa mengine. Chini ya utaratibu huo, kuna vifungu kama *personal emoluments*, *employment allowances*, *educational materials*, *supplies and services* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti yetu, kifungu cha *employment allowances*, ni mkusanyiko wa vijifungu vidogo vifuatavyo:-

Nauli ya wafanyakazi wanapokwenda likizo, posho ya chakula cha Askari wetu wa Jeshi la Ulinzi, Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto, posho ya kujikimu nje ya kituo cha kazi – ndani ya nchi, posho ya kujikimu nje ya kituo cha kazi – nje ya nchi, posho ya Jimbo ya Wabunge, posho ya vikao, posho ya mazingira magumu katika kazi na kadhalika. *Employment allowances*, ni posho ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukitazama katika Kitabu cha Pili cha Matumizi ya Fedha za Serikali, Fungu la 42, Kifungu cha 2001, Bunge, *employment allowances* iliyopo, inajumuisha posho ya Jimbo, posho ya vikao na vikao ya kujikimu ndani ya nchi ambazo hulipwa ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kutekeleza majukumu yao ya uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, kifungu kingine kinachohitaji maelezo, kwa sababu miaka yote hii, hivi vifungu viwili vinazusha maswali ambayo mara nyingine inakuwa vigumu kuyaeleza

yakaeleweka, ni “*Not Classified Above*”. Kifungu hiki siyo kwamba ni sehemu ya kuficha fedha kama inavyofikiriwa mara nyingine au kudaiwa. Kifungu hiki ni mkusanyiko wa vijifungu vidogo vifuatavyo:-

Ni pamoja na mavazi ya kinga, tozo ya sheria, chakula cha wafungwa, mavazi, taalo, mablanketi kwa ajili ya wafungwa, sare maalum kwa Askari, gharama za mazishi, gharama za kusafirisha wafungwa, hati ya malipo ya msamaha wa kodi na tozo ya huduma ya utaalum na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa vifungu hivi viwili, vimepelekea na kutoa nafasi ya tafsiri ambayo siyo sahihi, Serikali tunakusudia kuvitazama upya na kuvivunjavunja, ili kujaribu kuvirahisisha na kuainisha yaliyomo na kama itawezekana tutavionyesha kwa mpangilio wa vifungu vitakavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili inahusu juhudi ambazo zinapaswa ziongezwe ili kuijumuisha sekta isiyo rasmi katika wigo wa kodi na ili kuhakikisha kuwa kila mtu nchini anayestahili kulipa kodi, analipa kodi ikiwa ni pamoja na walipaji wadogo wadogo katika sekta isiyo rasmi. Mamlaka ya Mapato Tanzania inaimarisha usimamizi wa kutoza kodi kwa mfumo wa vitalu (*block management*). Kwa mfumo huu, walipa kodi wote, wanatembelwa ili kusajiliwa na kuainishwa kodi stahili kulingana na hali halisi ya biashara yao. Ili kurahisisha utozaji kodi katika sekta isiyo rasmi, viwango vya kodi kutokana na makadirio ya mauzo ya mwaka, vinatumiwa.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu Serikalini, ni kwamba tufike mahali ambako kila Mtanzania ambaye ana pato, analipa kodi. Hiyo hatuwezi kuepuka kwa sababu misaada yote ambayo kwa kiasi kikubwa inatudhalilisha sisi, ni kodi za wananchi wa nchi nyingine na jambo hili tumeishaliona sasa haliwezekani kuendelea. Wenzetu wameshachoka na ni vizuri Watanzania tukalijua jambo hili. Kwa hiyo, tutakapokuja kuanza kuwa wakali kidogo kwenye kukusanya kodi, ninawaombeni mtuvumilie.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, kuna makampuni yanayofanya biashara kubwa lakini hayalipi kodi. Serikali imetambua tatizo la haya makampuni makubwa ambayo yanapata faida ya kibiashara, lakini hayalipi kodi ya mapato na kwa muda mrefu tu kwa sababu ya vivutio vya uwekezaji ambavyo walipewa kwa mujibu wa sheria zetu. Kama hatua za awali za kurekebisha kasoro hii, Serikali katika Muswada wa Fedha wa Mwaka huu 2008, inapendekeza kutoza kodi mbadala ya mapato kwa makampuni ya aina hii ambayo ni pamoja na makampuni ambayo mwaka hadi mwaka yanatuambia yanatengeneza hasara lakini hayafungwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoza kodi bidhaa na huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na ushuru wa bidhaa zinazozalishwa na makampuni ya aina hii. Kwa hiyo, kwa namna hii, wanalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, lakini, tunachozungumzia hapa ni kodi ya mapato. Kwa hiyo, katika bajeti hii, tutawasilisha mapendekezo ya kulipiza kiasi cha asilimia 0.30 cha kodi mbadala ya makampuni ambacho kimezingatia uwiano kati ya faida halisi na mapato ghafi pamoja na kiwango cha sasa cha kodi ya makampuni ambacho ni asilimia 30 ya mapato halisi. Kiwango hiki kimeangalia pia mlingano wa viwango vinavyotumika na nchi zenye kodi kama hii.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu Hati ya Ulipaji wa Kodi (*Tax Clearance Certificate*), itakayokuwa inatolewa kwa asasi zisizo za Serikali ili kuendelea kupata msamaha wa kodi kwamba itolewe na taasisi nyingine badala ya *TRA*. Matumizi ya *Tax Clearance Certificate* yalipendekezwa kama njia mojawapo ya kudhibiti misamaha ya kodi. Ilionekana kwamba hati hii ikitolewa na *TRA* ambao ndio wasimamizi wa misamaha ya kodi, itarahisisha utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa taasisi za kijamii, misamaha hutolewa ili kuziwezesha kutoa huduma za jamii. Lengo la hatua inayopendekezwa sasa ni kuhakikisha kuwa misamaha inayotolewa, inatumiwa kweli kwa faida ya jamii iliyokusudiwa. Asasi hizi zitatakiwa kuonyesha mipango yao ya mwaka na kuonyesha ina manufaa gani kwa jamii na inatekelezwe. Wale watakaoshindwa kuonyesha faida ya shuguli zao kwa jamii, hawatapata hati hizi.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Ndani kuwa chombo kinachojitegemea, naomba niseme kwamba Serikali tayari imeishaanza mchakato wa kuunda Idara ya Ukaguzi wa Ndani inayojitegemea. Mkakati huo, unalenga kuanzisha Idara hiyo ambayo itachanganya taaluma mbalimbali ili iweze kutoa mchango mzuri zaidi katika juhudi za Serikali za kuimarisha utendaji wa shughuli zake na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, Mamlaka ya Mapato kukamata magari yenye namba za usajili wa Zanzibar yanapokuja Tanzania Bara. Naomba nieleze kuwa, usajili wa magari siyo suala la Muungano kwa kuwa linasimamiwa na Sheria mbili tofauti. Kwa upande wa Tanzania Bara ni Sheria ya Uandikishaji na Uhamishaji wa Magari, Sura Na. 124 na kwa upande wa Tanzania Zanzibar Sheria inayotumika ni Sheria ya Vyombo vya Usafiri Barabarani ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, suala la uandikishaji wa magari, lilishawasilishwa katika Sekretarieti ya Mambo ya Muungano kama moja ya kero za Muungano ambapo ulitolewa mwongozo kuwa sheria za uandikishwaji magari Zanzibar na Bara, zioanishwe.

Mheshimiwa Spika, kabla ya zoezi hili kukamilika, sheria ya uandikishaji wa magari Zanzibar ikabadilishwa, ambapo sasa magari yenye namba za Tanzania Bara yatakayokwenda Zanzibar kuanzia tarehe 1/5/2008, yatawajibika kusajiliwa upya huko Zanzibar na Bodi ya Mapato ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna imani kuwa ikiwa sheria na taratibu zetu za usajili wa magari pande zote mbili za Muungano, zitafanyiwa marekebisho, muafaka wa suala hili utafikiwa na hivyo kufanya kero hii kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine, ni kwa nini gari zinazosajiliwa Tanzania Zanzibar, zinatozwa kodi ya uchakavu zinapoingia Tanzania Bara. Zanzibar ni eneo muhimu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama inavyotambulika kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Inapotokea magari kutoka Zanzibar yakatakiwa kwa mujibu wa sheria kusajiliwa Tanzania Bara, Sheria ya Uandikishaji ya Tanzania Bara, hutumika. Sheria hiyo, inatamka kuwa kabla gari husika halijasajiliwa, sharti kodi zote zilipwe.

Mheshimiwa Spika, magari kutoka Zanzibar yanapohamishiwa Tanzania Bara, hayatakiwi kutozwa upya kodi ya uchakavu pamoja na kodi nyingine kama vile ushuru wa forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani na ushuru wa bidhaa, iwapo kodi hizo zitakuwa zimetoza na kulipwa kikamilifu kule Zanzibar. Kama ilivyo kwa bidhaa nyingine, inapotokea na kudhihirika kuwa kodi iliyotozwa na kukusanywa Zanzibar, siyo kamilifu, tofauti ya kodi hiyo hutozwa na kukusanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie kidogo kuhusu bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani. Sikuwa na nia ya kufanya hivyo mpaka pale nilipomsikia Mheshimiwa Zitto mchana huu kazungumza. Kwanza, nitasema mambo mawili tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapato, Serikali imesema kwenye bajeti yake kwamba itaongeza mapato ya ndani kwa asilimia 31 mwaka huu. Bajeti ya Upinzani kama ilivyoitwa, inasema kwamba itaongeza mapato kwa asilimia 64, jumla ya trilioni 2.234 lakini sisi Serikali kabla hatujafikia lengo hili, tumekaa kwa muda mrefu sana na kukokotoa kwa aina zote tunazofahamu (*simulation*), uwezekano wa kukusanya mapato mwaka huu 2008/2009 na ndipo tukafikia asilimia 31. Sasa sisi tunajiuliza, wenzetu hawa watatoa wapi *TRA* nyingine ili iweze kukusanya mapato mara mbili ya sisi?

Mheshimiwa Spika, lakini pili, ni upande wa matumizi. Sisi tumesema, Serikali tutaongeza matumizi kwa asilimia 15. Wenzetu wanasema wataongeza matumizi kwa asilimia mbili tu, jumla ya shilingi bilioni 74 tu. Malimbikizo ya mishahara ya mwaka huu ya wafanyakazi wa Serikali peke yake ni bilioni 112, mimi nimejiuliza, hawa wenzetu wanataka kufukuza wafanyakazi wa Serikali au watafanya nini?

Mheshimiwa Spika, lakini ikiwa kweli unaniambia utakusanya mapato kwa asilimia 64 kwa mwaka huu, utahitaji gharama za kufanya hayo makusanyo. Ninafikiria basi, kama utakusanya trilioni mbili, unahitaji ongezeko kubwa zaidi kwenye matumizi yako.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika
muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja!

SPIKA: Ni ya kwanza.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Ni ya kwanza?

SPIKA: Ndio endelea!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI): Basi ngoja niongeze kidogo....

SPIKA: Samahani, nilivutiwa sana na mazungumzo yako Mheshimiwa Naibu Waziri, kumbe ni ya pili lakini umeeleweka ... (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):
Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Mimi niseme tu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ana bahati kweli kweli kuwa na wasaidizi wazuri kiasi hiki. Inafurahisha sana watu wa aina hii wako Hazina.

Kwa hiyo, tunaendelea sasa, Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, unazo dakika zisizozidi 60. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti, Mheshimiwa Jenister Mhagama, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa jinsi mliyosimamia na kuongoza Bunge wakati wa majadiliano ya hoja za Serikali nilizozitoa tarehe 12 mwezi huu, kuhusu taarifa ya hali ya uchumi mpango wa maendeleo na maendeleo ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda - Mbunge wa Handeni na Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kuwasilisha kwa umahiri mkubwa maoni ya Kamati yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed -Mbunge wa Wawi kwa maoni na ushauri wa Kambi yake kuhusu bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru wasaidizi wangu na kama ulivyoona Mwenyewe, naanzia na Manaibu Mawaziri - Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu Ndugu – Ndugu Grey Mngoja, Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Ramadhani Kija, Ndugu John Haule na Ndugu Laston Msongole, pamoja na Gavana wa Benki Kuu na wafanyakazi wote wa Benki Kuu, Mwenyekiti na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato na viongozi wote wa Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango na wafanyakazi wote wa Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, wasaidizi wangu wamefanya kazi kubwa sana, wachache wapo hapa Dodoma, lakini wako wengi ambao wapo Dar es Salaam na kila siku wanaleta masahihisho hapa Dodoma na wenyewe nao napenda niwashukuru.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru wote waliochangia kwa njia mbalimbali wakiwemo wale Waheshimiwa Wabunge waliotoa maoni yao kwa kuzungumza hapa Bungeni, waliotoa maoni yao kwa maandishi na wengine ambao walikuwa wakitoa maoni yao kila tulipokutana nje ya ukumbi huu, kwa michango yao mizuri ambayo itasaidia katika kusimamia utekelezaji wa bajeti hii na katika kuandaa bajeti za miaka ijayo. Kama ilivyo kawaida, naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni Mheshimiwa Abdallah Omari Kigoda, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Dr.

Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga na Mheshimiwa John Momose Cheyo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa William Jonathan Kusila, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwando, Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi na Mheshimiwa Yono Stanley Kevela. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mheshimiwa Ritha L. Mlaki, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Castor Raphael Ligalama, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Hamza Abdallah, Mwenegoha, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Ramadhan Athumani Maneno, Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mheshimiwa Maria Ibesh Hewa, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Fatma Abdalla Mikidadi, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Dr. Ferdinand Samson Mpanda, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Magalle John Shibuda, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Ibrahim M. Sanya, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Susan Anselm J. Lyimo, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mheshimiwa Maulida Komu, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Dkt. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Sumari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi wako 109, wengine walichangia kwa kuzungumza na vilevile wakatoa michango mingine kwa maandishi. Nao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi, Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Balozi Seif Iddi, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko,

Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka na Mheshimiwa Nuru A. Bafadhil. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Job Mheshimiwa Y. Ndugai, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana Mjini, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Col. Fete Saad Mgeni, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Mwamtumu B. Mahiza, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Mwajuma Hasan Khamis, Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mheshimiwa Ussi Amme Pandu na Mheshimiwa Eustace Osler Katagira. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Mohamed Habib J. Mnyaa, Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhan, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwando, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma na Mheshimiwa Kumbwa Makame Mbaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Andrew John Cheyo, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Dr. Luka J. B. Siyame, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Cap. John Komba, Mheshimiwa Zuleka Yunus Haji, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Mohamedi Ali Said, Mheshimiwa Kheri K. Ameir na Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Margaret Agnes Mkinga, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Guido Sigonda, Mheshimiwa Said A. Arfi na Mheshimiwa Hassan Claude Kigwalilo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Manju Salum Msambya, Mheshimiwa Mosi S. Mussa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Hubert Mntangi Mheshimiwa Hasnain Gulamabas Dewji, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma na Mheshimiwa Magalle John Shibuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ni 109. Naomba hizo dakika zisihesabiwe sasa hivi kwa ruhusa yako.

SPIKA: Sawa, endelea.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inathamini michango yote ya Waheshimiwa Wabunge na inaichukua kama nyenzo muhimu ya kuboresha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti hii. Maoni na ushauri wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Wabunge unaipa Serikali changamoto na ari ya kufanya vizuri zaidi na zaidi ili kupata matokeo yaliyotarajiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, wakati akiwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo alizungumza kuhusu moja ya changamoto kubwa zilizopo mbele yetu; ile ya kuhakikisha kuwa mafanikio yanayopatikana katika nyanja ya uchumi mpana yanajidhihirisha katika ubora wa maisha ya wananchi wote. Kwa maneno mengine, juhudi za kukuza uchumi zilenge katika kuboresha maisha ya Watanzania – yaani, ‘*broad-based growth*’. Hoja hii ya Kamati inafanana kabisa na malengo ya *MKUKUTA* na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Eneo la kwanza (*Cluster 1*) la malengo ya *MKUKUTA* ni kukuza uchumi ili kupunguza umasikini wa kipato hasa kwa njia ya ajira na uzalishaji. Ili kufikia malengo hayo mawili kwa pamoja, mipango yetu inaweka mkazo katika kuboresha mazingira ya uzalishaji ili tuweze kuzalisha kwa wingi zaidi na kwa ubora wa kuingia sokoni kwa faida ya wazalishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunawekeza katika miundombinu ili kupunguza gharama za usafiri na uchukuzi, kufungua fursa za masoko kwa wakulima, kupunguza gharama za pembejeo, kuongeza upatikanaji wa nishati, maji na kadhalika. Uwezo wetu wa kutoa huduma bora za elimu, afya, maji, usalama na kadhalika, unategemea kwa kiasi kikubwa mafanikio katika kukuza uchumi pamoja na mfumo wa kuhamisha rasilimali kutoka sekta za uzalishaji kwenda kwenye huduma za jamii, kupitia bajeti Serikalini na kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mkakati nilioueleza awali, Serikali itaendelea kuongeza fursa za wananchi wengi zaidi kushiriki katika uzalishaji mali na kuboresha kipato binafsi ili kuongeza hicho cha kugawana ili wananchi wote waweze kuishi maisha bora. Ninaamini kwamba mwelekeo wetu ndio huo na kwamba tutafika ili mradi kila mmoja wetu ataoe mchango wake.

Mheshimiwa Spika, moja ya matokeo ya mapitio ya mfumo wetu wa takwimu za Pato la Taifa ni kubainisha ukweli kwamba sekta za huduma zimekua kwa kasi kubwa ikilinganishwa na sekta za uzalishaji. Aidha, ni kweli kwamba katika historia ya baadhi ya chumi za dunia hatua ya kwanza ilikuwa ya uzalishaji viwandani kabla ya kufikia hatua ya kutegemea huduma. Ni kweli pia kwamba kadri uchumi unavyopanuka na kuwa wa kisasa, mchango wa kilimo katika Pato la Taifa unashuka kwa kuwa sekta nyingine zinakua kwa kasi zaidi ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, marekebisho ya Pato la Taifa kwa Tanzania Bara yalilenga kuimarisha ubora wa takwimu hizo ili ziweze kutoa picha halisi ya shughuli za kiuchumi nchini na ziweze kulinganishwa kimataifa kama ilivyoainishwa katika mfumo wa takwimu za Pato la Taifa wa Umoja wa Mataifa wa mwaka

1993 (*UN System of National Accounts 1993*). Kabla ya hapo, tulikuwa tukitumia mfumo wa takwimu za Pato la Taifa wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1968 ambao umepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, aidha, utayarishaji wa marekebisho hayo haukufanywa na wataalamu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu pekee, bali ni kwa ushirikiano na wataalam wa Wizara, Idara na Asasi mbalimbali za Tanzania Bara. Kazi hii iliongozwa na kusimamiwa na Mtaalam wa Takwimu za Pato la Taifa kutoka Uingereza chini ya Shirika la Maendeleo la Uingereza (*DFID*). Vile vile, ubora wa takwimu hizi ulihakikiwa na wataalamu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*).

Mheshimiwa Spika, aidha, nchi zote ulimwenguni zinatakiwa kutumia mfumo huu wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1993 katika kutayarisha Pato la Taifa. Kwa mantiki hii, Tanzania nayo inapaswa kutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, mtiririko huu wa kihistoria unaendelea kubadilika katika enzi hizi za utandawazi na teknolojia. Dunia imeshuhudia uchumi wa nchi za Mashariki ya Mbali ukikua kwa kasi kubwa, ukiongozwa na huduma za biashara; kwanza, zikafuata huduma za fedha na sasa, uwezo wa kuzalisha bidhaa unapanda kwa kasi. Ushindani katika masoko ya bidhaa ni mkali kiasi kwamba ni vigumu mno kwa wazalishaji wa nchi maskini kupenya katika masoko ya nchi zilizoendelea kwa bidhaa ambazo nchi hizo zinazalisha. Sote tunafahamu mwenendo wa mazungumzo kuhusu suala hili katika Shirika la Biashara Duniani (*WTO*) na hatuwezi kusubiri fursa hizo zifunguliwe kwa ridhaa ya wakubwa. Jambo la msingi ni sisi kuzitumia fursa tulizonazo kuongeza Pato la Taifa. Baadhi ya fursa ambazo wakubwa hawana na hawawezi kuzihamishia kwao ni vivutio vyetu vya utalii na jiografia ya nchi yetu kama lango kuu kwa nchi za eneo la Maziwa Makuu. Utalii ni huduma kama vile mawasiliano, mikopo ya mabengi na kadhalika.

Mikakati yetu ya maendeleo inalenga kutumia fursa hizi kuharakisha maendeleo yetu na ndiyo maana sekta ya utalii, biashara hasa ya Kikanda, pamoja na usafirishaji zinaonekana kukua kwa haraka. Kazi iliyo mbele yetu sasa ni ya kuimarisha sekta hizi ambazo zinaonyesha uwezo wa kujisogeza mbele zaidi ili mapato yanayotokana na maendeleo hayo yatumike kuimarisha uwezo wetu katika maeneo yanayokabiliwa na ushindani mkubwa zaidi. Lakini pamoja na yote haya, hatuwezi kujivunia fursa hizi kama hatuzalishi chakula chetu wenyewe cha kutosha kwanza, kisha kuwauzia majirani zetu.

Mheshimiwa Spika, samahani, nilimsahau Mheshimiwa Lucas Siyame, ambaye alitoa mchango wa Maandishi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge wamesisitiza umuhimu wa tahadhari na kuwa tayari kukabiliana na athari za mtikisiko katika uchumi wa dunia kwa uchumi wa nchi yetu. Katika hotuba yangu ya Bajeti nilielezea changamoto hii kwa kifupi na njia za kujihami na athari zinazoweza kuikumba nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ongezeko la bei ya mafuta duniani ni tishio kubwa sana kwa uchumi wa dunia nzima, hasa kwa sababu hakuna anayejua zitapanda mpaka wapi. Mambo makubwa yanayosukuma bei ya mafuta ya petroli ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Ongezeko kubwa la mahitaji ya mafuta hayo duniani, hasa China, India na Brazil ni nchi ambazo zinakua kwa kasi kubwa. Kuelekea mwisho wa mwaka, mahitaji katika nchi za Amerika ya Kaskazini na Ulaya yanatarajiwa kuongezeka pia kutokana na kuanza kwa majira ya baridi (*winter*);

(b) Kuvurugika mara kwa mara kwa hali ya usalama katika nchi zinazozalisha mafuta, hasa Mashariki ya Kati;

(c) Kupungua kwa akiba ya mafuta katika baadhi ya nchi ambazo ni watumiaji wakubwa wa bidhaa hiyo, hasa Marekani;

(d) Uwezo mdogo wa kuzalisha na kusafisha mafuta katika nchi zenye mafuta. Taarifa zinaonyesha kuwa uwezo wa visima kuzalisha mafuta kwa sasa unatumika karibu wote kutegemea mitambo iliyopo (*full capacity utilization*). Vivyo hivyo, viwanda vya kusafisha mafuta vinatumika kwa uwezo wake karibu wote. Hivyo, masoko hayategemei kuwa kunaweza kuweko ongezeko kubwa la upatikanaji wa mafuta yaliyosafishwa katika siku za karibuni na hiki ni kiashiria cha kutosha cha kwamba bei ya petroli itaendelea kupanda; na

(e) Kinachoweza kupunguza kasi ya ongezeko la bei ya mafuta ni ikiwa nchi zinazozalisha mafuta zitapunguza viwango vya faida zinazopata kutokana na mafuta, au kama China, India na Brazil zitapunguza mahitaji yao ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haina uwezo wa kuondoa yoyote kati ya sababu hizi za kupanda kwa bei ya mafuta na kwa kweli hivyo ndivyo zilivyo nchi nyingi duniani. Matokeo yake, dunia imeshuhudia bei ya pipa moja la mafuta ikipanda kutoka takribani *USD* 50 hadi *USD* 139 katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Mbaya zaidi, ziko taarifa zinazoashiria kuwa bei hiyo itafikia *USD* 200 kabla ya mwisho wa mwaka huu. Kwa hiyo, changamoto hii bado ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kutozigusa kodi zinazotozwa kwa bidhaa za mafuta ni sehemu tu ya mkakati wa kukabiliana na hali hii kwa kuzingatia mipaka ya uwezo wetu. Ni kweli kuwa, kulingana na mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia, bei za mafuta hapa nchini zinaweza zikapanda sambamba na kupanda katika soko la Kimataifa. Serikali, kupitia *EWURA* na *TPDC* imeandaa mikakati ya kupunguza makali ya tishio hili. Baadhi yake ni kama ifuatavyo:-

Kurekebisha utaratibu wa sasa wa kuagiza mafuta na kutumia ule wa ununuzi wa pamoja – (*bulk procurement of petroleum products*). Mfumo huu ambao unatumika pia katika nchi za Kenya, Namibia, Msumbiji na Ghana, unaonyesha kuwa unaweza kupunguza gharama kwa kiasi cha asilimia 20 hadi 30. Utaratibu wa sasa ambao kila kampuni inaagiza mafuta yenyewe, unakosa fursa ya punguzo la bei kwa wale wanaonunua kwa pamoja.

Kwa kushirikiana na wadau, *EWURA* inaandaa taratibu za kuanzisha mfumo shindanishi ili kampuni zote ziagize mafuta kwa pamoja. Inatarajiwa kuwa taratibu hizo zitakamilika ifikapo mwisho wa mwaka huu Desemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kurejea (*review*) gharama mbali mbali zilizomo kwenye bei ya mafuta. Baadhi ya gharama hizo ziko katika dola ya Marekani na zinalipwa kwa

asilimia ya gharama ya kuagiza mafuta kwenye soko la dunia (*percentages of FOB prices*). Mtindo huu wa gharama za huduma unachochea bei kupanda. Ili kuiwezesha *EWURA* kurejea gharama hizi, sheria na kanuni zilizotumiwa huko nyuma kuweka gharama hizi zitarekebishwa.

Njia nyingine ni kupunguza utegemezi kwa mafuta ya petroli kwa kutumia nishati mbadala kama gesi asilia ambayo tunayo nchini. Waziri wa Nishati na Madini atalielezea hili kwa ufasaha zaidi wakati akiwasilisha bajeti ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu pia watumiaji wa mafuta ya petroli tubadilike, tutumie mafuta kwa uangalifu mkubwa kwa kupunguza matumizi ya magari yasiyo ya lazima na hatua nyingine zitakazopunguza matumizi ya mafuta.

Mwisho, tuendeleo kumwomba Mwenyezi Mungu ili utafiti unaoendelea sehemu mbalimbali hapa nchini, ili hatimaye uweze kuleta mafanikio yanayotafutwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ya mwenendo wa uchumi wa dunia na ambayo inatokana na bei ya mafuta ya petroli, ni ongezeko la bei ya chakula.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba ya Bajeti, Serikali inakusudia kuitumia changamoto hii kama fursa ya kuongeza uzalishaji wa chakula wa kutosheleza mahitaji yetu wenyewe na kuuza ziada nje hasa katika nchi jirani. Hivyo, bajeti hii imezingatia azma hiyo na kwa kuanzia, Serikali imeongeza fedha za ruzuku ya mbolea kutoka shilingi bilioni 19.5 mwaka 2007/2008, hadi shilingi bilioni 29 mwaka 2008/2009.

Hata hivyo, Serikali inatambua kwamba bei ya mbolea kutoka nje ya nchi nayo imepanda sana. Kwa kuzingatia hili, Serikali inahimiza uzalishaji wa mbolea hapa nchini, kwa kuwa malighafi tunayo ya kutosha. Kwa kuanzia, Serikali inashirikiana na Kiwanda cha Minjingu ambacho kinazalisha mbolea ya kupandia, ili kizalishe mbolea ya kutosha. Kampuni ya Mbolea ya Tanzania (*TFC*), imekubali kutafuta fedha kutoka mabenki ili iweze kununua mbolea kutoka katika kiwanda hicho na kuisambaza kwa wakulima. Serikali itatoa dhamana ya mikopo hiyo kwa *TFC*.

Aidha, Serikali imetenga shilingi bilioni 3 za Mfuko wa Pembejeo za Kilimo. Serikali pia imeongeza fedha kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*SGR*) kutoka shilingi bilioni 5 mwaka 2007/2008 hadi shilingi bilioni 15.6 mwaka 2008/2009. Kwa sasa, Serikali imesitisha mauzo ya chakula nje ya nchi, kwa kuhofia kwamba nchi inaweza kukosa akiba. Nchi zinazoongoza kuzalisha chakula (hasa mchele) kama Thailand na Vietnam, zimezuia usafirishaji wa mchele nje ya nchi zao.

Mheshimiwa Spika, kasi ndogo ya kukua kwa uchumi wa dunia sambamba na mvurugano wa masoko ya fedha, vinaweza kuathiri chumi za nchi zinazoendelea kutokana na kupungua kwa watalii na wawekezaji kutoka nchi tajiri. Kwetu sisi, athari zinaweza kujitokeza katika mapato ya utalii hasa kwa kuwa soko la Marekani ambalo lilikuwa limeanza kuwa chanzo kikubwa cha watalii wanaokuja nchini liko katika hali ngumu. Katika ugawaji wa rasilimali, umuhimu wa kutekeleza mikakati maalum ya kukabiliana na athari hizi umezingatiwa. Aidha, njia pekee ya kuvutia uwekezaji katika hali hii ni kuendelea kuboresha mazingira ya biashara hapa nchini na kupunguza gharama za uzalishaji. Lengo hilo ni sehemu muhimu ya misingi ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi na Waheshimiwa Wabunge wengi wametoa maoni kuhusu sekta ya kilimo na mchango wake katika Pato la Taifa, ajira ya wananchi wengi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kueleza kuwa nakubaliana kabisa na wale wote waliosisitiza umuhimu wa sekta ya kilimo kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na kuwa Mwajiri Mkuu wa Watanzania, sekta ya kilimo ndiyo tegemeo letu katika jitihada za kujitegemea kwa chakula, aidha, sekta hiyo ni msingi wa mkakati wowote wa maendeleo ya viwanda nchini, kwani ujenzi wa viwanda vinavyotegemea malighafi kutoka nje hauwezi kuwa endelevu. Tatu, uwezo wa kupanua shughuli za kilimo tunao kwa kuwa tunayo ardhi nzuri na ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingi zinazokabili maendeleo ya sekta hii zimeainishwa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii, changamoto hizo kwa uchache ni kama ifuatavyo:-

- (a) Changamoto kubwa kuliko zote ni kuongeza tija katika kilimo kwa kutumia zana za kisasa za kilimo, mbegu bora, masoko yenye uhakika, elimu kwa wakulima nakadhalika. Mwezi Aprili, 2008, Bunge lilipitisha sheria ya “*Finance Leasing*” ambayo itasaidia kupatikana kwa zana za kilimo kwa njia ya ukodishaji. Napenda nitumie fursa hii kuzipongeza asasi za fedha na za kiraia, ikiwemo taasisi ya *SERO LEASE* inayokopesha vifaa mbalimbali kwa akina mama, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuwawezesha wakulima kupata vyanzo vitakavyoongeza uzalishaji na mapato ya wakulima.
- (b) Katika bajeti hii, zimetengwa fedha kwa ajili ya kuongeza kasi ya uzalishaji wa mbegu bora, kama ilivyowahi kuwa miaka ya nyuma.
- (c) Bajeti hii pia inaongeza fedha kwa ajili ya miundombinu ya umwagiliaji mashambani. Hapa napenda nisahihishe takwimu zilizotolewa na Kambi ya Upinzani kwamba nchi hii iliwahi kuwa na hekta 450,000 za kilimo cha umwagiliaji na kwamba sasa zimebakia hekta 298,000 tu. Ukweli ni kwamba nchi hii haijawahi kufikia hekta 450,000 za umwagiliaji tangu Uhuru. Mpango kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji ulioandaliwa mwaka 2003 ndio ulibainisha kuwa zinahitajika kuwekezwa angalau shilingi bilioni 20 kila mwaka ili kufikia hekta 405,000 ambazo zingetuwezesha kujitosheleza kwa uhakika kwa zao la mchele. Safari hiyo inaendelea vizuri na bajeti hii imelenga kuongeza kasi ya utekelezaji wa azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala jingine lililotolewa mapendekezo na Kamati ya Fedha na Uchumi ni umuhimu wa Serikali kuendelea kutafuta vianzo vipya vya mapato. Hapa, pia, napenda kukubaliana mia kwa mia na ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali wa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani umeelezwa katika aya ya 36 ya Hotuba ya Bajeti. Mkakati huo unalenga kupanua wigo kwa kukuza uchumi sambamba na kuimarisha utawala wa kodi.

Mkakati huu umetumika kuanzia miaka ya katikati ya 90 yalipofanyika mageuzi makubwa ya mfumo wetu wa kodi na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato (*TRA*). Mfumo wetu wa kodi umelenga kuwa shindani, kuvutia uwekezaji, kukuza uchumi na kuongeza fursa za

ajira. Kwa hiyo, kodi nyingi zilifutwa kipindi hicho na viwango vikapunguzwa. Matokeo yake ni kuongezeka kwa uwekezaji na kasi ya kukua kwa uchumi. Aidha, uimarishaji wa *TRA* kupitia Mipango Mikakati yake ya miaka mitano mitano umewezeshwa mamlaka hiyo kusimamia ipasavyo ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kukua kwa uchumi yanaibua fursa mpya za mapato kwa Serikali. Kwa mfano, kukua kwa Sekta ya Mawasiliano kumeibua fursa mpya ya mapato ambayo imevunwa ipasavyo.

Aidha, eneo la uvunaji wa rasilimali, hasa madini, uvuvi, mazao ya misitu na nyinginezo ni fursa mpya zinazoibuka hivi sasa kutokana na utekelezaji wa Sera tulizowekwa miaka 10 iliyopita. Serikali inatambua fursa hizi na inachukua hatua za kuzivuna ili kuongeza uwezo wa kutoa huduma muhimu za kiuchumi na kijamii. Uamuzi wa kupitia upya mfumo wa kodi za sekta ya madini na misamaha ya kodi, pamoja na taratibu zote za uvunaji wa maliasili zetu, ni sehemu moja kubwa ya mkakati huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa niko kwenye mapato, napenda nitoe ufafanuzi kuhusu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuhusu Kitabu cha Kwanza cha Bajeti ya 2008/2009 (*Financial Statement and Revenue Estimates for 2008/2009*). Hapa sina haja ya kusema mengi kwa sababu tumekipitia kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa hiyo, nataka niwasifu wale ambao walituoonesha kwamba mahali fulani fulani kulikuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya bajeti ya Serikali yanaainishwa katika Hotuba ya Bajeti na katika Vitabu vya bajeti Kitabu cha Kwanza hadi cha Nne. Aidha, kwa upande wa mapato uko Muswada wa Sheria ya Fedha, ambao ni sehemu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuwasilisha mapendekezo ya bajeti yake ya mwaka, Bunge linajadili na kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali yakiwa ni pamoja na kufanya marekebisho kadhaa katika bajeti iliyowasilishwa na Serikali. Hatimaye Bunge linapitisha bajeti kupitia "*Finance Act*" na "*Appropriations Act*" ambazo zinapitishwa mwisho wa shughuli za Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Bunge zinatamka kwamba Serikali itawasilisha mapendekezo ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo (Kitabu cha II hadi cha IV). Vitabu hivi vinawasilishwa katika Ofisi ya Bunge tayari kwa kutumiwa na Kamati za Bunge wakati wa kujadili bajeti za Wizara na Idara mbalimbali za Serikali. Kuhusu bajeti ya mwaka 2008/2009, vitabu hivyo viliwasilishwa katika Ofisi ya Katibu wa Bunge Dar es Salaam mwezi Mei, 2008.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umekuwa kwamba, Kitabu cha Kwanza cha Mapato kinachelewa kuwasilishwa kutokana hasa na vianzio kadhaa vya mapato vinachelewa kuthibitishwa na hasa vile ambavyo havitokani na kodi pamoja na vile vya misaada ya nje. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009, baada ya Kitabu cha Kwanza kupelekwa kwa Mpiga Chapa, zilipatikana taarifa mpya kuhusu makadirio ya mapato ya mauzo ya hisa za Serikali asilimia 21 katika benki ya *NMB*.

Mheshimiwa Spika, awali tulikuwa na makadirio ya shilingi bilioni 42, kisha yakapanda kuwa shilingi bilioni 58 na yakapanda tena siku za mwisho yakawa Shilingi bilioni 60.0, kutokana na bei ya hisa sasa kukadiriwa kuwa itafika shilingi 600 kwa hisa kulingana na hali ya

soko, nakala za Kitabu cha Kwanza pamoja na marekebisho (*Addendum*) zimeshagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ni vyema ikumbukwe pia kuwa vitabu vyote vya Bajeti vinavyowasilishwa Bungeni, vinafanyiwa marekebisho baada ya Bunge kupitisha Bajeti na kutolewa nakala mpya ambazo zimeingiza marekebisho na masahihisho yote yaliyoainishwa wakati wa mjadala wa bajeti, nataka kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba vitabu vyote vimeandikwa kama vilivyowasilishwa Bungeni, maana yake ni kwamba baada ya kupitiwa na Waheshimiwa Wabunge vyote vile vinarekebishwa na vinakuwa kama vilivyopitishwa na Bunge. Kwa hiyo, nadhani hilo lisiwape shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadiliana kwenye Kamati ya fedha tumefanya marekebisho, kama yalivyozungumzwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi na vile vile kwa namna fulani kama yalivyonukuliwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, nadhani sina haja ya kurudia lakini ujumla tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani walihoji tofauti ya mahesabu ya mapato katika Kitabu cha Kwanza ambacho kinaonyesha mchanganuo wa makadirio ya mapato, tofauti na hotuba ya Bajeti ambayo inaonyesha muhtasari wa makadirio ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza juzi nilipochangia hapa Bungeni, tofauti hizo za takwimu zimetokana na kuchelewa kupata uthibitisho wa baadhi ya taarifa za mapato, ambazo wakati zinathibitishwa, Kitabu cha Kwanza kilishapelekwa kwa Mpiga Chapa kwa ajili ya kuchapishwa.

Mheshimiwa Spika, tarakimu zinazorekebishwa kubwa ni tatu nazo ni kama zifuatavyo:-

- (i) Mapato kutokana na uuzaji wa hisa asilimia 21 za *NMB*, yanatakiwa yawe shilingi bilioni 60 – kiasi ambacho kimethibitishwa kuwa makadirio halisi ya mwisho kutokana na maoteo katika soko la hisa la Dar es Salaam.
- (ii) Fedha za msamaha wa madeni ya *IMF (MDRI)* hazikuwa zimejumlishwa katika tarakimu za misaada na mikopo ya nje katika Kitabu cha Mapato (Kitabu cha Kwanza), lakini zilikuweco katika kitabu cha hotuba ya Bajeti. Baada ya kuingiza marekebisho hayo, misaada na mikopo hiyo inakua Sh. 2,429,535/= ambayo ni sawa na tarakimu iliyoainishwa katika kitabu cha hotuba ya Bajeti (Sura ya Bajeti).
- (iii) Katika marekebisho niliyoyaeleza hapo juu na mengine madogo madogo katika Kitabu cha Mapato zimepatikana shilingi bilioni mbili za ziada ambazo zinapelekwa katika bajeti ya maendeleo ambako zitatengewa kukarabati viwanja vya ndege vilivyo katika hali mbaya sana, na kusaidia Wilaya zenye matatizo makubwa ya maji. Kwa hiyo, Kitabu cha Nne nacho kimefanyiwa marekebisho ili kuongeza hizo shilingi bilioni mbili katika Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yameingizwa katika vitabu hivyo viwili (cha Kwanza na cha Nne), imetengenezwa *Addendum* na vitabu hivyo pamoja na *Addendum* viliwasilishwa kwa Katibu wa Bunge ili kuwapatia Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya marekebisho hayo, Sura ya Bajeti (Ukurasa wa 48 wa Hotuba ya Bajeti) sasa inakuwa kama ifuatavyo:-

	<u>Shilingi</u>	<u>Milioni</u>
A. Mapato ya Ndani	4,728,595	
- Mapato ya Kodi	4,497,070	
- Mapato yasiyo ya Kodi	231,525	
B. Mikopo na Misaada ya Nje		
ikijumuisha MDRI/MCA-T	2,429,535	
C. Mauzo ya Hisa za Serikali	<u>60,000</u>	
Jumla ya Mapato	<u>7,218,130</u>	
D. Matumizi ya Kawaida	4,726,650	
E. Matumizi ya Maendeleo	2,491,480	
(a) - Fedha za Ndani		
- Ziada ya Bajeti ya Kawaida	2,000	
- Mapato ya Ubinafsishaji	60,000	
- Msamaha wa Deni IMF (MDRI)	66,322	
- Misaada ya Bajeti (GBS)	<u>812,058</u>	
		940,380
(b) Fedha za Nje (Basket na Miradi)	1,551,100	
Jumla ya Matumizi yote	<u>7,218,130</u>	

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walitaka ufafanuzi kuhusu fedha za ndani za matumizi ya maendeleo, kwa ufupi, fedha za ndani zinajumuisha vyanzo vifuatavyo:-

(i) Misaada ya Bajeti	
(<i>General Budget Support</i>)	– Sh. 812 bilioni
(ii) Fedha za ubinafsishaji	– Sh. 60 bilioni
(iii) Albaki kutoka kwenye Bajeti ya kawaida	– Sh. 2 bilioni
(iv) Msamaha wa deni la IMF (MDRI)	– <u>Sh. 66.3 bilioni</u>
Jumla	<u>Sh. 940.3 bilioni</u>

Misaada ya bajeti (*GBS*) hapa ni sehemu ya fedha za ndani kwa sababu fedha za *GBS* zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na zinachanganywa na mapato yetu wenyewe hivyo zinahesabiwa kama fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Kiongozi wa Upinzani na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa pongezi zake kwangu binafsi, Naibu Mawaziri, pamoja na Watendaji wote walio chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi na kwa kuutambua uzito wa kazi yetu. Mimi na wenzangu tumepokea pongezi hizo kama ishara njema ya Kambi ya Upinzani kuwa tayari kushirikiana na Serikali katika kutekeleza majukumu ya kuendeleza nchi yetu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Wizara ya Fedha na Uchumi iko tayari wakati wote kushirikiana nao panapokuwa na mawazo, maoni na mchango wowote unaolenga kuboresha utendaji wetu wa kazi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijaitendea haki Kambi ya Upinzani kama sitazungumza japo kidogo kuhusu kinachoitwa Bajeti Mbadala iliyosomwa hapa na Kiongozi wa Upinzani. Nampongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa jitihada zake na wenzake za kubuni alichokiita bajeti mbadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kuweka sawa baadhi ya mambo ambayo naona hayakukaa sawa katika hiyo bajeti mbadala ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, nianze na mapato kutokana na Uvuvi katika Bahari Kuu. Kama tunavyofahamu, suala hili liko chini ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority*), ambayo Sheria yake imepitishwa mwaka 2007 baada ya mashauriano kati ya pande mbili za Muungano. Kupitishwa kwa Sheria hiyo ni hatua ya mwanzo ya kuongeza mapato kutokana na kianzio hiki. Hatua ya pili ni kuipatia nyenzo za kazi Mamlaka hiyo, pamoja na Idara ya Uvuvi katika Wizara ya Maliasili na Utalii ili kusimamia uvuvi katika bahari kuu.

Maelezo ya kina kuhusu mkakati huu yapo katika Ibara ya 220, ukurasa wa 132 wa Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa Mwaka 2007 ambacho kiliwasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Bajeti Mbadala inajumuisha shilingi bilioni 67.5 kutokana na *Corporation Tax* ya asilimia 30 kama watalii wote wangetozwa *USD* 100 kwa siku wanayokuwapo nchini. Nafikiri kiasi hiki ni kikubwa na kwa sababu watalii wenyewe inaelekea kwamba wanapungua, ningeshauri pengine tutazame upya ili watalii hawa wasije wakakimbia.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeorodhesha maeneo mengine 19 ya mapato mapya. Tumeyapitia na kutafakari maeneo hayo, moja baada ya lingine. Naishukuru Kambi ya Upinzani, kwa mchango huo wa mawazo, nikiamini kwamba yametolewa kwa nia nzuri. Wataalam wangu watayapitia kwa kina na tutaona yale ambayo yanaweza yakatekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bajeti ya 2008/09 imejikita zaidi katika mambo makuu matatu:-

(i) Eneo la kwanza ni kuongeza mapato ya ndani ili kuimarisha uwezo wetu wenyewe wa kugharamia maendeleo ya nchi yetu. Dhana kubwa hapa ni kuondokana na utegemezi wa misaada ya wahisani. Kwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2008/2009, mapato ya ndani yataosha kulipia matumizi zote za kawaida. Fedha zote za Wahisani zitaelekezwa katika programu za miradi ya maendeleo.

Mapato ya ndani yanalingwa kuongezeka kwa asilimia 31 na yatafikia asilimia 18.5 ya Pato la Taifa. Pamoja na mapato ya Serikali, chanzo kingine kikubwa cha mapato ya kukuza uchumi na kusaidia maendeleo ya wananchi ni mikopo ya benki kwa wajasiriamali. Amana za wateja katika benki na vyombo vingine vya fedha ni zaidi ya shilingi trilion sita, ambazo kama zikikopeshwa kwa wajasiriamali ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya nchi yetu.

(ii) Jambo la pili kubwa katika bajeti hii, ni kuongeza kasi ya maendeleo ya elimu na miundombinu kama nguzo muhimu za maendeleo ya nchi. Sekta hizi mbili zimepewa sehemu kubwa ya bajeti katika mwaka 2008/2009. Vipaumbele vingine ambavyo tumevitaja ni afya, kilimo, maji, na nishati.

(iii) Eneo kubwa la tatu, ni kuweka mazingira ya kodi ambayo yanaongeza mapato ya Serikali, lakini hayachochei ongezeko la bei ya bidhaa na huduma, ukiacha bidhaa ambazo sio muhimu sana kwa maisha ya Watanzania. Kwa hiyo, Serikali imepunguza kodi nyingi, hasa ushuru wa forodha na *VAT* katika maeneo yanayogusa wananchi. Bajeti hii imezingatia msukumo wa bei zinazotokana na bei za mafuta ya petroli, chakula, malighafi ya viwanda na pembejeo za kilimo hasa mbolea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la misamaha ya kodi iliyowekwa kisheria kwamba ipunguzwe kwa asilimia 50 ili kuongeza pato la Serikali; Serikali inatoa misamaha ya kodi kupitia sheria za kodi na zisizo za kodi kwa nia ya kutoa vivutio vya uwekezaji au unafuu wa kodi kwa wawekezaji na makundi ya watu kwa nia ya kutekeleza Sera mbalimbali za Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa misamaha ya kodi inapunguza mapato ya Serikali. Lakini pale ambapo inabidi tuhamasishe wawekezaji tutaendelea kutoa misamaha hiyo. Lakini nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kama tulivyoahidi katika hotuba yangu kwamba misamaha ya kodi itapitiwa upya ili kuona ile yenye tija inaendelezwa na ile ambayo haina tija kwa kweli itabidi tuifute ili Serikali iweze kupata mapato ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la Benki Kuu kutafuta njia ya kudhibiti riba katika Soko la Fedha, kufuatia marekebisho yaliyofanyika katika sekta ya fedha kuanzia mwaka 1991. Riba za mabanki zinatawaliwa na soko. Katika kutekeleza sera hii Serikali ilianzisha soko la dhamana za Serikali ambalo hadi sasa ndilo mhimili wa uwekaji wa riba.

Kwa mujibu wa sera hii, jukumu la Benki Kuu ni kuhakikisha kuwa, soko la dhamana za Serikali linaendelezwa na kuboreshwa ili liweze kuweka riba zinazoendana na hali halisi ya uchumi. Benki Kuu kama mshiriki katika soko la dhamana za Serikali, hushiriki kwa nia ya kuendeleza soko na kutekeleza sera yake ya fedha, hususan kusimamia ukwasi katika uchumi.

Hivi karibuni, Benki Kuu imeimarisha sera yake ya fedha na ushiriki wake katika masoko. Idadi ya minada imepunguzwa ili kuongeza ushindani katika soko la dhamana za Serikali na lile la fedha za kigeni kama nyenzo za kudhibiti ukwasi. Kuimarika huku kwa sera, kumewezesha

soko kushusha riba za dhamana za Serikali kutoka kiwango cha wastani wa asilimia 16.42 mwezi Oktoba, 2007 hadi wastani wa asilimia 7.05 mwezi Aprili, 2008.

Kushuka huku kwa riba katika soko la dhamana za Serikali kumefuatiwa na kushuka kwa riba za ukopesaji kutoka mabanki ya biashara japo kwa kiwango kidogo. Riba za mikopo zimeshuka kutoka wastani wa asilimia 15.82 mwezi Juni, 2007, hadi wastani wa asilimia 14.09 Aprili, 2008. Kadhalika riba za amana za muda mrefu zimeongezeka toka wastani wa asilimia 7.28 Julai, 2007 hadi wastani wa asilimia 8.03 Aprili, 2008.

Soko la dhamana za Serikali litaendelea kuwa mhimili mkuu wa riba. Benki itaendelea na juhudi zake za kuboresha soko hili na pia sera yake ya fedha ili kuhakikisha kuwa riba hizo zinaendana na hali halisi ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya kwamba Benki Kuu isimamie vyema uimara wa shilingi na hoja ya kuimarisha kitengo cha Uchumi cha Benki Kuu, ningependa kutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi ya Tanzania inawekwa kwa nguvu ya soko. Sera hii imesaidia sana kuipa shilingi yetu thamani ambayo inalingana na hali halisi ya uchumi wetu. Katika muundo huu, Benki Kuu imeelekeza zaidi nguvu zake katika kujenga soko imara, lenye uwezo wa kuweka thamani ya shilingi inayoendana na hali halisi ya uchumi wetu.

Benki Kuu hushiriki katika soko hilo, kwa ajili ya kutekeleza sera yake ya fedha na kujenga akiba yetu ya fedha za kigeni bila kuingilia kati, nguvu ya soko katika uwekaji wa thamani ya shilingi. Hata hivyo, Benki Kuu katika jukumu lake la kuendeleza na kuimarisha soko, huhakikisha kwamba thamani ya shilingi iliyowekwa na soko inaendana na hali halisi ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya kukua kwa uchumi hayajawafikia wananchi ukuaji wa uchumi ni kigezo ama kiashiria kimojawapo katika kupima maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii. Ukuaji wa uchumi unatokana na badiliko la Pato la Taifa mwaka hadi mwaka ambapo ukuaji huo hujumuisha thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa katika nchi kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kukua kwa Pato la Taifa kuna maana kuwa shughuli za kiuchumi zimeongezeka na hivyo kuimarika kwa huduma na bidhaa zinazozalishwa.

Ni kweli wananchi wengi wanalalamika kuwa hawaoni manufaa ya kukua kwa uchumi, lakini tatizo kubwa hapa ni kuwa wanashindwa kuelewa kuwa wao wenyewe ndio wanafanya hizo shughuli za kiuchumi na huduma zinazokua. Vijana wengi wameajiriwa katika shughuli za ujenzi wa majengo na barabara na wanapata kipato huko na wanachangia katika ukuaji na uchumi lakini hawajui. Wengine wanajishughulisha na kilimo na wanachangia katika Pato la Taifa bila kujijua.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi ukuaji wa uchumi ni matokeo ya shughuli za kiuchumi zinazofanywa na Watanzania wenyewe. Ukuaji wa uchumi ndio unaoiwezesha Serikali kuongeza huduma za kijamii kama vile elimu, afya, maji na miundombinu ya barabara, kwa kuwa mapato ya Serikali yanapanda uchumi unapokua.

Matokeo ya ukuaji wa uchumi ni mchakato wa muda mrefu, hivyo manufaa yake katika kuleta maendeleo yataonekana vizuri baada ya kipindi fulani kama ambavyo ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hata hivyo, katika muda mfupi huu wa kutekeleza mageuzi ya kiuchumi hapa nchini tayari baadhi ya mafanikio yameanza kuonekana na hata kwa wananchi wa vijijini.

Kwa mfano, pamoja na mafanikio makubwa katika viashiria vya uchumi mpana baadhi ya huduma zimeanza kuwanufaisha wananchi kutokana na ukuaji wa Pato la Taifa, kama vile elimu, afya na mawasiliano kwa njia ya simu, hata vijijini wengi wanapata huduma hii. Sio hivyo tu, bali hata baadhi ya barabara kuu ambazo zilikuwa hazipitiki sasa zimeanza kupitika kwa urahisi zaidi na hivyo kuwezesha wakulima wengi kusafirisha mazao yao kwenda kwenye masoko mijini. Utalii pia umeongezeka na kuongeza fedha za kigeni na ajira. Serikali haijatangaza fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi ya gesi ya Songo Songo na *Mnazi Bay*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kwamba Serikali imetenga fedha za ndani na za nje katika fungu 58 ambalo ni la Wizara ya Nishati na Madini, kwa ajili ya kuendeleza miradi ya gesi ya Songo Songo na *Mnazi Bay*. Kazi kubwa zitakazofanyika katika miradi hii ni kujenga miundombinu ya kuchimba, kusafisha na kusafirisha gesi asilia hadi kwenye vinu vya umeme pamoja na matumizi mengine. Maelezo zaidi yatatolewa na Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha kwenye Halmashauri kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu nilipowasilisha mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2008/2009, ili kuthibiti matumizi ya Serikali katika ngazi ya Halmashauri, Serikali itapitia upya sheria ya Serikali za Mitaa, sura 290 pamoja na sheria ya Fedha za Umma, sura 348, kwa lengo la kuainisha marekebisho yanayostahili ili kumpa uwezo Mlipaji Mkuu wa Serikali akisaidiwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha kwenye Halmashauri. Kuna akaunti nyingi katika Halmashauri na hivyo kusababisha usimamizi wa fedha kwenye Halmashauri kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, suala la Halmashauri kuwa na akaunti nyingi na hivyo kusababisha matatizo ya kuzisimamia ambayo ni pamoja na kuzifanyia usuluhisho wa hesabu za benki ni suala ambalo Serikali imeamua kulifanyia kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kulikua na hoja kuhusu fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi maalum. Kiasi kilichotengwa kama matumizi maalum ni Tshs 364,391 milioni na mchanganuo wake na wapi zitakwenda ni kama ifuatavyo:-

- (i) Malimbikizo ya Nyongeza ya Mishahara Januari-Juni, 2008;
- (ii) Nyongeza ya Mtaji wa *TIB* wa bilioni 21;
- (iii) Malipo ya Mkopo wa Ujenzi wa Chuo Kikuu Dodoma;
- (iv) Malipo ya Mkopo wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu;
- (v) Gharama za Maandalizi ya Daftari la Wapiga Kura; na
- (vi) Kifungu cha Dharura ya Taifa.

Mapato yanayotokana na mapendekezo ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini yajumuishwe katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa Sekta ya Madini ilikamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais, ameelekeza utaratibu wa kuipitia taarifa hiyo ili kufikia maamuzi ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati hiyo. Maamuzi ya Serikali kuhusu utaratibu mpya wa kusimamia sekta ya Madini, ikiwemo mfumo mpya wa kodi, yanategemewa kuwa tayari kabla ya mwisho wa mkutano wa Bunge hili la Bajeti. Serikali italeta mapendekezo ya marekebisho ya Sheria zinazohusika wakati muafaka. *(Makofi)*

Kutodhibitiwa vizuri kwa walipakodi wakubwa wa nje ya Dar es Salaam baada ya kuhamishiwa katika Idara ya walipakodi wakubwa hili limeelezwa na Naibu Waziri, sina haja ya kulirudia.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la wahitimu wapya wa kilimo kwamba wawezeshwe ili wawekeze kwenye Kilimo. Ni kweli kwamba wataalam wahitimu wapya kutoka vyuoni kama *SUA* wakiwezesha kimtaji wataweza kuwekeza kwenye miradi ya kilimo.

Pamoja na ukweli huo, Serikali inaliangalia suala la uwezeshaji katika upana wake kwa maana ya kwamba wapo wananchi wenye uwezo wa kuanzisha miradi mizuri katika sekta mbalimbali kama wakiwezesha hususan kimtaji.

Kwa kuelewa hivyo na kwa lengo hili, Serikali imeanzisha jitihada mbalimbali ikiwemo mifuko ya dhamana ya mikopo ikiwamo ile inayosimamiwa na Benki Kuu na vilevile mfuko wa kuwawezesha wananchi kiuchumi (*Mwananchi Empowerment Fund*). Huu Mfuko wa mwisho ulizinduliwa mwezi Januari, 2008 na umeanza na mtaji wa shilingi milioni 400. Itaendelea kuongezwa kadri fedha zinavyopatikana. *(Makofi)*

Madhumuni ya mfuko huu ni kutoa dhamana ya asilimia 75 kwa mikopo ambayo wajasiriamali wataomba kutoka kwenye mabenki ya biashara na asasi nyingine za huduma za kifedha nchini. Mfuko huu ni kwa wajasiriamali Watanzania wa makundi yoyote yale.

Changamoto iliyoko ni kupata vyanzo vya uhakika vya rasilimali ya kupanua mfuko huu ili utosheleze mahitaji, kwani shilingi milioni 400 ni kiasi kidogo sana. Wakati jitihada ya kutafuta vyanzo inaendelea, mkakati mwingine wa Serikali ni kufanya mazungumzo na mabenki ya biashara nchini kwa lengo la kuyashawishi yalegeze masharti yao ili wananchi wengi zaidi wakiwemo wataalam vijana waweze kukopa kutoka huko.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipunguza viwango vya kodi na kupandisha kima cha chini cha mshahara kinachostahili kutozwa kodi hatua kwa hatua. Tumefanya uchambuzi wa mapendekezo ya Mheshimiwa Katagira ambaye alipendekeza kwamba kiwango cha chini kabisa iwe Sh. 300,000/= na kubaini kuwa kama tukiyatekeleza mapendekezo haya, Serikali itapoteza mapato kiasi cha shilingi bilioni 325. Kiasi hiki ni kikubwa sana kwa bajeti yetu kuweza kuhimili. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutoa unafuu kwa wafanyakazi wake wa kima cha chini kadiri bajeti itakavyoruhusu.

Mapato yanayotokana na matumizi ya simu, *air time* yabaki kama ilivyokuwa. Hoja ilitolewa kwamba makampuni ya simu nchini hayalipi kodi na wala hayajawekeza chochote, kwani hata ofisi zao zimo katika majumba ya kupanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makampuni ya simu nchini yamepewa leseni za kutoa kuduma za mawasiliano kama ndio shughuli ya msingi (*core activity*). Uwekezaji unaofanywa na makampuni haya ni wa vifaa na mitambo ya mawasiliano. Makampuni haya yanalipa kodi mbalimbali kama zilivyoainishwa katika sheria mbalimbali za kodi. Mchango wa kodi kutoka sekta hii ya mawasiliano katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 - 2007/2008 ulifikia Shilingi bilioni 499.6. Aidha, TRA imekuwa ikifanya ukaguzi wa makampuni ya simu sambamba na makampuni mengine ili kuhakikisha kuwa yanalipa kodi stahili kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, watanzania wenye fedha nje ya nchi wapewe *General Amnesty*, watanzania wenye fedha zao nje ya nchi walizozipata kihalali na kuziweka benki hawakatazwi kuzileta nyumbani. Narudia walizozipata kihalali. Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu ya mwaka 2006 inaharamisha fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi.

Kwa mujibu wa sheria hii pamoja na kanuni zake za mwaka 2007, mabenki na taasisi za fedha ni lazima ziwaifahamu wateja wao na kuweka kumbukumbu sahihi za mienendo ya hesabu za wateja wao. Kila sekta ina mdhibiti wake, kwa mfano: mabenki, bima, masoko ya fedha na mitaji, makasino, Wahasibu, wanasheria, wauzaji wa vito wote hawa wana wadhibiti wao.

Usafirishaji wa fedha taslimu pia unadhhibitiwa mipakani, viwanja vya ndege na bandarini. Ni lazima anayesafirisha fedha taslimu azionyeshe kwa Afisa wa Forodha na nchi nyingi zina viwango vinavyokubalika. Hauhitajiki msamaha kuingiza fedha halali nchini. Kwa mfano, Marekani ukienda na zaidi ya dola 10,000 hata usipozi-*declare* mashine itakuonyesha kwamba wewe una dola 10,000 kwa hiyo watakukamata.

Mheshimiwa Spika, suala la mikopo kwa wakulima na kupanua wigo wa mifuko ya huduma ya dhamana ni masuala ambayo yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge sambamba na wito wa kuanzishwa kwa benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kuweka mazingira mazuri ili wananchi walio na miradi midogo midogo au wenye miradi mipya, wakiwemo wakulima waweze kupata mikopo kwa urahisi kutoka benki za biashara na vyombo vingine vya fedha nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na:

(i) Kuimarisha huduma ya dhamana ya mikopo kwa ajili ya mauzo nje, huduma ambayo imeyawezesha mabenki kutoa mikopo kwa vyama vya ushirika na wafanyabiashara wengine wanaonunua mazao kutoka kwa wakulima na kuyauza nje ya nchi.

(ii) Kuimarisha huduma ya dhamana ya mikopo kwa ajili ya wenye miradi midogo midogo na ya kati. Huduma hii sasa imeanza kupata mwitikio mzuri na tayari miradi ipatayo 50 ikiwemo ya sekta ya kilimo yenye thamani ya shilingi bilioni sita imeshanufaika na mikopo kutoka benki za biashara. Kutokana na mwitikio huu, Serikali inakusudia kuongeza kiwango cha dhamana ili miradi midogo mingi zaidi iweze kupata mikopo.

(iii) Sheria ya mikopo kwa njia ya ukodishaji (*Finance Leasing*) imepitishwa na Bunge hili mwezi Aprili, 2008. Serikali inatarajia kuwa makampuni na mabenki yataanza

kukopesha vitendea kazi kwa wajasiriamali wadogo na wasio na dhamana ambao ni pamoja na wakulima.

(iv) Awamu ya kwanza ya Mfuko wa J.K. ilihusisha wajasiriamali wadogo wapatao 36,000 na kiasi cha shilingi 33.2 bilioni zilikopeshwa na benki za *CRDB* na *NMB* katika Wilaya zote nchini isipokuwa 25. Wilaya 41 zilipata mikopo chini ya kiwango kilichotarajiwa. Awamu ya pili iliyoanza hivi karibuni itahusisha benki za *CRDB*, Akiba *Commercial Bank* na benki za Wananchi 11.

Tofauti na awamu ya kwanza, mkazo mkubwa utawekwa katika kupatikana kwa mikopo katika Wilaya zote hususan zile ambazo hazikuhusika katika awamu ya kwanza na pia Kamati za Wilaya zitahusishwa katika kuamua fedha hizi zikopeshwe kwa nani kulingana na vipaumbele vyao. Aidha, katika awamu ya pili, fedha zilizokopeshwa na *CRDB* na kurejeshwa zitaendelea tena kukopeshwa sambamba na zile zilizotolewa katika awamu ya kwanza. Hivyo, ni dhahiri kuwa mfuko huu wa J.K. utakuwa wa manufaa makubwa kwa wajasiriamali wa vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati niliyoitaja hapo juu ambayo imeanza kutekelezwa, mikakati mingine ipo mbioni kutekelezwa, ikiwa ni pamoja na:-

(i) Benki Kuu kuanzisha utaratibu wa kukusanya na kusambaza taarifa za wakopaji (*credit information sharing system*) ili kuwawezesha raia wema kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha kwa urahisi.

(ii) Serikali kuandaa mikakati ya kuboresha huduma za kifedha katika maeneo ya vijijini (*Rural Financial Sector Strategy*).

(iii) Serikali inakusudia kutazama muundo wa *TIB* ili kabla hatujaunda benki ya Kilimo kuweza kuwa na idara katika benki ile ambayo inaweza ikashughulikia mikopo ya kilimo na mikopo ya pembejeo. Lakini mwishowe Serikali inatazama uwezekano wa kama benki ya kilimo inaweza ikaanzishwa mapema iwezekavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa haya niliyoyaeleza, naamini Waheshimiwa Wabunge wameona ni kwa jinsi gani Serikali ya Awamu ya Nne inavyolishughulikia suala la mikopo kwa wakulima na hatua iliyofikiwa na malengo ya siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Tume ya Pamoja ya Fedha, iliwasilisha katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mapendekezo ya formula ya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano baina ya pande mbili za Muungano. Pendekezo hilo linajumuisha uchambuzi na maelezo ya jinsi Tume ilivyofikia kutoa ushauri huo. Serikali mbili zinaendelea kuchambua mapendekezo hayo kwa mashauriano katika ngazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na vikao vya pamoja chini ya Makamu wa Rais.

Katika uchambuzi huo, ilionekana yapo maeneo ambayo yalihitaji ufafanuzi kwa kufanyiwa kazi zaidi na Tume. Maeneo hayo ni pamoja na:-

(i) Vigezo vilivyotumika katika kupendekeza formula hiyo;

- (ii) Utaratibu utakaotumika katika kuanzisha na kuendesha Akaunti ya Pamoja (*Joint Finance Account*) kwa mujibu wa Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na
- (iii) Utaratibu utakaotumika kuwezesha kuwepo kwa ushirikiano baina ya Serikali mbili katika maandalizi ya bajeti.

Tume ya Pamoja ya Fedha inaendelea kurejea ufafanuzi wa ziada katika vigezo vilivyotumika katika kuandaa *formula*. Lengo ni kukamilisha kazi hiyo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2008/2009. Aidha, Tume imepanga kuyafanyia kazi maeneo mawili yaliyosalia katika mwaka wa fedha 2008/2009.

Kuhusu changamoto zinazoikabili Tume, Wizara za Fedha na Uchumi za Serikali mbili kwa kushirikiana na wadau wengine wa masuala ya uhusiano wa kifedha zinaendelea kuisaidia Tume kukabiliana na changamoto hizo.

Aidha, kuhusu Tume kumaliza muda wake, ni kweli muda wa Tume umemalizika kama ilivyo kwamba Wajumbe wa Tume wanatoka pande zote mbili. Tumepeleka upande wa Zanzibar na Mheshimiwa Karume, ameshakubali majina ya kuingia kwenye Tume ile na huku Bara tunayo tayari. Kwa hiyo, nadhani wakati wowote mimi nitapeleka kwa Mheshimiwa Rais na wakati wowote Tume mpya itakuwa imeundwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta ghafi ya kula, Waheshimiwa Wabunge kadhaa wametoa maoni yanayotofautina kuhusu pendekezo la kuondoa ushuru wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula yanayoagizwa kutoka nje. Serikali imetafakari maoni ya Waheshimiwa Wabunge na imeona inahitaji muda wa kulitolea suala hili uamuzi.

Kwa hiyo, Serikali inaomba tuliache pendekezo hilo kama lilivyo na nitapata fursa ya mashauriano na wadau wote muhimu katika suala hili, wakiwemo wakulima wa mbegu za mafuta, Waheshimiwa Wabunge, waliotoa maoni kuhusu suala hili na hasa wale wanaotoka maeneo ambayo yanalima mbegu za mafuta kwa wingi, wenye viwanda vya kusindika mafuta wengine na kadhalika Mashauriano haya yatakapokamilika Bunge litaarifiwa ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamehoji kushuka kwa bajeti ya Maji. Katika hotuba yangu ya Bajeti aya 44 kifungu kidogo (*d*) nilieleza sababu ya kupungua kwa bajeti ya Sekta ya Maji. Serikali inaelewa tatizo la maji lilivyo katika nchi yetu. Ningependa kuchukua fursa hii kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu bajeti ya maji, kwani Waheshimiwa Wabunge karibu wote waliochangia wameonyesha kukerwa na punguzo la bajeti ya maji. (*Makofi*)

Ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa sekta ya maji ni kipaumbele na kuwa fedha zinazoonekana kupungua ni fedha za wafadhali. Uzoefu umeonyesha kwamba ahadi nyingi za wafadhili za fedha za miradi ya maji hazipatikani kama wanavyoahidi. Mfano hai ni mwaka huu wa fedha 2007/2008 ambapo kati ya Sh. 154,236,748,600/= zilizoahidiwa na wafadhili kama fedha za maendeleo za wafadhili kwa Wizara ya Maji, kiasi kilichopatikana ni shilingi bilioni 20 tu na Wilaya zote ambazo ziliahidiwa fedha za miradi ya maji hazikupata. (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, unasemaje? (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, nasema Wilaya zote ambazo ziliahiwa kupata hizi bilioni 154, nyingi hazikupata. Karibu zote hazikupata! Zilizopata ni zenye miradi ambayo inaendelea.

Kwa maelezo hayo, katika bajeti ya 2008/2009 tumeona ni busara kutenga kiasi cha shilingi bilioni 93.49 tu kama fedha za nje kwa fungu hili. Punguzo hili pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa Shinyanga na Kahama, ndizo sababu za kushuka kwa bajeti ya Maji. Vinginevyo tungenesema tuweke tena shilingi bilioni 200, lakini tukijua kwamba inawezekana hizo fedha zisipatikane.

Mheshimiwa Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba iwapo wafadhili wataleta fedha zaidi kwenye miradi ya maji, kibali cha Bunge kitaombwa kuongeza fungu la Wizara ya Maji kwa kiasi hicho kitakachopokelewa. Naamini Waziri wa sekta husika, atafafanua mipango ya Wizara yake atakapowasilisha bajeti yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna swali liliulizwa kwamba, kwa nini bei ya mafuta ya *petrol* Malawi ni ndogo kuliko Tanzania ingawa Malawi iko mbali? Sehemu kubwa ya mafuta ya petroli yaendayo Malawi yanapitia katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Katika hali ya kawaida, inategemewa kuwa bei za reja reja za mafuta hayo huko Malawi zitakuwa ni kubwa kuliko za Tanzania.

Katika utafiti tuliofanya, imedhihirika kuwa bei za mafuta Tanzania, hususani Dar es Salaam hazitofautiani sana na ni ndogo kuliko za huko Malawi kwa takwimu za tarehe 17 Juni, 2008. Bei za huko Malawi ni shilingi za Tanzania 2,093 kwa lita ya Dizeli na shilingi 1,968 kwa Petroli. Kwa Tanzania bidhaa hizo huuzwa kwa shilingi 1,930 dizeli na shilingi 1,680 kwa petroli. Kwa takwimu hizo, ni dhahiri kuwa bei za mafuta hayo Tanzania ni ndogo kuliko Malawi. Wafanyakazi wanalipa kodi nyingi zikiwemo kodi ya mapato na kodi za mlaji wakati wafanyabiashara wanalipa kodi ya mapato tu, kodi nyingine wao ni wakala kwani wanakusanya toka kwa watumiaji wa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, kuna swali pia kamba unafuu wa kodi kwa wafanyakazi unaosemwa na Serikali uko wapi?

Mheshimiwa Spika, Kodi ya Mapato inatozwa katika mapato ya mtu yeyote, mfanyabishara na mfanyakazi. Aidha, kodi nyingine zikiwemo kodi za bidhaa hulipwa na watu wote pale wanapotumia bidhaa zinazotozwa kodi, yaani bidhaa na huduma. Hivyo sio sahihi kusema kuwa wafanyabiashara wanalipa kodi ya mapato tu, kwani wafanyabiashara kama ilivyo kwa wafanyakazi nao hulipa kodi ya mlaji pale wanapotumia bidhaa na huduma zinazotozwa kodi. Unafuu unaopendekezwa na bajeti ya mwaka 2008/2009 ni wa kupandisha kiwango cha chini cha mapato kisichotozwa kodi kutoka Sh. 80,000/= hadi 100,000/= kwa mwezi na kupunguza viwango vya kodi kwa mapato mengine yanayostahili kutozwa kodi. Kwa nini *TRA* inakwamisha kutoa leseni kwa kampuni ya *Zanzibar Catering Services* ili iweze kutoa huduma za chakula kwenye ndege.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Zanzibar Catering Services*, imesajiliwa kwa lengo la kuhudumia ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar. Kampuni hii pia

iliomba isajiliwe na *ZIPA* ili iweze kufaidi vivutio vya Kodi. Aidha, Kampuni hii iliomba iruhusiwe kutumia utaratibu wa *inward processing* katika kuendesha biashara yao.

Zanzibar Catering Services walikataa ushauri huo na kuamua kuishitaki *TRA* Mahakamani huko Zanzibar. Lakini hata hivyo kampuni hii ilishindwa. Baada ya kesi hiyo walielekezwa tena utaratibu sahihi ambao walitakiwa kuufuata ikiwa ni pamoja na kutimiza na masharti ya *ZIPA*. Hadi leo hawajaonekana Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kukamilisha taratibu za kupewa leseni kwa utaratibu unaotambulika ndani ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki. Inapendekezwa kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha sifuri kwenye huduma kwenye huduma ya kutayarisha shamba, kuvuna miwa, kupakia, kupakua na kuisafirisha hadi kiwandani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya ongezeko la thamani, huduma za ukataji, upakiaji na usafirishaji wa miwa kama ilivyo kwa mazao mengine ya kilimo hazikuorodheshwa katika Jedwali la pili la Sheria ya *VAT*. Bidhaa au huduma zote zilizoorodheshwa kwenye Jedwali la pili la Sheria ya *VAT* ndizo pekee zilizosamehewa kodi na msamaha huo hauhuishi huduma nyingine zinazotolewa katika kufanikisha upatikanaji wa bidhaa hizo.

Serikali imepokea malalamiko kutoka kwa wakulima wa miwa wanaozunguka viwanda vya sukari, *out growers* na inalifanyia uchambuzi wa kina suala hilo ili kutafuta uvumbuzi wa kudumu sambamba na mazao mengine ya kilimo yaliyo kwenye utaratibu wa kampuni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na tatizo la ushuru wa mauzo ya korosho. Ushuru wa korosho ghafi inayouzwa nchi za nje unakusanywa na *TRA* kwa kiwango cha asilimia 10 ya thamani. Asilimia 6.5 ya kiasi hicho hurejeshwa kwa Halmashauri ambako korosho husika zimezalishwa na asilimia 3.5 inaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kuchangia gharama za uendeshaji wa zao hilo.

Mheshimiwa Spika, wadau wa zao la korosho ambao ni pamoja na vyama vya wakulima, Halmashauri za Wilaya katika maeneo yanayozalisha korosho, Bodi ya Korosho, Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Biashara, Biashara na Masoko na Ushirika na Mamlaka ya Mapato Tanzania walikubaliana utaratibu wa kukusanya na kugawana mapato kutokana na ushuru huu. Kwa mujibu wa makubaliano ya wadau *TRA* ilitakiwa iwasilishe mgao wa asilimia 6.5 kwa Halmashauri kupitia Bodi ya Korosho ambayo ingepaswa kugawa mapato hayo kwa Halmashauri zote husika kwa kuzingatia uzalishaji katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, ushuru uliokusanywa mwaka 2006/2007 ni shilingi bilioni 4.5 na mwaka 2007/2008 zilikuwa zimekusanywa shilingi bilioni 6.7 hadi mwisho wa mwezi Mei mwaka huu. Kwa hiyo, stahili ya Halmashauri za maeneo yanayozalisha korosho ni shilingi bilioni 7.15 kwa miaka hiyo miwili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kilio cha wakulima wa korosho ni dhahiri kuwa utaratibu huo wa kupitisha mgao kwenye Bodi haujaridhisha wadau hao wote. Kwa hiyo, kama Waziri wa Fedha, natangaza kwamba kuanzia Julai mosi, asilimia 6.5 ya ushuru unaokusanywa zitapelekwa moja kwa moja kwa Halmashauri husika kama Sheria inavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia michango ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu Ada ya Leseni za Magari, Serikali iinapendekeza kufanya marekebisho kidogo katika viwango vilivyokuwa vimependekezwa awali. Viwango vya awali na vile vinavyopendekezwa sasa ni kama ifuatavyo:-

Ukubwa wa Injini	Kilichopendekezwa Awali	Kiwango Kinachopendekezwa sasa
Usiozidi cc 500	Shs. 30,000	Shs. 30,000
cc 501 hadi cc 1500	Shs. 50,000	Shs. 50,000
cc 1501 hadi cc 2500	Shs. 120,000	Shs. 100,000
cc 2501 hadi cc 5000	Shs. 140,000	Shs. 150,000
Unaozidi cc 5000	Shs. 150,000	Shs. 150,000

Mheshimiwa Spika, naelekea kumaliza. Waheshimiwa Wabunge, wametoa ushauri wao kuhusu haja ya Serikali kuanza kutumia utaratibu wa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeshaanza mchakato wa kuingia katika utaratibu wa mikopo ya muda mrefu kutoka kwenye soko la mitaji ya nje. Chini ya utaratibu huo, hatua ya kwanza ni kwa nchi yetu kutathminiwa uwezo wa kukopesheka, yaani *sovereign credit rating*.

Aidha, Serikali inaendelea kutambua miradi ya maendeleo ikiwemo ya miundombinu ya barabara, reli na nishati itakayoweza kuzingatiwa mara taratibu zitakapokamilika. Ni mategemeo ya Serikali kwamba zoezi hilo la *sovereign rating* litakamilika kabla ya mwisho wa mwaka wa 2008/2009 ili Serikali iende sokoni na miradi itatekelezwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2009/2010. Kuna faida kuu mbili za mpango huu.

Kwanza, Serikali haitakopa kutoka vyombo vya ndani vya fedha kwa kuwa itaathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi na itachochea riba kupanda na kwa hiyo, mfumuko wa bei.

Pili, ni kuongezeka kwa uwezo wa uwezesaji katika miundombinu na kutumia fursa, yaani *physical space* kwa Serikali kutekeleza programu nyingine za muhimu za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 na 2008/2009 vipaumbele vikuu vya Serikali vimekuwa elimu na miundombinu. Sisi wote ni mashahidi kuwa sekta ya elimu imepanuka sana na pia imeboreka. Maeneo machache yaliyobaki yataendelea kuboreshwa ndani ya mwaka 2008/2009. Wote pia ni mashahidi kuwa miundombinu ya barabara imeboreka. Barabara nyingi hivi sasa zina lami na hata zile ambazo hazina lami zinapitika.

Kama nilivyosema awali, Serikali inakusudia kukopa katika soko la kimataifa kwa ajili ya miradi ya miundombinu. Ni tegemeo la Serikali kuwa ifikapo mwaka 2011/2012 barabara za Mtwara hadi Masasi, Masasi hadi Tunduru, Tunduru hadi Songea, Songea hadi Mbambabay na

barabara ya Itigi – Manyoni – Kigoma, barabara ya Minjingu – Kondoa – Dodoma - Iringa na barabara ya Korogwe – Handeni – Kilosa - Mikumi zitakuwa zimejengwa kwa kiwango cha lami. Baada ya kuimarisha miundombinu yote nchini, juhudi sasa zitaelekezwa kwenye sekta ya kilimo na sekta nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziko hoja zilitolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa - Mbunge wa Karatu kuhusu *EPA*, Kampuni ya *MEREMETA* na Kampuni ya *TANGOLD*. Kuhusu *EPA* napenda kukumbusha kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteua Kamati maalum inayojumuisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama Mwenyekiti, *Inspector General* wa Polisi na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU. Kamati hiyo imepewa muda wa miezi sita kumaliza kazi iliyopewa. Kamati itawasilisha taarifa yake kwa Rais ambaye ataamua hatua za kuchukuliwa.

Lakini ningependa kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wanaonisikiliza kwamba fedha za *EPA* hazikuwa fedha za Serikali wala fedha za Benki Kuu. Hizi fedha zilikuwa fedha za wafanyabiashara ambao kwa wakati ule waliilipa iliyokuwa *NBC* kwa ajili ya kuagiza bidhaa mbalimbali kutoka nje. Lakini *NBC* kwa wakati ule ilishindwa kuzilipa nje ya nchi kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubinafsisha *NBC* akaunti za fedha hizi zilihamishiwa Benki Kuu. Serikali haina hakika fedha hizi zitakaporudishwa zote zitafanyiwa nini kwa vile wenye fedha hizo wengi wao hawapo hapa nchini au wamekufa au wamelipwa kupitia *MDRA*. Kama alivyoahidi Waziri aliyenitangulia, Mheshimiwa Mama Zakia Meghji, baada ya Kamati kuwasilisha taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu litajulishwa matokeo ya mapendekezo ya Kamati hiyo na hatua zitakazokuwa zimechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza mengi yanayohusu Bajeti. Kulikuwa pia na suala la *MEREMETA* na *TANGOLD*. Haya yatafafanuliwa na Waziri anayehusika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kujibu hoja vizuri. Waheshimiwa Wabunge zoezi linalofuata sasa ni la kupiga kura, ambalo linatawaliwa na Kanuni ya 98(2), nitaishoma. Inasema: “Uamuzi wa Bunge wa kupitisha bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja” na Kanuni ya 79(8), inasema, nanukuu:

“Endapo Spika ataamuru kura zihesabiwe, Katibu atapiga kengele ya kuwaita Wabunge kwa muda wa dakika moja na baada ya muda huo Spika atamwagiza Katibu kumwita Mbunge mmoja mmoja kwa jina lake na kumwuliza anapiga kura yake upande gani na kurekodi kura hiyo.” Hili linatokana na Katiba Ibara ya Katiba ya 90(2)(b) ambayo inasema, nanukuu:

“Rais atakuwa na uwezo wa kulivunja Bunge wakati wowote isipokuwa tu kama Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali. Sasa haya ndiyo mazingira ambayo tunapiga kura. Ni vizuri kuyafahamu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, sasa nitamwomba Katibu kengele ipigwe, tushiriki kidogo tuingie katika kura na naona tuokoe muda, hakuna haja ya kuwahesabu Waheshimiwa Wabunge kwa sababu majina

yatakapoitwa na idadi yetu ni 318 tutajua ni kwa kiwango gani tumo humu. Najaribu tu kuokoa muda. Kwa hiyo, Katibu, kengele ipigwe sasa.

*(Hapa Kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge
Waliopo nje ya Ukumbi Waingie Ndani ya
Ukumbi wa Bunge)*

SPIKA: Kengele hiyo mnaisikia Waheshimiwa Wabunge? Lengo ni kuwaita walioko nje ndiyo maana humu haitupigii kelele sana. Sasa nasubiri dakika moja.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Hapa ninayo orodha ya Waheshimiwa Wabunge wote. Idadi yetu kwa sasa ni 318. Theluthi mbili ya Wabunge ni 212. Idadi ya Wabunge Kikatiba ni 323. Viti vilivyo wazi ni vinne. Hesabu haikubali hii? Aaah, mmoja ni mimi, alah! *(Kicheko)*

Kwa mujibu wa Kanuni, mimi sipigi kura kwa sababu napiga kura ya turufu mkifungana. Dakika moja imepita. Kwa hiyo, Katibu anza kuita majina na Waheshimiwa Wabunge mtasema kama kawaida, Ndiyo au Siyo.

(Hapa Upigaji Kura kwa Kuita Majina Ulianza)

1. Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda	Ndiyo
2. Mhe. Philip Sang'ka Marmo	Ndiyo
3. Mhe. Muhammed Seif Khatib	Ndiyo
4. Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya	Ndiyo
5. Mhe. Dr. Mary Michael Nagu	Ndiyo
6. Mhe. John Pombe Joseph Magufuli	Ndiyo
7. Mhe. Prof. Mark James Mwandosya	Ndiyo
8. Mhe. Dr. Hussein Ali Mwinyi	Ndiyo
9. Mhe. Capt. John Zefania Chiligati	Ndiyo
10. Mhe. Margaret Simwanza Sitta	Ndiyo
11. Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla	Ndiyo
12. Mhe. Stephen Masatu Wasira	Hakuwepo
13. Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa	Ndiyo
14. Mhe. Prof. Jumanne A. Maghembe	Ndiyo
15. Mhe. Dr. Shukuru J. Kawambwa	Ndiyo
16. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia	Ndiyo
17. Mhe. Sophia Mnyambi Simba	Ndiyo
18. Mhe. Dr. Batilda Salha Burian	Ndiyo
19. Mhe. Bernard Kamillius Membe	Ndiyo
20. Mhe. Mathias Meinrad Chikawe	Ndiyo
21. Mhe. Dr. Diodorus Buberwa Kamala	Ndiyo
22. Mhe. Shamsa Selengia Mwangunga	Ndiyo
23. Mhe. Mustafa Haidi Mkulo	Ndiyo
24. Mhe. Lawrence Kego Masha	Ndiyo
25. Mhe. William Mganga Ngeleja	Ndiyo
26. Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika	Ndiyo
27. Mhe. Celina Ompeshi Kombani	Ndiyo

28. Mhe. Johnson Paulo Mathias Mwanyika	Ndiyo	
29. Mhe. Anne Semamba Makinda	Ndiyo	
30. Mhe. Dr. Maua Abeid Daftari	Ndiyo	
31. Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje	Ndiyo	
32. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	Hakuwepo	
33. Mhe. Dr. Emmanuel John Nchimbi	Ndiyo	
34. Mhe. Mwantumu Bakari Mahiza	Ndiyo	
35. Mhe. Dr. Cyril August Chami	Hakuwepo	
36. Mhe. Dr. Milton M. Mahanga		Ndiyo
37. Mhe. Dr. Aisha Omar Kigoda	Ndiyo	
38. Mhe. Joel Nkaya Bendera	Ndiyo	
39. Mhe. Dr. David Mathayo David	Ndiyo	
40. Mhe. Christopher Kajoro Chiza	Ndiyo	
41. Mhe. Gaudentia Mugosi Kabaka	Ndiyo	
42. Mhe. Jeremiah Solomon Sumari	Ndiyo	
43. Mhe. Mohamed Aboud Mohamed	Ndiyo	
44. Mhe. Omar Yussuf Mzee	Ndiyo	
45. Mhe. Balozi Hamis Suedi Kagasheki	Ndiyo	
46. Mhe. Dr. Lucy Sawere Nkya	Ndiyo	
47. Mhe. Dr. James Mnanka Wanyancha	Ndiyo	
48. Mhe. Ezekiel Magolyo Maige	Ndiyo	
49. Mhe. Adam Kighoma Ali Malima	Ndiyo	
50. Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri	Ndiyo	
51. Mhe. Dr. Abdallah Omar Kigoda	Ndiyo	
52. Mhe. George Malima Lubeleje		Ndiyo
53. Mhe. Wilson Mutagaywa Masilingi	Ndiyo	
54. Mhe. Anne Kilango Malecela	Ndiyo	
55. Mhe. John Momose Cheyo	Ndiyo	
56. Mhe. Dr. Wilbrod Peter Slaa	<i>Abstain</i>	
57. Mhe. Kabwe Zuberi Zitto	<i>Abstain</i>	
58. Mhe. George B. Simbachawene	Ndiyo	
59. Mhe. Lediana Mafuru Mng'ong'o	Ndiyo	
60. Mhe. Abdisalaam Issa Khatib	Ndiyo	
61. Mhe. Omar Shabani Kwaangw'	Ndiyo	

62. Mhe. Jenista Joakim Mhagama	Ndiyo
63. Mhe. Job Yustino Ndugai	Ndiyo
64. Mhe. Gideon Asimulike Cheyo	Ndiyo
65. Mhe. Mohamed Hamisi Missanga	Ndiyo
66. Mhe. William Hezekia Shellukindo	Ndiyo
67. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	<i>Abstain</i>
68. Mhe. Halima James Mdee	Hakuwepo
69. Mhe. Shoka Khamis Juma	<i>Abstain</i>
70. Mhe. Grace Sindato Kiwelu	Hakuwepo
71. Mhe. Riziki Omar Juma	<i>Abstain</i>
72. Mhe. Chacha Zakayo Wangwe	Hakuwepo
73. Mhe. Dr. Ali Tarab Ali	<i>Abstain</i>
74. Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo	<i>Abstain</i>
75. Mhe. Said Amour Arfi	<i>Abstain</i>
76. Mhe. Mwanawetu Said Zarafi	<i>Abstain</i>
77. Mhe. Salim Abdallah Khalfani	<i>Abstain</i>
78. Mhe. Mhonga Said Ruhwanya	<i>Abstain</i>
79. Mhe. Salim Hemed Khamis	<i>Abstain</i>
80. Mhe. Anna Maulidah Komu	<i>Abstain</i>
81. Mhe. Mwadini Abbas Jecha	<i>Abstain</i>
82. Mhe. Magdalena Hamis Sakaya	<i>Abstain</i>
83. Mhe. Ibrahim Mohamed Sanya	<i>Abstain</i>
84. Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa	Hakuwepo
85. Mhe. Mohamed Habib Juma Mnyaa	<i>Abstain</i>
86. Mhe. Fatma Mussa Maghimbi	<i>Abstain</i>
87. Mhe. Masoud Abdallah Salim	<i>Abstain</i>
88. Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Hakuwepo
89. Mhe. Lucy Fidelis Owenya	<i>Abstain</i>
90. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Hakuwepo
91. Mhe. Ania Said Chaurembo	<i>Abstain</i>
92. Mhe. Omar Ali Mzee	<i>Abstain</i>
93. Mhe. Ali Said Salim	<i>Abstain</i>
94. Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili	<i>Abstain</i>
95. Mhe. Bakari Shamis Faki	<i>Abstain</i>
96. Mhe. Mohamed Ali Said	<i>Abstain</i>
97. Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga	<i>Abstain</i>
98. Mhe. Juma Said Omar	<i>Abstain</i>
99. Mhe. Ali Khamis Seif	<i>Abstain</i>

100. Mhe. Savelina Silvanus Mwijage	<i>Abstain</i>
101. Mhe. Khadija S. Ally Al-Qassmy	<i>Abstain</i>
102. Mhe. Mgeni Jadi Kadika	<i>Abstain</i>
103. Mhe. Maida Hamad Abdallah	Ndiyo
104. Mhe. Anna Margareth Abdallah	Ndiyo
105. Mhe. Mohamed Rished Abdallah	Ndiyo
106. Mhe. Mohammed Abdi Abdulaziz	Ndiyo
107. Mhe. Bahati Ali Abeid	Ndiyo
108. Mhe. Ali Haji Ali	Hakuwepo
109. Mhe. Fatma Othman Ali	Ndiyo
110. Mhe. Aziza Sleyum Ally	Ndiyo
111. Mhe. Ame Pandu Ame	Ndiyo
112. Mhe. Kheri Khatib Ameir	Ndiyo
113. Mhe. Ameir Ali Ameir	Ndiyo
114. Mhe. Idd Mohamed Azzan	Ndiyo
115. Mhe. Rostam Abdulrasul Azizi	Ndiyo
116. Mhe. Faida Mohamed Bakar	Ndiyo
117. Mhe. Feetlham Filipo Banyikwa	Ndiyo
118. Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga	Hakuwepo
119. Mhe. Gosbert Begumisa Blandes	Ndiyo
120. Mhe. Felister Aloyce Bura	Ndiyo
121. Mhe. Pindi Hazara Chana	Hakuwepo
122. Mhe. Dr. Raphael Masunga Chegeni	Ndiyo
123. Mhe. Andrew John Chenge	Ndiyo
124. Mhe. Diana Mkumbo Chilolo	Ndiyo
125. Mhe. Samuel Mchele Chitalilo	Ndiyo
126. Mhe. Mohammed Amour Chomboh	Ndiyo
127. Mhe. Paschal Contantine Degera	Ndiyo
128. Mhe. Hasnain Gulamabbas Dewji	Ndiyo
129. Mhe. Mohammed Gulam Dewji	Ndiyo
130. Mhe. Anthony Mwandu Diallo	Ndiyo
131. Mhe. Meryce Mussa Emmanuel	<i>Abstain</i>
132. Mhe. Col. Saleh Ali Farrah	Hakuwepo
133. Mhe. Stephen Jones Galinoma	Ndiyo
134. Mhe. Dr. Zainab Amir Gama	Ndiyo
135. Mhe. Josephien Johnson Genzabuke	Ndiyo
136. Mhe. Ali Juma Haji	Ndiyo
137. Mhe. Dr. Haji Mwita Haji	Ndiyo
138. Mhe. Zuleikh Yunus Haji	Ndiyo
139. Mhe. Hemed Mohammed Hemed	Ndiyo
140. Mhe. Maria Ibeshi Hewa	Ndiyo
141. Mhe. Parmukh Sing Hoogan	Ndiyo
142. Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma	Ndiyo

143. Mhe. Issa Kassim Issa		Ndiyo
144. Mhe. Yahya Kassim Issa		Ndiyo
145. Mhe. Athumani Said Janguo		Ndiyo
146. Mhe. Asha Mshimba Jecha		Ndiyo
147. Mhe. Rajab Ahmad Juma		Ndiyo
148. Mhe. Siraju Juma Kaboyonga	Ndiyo	
149. Mhe. Janet Bina Kahama		Ndiyo
150. Mhe. Nazir Mustafa Karamagi		Ndiyo
151. Mhe. Teddy Louse Kasella-Bantu		Ndiyo
152. Mhe. Mariam Reuben Kasembe		Ndiyo
153. Mhe. Eustace Osler Katagira		Ndiyo
154. Mhe. Vita Rashid Kawawa		Ndiyo
155. Mhe. Gaudence Cassian Kayombo		Hakuwepo
156. Mhe. Charles N. Keenja		Ndiyo
157. Mhe. Yono Stanley Kevela		Ndiyo
158. Mhe. Vuai Abdallah Khamis		Ndiyo
159. Mhe. Mwajuma Hassan Khamis		<i>Abstain</i>
160. Mhe. Hassan Rajab Khatib		Ndiyo
161. Mhe. Hassan Chande Kigwalilo		Ndiyo
162. Mhe. Felix Ntibenda Kijiko		Hakuwepo
163. Mhe. Estherina Julio Kilasi		Ndiyo
164. Mhe. Juma Hassan Killimbah	Ndiyo	
165. Mhe. Aloyce Bent Kimaro		Ndiyo
166. Mhe. Halima Omar Kimbau	Ndiyo	
167. Mhe. Fuya Godwin Kimbita		Ndiyo
168. Mhe. Paul Peter Kimiti		Ndiyo
169. Mhe. Rosemary Kasimnbi Kirigini		Ndiyo
170. Mhe. Capt. John Damiano Komba		Ndiyo
171. Mhe. Suleiman Omar Kumchaya		Ndiyo
172. Mhe. William Jonathan Kusila		Ndiyo
173. Mhe. Al-Shymaa John Kwegyir		Ndiyo
174. Mhe. Florence Essa Kyendesya		Ndiyo
175. Mhe. Michael Lekule Laizer		Hakuwepo
176. Mhe. James Daudi Lembeli		Ndiyo
177. Mhe. Castor Raphael Ligallama		Ndiyo
178. Mhe. Devota Mkuwa Likokola		Ndiyo
179. Mhe. Dr. Festus Bulugu Limbu		Ndiyo
180. Mhe. Sameer Ismail Lotto		Hakuwepo
181. Mhe. Edward Ngoyai Lowassa		Ndiyo
182. Mhe. Emmanuel Jumanne Luhahula		Ndiyo
183. Mhe. William Vangimembe Lukuvi		Ndiyo
184. Mhe. Riziki Said Lulida		Ndiyo
185. Mhe. Anna Richard Lupembe		Ndiyo
186. Mhe. John Paul Lwanji		Ndiyo
187. Mhe. Clemence Beatus Lyamba		Ndiyo
188. Mhe. Ernest Gakeya Mabina		Ndiyo
189. Mhe. Joyce Nhamanilo Machimu		Ndiyo

190. Mhe. Ephraim Nehemia Madeje	Ndiyo
191. Mhe. Dr. Binilith Satano Mahenge	Ndiyo
192. Mhe. Yusuf Rajab Makamba	Ndiyo
193. Mhe. Jackson Muvangila Makwetta	Ndiyo
194. Mhe. Benito William Malangalila	Ndiyo
195. Mhe. John Samwel Malecela	Ndiyo
196. Mhe. Halima Mohammed Mamuya	Hakuwepo
197. Mhe. Ramadhani Athumani Maneno	Ndiyo
198. Mhe.Eng. Stella Martin Manyanya	Ndiyo
199. Mhe.Vedastusi Mathayo Manyinyi	Ndiyo
200. Mhe. Abdul Jabiri Marombwa	Ndiyo
201. Mhe. Masolwa Cosmas Masolwa	Ndiyo
202. Mhe. Haroub Said Masoud	Ndiyo
203. Mhe. Janeth Mourice Massaburi	Ndiyo
204. Mhe. Joyce Martin Masunga	Hakuwepo
205. Mhe. Zubeir Ali Maulid	Ndiyo
206. Mhe. Lucy Thomas Mayenga	Hakuwepo
207. Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka	Ndiyo
208. Mhe. Monica Ngezi Mbega	Ndiyo
209. Mhe. Mwanne Ismaily Mchemba	Hakuwepo
210. Mhe. Zakia Hamdani Meghji	Hakuwepo
211. Mhe. Mariam Salum Mfaki	Hakuwepo
212. Mhe. Feteah Saad Mgeni	Ndiyo
213. Mhe. Laus Omar Mhina	Hakuwepo
214. Mhe. Zabein Muhaji Mhita	Ndiyo
215. Mhe. Fatma Abdallah Mikidadi	Ndiyo
216. Mhe. Margreth Agness Mkanga	Hakuwepo
217. Mhe. Dunstan Daniel Mkapa	Ndiyo
218. Mhe. Nimrod Elirehema Mkono	Ndiyo
219. Mhe. Rita Louise Mlaki	Ndiyo
220. Mhe. Martha Mosses Mlata	Ndiyo
221. Mhe. Dr. Charles Ogesa Mlingwa	Ndiyo
222. Mhe. Herbert James Mntangi	Ndiyo
223. Mhe. Ali Ameir Mohamed	Ndiyo
224. Mhe. Salim Yussuf Mohamed	<i>Abstain</i>
225. Mhe. Elisa David Mollel	Ndiyo
226. Mhe. Balozzi Dr. Getrude I. Mongella	Hakuwepo
227. Mhe. Dr. Samson Ferdinand Mpanda	Ndiyo
228. Mhe. Benson Mwailugula Mpesya	Ndiyo
229. Mhe. Luhaga Joelson Mpina	Ndiyo
230. Mhe. Kilontsi Muhama Mporogomyi	Hakuwepo
231. Mhe. Basil Pesambili Mramba	Hakuwepo
232. Mhe. Felix Christopher Mrema	Ndiyo
233. Mhe. Raynald Alfons Mrope	Ndiyo
234. Mhe. Dr. Ibrahim Said Msabaha	Ndiyo
235. Mhe. Ruth Blasio Msafiri	Ndiyo
236. Mhe. Manju Salum Omar Msambya	Ndiyo

237. Mhe. Dr. James Alex Msekela	Ndiyo
238. Mhe. Balози Abdi Hassan Mshangama	Ndiyo
239. Mhe. Mgana Izumbe Msindai	Ndiyo
240. Mhe. Mwinchoum Abdulrahman Msomi	Ndiyo
241. Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu	Ndiyo
242. Mhe. Prof. Idris Ali Mtulia	Ndiyo
243. Mhe. Mtutura Abdallah Mtutura	Ndiyo
244. Mhe. Mudhihir Mohamed Mudhihir	Ndiyo
245. Mhe. Joseph James Mungai	Hakuwepo
246. Mhe. James Philipo Musalika	Ndiyo
247. Mhe. Omar Sheha Mussa	Hakuwepo
248. Mhe. Mossy Suleiman Mussa	Ndiyo
249. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu	Ndiyo
250. Mhe. Dorah Herial Mushi	Hakuwepo
251. Mhe. Dr. Harrison George Mwakyembe	Hakuwepo
252. Mhe. Prof. Raphael Benedict Mwalyosi	Ndiyo
253. Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa	Ndiyo
254. Mhe. Ludovick John Mwananzila	Ndiyo
255. Mhe. Mbaruk Kassim Mwandoro	Ndiyo
256. Mhe. Thomas Abson Mwang'onda	Ndiyo
257. Mhe. Harith Bakari Mwapachu	Ndiyo
258. Mhe. Hamza Abdallah Mwenegoha	Ndiyo
259. Mhe. Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya	Hakuwepo
260. Mhe. Damas Pascal Nakei	Hakuwepo
261. Mhe. Benedict Ngalama Ole-Nangoro	Ndiyo
262. Mhe. Richard Mganga Ndassa	Ndiyo
263. Mhe. Philemon Ndesamburo	Abstain
264. Mhe. Dr. Juma Alifa Ngasongwa	Hakuwepo
265. Mhe. Sigifrid Seleman Ng'itu	Ndiyo
266. Mhe. Kingunge Ngombale-Mwiru	Ndiyo
267. Mhe. Cynthia Hilda Ngoye	Ndiyo

SPIKA: Katibu subiri kwanza.

Waheshimiwa wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) nitaisoma, “*Iwapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zimemalizika kabla ya saa 01:45, yaani hiyo jioni, Spika ataliahirisha Bunge bila kuhoji. Lakini iwapo zimesalia dakika 10 kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao na Bunge au Kamati ya Bunge au Kamati ya Matumizi, bado haijamaliza shughuli zake, Spika anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge au Kamati ya Bunge zima au Kamati ya Matumizi ili kukamilisha shughuli zilizobaki.*” Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni dakika 10 kufikia 01:45 na ninavyotazama orodha hii inavyokwenda hadi tupate matokeo, tusije tukaathiri Kanuni hii. Kwa hiyo, natumia Kanuni hiyo kuongeza muda wa Bunge kukaa kwa kipindi kisichozidi dakika 30.

Katibu, endelea.

(Hapa zoezi la upigaji kura liliendelea)

268. Mhe. Hadija Saleh Ngozi	Ndiyo
269. Mhe. Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi	Ndiyo
270. Mhe. Juma Suleiman Nh'unga	Ndiyo
271. Mhe. Juma Abdallah Njwayo	Ndiyo
272. Mhe. Dr. Omari Mzeru Nibuka	Ndiyo
273. Mhe. Sijapata Fadhili Nkayamba	Ndiyo
274. Mhe. Said Juma Nkumba	Ndiyo
175. Mhe. Daniel Nicodem Nsanzugwanko	Ndiyo
276. Mhe. Tatu Musa Ntimizi	Hakuwepo
277. Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu	Ndiyo
278. Mhe. Ponsiano Damiano Nyami	Ndiyo
279. Mhe. Richard Said Nyaulawa	Hakuwepo
280. Mhe. Esther Kabadi Nyawazwa	Ndiyo
281. Mhe. Ussi Ame Pandu	Ndiyo
282. Mhe. Mwaka Abdulrahaman Ramadhan	Ndiyo
283. Mhe. Shally Josepha Raymond	Hakuwepo
284. Mhe. Mchungaji Dr. Getrude P. Rwakatare	Hakuwepo
285. Mhe. Kabuzi Faustine Rwilomba	Hakuwepo
286. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq	Hakuwepo
287. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said	Hakuwepo
288. Mhe. Bujiku Philip Sakila	Hakuwepo
289. Mhe. Kidawa Hamid Salehe	Ndiyo
290. Mhe. Ahmed Ali Salum	Ndiyo
291. Mhe. Salum Khamis salum	Ndiyo
292. Mhe. Prof. Philemon Mikol Sarungi	Ndiyo
293. Mhe. Lukas Lumambo Selelii	Ndiyo
294. Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka	Ndiyo
295. Mhe. Haji Juma Sereweji	Ndiyo
296. Mhe. Peter Joseph Serukamba	Ndiyo
297. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby	Ndiyo
298. Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah	Ndiyo
299. Mhe. Beatrice Matumbo shellukindo	Ndiyo
300. Mhe. Jacob Dalali Shibiliti	Ndiyo
301. Mhe. Magalle John Shibuda	Ndiyo
302. Mhe. Dr. Guido Gorogolio Sigonda	Ndiyo
303. Mhe. Mohamed Said Sinani	Ndiyo
304. Mhe. Dr. Luka Jelas Siyame	Ndiyo
305. Mhe. Mohammed Rajab Soud	Ndiyo
306. Mhe. Ali Haroon Suleiman	Ndiyo
307. Mhe. Abdallah Salum Sumry	Ndiyo
308. Mhe. Eliatta Namdumpe Switi	Ndiyo
309. Mhe. Hafidh Ali Tahir	Hakuwepo
310. Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Ndiyo
311. Mhe. Kaika Saning'o Telele	Ndiyo
312. Mhe. Fred Mpendazoe Tungu	Ndiyo
313. Mhe. Martha Jachi Umbulla	Ndiyo

314. Mhe. Zaynab Matitu Vulu	Hakuwepo
315. Mhe. Anastazia James Wambura	Ndiyo
316. Mhe. Godfrey Weston Zambi	Ndiyo
317. Mhe. Mzee Ngwali Zubeir	Ndiyo
318. Mhe. Mussa Azan Zungu	Hakuwepo

SPIKA: Katibu, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, alikuwa Zahanati. Ningeomba usome jina lake, nadhani ameingia ili aweze kukubali, kukataa au kutokupiga kura.

ND. DR. THOMAS D. KASHILILAH – KAIMU KATIBU WA BUNGE: Mhe. Gaudence Kayombo.

MHE. GAUDENCE KAYOMBO: Ndiyo! (*Makofi*).

SPIKA: Sasa Waheshimiwa Wabunge, tutasubiri zijumlishwe. Wakati tunasubiri zijumlishwe nilitaka kufafanua tu juu ya kile kinachoitwa *Abstain*. Ku-*abstain*, maana yake ni kutokuamua, yaani huungi mkono wala hukatai. Kwa hiyo, wala haihesabiki katika maana ya kuhesabu zile kura, ni kama vile mtu labda hupo, ni kama wale waliokwenda Mtera. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. JOHN S. MALECELA: Taarifa kwa Spika.

SPIKA: Mheshimiwa Malecela, taarifa!

MHE. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Spika, ningependa niwaarifu Wabunge, watu wanapotajwa majina hawapo, basi inakuwa tu ni Mtera, napenda kuwaarifu kwamba wanaokwenda Mtera, ni wana-CCM, wapinzani huwa tunasema wamekwenda Mitini. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa, nitashauriana na Kiongozi wa Upinzani, ili tupate jina mbadala kwa lile la Mtera, wao sijui tutumie lipi? (*Makofi/Kicheko*).

MHE. WILBROAD P. SLAA: Mimi nawakaribisha Karatu. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ili kuokoa muda, ngoja nisome matangazo ili tusilazimike tena kuingia katika matangazo.

Semina ya kesho ya masuala ya usalama sio saa 3:00, ni saa 4:00 asubuhi. Kuna maandalizi fulani ndani ya Ukumbi yanahitajika pale Pius Msekwa, kwa hiyo, tumekubaliana na watoa mada kwamba itakuwa ni saa 4:00 asubuhi, kesho tarehe 21 mwezi huu wa Juni, Jumamosi (*Makofi*).

La pili, Mheshimiwa William Shellukindo - Mratibu wa Klabu ya Bunge (*Range Club*), walenga shabaha wa Bunge, anawafahamisha kuwa msafara wa kwenda *JKT* Makutupora kwenye zoezi la kulenga shabaha siku ya Jumapili, tarehe 22 Juni, utanzia kwenye viwanja vya

Bunge, hapo nje saa 3:00 asubuhi. Magari mawili yameandaliwa kwa ajili ya msafara huo, lakini pia usafiri binafsi unaruhusiwa, ila tuzingatie muda.

Kwa hiyo, kutakuwa na magari hapa nje ya kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge, maana *Bunge Range Club* ina mchanganyiko wa Waheshimiwa wabunge na pia Watumishi. Kwa hiyo, ni Jumapili, keshokutwa, tarehe 22 mwezi huu wa Juni, saa 3:00 asubuhi kutokea hapa ama kama mwenye usafiri binafsi ni Makutupora, kule mnakokutana.

Tatu, nafurahi kuwatangazia kwamba Mheshimiwa *Captain John Komba*, amefaulu kupata shahada ya *BA Political Science*. Yule pale! Naomba asimame. (*Makofi*)

(*Hapa Mhe. Captain John Komba, alisimama na kuonekana*)

Mheshimiwa *Captain Komba*, alikuwa anachukua mafunzo kwa mtindo wa *Open University* na hii iwahamasishe wengine mnaotaka Shahada ya kwanza, ya pili, kuweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, amepata *BA Political Science* kutoka *Washington International University* Marekani na ameniletea Ofisini, nimeiona na nadhani tumpongeze sana Mheshimiwa *Captain John Komba*. (*Makofi*)

Kumbe ana vipaji vingi tu, ni mchangiaji mzuri katika Bunge, anaongoza kundi zuri sana la usanii katika mambo ya muziki, ana bendi mpya inaitwa, *TOT Respect* na wakati huo alikuwa akisoma kujipatia Shahada. Kwa kweli, wananchi wa Jimbo lako hawakukosea kukuchagua. Hongera sana! (*Makofi*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Naam, Mheshimiwa William Shellukindo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, katika lile tangazo kuna sehemu ya mavazi, naomba mwongozo wako. Nadhani ingesomwa vilevile katika lile tangazo.

SPIKA: Eeh, nilipitiwa. Kweli kwenye tangazo la *Bunge Range Club*, wahusika wote siku hiyo lazima wavae *track suit*. Hapana, wamesema *track suit*, hawakusema *combat*, ni *track suit*. Samahani Mheshimiwa, nilisahau hilo. Wanachama watakaoshiriki kwenye zoezi la kulenga shabaha wavae *track suits*.

Kabla ya hapo, la ziada, wafuatao nimeombwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, niwatamke kwa sababu walichangia kwa maandishi na haikuwezekana kuwatamka yeye mwenyewe. Mheshimiwa Abdallah Khamis, Mheshimiwa Elieta Switi, Mheshimiwa Rosemery Kirigini, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa *Professor* Juma Athuman Kapuya, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Salum Yusuf Mohamed. (*Makofi*)

MHE. WILBROAD P. SLAA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo Dokta Slaa.

MHE. WILBROAD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 98(2), kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ambayo inataja namna ya kupiga kura katika bajeti, haikufafanua utaratibu wa upigaji isipokuwa mhusika ataitwa kwa jina.

Sasa kimataifa na kwa bahati nzuri sisi umetutuma kwenye mabunge mengi na uzoefu tulioupata katika safari zote ulizotutuma ni kwamba katika taratibu za kimataifa kuna njia tatu za kupiga kura. Kuna wanaosema *Yes*, kuna wanaosema *No* na kuna wanaokuwa na *Abstention*. *Abstention* sio sawa na kwenda Mtera, *abstention* ni kwamba anayepiga kura ya *abstention* anakuwa yeye hachukui upande wowote katika zile mbili na kwa sababu hachukui upande wowote. (*Makofi*)

(*Hapa Waheshimiwa, walipiga kelele*)

SPIKA: Mpeni nafasi

MHE. WILBROAD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, ni kwamba anakubaliana na sehemu ya yaliyosemwa na anakataa sehemu nyingine na kueleza hiyo *dissatisfaction* yake, ndio anasema *abstention* ili yale anayoyakataa yaweze kufanyiwa kazi. Kwa kuhakikisha hiyo, hata chombo tulichoweka mbele ya Wabunge, tunganza kukitumia katika mitambo ambayo ni *electronic* ina *provide Yes, No* na *Abstention*. Bahati mbaya labda sisi wengine hatuko *exposed* kwa utaratibu huo. Nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Aah, nilikwishalieleza hilo kwamba ukiwa huna upande wowote, basi kura ya namna hiyo, haikuongezeka kwenye Ndiyo wala Hapana. Kwa hiyo, inabaki kwamba haina *effect* yoyote, yaani inaweza kuwa ni nzuri kwa maana tu itasikika hivyo, lakini haipunguzi sana uzito wa waliokubali au walikataa kama wapo.

Nikumbushe tu kwamba, mtunzi mmoja wa vitabu anaitwa Milton nadhani, Mwingereza, alipata kusema, nanukuu: “*The hottest place in hell is reserved for those who remain neutral in a crisis*”, mwisho wa kunukuu. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Kama ni suala hilo nimekwishafanya *rulling*.

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Ni lingine.

SPIKA: Mwongozo Mheshimiwa Wangwe.

MHE. CHACHA Z. WANGWE: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68, Mheshimiwa Malecela, amezungumza maneno hapa ambayo kwa tafsiri yangu ya Katiba amevunja Ibara ya 13(4) na (5) ya Katiba, kwa sababu mimi siwezi kuchukulia kwamba alikuwa anafanya mzaha, alikuwa *serious*. Inasema hivi:

“Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yeyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi.” Tano inasema: “Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Ibara hii, neno Kubagua maana yake ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali

kwa kuzingatia utafawao, kabila, mahali walipotokea, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini, jinsia au hali yao ya maisha kwa namna ambayo watu wa aina fualani wanafanywa au kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni na kuwekewa vikwazo au masharti au vipingamizi ambapo watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti na wanapewa fursa au faida iliyoko nje ya masharti au sifa za lazima isipokuwa...'. (Makofi/Kicheko)

Hivyo ndivyo inavyosema, naomba mwongozo wako Mheshimiwa, kama hajavunja na kama ameivunja achukuliwe hatua gani? (Kicheko)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Ibara aliyoitaja Mheshimiwa Chacha Wangwe, inahusu haki za msingi za raia. Kwenda Mtera sio haki ya msingi. Lakini kama anataka atamkwe anakwenda Mtera, anakielewa Chama ambacho watu wake wasipokuwapo Bungeni, basi wanakuwa wamekwenda Mtera! Kwa hiyo, Mheshimiwa John Samwel Malecela, hakufanya kosa lolote, wala hakuvunja Katiba, bado natoa wito kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, tushauriane ili tupate jina rasmi kwa ajili yao. (Makofi/Kicheko)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Taarifa.

SPIKA: Taarifa, Mheshimiwa Zitto!

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, napenda kukupa taarifa tu kwamba Mheshimiwa John Samwel Malecela ni Makamu Mwenyekiti Mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi na Mheshimiwa Chacha Wangwe ni Makamu Mwenyekiti wa *CHADEMA* (Kicheko).

SPIKA: Sawa sawa! Taarifa hiyo ni sahihi (Kicheko).

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Spika, Taarifa. Niko huku, Mudhihir!

SPIKA: Loh, aah! Mheshimiwa Mudhihir! Ndiyo Mheshimiwa Mudhihir!

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Nilikuwa napenda tu kutoa taarifa kwamba ukitaka kujua tofauti ya *CHADEMA* na *CCM*, angalia Makamu Mwenyekiti Mstaafu na Makamu Mwenyekiti ambaye yuko madarakani. Asante sana. (Kicheko)

SPIKA: Kwa kuwa ni vyama vingi, lazima wawe tofauti. Hawawezi kuwa sawa! (Makofi/Kicheko)

MATOKEO YA KURA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya upigaji kura. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliopiga kura ni 272, hakuna iliyoharibika kwa sababu wote walitamka walichokitaka. Idadi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao hawapo ni 46. Sasa kura za hapana, hakuna. Idadi ya Wabunge ambao hawakupiga upande wowote, yaani *Abstain*, ni 36. Waliopiga kura za Ndiyo ni 236. Kwa kuwa, hili ni suala la kupitishwa kwa theluthi mbili na

theluthi mbili ni Wabunge 212 kwa hiyo, nafurahi kutangaza kwamba kwa kura hizo Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2008/2009 imepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali
yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru nyote nikianzia Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye amekuwa akiongoza shughuli za Serikali humu Bungeni. Mheshimiwa waziri wa Fedha, leo ni siku ya nane, kikao cha nane, tumefanya kazi nzuri hadi kufikia hapo. Kama kawaida mjadala umekuwa una hamasa kubwa kwa sababu tunazungumza mambo ya msingi. Kwa hiyo, tuendeleo tu kusameheana kwa sababu sote lengo letu ni kujenga Taifa letu. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote na nawatakia *weekend* njema.

Sasa hivi, naliahirisha Bunge, hadi hapo saa 03:00 asubuhi, Jumatatu, tarehe 23 Juni, 2008 hapa hapa katika ukumbi huu Dodoma.

*(Saa 01.57 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,
Tarehe 23 Juni, 2008, saa 3.00 Asubuhi)*